

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Kumi – Tarehe 20 Aprili, 2017

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa tukae. Leo ni Kikao cha Kumi, tunaendelea na Mkutano wetu wa Saba, Katibu.

DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:

KIAPO CHA UAMINIFU

Mbunge afuataye aliapa:-

Mhe. Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mchungaji Rwakatare, tunakukaribisha sana. Huko uko karibu na Mheshimiwa Lijualikali na Mheshimiwa Susan Kiwanga. *(Makofi/Kicheko)*

Katibu tuendeleee.

DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

SPIKA: Maswali kwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu. *(Makofi)*

Simuoni Kiongozi wa Upinzani kwa hiyo tunaendelea, aah, yupo leo. Mheshimiwa Freeman Mbowe kama una swali tafadhali. *(Kicheko)*

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Mheshimiwa Waziri Mkuu nafikiri una hakiki kutokana na vyanzo vyako mbalimbali kwamba Taifa katika wakati huu linakumbwa na sintofahamu, hofu na taharuki nyingi zinazosababishwa mambo kadhaa.

Mheshimiwa Spika, moja na la msingi ambalo napenda kukuuliza ni kwamba kuna hofu kuhusu haki ya kikatiba ya kuishi na kupata hifadhi. Kuna hofu kuhusu haki ya kikatiba ya kupata na kutoa habari ambayo inaweza kuchagizwa kwa kiwango kikubwa na kukosekana kitu kama uhuru wa Bunge kusikika kwa wananchi ambao wametutuma mahali hapa.

Mheshimiwa Spika, kuna hofu kuhusu watu kupotea, watu kutekwa na jambo hili limetawala sana kwenye mijadala katika mitandao na vyombo vya habari na mfano halisi ukiwemo kupotea kwa msaidizi wangu Ben Saanane ni miezi sita sasa Serikali haijawahi kutoa kauli yoyote, haielezi ni nini kinafanyika jambo ambalo linapelekea pengine kuamini aidha, Serikali haitaki kufanya uchunguzi ama imeshindwa kufanya uchunguzi. Mheshimiwa Waziri Mkuu unalipa Taifa kauli gani kuhusu hofu na taharuki hii ambayo imelikamata Taifa? *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbowe, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge amezungumzia kwamba Taifa lina hofu ya kikatiba kwenye maeneo kadhaa lakini pia amerejea michango mbalimbali

ya Waheshimiwa Wabunge iliyokuwa inazungumzia suala la usalama wa nchi kwamba Taifa na Watanzania wana hofu na kwamba bado Serikali hatujatoa kauli.

Mheshimiwa Spika, kupitia majibu yangu lakini pia wakati wa bajeti yangu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, jambo hili mara lilipojitokeza tulitoa taarifa ya awali na mimi niliwasihi Watanzania kwamba Taifa letu kwanza ni Taifa ambalo kwa miaka mingi limekuwa na utamaduni mzuri wa watu kuheshimiana, watu kufuata misingi, kanuni, sheria na taratibu. Pia tunatambua kuwa kumetokea matukio mbalimbali kwa miaka mingi huko na matukio haya tumeendelea kuyaachia vyombo vya usalama kufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa jambo ambalo limejadiliwa sana na Waheshimiwa Wabunge na hofu ambayo imekuwa ikielezwa kwamba Watanzania wana hofu, nilitumia nafasi yangu kuwasihi Watanzania kwanza waiamini Serikali yao kwamba moja kati ya majukumu ya Serikali yetu ni kuhakikisha Watanzania wanaishi kwa amani na kwa uhakika wa ulinzi wa wao wenyewe na mali zao wakati wote. Pia hata Serikali yetu nayo imeweka azma hiyo na kwamba jambo hili tunaendelea kuliimarisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kupitia michango hiyo pia hata Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alieleza na mimi nikarejea kuimarisha hili kwamba Watanzania tunaomba mtupe muda, vyombo vyetu vinaendelea kufanya kazi ya kuchunguza ili tuweze kubaini ni nini hasa sasa kinatokea na ni kwa nini Watanzania wanafikia hapo kuwa na hofu. Haya yote huwezi kutoa matamko hadharani zaidi ya kuwasihi Watanzania kuwa watulivu na kutoa ushirikiano kwa Taifa na kwamba vyombo vyetu vinapofanya kazi kama tutaweza kueleza haraka maazimio yetu tunaweza tukapoteza njia nzuri ya kupata vyanzo vya kwa nini kasoro hizi zinajitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nirudie tena na nimsihi sana Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwamba Serikali ipo na

imesikia haya kutoka kwenye michango ya Waheshimiwa Wabunge. Naomba niwasihii tena Watanzania kuwa na imani na Serikali yenu kwamba tunaendelea na ufuatiliaji wa matukio yote yaliyozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge tuone kwa nini yanajitokeza, nani anasababisha kwa sababu vyanzo vya matatizo haya ni vingi na vinahitaji uchunguzi wa kina ili tuweze kujua hasa dosari iko wapi na tuweze kudhibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wito wangu kwa Watanzania, tuendelee na utamaduni wa kutoa taarifa kwa vyombo vyetu pindi tunapojua kwamba hapa kuna jambo au linaandaliwa au limetokea na aliyesababisha ni fulani ili tuweze kuchukua hatua za papo kwa papo ili tuweze kunusuru watu wengine wasiweze kukubwa na matukio hayo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge mwenzangu na Kiongozi mwenzangu hapa Bungeni tuendelee kuipa muda Serikali kufanya ufuatiliaji wa jambo hili na baadaye tutakapogundua kabisa tutakuja kuwapa taarifa ili Watanzania wawe na uhakika na shughuli zao wanazoendelea nazo. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani, swali fupi la nyongeza.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kukiri kwamba Taifa letu lina historia ya watu kuheshimiana, ni jambo jema na ni kweli tumekuwa na historia hiyo na hofu ninayoizungumza ndiyo hiyo hiyo kwamba ustaarabu na utamaduni huo unaonekana kupotea kwa kasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kututaka tuiamini, tuipe muda lakini hapa tunazungumzia kifo au kupotea kwa mtu. Jambo hili linazua hofu kwa familia na kwa Watanzania wote katika ujumla wake. Nina hakika mtu yeyote mwenye mapenzi mema na nchi yetu anaona jambo hili linataharuki kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ni utamaduni wa nchi yetu kushirikiana na mataifa mbalimbali katika maeneo

mbalimbali na kwa sababu mataifa yanatofautiana katika uwezo wa kufanya tafiti, uwezo wa kufanya uchunguzi na kipekee nikizungumza Uingereza ambayo tuna mahusiano mazuri nao wametumika maeneo mbalimbali duniani pale ambapo panaonekana pana uzito wa kiuchunguzi, taasisi yao ya *Scotland Yard* ina uwezo wa kusadia. Kama ambapo ilifanyika Kenya wakati amepotea na ameuwawa katika mazingira ya kutatanisha Robert Ouko aliyekuwa Kiongozi katika Jamhuri ya Kenya watu wakaomba Serikali kama imeshindwa kuchunguza iombe *Scotland Yard* watoe msaada na wana utaalim mkubwa katika *forensic investigation* na waliweza kufanya hivyo na wakatoa taarifa yao iliyokuwa sahihi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kutokana na mazingira hayo basi kwa nini Serikali isitoe kauli kwa sababu miezi sita ni mingi na hofu inazidi kuwa kubwa, kwa nini Serikali isione umuhimu wa ku-*engage Scotland Yard* iweze kuja kusaidiana na jeshi letu na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama ili kuonyesha ile nia njema kujaribu kuchunguza jambo hili kwa haraka kwa sababu wenzetu tukiri wana teknolojia ya ziada. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile Waziri Mkuu atakumbuka katika uhuru na haki niliyoizungumzia hapa hajatoa kauli yoyote kuhusu kurushwa kwa *Bunge live*. Hebu tupe kauli ya Serikali basi turejee utamaduni wetu wa Kitanzania Bunge hili lisikike kwa wananchi ambao wametutuma hapa ndani. Tunaomba kauli ya Serikali kwenye hilo vilevile. (Makofi)

(Hapa sauti ilikatika kutokana na tatizo la kiufundi kwenye vipaza sauti)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naona vipaza sauti havifanyi kazi.

SPIKA: Nadhani sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu tunaweza tukaendelea, majibu tafadhali, Makatibu mlinde muda.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Mbowe, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, najua kuna maswali mawili, la kwanza ni lile la kwa nini Serikali isishirikiane na mataifa mengine katika kufanya uchunguzi wa matukio kadhaa ndani ya nchi. Kwanza, nataka nikuthibitishie kwamba Taifa letu linayo mahusiano na mataifa kadhaa ambayo tunashirikiana kwenye mambo mbalimbali ikiwemo na mambo ya kiulinzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na matukio haya yanayojitokeza huku ndani, nikuhakikishie pia Taifa letu lina uwezo wa ndani wa kufanya ufuatiliaji wa kutambua matukio haya ya awali ya mtu kufariki au kutoweka mahali. Baada ya familia husika kutoa taarifa tunaweza tukafanya uchunguzi huo na baadaye tukaweza kubaini vyanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nimesema yote haya lazima mtuamini Serikali kwamba tunayo nia njema kabisa ya kutambua vyanzo na namna ya kudhibiti uendelezaji wa matukio yote ambayo yamejitokeza nchini. Kwa hiyo, mimi niseme kwamba...

MHE. FREEMAN A. MBOWE: *(Alizungumza bila kutumia kipaza sauti).*

WAZIRIMKUU: Sasa unaniuliza swali la tatu tena? Niache nijibu basi kwa sababu mimi najua cha kujibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kwamba Serikali haina kikomo cha uchunguzi kutegemea na *nature* ya tatizo lenyewe. Familia ya mtajwa aliyetangulia mbele za haki au vinginevyo hata sina uhakika, tunaweza kusema kwamba uchunguzi huu utakapokamilika taarifa itatolewa. Ingawa umesema kwamba ni miezi sita lakini kama ambavyo nimesema kwenye jibu la msingi kwamba itategemea kama vyombo vyetu vinapata msaada kutoka kwenye jamii na vyanzo vingine

na teknolojia ambayo tunaitumia kuweza kufikia hatua ya kupata majibu ya uchunguzi ambao tunautoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado naendelea kutoa kauli ya kuwaomba Watanzania kuwa watulivu na kuamini jeshi letu kwamba linafanya kazi. Vilevile sisi Serikali jambo hili ni letu, Watanzania watupe ushirikiano wa kutuhabarisha vyanzo vya matukio haya ili tuweze kufikia hatua muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge alitaka pia kupata ufafanuzi wa jambo la pili ambalo lilishazungumzwa na Bunge lililopita na maamuzi yalishatolewa ya kwamba Bunge letu litakuwa limeweka utaratibu wa namna ya kuwafikishia matangazo Watanzania. Utaratibu huo unaendelea na Watanzania wanapata matangazo kupitia utaratibu ambao tumeuandaa. Kwa hiyo, tutaendelea kuboresha kadiri ambavyo tunaona inafaa ili kuweza kuwafikishia ujumbe Watanzania. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu. Swali linalofuata litaulizwa na Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na afya njema.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ushahidi wa kutosha kabisa kuhusiana na wizi unaofanyika kwenye biashara yetu ya korosho hasa katika Mikoa ya Mtwara na Lindi kutokana na kazi iliyofanywa na TAKUKURU iliyobainisha kwamba kumekuwa na upotevu wa kiasi kikubwa sana cha fedha ambacho ni takribani shilingi za Kitanzania bilioni 30 kutoka kwenye Bodi ya Korosho. Hata hivyo, mimi binafsi na naamini na wengine hawajasikia tamko lolote juu ya jambo hili kutoka Serikalini. Je, leo Serikali inatuambia nini kuhusu ubadhirifu huu uliotokea hapa nchini kwetu hasa kwa wananchi wa Mikoa ya Mtwara na Lindi kwa sababu jambo hili linaweza kutokea sehemu yoyote ndani ya nchi yetu? Naomba majibu ya Serikali. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa kwa swali hilo. Majibu Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salma Kikwete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa vyama vyetu vya ushirika nchini umeweza kuanza kuonyesha dalili ambayo si nzuri kwa sababu ya upotevu mkubwa wa mapato ya fedha za ushirika ambayo pia inapelekea kukatisha tamaa wakulima wetu kote nchini. Ni kweli kwamba Serikali imechukua hatua thabiti kufanya mapitio ya vyama vyote vya ushirika kwa mazao yetu makubwa ambayo yanatuingizia pato kubwa nchini na yanaleta manufaa kwa wakulima wetu. Tulianza na zao la korosho baada ya kupata tuhuma hizo tulipeleka wakaguzi *COASCO* na baadaye tukapeleka *TAKUKURU* kwa uchunguzi zaidi lakini kupitia vikao mbalimbali vya wadau wa mazao yenyewe huwa wanabainisha kasoro zinazojitokeza kwenye uendeshaji wa mazao hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa kumbukumbu zangu na kwa kuwa mimi mwenyewe pia ni mdau wa zao la korosho tulikuwa na kikao Bagamoyo ambacho pia kilitoa taarifa ya ubadhirifu wa shilingi bilioni 30 kwa Bodi yetu ya Korosho Mkoani Mtwara. Serikali iliunda timu maalum pamoja na *TAKUKURU* kwa ajili ya uchunguzi, lakini baadaye uchunguzi ulibaini kwamba hasara ile ni ya shilingi billioni sita na siyo shilingi bilioni 30 kwa Bodi ya Korosho na hasara ile haikusababishwa na Bodi ilisababishwa na Vyama Vikuu pamoja na Vyama vya Ushirika vilivyoko kwenye ngazi za kijiji na kata. Hatua kadhaa zimechukuliwa kwa watendaji wote ambao wamehusika kwenye ubadhirifu. Vyama vya msingi na vyama vikuu vyote vilifanyiwa uchunguzi na hatua thabiti zimeanza kuchukuliwa na nyingine zitaendelea kuchukuliwa kadiri tunavyoendelea.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka niwaambie Watanzania kwamba jambo hili la ushirika haliko kwenye zao la korosho pekee liko pia kwenye mazao kama tumbaku,

pamba, kahawa, chai na mazao mengine yote makuu. Tumeanza kufanya mapitio ya kaguzi za kina kwenye ushirika wa mazao haya kubaini ubadhirifu ili tuweze kufanya marekebisho ya namna nzuri ya kuendeleza mazao haya ili wakulima waweze kupata tija. Kwa sasa tunaendelea na zao la tumbaku, ukaguzi unaendelea na tumeanza na chama kikuu sasa tunaenda kwenye *AMCOS* tukishamaliza tutaenda kwenye mazao mengine yakiwemo pamba, kahawa, chai na yale yote ambayo yameunda ushirika kwa lengo la kuwalinda wakulima, kuhakikisha kwamba fedha za wakulima zinawafikia wakulima wenyewe na hii ni pamoja na kuondoa tozo ambazo zimewekwa na vyama vyenyewe ambavyo pia vinamletea hasara mkulima.

Mheshimiwa Spika, naomba kusisitiza tu kwa Mheshimiwa Mbunge kwamba hatua hizi zinaendelea kuchukuliwa na tutaendelea kuhakikisha kwamba ushirika nchini unaimarika na unaongozwa na watu waaminifu ambao hawatawaletea hasara wakulima wetu, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema, ooh, Mheshimiwa umesimama swali la nyongeza.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Ndiyo Mheshimiwa.

SPIKA: Ahsante sana, una nafasi kabla ya Mheshimwa Lema, swali fupi la nyongeza.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu yake mazuri Waziri Mkuu naomba nimuulize swali la nyongeza. Haijalishi kwamba ni kiasi gani cha pesa kilichochukuliwa, ufahamu wangu ulikuwa ni hizo lakini nimepata majibu kwamba ni bilioni 6. Sasa hizi shilingi bilioni 6 kwa sababu hii ni haki ya wananchi, je, wanchi hawa wanazipataje? *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salma Kikwete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, stahili ya msingi hapa ni wakulima kupata haki yao ya msingi lakini kwa kuwa tulianzisha huo uchunguzi na tulihusisha vyombo vyetu na vina utaratibu kwa hiyo vitakapokamilisha kabisa uchunguzi hatua kali zitachukuliwa. Inawezekana pia moja kati ya hukumu itakayotolewa ni pamoja na kurejesha fedha kwa wale wote waliothibitika kwamba fedha hizo wamezipoteza na hiyo ndiyo njia sahihi ambayo tunatarajia vyombo vyetu vinaweza vikatoa maamuzi hayo ili wakulima waweze kupata stahiki yao ili waendeleo pia kuboresha kilimo kwa msimu ujao. Tutaendelea kufanya hilo kwa mazao yote ambayo fedha hii inapotea, tutawasiliana kuona sheria zinazotumika lakini ni vyema tukaona kabisa kwamba sheria inayowataka wakulima warejeshewe fedha inaweza kuwa nzuri zaidi ili haki yao isiweze kupotea kabisa. Serikali itasimamia jambo hilo pia.

SPIKA: Mheshimiwa Lema.

MHE: GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi ya kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu jitihada za Serikali ya Awamu hii ya kupigania sera ya Tanzania ya viwanda ambalo ni jambo muhimu sana kila mtu mwenye akili timamu analipongeza. Hata hivyo, ili suala la viwanda liweze kuwa ni la uhakika na kweli ni lazima *investors* ama wafanyabiashara wawe na mazingira huru na mazingira yasiyokuwa na mashaka katika utekelezaji wa shughuli zao za kila siku za biashara ili kuelekea katika *investment* hizo za viwanda.

Mheshimiwa Spika, *Tanzania Revenue Authority (TRA)* wamekuwa wakitesa na kusumbua sana wafanyabiashara hasa wa mikoa mikubwa kama Dar es Salaam, Arusha,

Mwanza na Mbeya. Katika kila mkoa na hasa mimi nakotoka Arusha, *TRA* wamekuwa wakitumia Polisi, Usalama wa Taifa na TAKUKURU kuwasumbua wafanyabiashara, kuwatishia mpaka kesi za *money laundering* kwenye masuala yanayohusu kodi. Sasa ili wafanyabiashara hawa waweze kufanya kazi zao kwa uhakika na waweze kuwa na *confidence* ya uwekezaji katika Taifa hili, nini kauli ya Serikali juu ya mfumo wa *TRA* unaotumika sasa wa kusumbua na kuwapa taabu wafanyabiashara katika shughuli zao za kila siku? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Godbless Lema, Mbunge wa Arusha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba tunacho chombo ambacho kinawajibika katika ukusanyaji wa kodi kutoka kwa walipa kodi wetu wakiwemo wafanyabiashara. Pia wafanyabiashara hawa pamoja na haki yao ya kulipa ambayo kila mmoja ni wajibu wake kulipa tunatambua kwamba wako wafanyabiashara ambao wana madeni sugu. Jambo ambalo nalieleza nimelishuhudia pia hata kwenye televisheni na tuliwahi kupata taarifa na Mkuu wa Mkoa wa Arusha pale ambapo *TRA* kupitia chombo chake Makao Makuu kiliunda *task force* ya ufuatiliaji wa madeni sugu kwa wadaiwa sugu na wadaiwa sugu wale si wote lakini wachache hawataki kabisa kulipa pamoja na kwamba wanajua wao ni wadaiwa sugu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, *task force* ilikuwa na mkakati wa kuwapitia wadaiwa sugu wale wachache ili waweze kulipa madeni yao. Sasa ile *task force* iliundwa kwa pamoja na *TRA* wenyewe, kulikuwa na Jeshi la Polisi pamoja na TAKUKURU ili kuona kuwa wanapokwenda kule hakutumiki vitendo ambavyo havikubaliki kama vile utoaji wa rushwa ili madeni hayo yasilipwe au namna nyingine yoyote ambayo pia mfanyabiashara anaweza kuona kwamba si sahihi kwake. Kwenye msafara ule tuchukue mfano wa Arusha

tulipata taarifa kwamba Polisi walikuwa wanatembea na silaha lakini si kwa lengo la kumtisha mfanyabiashara ni kwa sababu ya utaratibu ambao jeshi inao hasa wanapokwenda kufuata fedha kama zinaweza kulipwa papo kwa papo. Kwa hiyo, ile ilileta mtikisiko kidogo kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, nataka nitumie nafasi hii pia kumshukuru Mkuu wa Mkoa wa Arusha kwamba aliita wafanyabiashara pamoja na *TRA* na kueleza kwanza umuhimu wa ulipaji kodi kila mmoja atambue na walipaji sugu watambue kwamba ni haki yao kulipa kodi kwa biashara ambayo wameifanya. Pia alieleza vyombo vyetu zile silaha iwe ni kwa ajili ya kulinda tu ule msafara kwa sababu pia wanahusika kukusanya fedha lakini sio kwa ajili ya kumtisha mfanyabiashara. Kwa hiyo, aliweza kurudisha amani na kuondoa mashaka waliyonayo wafanyabiashara na kuwafanya wafanyabiashara na *TRA* kuwa marafiki na huo ndio msisitizo wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nataka niwaambie wafanyabiashara kwamba *TRA* inao utaratibu wa wafanyabiashara ambao wanadhani wanatendewa sivyo. *TRA* imeunda dawati ambalo liko katika kila mkoa la kusikiliza kero za wafanyabiashara pindi inapotokea kuna vitendo ambayo si sahihi. Kwa hiyo, watumie madawati hayo kupeleka malalamiko yao na tunaamini madawati hayo yatafanya vizuri. Jambo la msingi kwa wafanyabiashara na walipa kodi wote ni kufahamu kwamba ni muhimu kulipa kodi kwa ajili ya maendeleo yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nimhakikishie kwamba Serikali inaheshimu wafanyabiashara, Serikali inatambua wawekezaji wote pamoja na wale wanaoendesha viwanda na maeneo mengine na tutawapa ushirikiano, waendeleo kutambua umuhimu wao wa kulipa kodi na sisi tutaheshimu kodi yao wanayotupa na kila mmoja ajue wajibu wake. *TRA* yetu kama ambavyo tumesema iendeleo kutoa elimu kwa wafanyabiashara na walipa kodi wote ili tuweze kupata kodi kwa njia ambayo haimpelekei hofu mfanyabiashara. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Lema ameridhika, tunaendelea.
(Kicheko)

MHE. GODBLESS J. LEMA: Ninalo Mheshimiwa.

SPIKA: Mheshimiwa Lema swali fupi sana la nyongeza.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu yake. Kwa sababu *TRA* ina sheria zake na kwa sababu amekiri kwamba hii *task force* inakuwa-*engaged* kwa wale wafanyabiashara ambao ni wadeni sugu wa *TRA*. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa vile kuna sheria zinazoendesha shirika hili la kodi, ni kwa nini sheria hizo zisitekelezwe kwa kina na kwa uthabiti kuliko kutumia *task force* ya Jeshi la Polisi, TAKUKURU pamoja na Usalama wa Taifa kitu ambacho kinatia hofu sana wafanyabiashara hao.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba TAKUKURU, Usalama wa Taifa na Jeshi la Polisi hawafahamu mambo yanayohusu kodi. Sasa hata kama ni *task force* kwa nini isiwe inahusisha *TRA* wenyewe pamoja na sheria zao za kodi ambazo zinajulikana nini kitafanyika iwapo mfanyabiashara ataendelea kukaidi kulipa kodi katika Taifa hili? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Godbless Lema kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimesema *task force* ni kwa ajili ya wale ambao kwa makusudi hawataki kutekeleza sheria ya ulipaji wa kodi kwa kuwatembelea kwenye maeneo yao, siyo wote ni wachache wale sugu. Nimeeleza kwamba *task force* hii imejengwa na *TRA* wenyewe Polisi na TAKUKURU na hapa kila mmoja ana wajibu wake. Kama mlipa kodi anaamua kulipa mpaka afuatwe na kwa sababu wanakusanya fedha Polisi yeye yuko pale kwa ajili ya ulinzi wa fedha ambayo inakusanywa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU yuko pale kuona kwamba hakuna nafasi ya rushwa kutokea. Kwa sababu pale inakwenda kumuuliza na wakati mwingine mlipa kodi sugu anaweza kudhani kwamba anadaiwa fedha nyingi akatamani kufanya makubaliano na Afisa wa *TRA* kwa lengo la kutoa rushwa. Kwa hiyo, mtu wa TAKUKURU yuko pale kuhakikisha kwamba hakuna jambo lolote linalohusiana na rushwa linalofanywa kati ya mdaiwa sugu ambaye hakutaka kulipa yeye mwenyewe labda angeweza kushawishi alipe kidogo ili jambo lake liweze kuisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kila mmoja ana wajibu wake lakini mwenye dhamana kubwa pale ni *TRA* kukumbushia sheria, kuonyesha kipindi ambacho amekaa bila kulipa na kwamba sasa anatakiwa kulipa kodi na kwa kuwa ni mdaiwa sugu basi pale inaonekana kwamba hataki kuchukua hatua hiyo wanatakiwa kumpeleka Polisi hata kama itakuwa alikuwa hana notisi. Kwa hiyo, timu ile inalenga zaidi kuhakikisha kwamba hakuna vitendo vya uovu vinavyoendelea kwenye uendeshaji wa zoezi lile lakini halilengi kumtisha mfanyabiashara. Polisi hawajibiki kumtisha wala TAKUKURU hausiki na mfanyabishara isipokuwa ni *TRA* mwenyewe kama ambavyo nimeeleza.

Mheshimiwa Spika, kwa hili nataka niwahakikishie wafanyabiashara, pamoja na haya yote yanayoendelea kwamba *task force* inapita kwenye maeneo haya haina nia mbaya kabisa na wafanyabiashara wetu na wawe na amani. Cha msingi zaidi kila mmoja sasa aone umuhimu wa kulipa kodi bila shuruti ili shughuli zetu ziweze kwenda kama ambavyo tumekubaliana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Venance Mwamoto.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Spika, nami naomba nimuulize swali Mheshimiwa Waziri Mkuu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa moja ya sababu ambazo zilipelekea wananchi wengi kutoa ridhaa kwa

Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuongoza ilikuwa ni ahadi nzuri ambazo zilitolewa. Pamoja na kuwa ahadi hizo nyingi zimeanza kutekelezwa lakini kulikuwa kuna kilio kikubwa sana cha wafanyakazi kwa ujumla kutokana na malimbikizo ya madeni na mishahara yao na hasa walimu. Serikali inasemaje kuhusu suala hili ili waweze kupata moyo wa kuona kweli zile ahadi ambazo walipewa na mgombea wa Chama cha Mapinduzi zimetekelzwa? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Mwamoto hilo si lingemsumbiri Mheshimiwa Angellah Kairuki baadaye leo, Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Venance Mwamoto Mbunge wa Kilolo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali tunao watumishi wengi walimu wakiwemo na kama watumishi kwa sababu wanafanya kazi zao za kila siku na nyingine zinahitaji kulipwa malipo ya ziada mbali na malipo ya mshahara, nikiri kwamba tunadaiwa na watumishi wetu ikiwemo na walimu pia. Hata hivyo, Serikali yetu imeahidi kumaliza kwa kiasi kikubwa kero hii ya madeni kutoka kwa watumishi wetu wa Serikali walimu wakiwemo. Hatua ya awali ambayo tumeichukua ni kufanya mapitio ya madeni yetu yote tunayodaiwa na watumishi ikiwemo na walimu.

Mheshimiwa Spika, madeni ya walimu yote yalishakusanywa na yalihakikiwa kwanza na Wakaguzi wa Ndani wa kila Halmashauri mahali walipo lakini madeni yale pia yameendelea kuhakikiwa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa maana ya timu ambayo imeundwa pamoja na Wizara ya Fedha ili kuona uhalali wa madeni hayo baada ya kuwa tumegundua kuwa baadhi ya madeni yamepandishwa kwa kiasi kikubwa ambayo sio halali. Kwa hiyo, kila hatua tunayoifikia ya kukusanya madeni na kuyahakiki tukishapata kiwango tunaendelea kulipa. Kwa hiyo, Serikali imeendelea kulipa madeni ya wafanyakazi na inataka iwahakikishie wafanyakazi kwamba madeni yao yatalipwa na hiyo ndiyo

stahili yao na kwa sababu tumeanza kulipa, tunaendelea kulipa kadri ambavyo tunamaliza kuhakiki ili tuweze kuondokana na madeni haya. Pia Serikali haijaishia hapo. Tumeweka utaratibu wa kudhibiti uzalishaji wa madeni kwa watumishi wetu na kuisitiza watu wafuate Kanuni na taratibu za eneo linazozalisha madeni ili tuweze kuondoa madeni ambayo sio muhimu wakati mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nataka nitumie nafasi hii pia kusema kwamba baadhi ya madeni ambayo hayana viwango vikubwa yanaweza kulipwa kwenye Halmashauri zenyewe mbali ya kulipwa na Serikali Kuu. Lazima nimshukuru Mkurugenzi Mtendaji wa Jiji la Arusha ambaye kupitia mapato yake ya ndani na kupitia Baraza lake la Madiwani waliweza kulipa madeni ya watumishi wao hasa walimu ya zaidi ya shilingi milioni mia moja na zaidi. Kwa hiyo, mfano huu ni mzuri kwa Wakurugenzi wengine kwenye Halmashauri nyingine ili kuondoa kero kwenye maeneo yao. Wanaweza kutenga fedha kupitia mapato yao ya ndani kulipa watumishi wao wakiwemo walimu ili kuondokana na ule mlolongo ambao tunatakiwa tuhakiki. Wakishahakiki wakijiridhisha na hasa baada ya kuwa tumedhibiti madeni na wao wanaweza kuruhusu kazi fulani zifanywe, wazitengenezee bajeti ili waweze kulipa moja kwa moja kuondokana na kero zinazoweza kupatikana kwa wafanyakazi. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Muda wa maswali umeisha, unaweza kurudi sasa mahali pako. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea, Katibu.

DKT. THOMAS KASHILILAH – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Maswali ya kawaida. Tunaanza na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Swali la Mheshimiwa Mbunge wa Mafinga Mjini, Mheshimiwa Cosato David Chumi.

Na. 80

Ununuzi wa Magari ya Wagonjwa

MHE. COSATO D. CHUMI Aliuliza:-

Serikali katika mwaka huu 2016 imeelekeza wazi kuwa haina mpango wa kununua magari ya wagonjwa na kwamba jukumu la kununua magari hayo limeachiwa Halmashauri za Wilaya ambazo hazimudu kununua magari hayo hali inayowafanya baadhi ya wahisani kujitolea kununua magari hayo.

Je, ni lini Serikali italeta mapendekezo ya kubadilisha sheria hiyo ili magari hayo yaingie kwenye Jedwali la Saba na hivyo kupata msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Jimbo la Mafinga Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa sasa haina mpango wa kuleta mapendekezo ya kubadilisha Sheria ya Ununuzi wa Magari ya Kubebea Wagonjwa. Jukumu la kununua magari hayo ni la Halmashauri husika ambao wanatakiwa kutenga fedha na kuhakikisha kuwa wananunua magari hayo kulingana na mahitaji. Wizara pindi inapopata misaada kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo imekuwa ikigawa magari hayo katika Halmashauri mbalimbali nchini kwa kuzingatia mahitaji.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya mwaka 2014, Jedwali la Saba imeeleza kuwa ununuzi wa vifaa tiba utapatiwa msamaha baada ya kuridhiwa na Waziri mwenye dhamana ya afya. Magari ya kubebea wagonjwa ambayo yana vigezo ambavyo vimewekwa, huombewa msamaha wa kodi na Waziri wa Afya ambapo hupatiwa *exemption certificate* yaani hati ya msamaha na Wizara ya Fedha na Mipango baada ya kujiridhisha kuwa yana vigezo stahiki. Niwasihi Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote wenye nia ya kusaidia kukabiliana na changamoto hii kwa kununua magari, kuwasiliana na Wizara ya Afya kuhusu vigezo vinavyotakiwa kabla ya kuagiza magari hayo ili yaweze kustahili kupatiwa msamaha wa kodi.

Mheshimiwa Spika, sanjari na hilo, nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge kuzihimiza Halmashauri zote nchini kuhakikisha zinatenga fedha za ununuzi wa magari haya kulingana na uhitaji halisi katika Halmashauri husika.

SPIKA: Mheshimiwa Chumi nimekuona, swali la nyongeza.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika sheria hii na kwa mujibu wa watu wa *TRA*, magari ya *ambulance* yana-*fall* katika *HS Code 87039010* ambayo kitaalamu kwenye kodi inakuwa *zero rated* yaani haina kodi isipokuwa inatakiwa kulipiwa kodi ya *VAT*. Sasa swali langu la kwanza, kwa kuwa kwa mwaka wa pili sasa mfululizo Serikali haijaweza kutenga fedha za kununua magari ya wagonjwa, inaonaje Wizara ikaanzisha mchakato wa kubadilisha sheria kwa kuileta hapa Bungeni ili magari ya wagonjwa yaingie kwenye *item no. 7* kusudi na yenyewe ya-*enjoy* msamaha wa kutolipa *VAT*? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Serikali imekiri kwamba haitaweza kununua magari ya wagonjwa isipokuwa Halmshauri zenyewe zitafute fedha kwa ajili hiyo

na Halmashauri nyingi hazijaweza kuwa na uwezo huo wa kununua hayo. Pia Waheshimiwa Wabunge wengi wanaomba misaada kutoka kwa watu mbalimbali jambo ambalo siyo *guaranteed* kwamba utapata gari. Je, Serikali iko tayari kwa wale Waheshimiwa Wabunge na Halmashauri ambazo zitapata magari ya misaada kuwalipia gharama za VAT?

SPIKA: Hivi kumbe magari ya wagonjwa yanalipa VAT?Majibu Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, kwanza, mpaka sasa utaratibu ambao unatumika haujaleta usumbufu wowote ule kama Mbunge ama mwananchi yeyote yule mwenye nia ya kutaka kununua gari la wagonjwa atauelewa na kuufuata kwa kadiri ambavyo umewekwa. Sheria ya Kodi ya mwaka 2014 ambayo inasimamiwa na wenzetu wa Wizara ya Fedha na Mipango imempa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya afya kwa maana hiyo kwa sasa ni Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kutoa mapendekezo ya msamaha kwa Waziri mwenzake wa Fedha na Mipango kwa magari na vifaa mbalimbali ambavyo vimeainishwa kwenye Jedwali la Saba la sheria hiyo ninayoisema.

Mheshimiwa Spika, hakujawahi kuwa na utata/shida yoyote ile kama mtu atafahamu utaratibu huu na akatoa taarifa kwa Waziri wa Afya kwamba ana malengo ya kuagiza gari la wagonjwa ama vifaa mbalimbali ya hospitali na Waziri wa Afya akiridhia basi atawasiliana na mwenzake Waziri wa Fedha na Mipango na mara nyingi kodi zote huwa zinakuwa *waved* (zinaondolewa). Kwa maana hiyo, hakuna haja ya kufanya mabadiliko yoyote ya kisheria.

Mheshimiwa Spika, lakini swali lake la pili la nyongeza kwamba Serikali ibadili utaratibu huu kwa sababu imeshindwa kuagiza *ambulance*, hapana. Kipaumbele cha kununua *ambulance* kwa kweli kinapaswa kutoka kwenye

Halmashauri zenyewe husika na Halmashauri kama mamlaka za Serikali zinazojitegema, zinafahamu zaidi mahitaji yake na kipato chake. Halmashauri zinapaswa tu kuweka kipaumbele kwenye kununua magari ya wagonjwa na wakishirikiana na sisi hakuna kitakachoshindikana watapata magari hayo. Sisi kama Wizara ya Afya tunachokifanya kwa kuwa tuna-*access* na wadau mbalimbali wa maendeleo tumekuwa tukishirikiana nao kuwaomba watusaidie kununua magari hayo ambayo mara kwa mara tumekuwa tukiyatawanya kwenye Halmashauri mbalimbali nchini lakini sio jukumu letu la msingi kufanya hivyo.

SPIKA: Mheshimiwa Martha Mlata na Mheshimiwa Rhoda Kunchela.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri lakini naomba nimuulize. Hivi kwenye habari ya wagonjwa haya mambo ya kodi yanatoka wapi jamani kwenye magari yao? Kwa sababu hiyo sio biashara ni huduma. Kwa hiyo, naomba aniambie hiyo ni biashara au ni huduma kwenye masuala ya VAT? Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Singida. Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, kama Serikali tumeiona changamoto hiyo na tumeanza kuifanyia kazi. Niwaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba tunapokuja na sheria mpya jambo hili yawezekana likawa limepatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali yetu ni kuhakikisha wananchi wetu wanapata huduma hasa za afya katika mrengo ulio mzuri na bila usumbufu wowote. Kwa hiyo, niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba jambo hili Serikali tumeliona na hasa hili la kodi ya VAT ambalo liko chini la Wizara ya Fedha na Mipango. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri nashukuru sana kwa kuliona hilo. Mheshimiwa Rhoda.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Spika, nataka kuuliza swali kuhusiana na changamoto ya gari katika Hospitali ya Wilaya ya Mpanda. Hospitali hii imepandishwa hadhi kutoka kwenye Wilaya kwenda kwenye Mkoa, lakini pia gari lililopo pale ni bovu na halikidhi haja ya Watanzania waliopo katika Mkoa wa Katavi. Je, ni lini Serikali itaongeza nguvu katika Halmashauri ili gari lingine lipatikane katika Manispaa ya Mkoa wa Katavi? Ahsante.

SPIKA: Swali la msingi lilihusu VAT lakini Naibu Waziri nina hakika unaweza ukalijibu hilo. Majibu kwa kifupi tafadhali Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, kwanza Hospitali ya Mpanda haijapandishwa hadhi na kuwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ila kwa sasa inatumika tu kama Hospitali ya Rufaa ya Mkoa lakini yenyewe bado ni Hospitali ya Wilaya ya Mpanda. Kwa sasa Mkoa wa Katavi unajenga Hospitali mpya ya Rufaa ya Mkoa, wapo kwenye mchakato huo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu gari la wagonjwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda ni kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba utaratibu ni kwa Halmashauri yenyewe kuweka kipaumbele kwenye kununua gari la wagonjwa kama Halmashauri inaona inalihitaji kwa wakati huo. Sisi kama Serikali Kuu, wajibu wetu siyo kuwapangia vipaumbele Halmashauri zote nchini. Halmashauri zenyewe zinapaswa ziweke vipaumbele vyao, watumie vyanzo vyao mbalimbali vya fedha na hata ruzuku inayotoka Serikali Kuu wanaweza wakaitumia kwa namna yoyote ile watakavyoona wao wenyewe kwenye Halmashauri yao ili waweze kununua gari la wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo kuhusiana na Mpanda mahsusi kama tutapata fursa ya misaada ya magari, nilikwishamuhidi Mheshimiwa Kakoso lakini pia Mheshimiwa

Mhandisi Kamwelwe kwamba tutatoa kipaumbele cha kipekee kwa Mkoa huu mpya wa Katavi kwa sababu nilifanya ziara pale na nikaona kwa kweli miundombinu yake ipo katika hali mbaya. Nilisema kama kutatokea sisi tukapata *ambulances* pale Wizara ya Afya huu ni katika Mikoa ambayo tutaipa kipaumbele cha kwanza.

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Swali la Mheshimiwa Mary Chatanda, kwa niaba yake Mheshimiwa Shekilindi.

Na. 81

Madai ya Fedha za Likizo na Upandishaji Vyeo

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI (K.n.y. MHE. MARY P. CHATANDA) Aliuliza:-

Serikali imekuwa ikitoa majibu ya upandishwaji wa madaraja na fedha za likizo kwa walimu nchini na katika Chuo cha Ualimu Korogwe kuna walimu na watumishi ambao wanadai kupandishwa vyeo na fedha za likizo.

(a) Je, Serikali ina mpango gani kuwapandisha daraja wale wanaostahili?

(b) Je, ni lini Serikali italipa madai yao ya fedha za likizo ambazo hawajawahi kulipwa?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Elimu, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mbunge wa Korogwe Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imekuwa ikiwapandisha vyeo watumishi wake wenye sifa kila mwaka. Kwa mfano, katika mwaka wa 2015/2016, Wizara iliwapandisha vyeo watumishi 2,272 kati yao watumishi 71 ni wa Chuo cha Ualimu Korogwe.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kulipa madeni mbalimbali ikiwa ni pamoja na fedha za likizo kwa walimu/watumishi katika sekta ya elimu, ambapo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016 hadi mwezi Juni, 2016 jumla ya shilingi 22,629,352,309.99 zililipwa kwa walimu 63,814. Aidha, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya shilingi 10,505,160,275.80 zimelipwa kwa walimu 22,420 na hivyo kufanya jumla ya walimu waliolipwa katika kipindi hicho kufikia 86,234. Katika malipo haya, jumla ya shilingi 13,415,410 zimelipwa kwa ajili ya madeni ya fedha za likizo kwa watumishi sita wa Chuo cha Ualimu Korogwe. Uhakiki wa madeni ya miaka ya nyuma unaendelea kuratibiwa na mamlaka husika na taratibu za malipo zitakamilishwa kwa wale watakaostahili.

SPIKA: Swali la nyongeza, endelea Mheshimiwa.

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza na nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, nini *commitment* ya Serikali juu ya kuwapandisha madaraja watumishi hawa kwa wakati?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, katika bajeti ya mwaka huu, Serikali imetenga kiasi gani cha fedha ili kuondoa adha hii wanayoipata walimu? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, kimsingi ni kwamba kama ambavyo

tumekuwa tukizungumza kila wakati ni kwamba madaraja ya watumishi husika ikiwemo walimu yatakuwa yanapandishwa mara baada ya zoezi la uhakiki ambalo pengine wengine hawapendi kulisikia lakini ni zoezi muhimu sana litakapokamilika. Kwa hiyo, nikuhakikishie tu kwamba mara zoezi hilo likishakamilika tutafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili kuhusiana na kiasi gani cha bajeti kimetengwa, naomba tusiwahishe shughuli, siku yetu ya bajeti mtapata majibu mazuri zaidi. Ahsante sana. (Makofi)

SPIKA: Jamani si mmeambiwa msiwahishe shughuli? Mheshimiwa Magdalena Sakaya nilikuona.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika majibu yake ya msingi amesema kwamba ziko fedha ambazo zimelipwa kwa madai ya walimu lakini ni kidogo sana kuendana na madai halisi ya walimu wa Tanzania kwa miaka karibu mitatu iliyopita. Kwa Wilaya ya Kaliua tu walimu wa sekondari wanadai shilingi 221,347,561 kwa mwaka 2015/2016 tu. Ni lini sasa madai haya ya walimu kwa Wilaya ya Kaliua yatalipwa kwa wakati?

SPIKA: Hivi madai hayo yanalipwa na TAMISEMI au Wizara ya Elimu? Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, kimsingi tunatambua kwamba kuna madeni ya walimu lakini naomba pia mnikubalie kwamba kweli kuna baadhi ya madeni sio madeni halali. Uzoefu unaonesha kwamba baada ya uhakiki kuna baadhi ya madeni yanashuka mpaka kufikia moja ya tatu kitu ambacho kinasikitisha na kimekuwa kikichelewesha kuwalipa walimu kwa wakati pamoja na watumishi wengine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni rai yangu kwa watumishi wote waone jambo la kulipwa ni haki yao lakini vilevile ni vyema madai yakawa halali ili kuepusha usumbufu usio wa lazima. Haipendezi sana mtu umedai halafu baadaye unaambiwa hayo madai hayastahili kwa sababu taratibu na kanuni zetu tunazijua na hivyo unaweza ukajua ni kipi unastahili na kipi hustahili.

Kwa hiyo, niseme tu kwamba kwa maneno ya Mheshimiwa Mbunge tutajitahidi kufuatilia katika Wilaya au Jimbo lako kuona kwamba hawa watumishi wanaostahili kulipwa waweze kulipwa kwa wakati baada ya uhakiki.

SPIKA: Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa sababu ya muda, swali la Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumba, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashiriki.

Na. 82

Uharibifu wa Mazingira Chanzo cha Mto Ruvu

MHE. OMARY T. MGUMBA Aliuliza:-

Mto Ruvu ndiyo chanzo kikuu cha maji katika Mkoa wa Dar es Salaam.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutenga fedha za kutunza mazingira katika vyanzo vya maji ambavyo viko katika hatari ya kukauka kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa na shughuli za kibinadamu?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwashirikisha wataalam wa SUA katika utunzaji wa mazingira katika vyanzo vya maji katika Mkoa wa Morogoro?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumba, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa miaka mitano wa kutunza na kuhifadhi vyanzo vya maji ambao utekelezaji wake ulianza mwaka wa fedha 2014/2015. Wizara yangu inatenga fedha za utekelezaji wa mpango huu katika bajeti yake kila mwaka. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 kiasi cha shilingi bilioni 2.1 kilitengwa kwa ajili ya mpango huo.

Mheshimiwa Spika, suala la utunzaji wa vyanzo vya maji ni mtambuka, ambalo linahitaji ushirikishwaji wa wadau ikiwa ni pamoja na wataalam kutoka sekta mbalimbali zikiwemo sekta za kilimo, madini, viwanda, mazingira na misitu. Mkoa wa Morogoro uko kwenye Bonde la Wami/Ruvu na wataalam na wadau wengine wanashirikishwa katika utekelezaji wake. Mpango huu pamoja na mambo mengine umeainisha maeneo ya vyanzo vya maji na kuweka mikakati ya jinsi ya kutunza na kuhifadhi maeneo hayo ili vyanzo hivyo visiharibike. Aidha, kupitia Bodi ya Maji ya Bonde la Wami/Ruvu wataalam wamekuwa wakishirikishwa katika kufanya utafiti na ukusanyaji wa takwimu na taarifa mbalimbali muhimu ili zitumike katika kutoa maamuzi sahihi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji.

SPIKA: Mheshimiwa Mgumba swali la nyongeza.

MHE. OMARY T. MGUMBA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, pamoja na majibu mazuri ya Serikali kupitia Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, lakini swali langu la msingi lililenga mahsusi vyanzo vya maji vilivyopo katika Mkoa wa Morogoro hususan katika Milima ya Uluguru katika Vijiji vya Tegetero, Kinole, Mgeta na

Hewe lakini majibu yamekuwa ya jumla mno. Sasa nataka kujua katika pesa hizi zilizotengwa shilingi 2.1 bilioni kwa ajili ya utunzaji wa maji ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya kutunza vyanzo vya maji katika Mkoa wa Morogoro ambao ndiyo chanzo cha Mto Ruvu ambao unategemewa kwa ajili ya maji ya Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na kadhalika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika Mkoa wa Morogoro tuna Chuo cha cha Kilimo cha Sokoine ambacho kina wataalam waliobobea katika masuala haya ya utunzaji wa mazingira hususan katika kilimo na wako tayari kutumika kama muda wote wanavyojitolea lakini tatizo ni uwezesaji. Je, Serikali ina mpango mkakati gani wa kuwawezesha wataalam hawa ili washiriki katika utunzaji huu wa mazingira kwa weledi zaidi?

SPIKA: Majibu ya swali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Injinia Isack Kamwelwe.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza anasema alitaka kusikia kuhusu Milima ya Uluguru na ni kweli Mto Ruvu unatokea milima hiyo na katika ziara yangu nimekwenda kuona kule unakotokea. Kwanza kabisa, ni kiasi gani cha fedha kimetengwa, Mheshimiwa Mgumba kwa vile maji yanatumika Mkoa wa Dar es Salaam zaidi, DAWASA peke yake wanatoa shilingi bilioni 1 kwenye Bonde la Wami Ruvu kwa ajili ya kushughulikia Mto Ruvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kiasi hiki cha shilingi bilioni 2.1 kilichotengwa siwezi kusema ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili hiyo lakini ni fedha nyingi sana ambayo inapelekwa kwenye Bonde letu la Wami Ruvu kwa sababu hii Taasisi ya Bonde la Wami Ruvu iko moja kwa moja chini ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Hata hivyo, upo ushirikiano mzuri na Mkoa wa Morogoro kuhakikisha kwamba rasilimali hii inatunzwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wataalam wa Chuo cha Sokoine, kama nilivyosema ushirikiano upo, kwa hiyo wote

tunashirikiana, tunapata utaalamu wa wasomi wetu wa Chuo cha Sokoine na wanajadili na ndio maana utaona kwamba Bwawa la Mindu limewekewa mipaka na tayari kuna miti inapandwa kwa ajili ya kulinda bwawa lile. Utaalamu wote huo tunaupata kutoka Chuo cha Sokoine. Kwa hiyo, tunawashirikisha hawa watu ili kuweza kuwa na makubaliano ya pamoja kuhakikisha kwamba tunatunza rasilimali hizi.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, bado tuko Wizara hiyo hiyo ya Maji, swali la Mheshimiwa Mary Deo Muro, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 83

Kusambaza Maji kwa Wananchi waishio Pembezoni mwa Bomba Kuu la Ruvu Juu - Mlandizi Dar es Salaam

MHE. MARY D. MURO Aliuliza:-

Maji ni mahitaji muhimu kwa wanadamu na viumbe vyote lakini gharama za maji ni kubwa sana.

Je, ni lini Serikali itawasambazia maji wananchi waishio pembezoni mwa bomba kuu la Ruvu Juu Mlandizi - DSM katika maeneo ya Pangani, Lumumba, Kidimu na Zogowale ikizingatiwa kuwa maeneo hayo yapo karibu na bomba hilo?

SPIKA: Majibu ya swali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Injinia Isack Kamwelwe.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mary Deo Muro, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa mradi maeneo mengi ndani ya kilometa 12 ya pembezoni mwa

bomba kuu la Ruvu Juu yameanza kupata huduma ya maji. Hata hivyo, maeneo ambayo bado hayajaanza kupata huduma ya maji yatakata huduma hiyo baada ya utekelezaji wa miradi mipya ya kujenga mtandao wa mabomba ya kusambaza maji katika maeneo yote ambayo hayana huduma hiyo. Miradi hii itatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Kwa kuanzia, tayari tunaye mkandarasi anayejulikana kwa jina la *M/S Jain Irrigation System Limited* ameanza kazi ya ujenzi wa mabomba ya usambazaji katika maeneo ya Malamba Mawili, Msigani, Mbezi Luis, Msakuzi, Kibamba, Kiluvya, Mloganzila na Mailimoja na atakamilisha kazi hiyo mwaka huu 2017. Maeneo ambayo yanapata maji kutoka Bomba la Ruvu Juu ni pamoja na Mlandizi na vitongoji vyake, Visiga, Misugusugu, Soga, Korogwe, Picha ya Ndege, Kwa Mathias, Tumbi, Mailimoja, Pangani, Kiluvya, Kibamba, Mloganzila, Mbezi kwa Yusufu, Mbezi Mwisho, Kimara, Kilungule, Mavurunza, Baruti, Kibo, Kibangu, Tabata, Segerea, Kinyerezi na Karakata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha za usambazaji maji katika bajeti 2017/2018 ili maeneo yote ya pembezoni mwa bomba kuu la Ruvu Juu, toka Mlandizi hadi Dar es Salaam umbali wa kilomita 12 yakiwemo maeneo ya Pangani, Lumumbana, Kidumu na Zugowale yapate huduma ya maji.

SPIKA: Mheshimiwa Muro nilikuona, swali la nyongeza.

MHE. MARY D. MURO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa miradi yote iliyojengwa katika Wilaya ya Kibaha Mjini iko chini ya viwango na imetokana na kwamba Wilaya ya Kibaha haina Mhandisi wa Maji anayetumika pale ni Mhandishi wa Mazingira. Je, ni lini Kibaha italetewa mtaalamu wa maji?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa ametaja kwamba Pangani iko miongoni mwa kata zitakazopata

maji, lakini Pangani ina mradi ambao umegharimu shilingi milioni 531 ambao umejengwa chini ya kiwango kwa mabomba kuunganishwa na moto badala ya *connector*. Je, yuko tayari kufuatana na mimi kwenda kujionea ubadhirifu uliofanyika? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Mhandisi Lwenge.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyotoa kuelezea mafanikio ya mtambo wa Ruvu Juu maana ndio lilikuwa swali la msingi, kuona kwamba maeneo yale ambayo mtambo ule umepitisha maji yanapata maji kwa sasa baada ya kuwa umekamilika. Haya maswali mawili anayoongezea ni tofauti na lile swali la msingi. Maswali anayoyauliza ni miradi inayotekelezwa na Halmashauri ya Kibaha.

Mheshimiwa Spika, hii ni sehemu nyingine lakini hata hivyo tutakupa majibu kwamba kama miradi ya Kibaha Mjini anasema yote imetekelezwa chini ya kiwango, hii ni kazi ambayo inabidi twende tukaiangalie, hatuwezi kuwa na jibu hapa, maana yake hatuelewi hilo. Mimi taarifa niliyonayo kwamba kazi zimefanyika lakini kama ni kweli iko chini ya kiwango tutakwenda kuliangalia.

Mheshimiwa Spika, pia huo mradi wa Pangani anaousema ana wasiwasi wa utekelezaji wake, nao naomba pia tupewe nafasi tutakwenda kuangalia na kama kuna tatizo tutachukua hatua kulingana na taratibu zetu za kusimamia miradi ya maji.

SPIKA: Nawaona lakini jinsi mlivyo wengi, lakini kwa historia ya maswali haya Mheshimiwa John Mnyika huwa hakosi swali la nyongeza. Mheshimiwa John Mnyika swali la nyongeza tafadhali.

MHE. MARY D. MURO: Mheshimiwa Spika, bado *Engineer* hajajibu swali langu.

SPIKA: Tuendelee Mheshimiwa John Mnyika swali la nyongeza.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Katika majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri amesema mradi wa Ruvu Juu umekamilika na kwamba maeneo ya ndani ya kilometa 12 kutoka bomba kuu yanapata maji hivi sasa na ameyataja maeneo ya Kibamba, Mbezi, Msigani na kwingineko ambayo yako ndani ya Jimbo la Kibamba. Ukweli ni kwamba ule mradi haujakamilika, yapo maeneo ambayo yana mabomba ya Mchina ambayo maji bado hayatoki.

Mheshimiwa Spika, napenda Mheshimiwa Naibu Waziri ajibu ukweli, kwa maeneo ambayo yana mabomba ya maji lakini maji hayatoki mpaka sasa, ni lini maji yatatoka kama anavyosema mradi umekamilika? Je, yuko tayari baada ya hapa twende tukakague huo mradi anaosema umekamilika lakini maji hayatoki?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, *Engineer* Lwenge majibu.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, tunaposema kwamba mradi umekamilika ni kwamba sasa maji yameanza kutoka na tumeanza kusambaza. Kwenye jibu la msingi tumeelezea kwamba tutakwenda kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Awamu ya kwanza tumeleza maeneo ambayo tayari yameanza kupata maji.

Mheshimiwa Spika, maeneo hayo anayosema ya mabomba ya Mchina ni sehemu ambayo maji yale yatakwenda. Yamechelewa kufika kwa wakati kwa sababu kulikuwa kuna tatizo la umeme pale Ruvu Juu. Sasa hivi tayari mitambo imeshawashwa na imeshajaribiwa tayari maji yameanza ku-*flow* mpaka tanki la Kibamba, kwa hiyo, tunaendelea kuunganisha. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge tutakwenda kuangalia hayo maeneo unayosema yana mabomba ya Mchina kwamba yameanza kupata maji au vipi lakini lengo letu ni maji yale yafike kule.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu sasa hivi kwa mitambo hii miwili, ya Ruvu Chini na Ruvu Juu tunazalisha lita milioni 466 kwa siku, ni maji mengi sana. Kwa hiyo, kazi yetu kubwa ni kuhakikisha kwamba mitandao ile ambayo ina mabomba inapata maji lakini maeneo mengine yale ambayo hayana mitandao, Serikali inaweka bajeti yake. Hata bajeti ambayo nitaisoma baada ya wiki moja nitaelezea mipango ambayo tumeiweka kwa ajili ya fedha za ndani kuweza kusambaza maji zaidi maeneo ambayo hayana mtandao.

SPIKA: Ahsante sana. Tunamalizia na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na swali la Mheshimiwa Raisa Abdallah Mussa.

Na. 84

Kuboresha Balozi za Tanzania

MHE. RAISA ABDALLAH MUSSA Aliuliza:-

Ofisi za Balozi za Tanzania hazipo katika hali nzuri na hii inatokana na ukosefu wa upatikanaji wa fedha ambazo zingewezesha kuimarisha Balozi hizi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha tatizo hili linapatiwa ufumbuzi wa haraka ili kuendana na maendeleo ya dunia?

SPIKA: Majibu ya swali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dkt. Susan Kolimba.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFIKA MASHARIKI Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Raisa Abdallah Mussa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuendelea kukarabati na kujenga majengo ya ofisi na makazi ya watumishi Balozi na imekuwa ikitekeleza jukumu hilo kwa kutumia fedha za bajeti ya maendeleo zinazopangwa kwa kila kipindi cha mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kupitia mpango wa Wizara wa miaka kumi na tano wa ujenzi, ununuzi na ukarabati wa majengo ya ofisi na makazi ya watumishi wa ubalozi ulioanza kutekelezwa mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara imefanikiwa kutekeleza miradi mbalimbali kwenye Balozi zetu kama vile kufanikisha ujenzi wa jengo la Ubalozini wa Tanzania - New Delhi (India); ununuzi wa jengo la Ofisi ya Ubalozini Tanzania - Washington D.C (Marekani); ununuzi wa jengo la Ofisi ya Ubalozini wa Tanzania - New York (Marekani); ununuzi wa jengo la Ofisi na makazi ya Balozi, Ubalozini wa Tanzania - Paris (Ufaransa); ukarabati wa makazi ya Balozi, Ubalozini wa Tanzania - Nairobi (Kenya) na ukarabati wa makazi ya Balozi, Ubalozini wa Tanzania - Tokyo (Japan).

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara itakamilisha ukarabati wa jengo la ghorofa tisa la ofisi na makazi lililopo Ubalozini wa Tanzania Maputo (Msumbiji); ukarabati wa makazi ya Balozi na nyumba za watumishi zilizopo Ubalozini wa Tanzania Stockholm (Sweden); na ukarabati wa jengo la Ofisi na makazi ya Ubalozini yaliyopo Khartoum (Sudan).

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Wizara inaandaa mpango mwingine wa miaka kumi na tano wa ujenzi, ununuzi na ukarabati wa majengo ya ofisi na makazi ya watumishi Ubalozini utakaoanza kutekelezwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya miradi itakayotekelezwa ni ukarabati wa jengo la ofisi na makazi ya watumishi kwenye Balozi za Tanzania Harare (Zimbabwe); Kampala (Uganda); Beijing (China); Pretoria (Afrika Kusini); na Cairo (Misri); ukarabati wa nyumba za Ubalozini zilizopo kwenye Ubalozini wa Tanzania Lilongwe (Malawi); Kinshasa (DRC); ukarabati wa jengo la zamani la Ofisi ya Ubalozini lililopo Washington DC; ukarabati wa miundombinu ya Chuo cha

Diplomasia kilichopo Kurasini na ujenzi wa Ubalozzi wa Tanzania - Addis Ababa (Ethiopia) na Ofisi ya Ubalozzi wa Tanzania - Muscat (Oman).

Mheshimiwa Spika, mikakati ya kutekeleza mpango huu ni kuendelea kutumia bajeti ya maendeleo ya Serikali, kuishirikisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kama vile Taasisi ya Miradi ya Maendeleo ya Miundombinu na kwa kutumia utaratibu wa karadha katika kutoa mikopo ya kutekeleza miradi ya maendeleo Ubalozini kwenye nchi za uwakilishi ambapo utaratibu huo unatumika.

SPIKA: Mheshimiwa Raisa swali la nyongeza.

MHE. RAISA ABDALLAH MUSSA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na mlolongo mrefu ambao majibu yake yamepatikana, Watanzania tunaona aibu majengo yetu yaliyopo nje pindi tukitembelea Ofisi za Mabalozzi. Kwa muonekano wa wazi kabisa ni kwamba bajeti hasa inayopangwa ambayo ameisema Mheshimiwa Naibu Waziri hapa ni kwamba haikidhi haja na kutotolewa kwa wakati ile bajeti yenyewe iliyopangwa. Swali la kwanza, je, Wizara haioni umuhimu ya kuachia mapato ya viza au vyanzo vingine vya mapato vinavyopatikana katika Balozi zetu wakaachiwa wenyewe kule Ubalozini ili wakashughulikia suala la kuziimarisha Balozi zetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, suala la uchakavu wa ofisi na majengo ni la muda mrefu. Mimi siyo Mbunge wa kwanza na wala hili si Bunge la kwanza kuulizwa masuala haya kuhusu Balozi zetu, lakini inaoneka kama tunababaishwa sasa hatupewi uhalisia ni upi.

Je, ni lini Serikali itaacha ubabaifu wa majukumu yake ya majengo haya ambayo sasa inaonesha uchakavu ni endelevu? *(Makofi)*

SPIKA: Hasa mnapiga makofi ubabaifu upi? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Nje majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, kuhusu Serikali kuachia ukusanyaji wa maduhuli kwa maana ya pesa zinazotokana na *visa* zitumike kule Ubalozini ili kufanya ukarabati katika Balozi zile zenye uchakavu wa majengo na kadhalika, nafikiri Mheshimiwa Mbunge pia ana uzoefu na Bunge hili linajua kwamba siku za nyuma maduhuli hayo yalikuwa yanaruhusiwa kutumika katika Balozi zetu. Hata hivyo, ilionekana kwamba zinapobakishwa pale baadhi ya Balozi zetu zilikuwa hazitumii vizuri maduhuli yale na utaratibu ule ukabadilishwa wakashauri urudishwe Serikalini.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi hatuwezi tukasema tunaweza tukaachia tu hivi hivi, suala hili sisi tulilipeleka tukalijadili na tumeona kwamba baadhi ya Balozi bado hazijawa na nidhamu ya matumizi mazuri ya maduhuli wanayokusanya katika Balozi husika. Lakini pale tutakapokuwa tumeona kwamba maduhuli au pesa wanazopelekewa wanatumia kwa utaratibu uliowekwa, basi sisi hatutasita kwa sababu tunachotaka ni kuhakikisha kwamba Balozi zetu zinakuwa katika hali nzuri na zinajenga taswira nzuri ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kwamba Serikali iache ubabaishaji, nafikiri Serikali haifanyi ubabaishaji. Ndiyo maana tumesema pamoja na kwamba tunaweka bajeti ya maendeleo ili iweze kutatua tatizo na changamoto ya ukarabati wa majengo yetu ambayo ni machakavu lakini tumesema pia kwamba kuna mpango kazi ambao tumeweka kwa utaratibu kwamba majengo tuliyonayo mangapi na yapi yamechakaa zaidi na yapi yaanze kutengenezwa. Serikali hata siku moja haitakuwa inatumia ubabaishaji katika kutekeleza kazi zake. Hilo tunamhakikishia Mheshimiwa kwamba tutalitekeleza ipasavyo. (*Makofi*)

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, swali la mwisho la nyongeza.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naibu Waziri ametaja miradi mingi *very*

ambitious lakini ukweli ni kwamba kwenye Balozi zetu kuna ukata sana kiasi kwamba kuna Balozi zinawakilisha nchi kadhaa, mfano Balozi wa Malaysia anawakilisha mpaka Singapore na Brunei, wa Msumbiji nadhani mpaka Swaziland lakini wanashindwa kutembelea nchi wanazoziwakilisha kwa sababu ya ukata kiasi kwamba hata Ubalozzi umekuwa sio *deal* tena.

Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri amezungumzia tu *infrastructure* lakini hawajazungumzia hali za Mabalozzi wenyewe na *staff*. Sasa Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba wanaboresha masuala ya kibajeti na kifedha kwenye Balozi zile ambazo zinawakilisha nchi kadhaa ili kutokuathiri mahusiano yetu ya kibalozi na zile nchi ambazo wanatakiwa hawa watu wakatuwakilisho?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, kwanza niseme tu kwamba mtu anapoteuliwa kwenye utumishi wa umma sio *deal* ni wajibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili kuhusu kusema kwamba tutakarabati sehemu mbalimbali na tumeweka miradi mingi lakini inaonekana baadhi ya Balozi zinasimamia nchi nyingi sana na kwamba kuna ukata. Sisi kama Serikali mipango yetu inatokana na ukusanyaji wa mapato ya kodi zilizoko ndani ya nchi husika. Kama Wizara, bajeti yetu inapangwa kutokana na ukomo wa bajeti tunaopewa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi tutakuwa tunahakikisha kwamba pesa tunazopewa na hata tunavyozigawa, hatugawi kwa aina moja kwa maana ya hela zinazofanana, inategemea Balozi anasimamia nchi ngapi na gharama za uendeshaji wa maisha katika nchi husika yakoje. Ndiyo maana unakuta katika mwaka huu wa fedha tumeanzisha Balozi nyingine sita ili kuhakikisha kwamba tunapunguza mzigo wa usimamizi wa Balozi kwa nchi husika.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Susan Kolimba.

Waheshimiwa Wabunge, muda hauko upande wetu, sasa tuendeleo na mambo mengine, nikianza na matangazo ya wageni walioko Bungeni. Tupo na wageni mbalimbali walioambatana na Mchungaji Getrude Rwakatare ambao wamemsindikiza katika kuapishwa kwake leo asubuhi, wakiongozwa na Mchungaji James Mwaipya kutoka Kanisa la Mikocheni, Mlima wa Moto. Mchungaji Mwaipya, pale ulipo, karibu sana. (*Makofi*)

Pia, wapo wanae wanne, wa Mheshimiwa Dkt. Getrude Rwakatare, Ndugu Kellen Rwakatare, Ndugu Humphrey Rwakatare, Ndugu Tibe Rwakatare na Ndugu Mutta Rwakatare, wote msimame. Hawa ni watoto wa Mheshimiwa Rwakatare. Karibuni sana na tunawashukuru kumsindikiza mama kuja hapa mjengoni. (*Makofi*)

Wageni wengine wote mliopo kwenye *galleries* mnakaribishwa sana hapa Bungeni, karibuni sana. (*Makofi*)

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, *Engineer* Atashasta Nditiye, anawaomba Wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii, mkutane saa 07.00 mchana, kutakuwa na Kikao cha Kamati katika Ukumbi wa *Utawala Annex, dispensary*.

Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club*, Mheshimiwa William Mganga Ngeleja kwa niaba ya wanachama wote wa *Bunge Sports Club* anaomba kuwatangazia wanamichezo wote kwamba kuwa mazoezi yameshaanza rasmi jana. Mazoezi haya yako kwenye viwanja vya Chuo cha Biashara (*CBE*) kwa michezo ya mpira wa miguu na *volleyball*. Kwa mpira wa pete (*netball*) mazoezi yao yatafanyika kwenye viwanja vya shule ya sekondari ya Dodoma.

Jumatano ijayo kutakuwa na mechi kati ya Bunge la Jamhuri ya Muungano na Baraza la Wawakilishi, ambayo tutawatangazia wakati utakapofika, kwa ajili ya Sherehe za

Kuadhimisha miaka 53 ya Muungano, ambapo michezo hiyo itafanyika hapa Dodoma kwenye viwanja vya Jamhuri. Kwa hiyo, naomba mazoezi haya Waheshimiwa tuhudhuri kwa sababu nimeshamhakikishia Spika wa Baraza la Wawakilishi kwamba watakapokuja hawa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwenye michezo hii watapigwa mabao mengi sana, kwa hiyo, mazoezi muhimu yanahitajika. *(Makofi/Kicheko)*

Pia nilipokea maombi hapa ya baadhi ya Wabunge wa mchezo wa *netball*, wanasema wanapendekeza kwamba siku moja ufanyike mchezo wa *netball* kati ya Wabunge wa Upinzani na Wabunge wa Chama Tawala. Kwa hesabu zangu za haraka haraka, Upinzani watafungwa sana, kwa hiyo, sijasuhusu hiyo mechi bado. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyowatangazia hapo kabla kesho tutakuwa na shughuli nzito na kubwa ya kumuaga mwenzetu, Marehemu Dkt. Elly Macha kwa taratibu zetu zile ambazo tumezizoea.

Kwa hiyo, ratiba yetu ya kesho itakuwa imevurugika kwa kiasi kikubwa lakini kwa sababu ya jambo hilo kubwa naomba wote tuipe ushirikiano Meza ili zoezi hilo la kesho liweze kwenda *uninterrupted*.

Kwa hiyo, leo tutajitahidi kabisa ili Hoja ya Serikali ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora tuweze kuimaliza. *(Makofi)*

Kwa hiyo, watakaopata nafasi ya kuchangia na wale ambao hamtapata nafasi mtuelewe hivyo kwamba ni kutokana na mazingira hayo inabidi twende hivyo.

Kwa jinsi hiyo leo miongozo sitaruhusu tutaenda nayo wakati mwingine. Kwa hiyo, tunaanza na uchangiaji, Katibu tuendeleo.

NDG. NENELWA M. WANKANGA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 - Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Majadiliano yanaendelea, naanza na upande wa CUF, Mheshimiwa Salma Mwassa atakuwa wa kwanza halafu tutafuatia CCM majina nitayataja baadaye.

MHE. SALMA M. MWASSA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na uhai. Vilevile napenda kukishukuru chama changu kwa kunipa nafasi ya kuendelea kuwepo katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nielekeze mchango wangu kwenye Wizara hii ya TAMISEMI. Wizara hii kwa kweli ndiyo nchi, ndiyo inayoangalia Taifa zima la Tanzania hasa kwa upande huu wa Bara. Kwanza kabisa, nijielekeze kwenye mpango mzima wa elimu. Katika hotuba ya Waziri wa TAMISEMI, ukurasa wa 23 unaongelea miundombinu. Kwa kweli bado miundombinu katika elimu yetu siyo mizuri kwani upungufu wa miundombinu ni mkubwa sana. Kwanza nijielekeze kwenye upungufu wa vyoo. Niliangalia kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri aliongelea kuhusu upungufu wa matundu ya vyoo....

SPIKA: Naomba wale wote mnaotoka mtoke bila kelele wala vurugu.

MHE. SALMA M. MWASSA: Upungufu wa vyoo kwa kweli bado ni tatizo kubwa. Sasa kama mpaka sasa hivi tunaongelea upungufu wa matundu 517,600 kwa ujumla wake lakini nikiangalia kabisa upungufu huu 50% upo katika

Mkoa wa Dar es Salaam kutokana na mlundikano mkubwa wa wanafunzi. Vilevile upungufu huu wa vyoo unafanya wanafunzi wetu kwanza wasome *in uncomfortable way* halafu vilevile unasababisha magonjwa makubwa hasa *UTI*. Sasa hivi *ratio* kwa Mkoa wa Dar es Salaam kwenye tundu moja inaenda kati ya wanafunzi 80 - 100 wanatumia tundu moja la choo katika shule zetu za msimngi. Sasa nijjulize, haya magonjwa kama ya *UTI* hasa kwa upande wa wanafunzi wa kike yataisha? Hayawezi kwisha. Tunatumia gharama kubwa sana za matibabu ya *UTI* na kusababisha watoto kutokusoma kabisa.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile niende kwenye vyumba vya madarasa, nako kuna upungufu wa takribani 200,000 na kwenye nyumba za walimu 182,000. Takwimu hizi bado ni kubwa sana, vyumba vya madarasa kwa sasa yaani ni *issue*. Huu mpango wa elimu bure umesababisha darasa moja sasa liwe na wanafunzi kati ya 200 - 400 hasa kwenye Mkoa wa Dar es Salaam. Mimi naomba kabisa Serikali ije na mkakati wa kupunguza huu uhaba wa madarasa hasa kwenye Mkoa wa Dar es Salaam na Tanzania nzima kwa ujumla, yaani itueleze kabisa itafanyaje? Kama haiwezekani basi Halmashauri zipewe uwezo yaani kusimamiwa ili zikope zianze utaratibu huu wa kujenga vyumba vya madarasa kama ilivyokuwa kwenye madawati. Madawati tumeona kabisa sasa hivi yameenda vizuri mpaka Bunge lenyewe limechangia madawati, basi sasa sera ya madarasa na matundu ya vyoo ianze upya, tuendeleo kabisa kusema kwamba, sasa hivi katika kila wilaya na mkoa lazima huu upungufu wa vyoo na vyumba vya madarasa uishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile niongelee uhaba wa walimu. Uhaba wa walimu bado ni tatizo hasa walimu wa hesabu na sayansi kwa ujumla. Kulikuwa na ile programu ya walimu kwenye Chuo Kikuu cha Dodoma, imeingiliwa, ikavurugwa vurugwa, hatuelewi walimu wale wanamaliza lini au wataajiriwa lini au itakuwaje. Kwa hiyo, uhaba wa walimu pia ni tatizo hasa katika upande wa masomo haya ya sayansi na hisabati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije kwenye masuala ya afya niongelee suala la kujenga Hospitali za Wilaya hasa kwenye wilaya hizi mpya. Kwanza tukiangalia kwenye Mkoa wa Dar es Salaam kuna tatizo kubwa la mlundikano wa wagonjwa hasa kwenye Hospitali za Mwananyamala, Ilala na Amana. Kuna hizi Wilaya mpya za Kigamboni na Ubungo ambazo mpaka sasa hazina hii huduma kabisa ya Hospitali ya Wilaya. Naomba Waziri wakati anapokuja kuhitimisha atueleze atajenga lini Hospitali za Wilaya kwenye hizi Wilaya mpya ikiwemo Ubungo na Kigamboni ziwe au zilizopo zipandishwe mfano Hospitali ya Mbezi.

Vilevile Hospitali za Ilala, Temeke, Mwananyamala zimepandishwa kwenda kwenye hadhi ya mkoa sasa Hospitali za Wilaya ziko wapi? Kwa hiyo, namuomba Waziri katika vipaumbele vyake kuwe na Hospitali za Wilaya kila wilaya na ziwe na vifaa vyote muhimu vya afya ikiwemo magari ya wagonjwa, *labor* zinazoeleweka, vifaa vya kujifungulia ili huduma za afya ziwe sahihi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije katika ujenzi wa majengo ya ofisi katika wilaya. Bado ofisi za wilaya hazina ule mwonekano wa majengo ya Wilaya hasa kwa wilaya mpya. Hivi inakuwaje unaigawa Wilaya halafu unaenda kukodi jengo kwenye majengo ya mtu binafsi? Basi hayo majengo ya watu binafsi yangukuwa angalau yana nafasi kubwa lakini sivyo. Sasa sasa hivi wilaya hizi zimekuwa kama kitu cha ajabu, hazina majengo yanayoeleweka hasa Wilaya mpya mfano Kigamboni au Ubungo. Unakuta chumba cha 10 kwa 10 kina idara zaidi ya tatu mpaka tano. Mkuu wa Idara yuko humo humo, wafanyakazi wa kawaida wako humo humo kwenye hicho chumba yaani ni vurumai hata mafaili huwezi kujua yanakaa wapi. Kwa hiyo, mimi naomba kabisa hasa kwenye hizi Wilaya mpya, kwa mfano Wilaya ya Ubungo na Kigamboni, Waziri anapokuja kuhitimishia atueleze majengo haya yatajengwa lini na kama anaendelea kukodi atakodi kwa muda gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niongelee maslahi ya watumshi. Kwa kweli maslahi ya watumishi katika ngazi

ya utumishi wa umma kwa kweli bado ni tatizo. Mishahara ni midogo, mmeendelea kupunguza posho, zingine mmeziondoa kabisa, stahiki kwa viongozi pia hazieleweki. Mnasema kwamba mnakuja kuleta uwiano wa mishahara kwa kuangalia ile mikubwa na kima cha chini, lakini sasa mbona huu mshahara wa kima cha chini hauangaliwi kabisa? Kwa muda mrefu mshahara wa kima cha chini umekuwa mdogo sana. Wafanyakazi wa umma sasa imekuwa taabu yaani wanafanya kazi kwa mshahara mdogo, hawapandishwi madaraja yaani *totally* wamekuwa *confused*, wamekata tamaa hata ya kuwa watumishi wa umma. Madaraja yao hawapandishwi mnasema sasa hivi kwanza tunahakiki, lakini kuhakiki kunazuia mtu kupanda daraja? Inakuwaje mtu miaka mitatu hupandi daraja? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe hapa ni *declare interest* nilikuwa mtumishi wa umma, nimekaa miaka karibu mitatu sijapandishwa. Naomba suala hili liangaliwe upya. Mtu mpandishe cheo kutokana na elimu yake na anavyoweza kufanya kazi. Bila kumpandisha madaraja hii *motive* ya kufanya kazi mtu ataipata wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile pia tuangalie mishahara yao bado ni midogo mno. Halafu posho zao nyingi mmezikata yaani hazieleweki. Kama mnakata posho basi muangalie ule uwezekano na maisha halisi ya mtumishi wa umma inakuwaje. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, vilevile kumekuwa na mlundikano wa kazi kwenye ofisi hizi za umma kutokana na kutoajiri watu. Vijana wamejaa huko mtaani hawaajiriwi na kazi zimerundikana huku. Hawa watu mmewaondolea hata posho za mazingira magumu lakini mlundikano wa kazi umezidi kwenye ofisi za umma kwa idara zote hasa Halmashauri yaani unakuta kazi ya watu 10 anafanya mtu mmoja. Vilevile *overtime*, *extra-duty allowance*, zote zimeondolewa huyu mtu anafanyaje kazi? Kwa hiyo, naomba kabisa muangalie tena suala hili. (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Salma Mwassa.

MHE. SALMA M. MWASSA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mchangiaji atakayefuata atakuwa Mheshimiwa Anne Kilango Malecela lakini kabla hujaanza kuchangia, naomba nimpishe Mwenyekiti, Mheshimiwa Andrew Chenge.

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge, hizi Wizara mbili ni muhimu sana hebu kila mtu atumie dakika kumi vizuri zaidi kuliko kuzipoteza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niseme mimi nimekuwepo Bungeni hapa tangu mwaka 2000. Suala nitakaloliongea leo nimeliongea tangu mwaka 2001, naongelea upande wa TAMISEMI. Wilaya ya Same ni kubwa sana katika Mkoa wa Kilimanjaro. Mkoa wa Kilimanjaro una Wilaya saba lakini Wilaya ya Same ina ukubwa wa kilomita za mraba 5,152 ambazo ni sawa na asilimia 40 ya Mkoa mzima wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Same hiyo ina majimbo mawili, Same Magharibi na Same Mashariki. Makao Makuu ya Wilaya yako Same Magharibi yako katika Kata ya Same ambayo ndiyo ya mwisho unakwenda Wilaya ya Mwangi. Jimbo la Same Mashariki liko mwishoni na Mkoa wa Tanga. Kata ya kwanza inaanza Bendera, Kiurio, Ndungu, Kalemawe, Maore hapa ni tambarare. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo linapojitokeza ni hapa. Tunapata tatizo kwamba Hospitali ya Wilaya ya Same iko, Kata ya Same ambako ni mbali sana na Jimbo la Same Mashariki. Kwa hiyo, athari kubwa inawakuta kina mama wajawazito, hili suala nimeliongelea kwa miaka 15. Kina mama wengi sana kutoka Jimbo la Same Mashariki wanapohitaji huduma ya upasuaji dakika za mwisho anataka kujifungua anagunduliwa kwamba upasuaji unahitajika ni lazima apelekwe Same, wengi sana wanapoteza maisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia 2010-2015 tumepoteza akina mama 18 na watoto wao. Hao ni wale waliofika Same. Walioipotezea maisha majumbani au kwenye zahanati sina takwimu za kusema. Watoto wachanga 28 wamepoteza maisha. Namshukuru sana Mheshimiwa Jafo alikuja Wilaya ya Same. Wabunge hatukuwa na habari tungekuja tukulalamikie kule kule, lakini mimi kwa sababu nimesema kwa miaka 15 naiomba sasa TAMISEMI ione umuhimu wa hapa Ndungu ndani ya Jimbo la Same Mashariki kwenye Makao Makuu ya Jimbo la Same Mashariki, kile kituo cha afya kipate huduma ya upasuaji. Inapokuja kuzungumzia akina mama nitapaza sauti mpaka dakika ya mwisho. Jimbo la Same Mashariki akina mama wanapoteza maisha sana kwa sababu ya kukosa huduma ya upasuaji. Kipare tunasema; *“wekienda kutana na nashindaki taganyamaa.”* Naomba nitafsiri, wewe kama umebeba nyama kichwani nzi watakufuata. Sasa kama unataka wale nzi wasikufuate hiyo nyama itupe. Hili suala ili nisilipigie makelele Serikali malizeni hili jambo, hamtanisikia tena nikisema. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapo nimetoka TAMISEMI nije Wizara ya Utumishi na Utawala Bora. Mimi nazungumzia Mfuko wa Rais wa Kujitegemea. Huu Mfuko wa Rais wa Kujitegemea umeanza takribani miaka 33 iliyopita. Mimi nimeungalia vizuri Waheshimiwa Wabunge, huu mfuko unawasaidia akina mama na vijana wanapata mahali pa kukopea kwa ajali ya miradi midogo dogo ya kujiendeleza ili waweze kujitengemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku duniani, nizungumzie Tanzania na Afrika akina mama pamoja na vijana ni wazalishaji wakubwa sana na mjue akina mama ndiyo wanaoangalia vijana, sijui mmenielewa? Kwa hiyo, mama anacheza kotekote anazalisha na anaangalia vijana. Huu Mfuko wa Rais wa Kujitegemea takribani miaka 33 sasa hivi lakini umeonyesha kufanya vizuri sana. Kwa sababu gani nasema hivyo Mwenyekiti? Inapokuja kwenye marejesho hawa wanarejesho asilimia mia moja hakuna matatizo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili naomba nizungumze kwa unyenyekevu. Kwanza tuwapongeze wanaoratibu mfuko huu kwa sababu mahali popote ambapo kuna kukopa kurejesho kuna matatizo, lakini hawa wanarejesho asilimia 100 ina maana wanaoratibu mfuko huu wanafanya kazi vizuri sana. Hata hivyo, kuna changamoto kwamba Serikali haiwapi pesa za kutosha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo huu Mfuko wa Rais wa Kujitegemea inapokuja kwenye *repayment* ni 100% jamani kwa nini wasipewe fedha za kutosha? Kazi wanayoifanya inawasaidia akina mama na vijana kwa hiyo moja kwa moja inachangia kwenye uchumi. Naiomba Serikali mfuko huu uangaliwe vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo hapo tu, tangu 33 iliyopita mfuko huu uko kwenye Mikoa mitano tu ya Dar es Salaam, Lindi, Njombe na mwingine wa tano mniwie radhi nimeusahau. Ombi langu kwa unyenyekevu mkubwa, Mheshimiwa Waziri wa Utumishi naomba unisikilize, kwa sababu marejesho ni 100% hebu sasa ongezeni mikoa mingine mitano. Katika hiyo mikoa mitano itakayoongezwa naomba Mkoa wa Kilimanjaro uwepo. Ukienda Same Magharibi akina mama wa Ruvu wanalima vitunguu wakipata mikopo watafanya kazi vizuri. Ukija Same Mashariki kuna akina mama wanaolima tangawizi na mpunga wakipata mikopo hiyo watafanya kazi vizuri zaidi. Naomba iongezwe mikoa mingine mitano na huu mfuko upewe pesa za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Hassan Masala atafuatiwa na Mheshimiwa Flatei Massay na Mheshimiwa Aisharose Matembe ajiandae. Mheshimiwa Masala

WABUNGE FULANI: Hayupo.

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Flatei.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru kwa kupata nafasi hii. Mchango wangu unaanza na sifa. Kwa sisi tunaoabudu na tunaosali kwa Kikristo ukitaka kuomba lazima kwanza uanze na nyimbo za sifa ili Mungu au Bwana wetu Yesu Kristo afahamu kwa kweli unamsifu ili akupe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwanza naanza pia kwa kumpongeza Rais wetu kwa kazi anayoifanya katika Serikali hii ya Awamu ya Tano. Pia nawapongeza Mawaziri wote lakini kubwa nimpongeze Naibu Waziri wa TAMISEMI kwa sababu kwanza amefika kwenye Wilaya yangu na kutatua kero za wafanyakazi zilizoko ndani ya Halmashauri ya Mbulu Vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto ambazo zipo katika maeneo mengi hasa TAMISEMI ninao mchango mdogo ambao napenda kuuzungumzia leo. Serikali za Mitaa ilipaswa kukusanya mapato takribani shilingi milioni 332 lakini kwa bahati mbaya imekusanya shilingi milioni 232, ni sawa na asilimia 70. Ushauri wangu wa kweli katika kukusanya mapato ni vema sasa Wizara ikaelekeza msukumo kwa Maafisa Maduuli ili kutumia mashine za *EFD* kukusanya mapato ambayo itasaidia Halmashauri zetu kuongeza mapato yanayoonekana kabisa. Kwa sababu *research* inaonyesha Halmashauri chache hazitumii mashine kukusanya mapato ya ndani. Kwa hiyo, niombe Wizara hii iweze kupeleka moja kwa moja nguvu zake na kuwashauri

Maafisa Maduuli kusaidia ukusanyaji wa mapato ili Halmashauri zetu ziweze kujiendesha vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine tunazo ahadi ambazo zimewekwa katika maeneo yetu ya Miji Midogo. Kwa mfano Mbulu Vijijini tuna ahadi ya Mheshimiwa Rais na naamini sasa kutokana na *Road Fund* mnaweza kutusaidia ahadi ya kilometa tano ya lami iliyowekwa katika Mji Mdogo wa Hyadom. Nafikiri Mheshimiwa Jafo umefika na umepata maswali ya ndugu zetu wananchi wa pale ambao wametaka ile ahadi walau itekelezwe ili mji ule upate sifa hata ya kuwa na lami na kilometa mbili za Ndongobesh. Pia nafikiri umeonana na wananchi wa Dongobesh waliokulilia hasa ule mradi wa maji umaliziwe tu, imebaki hela kidogo shilingi milioni 600. Baada ya kushukuru kwa kutupa shilingi bilioni 1.8 malizieni basi ule mtaro ili maji yawezekwenda na wananchi wafaidike katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema nimesifu mapema ili ujue kwa kweli nahitaji kuomba. Kwa kweli maji ndiyo msingi hasa wa maendeleo ya wananchi wetu hasa kwenye kilimo. Katika haya basi mtusaidie kwa sababu Serikali imeshawekeza hela ya kutosha bado tu eneo dogo la kuweka mtaro wa maji kwenda kwa watumiaji ili kilimo kianze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao viongozi wetu wengine wanaotusaidia kwenye kazi kwa mfano Wenyeviti wa Vitongoji, Wenyeviti wa Vijiji na Madiwani. Madiwani wako wenzangu wamezungumzia sana kwamba posho yao ni ndogo na wanasimamia miradi mikubwa ambapo kimsingi wanafanya kazi nzuri sana. Niombe leo TAMISEMI waangalie namna nzuri ya kuwasaidia Madiwani hawa kwa kuwapandishia posho yao kidogo ili angalau wafanye kazi inayotakiwa kikamilifu kwa kusimamia Serikali za Mitaa hasa kwenye Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia vijiji vyetu, Wenyeviti wa Vijiji wanafanya kazi nzuri sana lakini bahati mbaya sana hawana hata posho. Kama inashindikana

kuwalipa kwa muda wote wapatieni basi bakshishi kwa muda fulani wafurahi na waone Serikali yao inawajali. Hata ndugu zetu Wenyeviti wa Mitaa na Vitongoji naomba muone namna ya kuwasaidia katika mapato yetu ya ndani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo tatizo hasa katika Wizara ya Utumishi. Namuomba sana dada yangu anisaidie hasa tatizo la upungufu wa watumishi. Halmashauri yangu inakabiliwa na upungufu mkubwa wa watumishi lakini pia tuna Wakuu wa Idara ambao wanakaimu kwa muda mrefu sana. Zaidi ya 80% ya Wakuu wa Idara wa Mbulu Vijijini kwenye Halmshauri yangu wanakaimu. Niombe basi wapandishwe washikilie hayo madaraka nao waone kwamba Serikali yao inawajali maana wamekaa kwa muda mrefu hawajui waende mbele au warudi nyuma. Mheshimiwa Waziri naamini wewe ni makini na unasikiliza haya, angalia Mbulu Vijijini kwa namna ya pekee sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara pia iangalie, tumeshafanya mabadiliko ya Sheria ya Manunuzi lakini kuna sintofahamu ya kutumia *force account* kwenye Halmashauri. Naomba basi Wizara isaidie na ije na kanuni ya kutumia ile *force account* ili watumishi waelewe namna ya kuitumia na kupunguza gharama ya miradi katika maeneo yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nishukuru katika ajira mmetusaidia kwa kutupatia walimu wachache wa sayansi. Sisi tuna upungufu mkubwa sana wa walimu katika maeneo yetu. Niombe basi wakati ujao ajira za walimu hasa wa sayansi ziongezeke, lakini pia tunaomba ajira ziongezeke kwa Watendaji wa Vijiji na Watendaji wa Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi umetoka maelekezo na waraka kuwaelekeza Wakurugenzi wawaondoe walimu katika kukaimu nafasi za kata na vijiji. Wananchi wetu sasa wameamua kuwaweka watu ambao wanawalipa wenyewe ili wasaidie kuzikaimu nafasi hizi za Watendaji wa Kata na Vijiji. Naomba Wizara iangalie namna gani ya kuajiri Watendaji hawa wa Kata na Vijiji. Wako watu

wamemaliza shule na wana weledi wa kufanya kazi hizi hasa katika maendeleo ya jamii. Ni vigumu sasa kusaidia wananchi kwa sababu wale wanaoshika nafasi hizi hawana ule weledi wa kutoka. Kwa sababu Serikali za Vijiji ndiyo zinawalipa kwa hiyo wanaajiri mtu yeyote tu wanaoona anafaa na anakaa pale ofisi walau kufungua na kufunga kwa hiyo hawezi kuwasaidia wananchi katika kuibua miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako Maafisa Maendeleo ya Jamii wengi sana wamemaliza vyo wako vijijini, Wizara iangalie tu namna ya kuwaajiri. Maana Serikali huku juu mnafanya kazi nzuri hapa katikati kwa Wakuu wa Mikoa vizuri, kwa Wakuu wa Wilaya vizuri, kwa Wakurugenzi vizuri, Wakuu wa Idara vizuri, kule vijijini wanakaimu watu wa kaiwada tu, tusaidieni basi tuleteeni wataalam ambao wataweza kufanya kaz kwa kuajiriwa na kuibua miradi, maana sasa hivi miradi inatoka juu inakuja chini. Kwa mimi niliyesoma Maendeleo ya Jamii wanasema *top-down* inatakiwa iwe *bottom-up* yaani miradi itoke chini kwa wananchi ili walau wao wenyewe waweze kujipangia miradi yao na waone miradi hii ni ya kwao na waiendeleze na wananchi wanaweza kufanya kazi hii kwa uhakika zaidi. Kwa hiyo, nilitaka niyaseme haya ili walau Serikali isaidie katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa naomba nizungumzie habari ya mikopo ya vijana na wanawake. Katika Halmashauri zetu zile asilimia tano, tano kufikia asilimia kumi ni vigumu kutekelezeka kwa sababu hii. Fedha zinazoenda kwenye Halmashauri kama *OC* haziendi kwa wakati au haziendi kabisa. Kwa hiyo, Mkurugenzi anaona kuliko undeshaji wa Halmashauri ukwame anatumia zile fedha za mikopo ya vijana ambayo anatakiwa itoke kwa mujibu wa kanuni. Hawezi kutoa kwa sababu hana fedha za kutumia, kwa hiyo basi anakwenda kutumia zile fedha za mikopo ya vijana. Naomba Serikali ijitahidi kupeleka fedha walau fedha hizo ziweze kwenda...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Aisharose Matembe atafuatiwa na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi na Mheshimiwa Hasna Mwilima ajandae.

MHE. AISHAROSE N. MATEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na neema kwa kutujalia uzima na afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumpongeza sana Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Simbachawene, lakini pia na Naibu wake Mheshimiwa Jafo pamoja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa Angellah Kairuki. Napenda kuwapa moyo mnanfanya kazi nzuri, endeleeni na moyo huo huo na kazeni buti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo moja kwa moja nijielekeze kwenye hoja iliyoopo mezani nikianza na suala la elimu bure. Napenda kuipongeza Serikali kwa mafanikio makubwa waliyoyapata kwa muda mfupi kwa kutoa elimu bure. Jambo hili limejidhirisha wazi, kwa mwaka 2017 jumla ya wanafunzi milioni 3.8 wa darasa la awali na la kwanza waliweza kuandikishwa. Uandikishaji huo ni sawa na ongezeko la wanafunzi 300,000 ambao waliweza kuandikishwa kwa mwaka 2016. Ongezeko hilo limechangiwa na wazazi wengi kuhamasika na Waraka wa Elimu Bure na kupeleka watoto wao shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini elimu bure imekuja na changamoto zake zikiwepo uhaba wa madawati, vyumba vya walimu, vyumba vya madarasa, upungufu wa walimu na matundu ya vyoo. Mfano kwa Mkoa wa Singida kuna upungufu wa madarasa 5,547 na nyumba za walimu 5,580. Idadi hii ni kubwa sana ambapo kwa bajeti zilizotengwa

katika Halmashauri zetu haziwezi kukamilisha ujenzi wa miundombinu kwa kukarabati shule zetu zilizoko vijijni na hata zilezilozengwa chini ya mpango wa *MMEM* /na *MMEM II*. Hali ni mbaya na hasa kwa shule zetu zilizopo vijijini ambazo hazimfanyi mwalimu kufundisha kwa utulivu, lakini vilevile hazimfanyi mwanafunzi kupokea kile anachofundishwa na mwalimu. Bila mazingira bora ya kufundishia hakuna elimu bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwa Wilaya ya Ikungi tu pekee, ina uhaba wa shule 568 na upungufu wa walimu 490, vilevile ina uhaba wa vyumba vya madarasa 568. Hivyo, naiomba Serikali yangu sikivu kuangalia mpango mahususi ambao utawezesha ujenzi wa miundombinu hii ya elimu kukamilika, lakini pia kuboresha mazingira ya kufundishia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuweza kujenga maabara 5,562, lakini ni ukweli usiopingika, miundombinu ya maabara zetu bado hazijakaa vizuri na hasa maabara zilizopo katika Mkoa wangu wa Singida. Naishauri Serikali kukamilisha miundombinu hiyo kwa haraka iwezekanavyo ili kuwawezesha wanafunzi hao kujifunza masomo ya sayansi kwa vitendo, lakini pia kwa ukamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda, bila ya kuwandaa wanafunzi wetu kuwa wanasayansi, ni vipi tutayafikia malengo yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka kuchangia ni suala la watumishi wa umma. Wapo madaktari na wauguzi ambao wanatazama afya za Watanzania, lakini pia wapo walimu ambao pia ndiyo msingi wa maendeleo kwa kwa Taifa letu. Bila elimu bora hakuna maendeleo na bila walimu bora hakuna mambo yatakayoweza kufanyika kwa weledi, ujuzi na ufanisi. Watumishi hawa wamekuwa wakifanya kazi kubwa na ngumu na bado maslahi na stahiki zao zimekuwa ni ndogo sana ukilinganisha na kazi wanazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kuchangia na ninaona siyo zuri pia kwa watumishi, ni watumishi wengi kutokupandishwa madaraja kwa wakati. Jambo hili linawavunja sana moyo watumishi wa umma. Ninatambua kwamba zoezi la uhakiki wa watumishi wa umma limekamilika, hivyo basi ni wakati muafaka wa kuwapa watumishi wetu kile kinachostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la afya. Sera ya Afya ya mwaka 2007 imehitaji kila kijiji kuwa na zahanati moja, lakini katika Wilaya ya Singida ambayo ina kata 21 kuna zahanati 26 tu ambazo hazikidhi mahitaji ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile zahanati zilizopo zina upungufu mkubwa wa vifaa tiba lakini pia na wataalamu. Jambo hili linasababisha msongamano sana katika hospitali zetu za Wilaya, lakini pia vilevile msongamano katika hospitali yetu ya rufaa ya Mkoa wa Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali inakuwa ni mbaya zaidi pale mama mjamzito anapohitaji huduma ya afya katika zahanati zetu ambapo hakuna huduma za upasuaji, hakuna *theatre*, hakuna huduma za damu safi na salama. Unategemea mama mjamzito aende wapi iwapo atakumbwa na kadhia hii ya kwenda kujifungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kuchangia ucheleweshaji wa fedha za miradi ya maendeleo. Nakubaliana na mfumo wa Serikali kwamba baadhi ya mapato kuingizwa moja kwa moja kwenye mfuko wa Serikali Kuu na naipongeza sana Serikali, lakini mfumo huu una changamoto zake. Moja ya changamoto ni kusababisha baadhi ya Halmashauri kutokutekeleza majukumu yake kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua hapo awali kabla ya kutumika kwa mfumo huu kulikuwa na mianya mingi ya rushwa na upotezaji wa fedha za umma, lakini kwa sasa

hali ya fedha za miradi ya maendeleo zitoke kwa wakati ili kusaidia kuharakisha upatikanaji wa huduma kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni kuhusu Madiwani wetu. Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia wamechangia kuhusu Madiwani. Madiwani wanafanya kazi ngumu; wa ndio kiungo kati ya Wabunge na wananchi. Tunapokuwa huku Bungeni kufanya shughuli zetu, wenyewe wanakuwa karibu na wananchi. Hivyo, naomba Serikali iangalie Madiwani wetu na Wenyeviti wa Vijiji kwa jicho pana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, atafatiwa na Mheshimiwa Hasna Mwilima na Mheshimiwa Doto Biteko ajiandae.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na mwingi wa utukufu, kwa kunijalia uzima siku hii ya leo na hatimaye kuweza kusimama hapa ili nami niweze kuchangia Bajeti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma vizuri Bajeti ya TAMISEMI, ni nzuri sana. Ukiisoma inaleta raha, ambayo kimsingi Wizara hii inahitaji pesa takribani shilingi trilioni 6.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mwaka huu wa fedha tunaokwenda 2017/2018 baada ya kuwa Bajeti ya msimu uliopita imetekelezwa kwa asilimia 75.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kabisa changamoto kwa msimu uliopita zilikuwa nyingi, basi Wizara hii ijipange vizuri kuhakikisha kwamba bajeti hii inayokuja sasa iweze kutekelezeka kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye asilimia 10 za vijana na wanawake ambazo zinatolewa kutokana na mapato ya ndani ya Halimashauri zetu kwenye maeneo mbalimbali hasa kwa Mkoa wetu wa Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Mjumbe wa Kamati ya LAAC, ambaye nimekuwa nikiona kwa macho yangu mwenyewe namna gani jambo hili linatekelezwa kwenye Halmashauri mbalimbali. Jambo hili limechukuliwa tu kama ni jambo ambalo siyo muhimu sana kwa sababu bado halijatanguliwa sheria; likitungiwa sheria mahususi itasaidia hawa Wakurugenzi kuona kwamba ni muhimu na watalitekeleza kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hivyo naipongeza sana Kamati ya LAAC lakini pia na CAG ambaye anatusaidia kukagua hayo mahesabu na kuona hali halisi. Kamati hii imesimamia vizuri na sasa hivi Halmashauri zote zimeanza kupeleka pesa asilimia tano kwa vijana na asilimia tano kwa wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Wakurugenzi wote ambao wameanza kutekeleza jambo hili na ninaomba waendeleo kufanya hivyo na wale wote wanaopewa fedha hizo wasidhani kama ni zawadi, basi hii ni kama *Revolving Fund*, inatakiwa ipelekwe kwa wengine na wengine waweze kufaidi baada ya wengine kurejesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye posho za Madiwani. Waheshimiwa Wabunge wenzangu pia wamesema kwamba Madiwani ndio wale ambao wanafanya kazi hasa moja kwa moja kwa wananchi na sisi tukiwa wakati mwingine tunatekeleza majukumu yetu katika vikao mbalimbali vya Bunge, nao siku zote wamekuwa na wananchi; wakiamka asubuhi wapo na wananchi majumbani kwao. Sisi wakati mwingine tunaweza tukasema, nimesafiri nimeenda huku, lakini wao wanafanya kazi moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilidhani Serikali yetu ione uhumimu wa kuwaongezea posho Waheshimiwa Madiwani. Wizara hii ya TAMISEMI, tafadhali sana, naomba hata kama kuna sheria au kanuni basi ziletwe hapa Bungeni tuzirekebishe ili nao waweze kufanya kazi wakiwa wakiwa na mori mzuri ambapo kimsingi watakuwa wamewezeshwa vizuri lakini pia waweze kupatiwa vitendea kazi kwa maana ya usafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yao ya utawala wakati mwingine unakuta Madiwani wengine wapo vijijini, anatembelea vijiji karibu vinne au vitano; ataenda kwa baiskeli au kwa mguu. Basi Serikali ione umuhimu wa kuwatafutia hata magari ili waweze kufanya kazi zao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika TAMISEMI pia kwa masikitiko makubwa sana, bado Wizara hii ya TAMISEMI na Utawala Bora pia niseme hamjaona umuhimu wa Mbunge Viti Maalum. Mbunge wa Viti Maalum anafanya kazi kubwa sana. Eneo lake la utawala ni la Mkoa mzima, lakini bado kwa mujibu wa kanuni, Mbunge wa Viti Maalum yeye ni Diwani wa Halmashauri anayotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza, Mbunge huyu hawezi kuingia kwenye Kamati ya Fedha na kuweza kuona changamoto zinazowakabili wanawake, wanatengewa fedha kiasi gani ili ziweze kuwafikia. Nani anawasemea huko ilihali sisi Wabunge wa Viti Maalum ndio tupo kwa mujibu ili kuwasemea wanawake wenzetu, lakini kwenye Kamati za Fedha hatuingii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ya Utawala Bora, muone umuhimu wa kufanya hili na TAMISEMI pia tunataka Wabunge wanawake waingie humo na wanawake Madiwani wa Viti Maalum waingie humo ili waweze kuwasemea wanawake wenzao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwa walimu. Katika Mkoa wangu wa Ruvuma, walimu wanapata shida sana,

wanafanya kazi kubwa sana ya kuhakikisha mtoto ambaye hajui 'a' wala 'be' anafikia mahali ambapo anaweza kusoma na kuandika. Hii kazi ni kubwa sana.

Hata wewe Mheshimiwa Waziri ulioko hapa, nawe ulianza a, be, che. Kwa hiyo, kumbuka, kama mwalimu yule asingeweza kukufundisha akawa na mazingira mazuri, ni wazi kwamba wewe usingefikia hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Wizara ione umuhimu wa walimu kuwezeshwa wakawa na mazingira mazuri ya kufanyia kazi. Pia walimu wangu wa Mkoa wa Ruvuma wote katika Wilaya zote, nikianza na Nyasa, Mbinga, Tunduru, Namtumbo, Songea Vijijini na Songea Mjini hawa wote wana madeni. Madeni yao yanafikia takribani shilingi bilioni tatu. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind-up* aniambie hawa walimu wanalipwaje hizo pesa zao? Mimi na wewe tutakuwa sambamba, vinginevyo Mheshimiwa Waziri nitakama shilingi ya mshahara wako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende sasa kwenye shule za sekondari. Kuna shule za sekondari zinazoanza katika Wilaya ya Namtumbo, ndiyo zinaanza kidato cha tano. Shule hizi zimetelekezwa, hazipelekewi fedha kwa ajili ya mahitaji mbalimbali katika shule hizo ni Nanungu sekondari iliyoko katika Wilaya ya Namtumbo pamoja na shule ambayo inayoitwa Pamoja sekondari, shule ya Namabengo na shule ya Nasuri. Shule hizi zimetelekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri wa TAMISEMI, tena bahati nzuri Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI tulienda wote katika shule ya Nasuri katika Kata ya Namtumbo, ulishuhudia pale, lakini wale watoto uliwaona wameng'aa kwa uso, lakini ndani yake hawana huduma za mzingi. Naomba tafadhali utakapokuja, uniambie hawa watoto wanapataje huduma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la utawala bora. Nachukua nafasi hii kumpongeza sana

Mheshimiwa Rais wangu wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania; na hili nitalisema wazi wazi na nitatembea kifua mbele nikilisema. Mimi kama Mbunge wa Chama cha Mapinduzi, nataka niwaambie kwamba Mheshimiwa Rais wangu anafanya anafanya kazi nzuri. Ninacho cha kusemea ninaposimama hapa, kwamba ameweza kudhibiti mianya ya rushwa; lakini pia ameweza kupambana na madawa ya kulevya; amerudisha nidhamu kwa watumishi wa umma; bado ameweza kusimamia na kudhibiri matumizi ya fedha katika nchi yetu. *(Makofi)*

Ndugu zangu, kwa wale wote wanaoitakia mema nchi hii ni lazima watasema kwenye jambo hili. Tunaweza tukasema wakati wowote ule kwa sababu tunajua kwamba Rais wetu anatekeleza na anasimamia vizuri ilani, licha ya shughuli nyingi anazokuwa anazifanya ikiwepo pamoja na ndege ambazo zimekuja. Nchi hii ilikuwa haina ndege, ni nchi iliyokuwa inatia aibu, lakini kwa kipindi kifupi cha mwaka mmoja na nusu, tayari tumeona ndege, usafiri wa anga unakwenda barabara. Maeneo mbalimbali viwanja vinaendelea kurekebishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili mimi nitalisema tena kwa kifua mbele. Wale wanaochukia na wajinyonge tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, Mheshimiwa Rais wangu wa Jamhuri ya Muungano, kwa haya aliyoyafanya ya kuweza kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya na mengine, ni lazima...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MBUNGE FULANI: Malizia.

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Msemaji wetu anayefuata ni Mheshimiwa Hasna Mwilima, Mheshimiwa Doto Biteko na Mheshimiwa Subira Mgalu ajiandae.

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema ya kuweza kusimama hapa kuchangia kwenye Wizara hizi mbili; kwenye mwelekeo wa bajeti inayokuja mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Wizara ya TAMISEMI. Kumekuwa na changamoto kubwa sana kwenye Wilaya 19 zilizoanzishwa hapa nchini ikiwemo Wilaya ya Uvinza. Ninavyoongea, tangu Wilaya ya Uvinza ianzishwe, haina Hospitali ya Wilaya. Tunatambua kabisa kwamba Wizara ya TAMISEMI ni Wizara mtambuka, ndiyo inayosimamia masula yote ya Halmashauri zote nchini. Sasa namwomba sana Mheshimiwa sana Waziri, akiungana na Naibu wake waone ni jinsi gani wanaweza kutupitishia maombi. Tumeleta barua ya maombi kwenye maombi maalum, shilingi bilioni mbili; tunaomba hizo shilingi bilioni mbili tupewe ili tuweze kujenga hospitali na tayari tumetenga eneo la ujenzi, ekari 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ukipitia kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri, ya mwelekeo ya mapato na matumizi ya bajeti ya 2017/2018, ukurasa wa 103 utaona kwamba kwenye Mfuko wa Pamoja wa Afya, Halmashauri ya Uvinza haijapangiwa hata shilingi moja. Tuna Halmashauri takriban tisa, lakini tuna Majimbo manane. Kati ya Majimbo hayo, ni Jimbo moja tu ndilo linaloongozwa na mwanamke. Sasa ninaanza kupata shida na msemaji mmoja aliongea juzi ndugu yangu Mheshimiwa Chikambo kwamba Wizara inaongozwa na wanaume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwanamke, yaani Halmashauri zote zitengewe pesa kwenye Mfuko wa Pamoja wa Afya, Halimashauri yangu ya Uvinza isitengewe hata thumni, kulikoni? Mheshimiwa Waziri nazungumzia kwenye pesa zile za nje za *forex*; sina hata thumni, nimejisikia vibaya

sana. Nimeangalia kwenye ule ukurasa, nikanyong'onyea, nikasema kulikoni? Ila sina mashaka, Mheshimiwa Simbachawene ni jirani yangu, nadhani utaliangalia hili na utarekebisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kwenye ukurasa huo huo kwenye pesa za lishe na ulinzi wa mtoto, sina hata thumni. Wakati Halmashauri yangu ya Mkoa wa Kigoma inapitisha bajeti, Hazina ilikubali kututengea pesa; nasi tuna watoto 86,388 ambao wapo chini ya umri wa miaka mitano. Sasa ninashangaa, Hazina wamekubali kutuwekea shilingi 86,388,000 lakini kwenye hiki kitabu hakuna hata shilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, nakuomba sana, kulikoni? Maana yake ukiona mwanamke amepita kwenye Jimbo, ujue alipambana kweli kweli, siyo mambo ya *ki-sport sport!* Hatukuwa na mambo ya *ki-sport sport* mpaka tukaingia hapa. Sasa tunaomba Mheshimiwa Waziri unisaidie kama ambavyo Majimbo mengine yalivyopata pesa, basi nami naomba unifikirie. Utakapokuja kufanya majumuisho hapa, uniambie utanisaidiaje kwenye huo Mfuko wa Pamoja wa Afya pamoja na lishe na ulinzi wa mtoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, naomba nizungumzie Kituo cha Afya cha Nguruka. Tarafa ya Nguruka ina Kata nne na hiki kituo kinahudumia wananchi zaidi ya 100,000 na kitu na wanahudumia vilevile Kata ya Usinge kutoka Wilaya ya Kaliua. Sasa tumekuwa tunaomba mara kwa mara kupewa pesa ya kuweza kukipanua hiki Kituo cha Afya ili kiweze kuwa na huduma zinazostahili sambamba na kuongeza wodi ya wanaume na wodi ya wanawake. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI aweze pia kutuanguka katika suala la Kituo chetu cha Afya cha Nguruka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia hayo, naomba pia nizungumzie Mfuko wa Barabara. Mfuko wa Barabara kwa bajeti hii tunayokwenda kumaliza tarehe 30 Juni, tuliidhinishiwa shilingi milioni 695, lakini hadi sasa

tumepokea asilimia 45 tu. Sasa kwenye hii *coming budget* tunayotarajia ambayo itaanza tarehe 01 Julai, tumepitishiwa shilingi milioni 495 tu na sisi kwenye Jimbo letu, kwenye Halmashauri hii, hakuna barabara yoyote yenye lami. Mtandao wa barabara ambazo zina changarawe ni kilometa 44 tu na siyo zaidi ya hapo. Kwa hiyo, naomba hebu tuwe tunaangalia hizi Halmashauri mpya, tuwe tunazipa kipaumbele zaidi kuliko zile Halmashauri ambazo zimeanzishwa miaka mingi. Niliona hilo nalo nilizungumzie. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie suala la uanziswaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Nguruka. Tumekuwa tunaleta barua kwenye Wizara hii ya TAMISEMI na huko nyuma tuliambiwa kwamba hakuna shida, Mamlaka ya Mji Mdogo inaweza ikaanzishwa, lakini changamoto ambayo tunayo ni nini? Kata ya Nguruka ina vijiji viwili; Kata ya Itebula ina vijiji viwili; Kata ya Mganza ina vijiji sita; na Kata ya Mteguanoti ina vijiji vine. Sasa unaangalia kwamba kama hatuwezi kuongeza, maana yake hizi Kata ni kubwa mno. Tunachoomba Wizara ya TAMISEMI mmesema hamna mpango wowote wa kuongeza Kata, wala vijiji, lakini kuna Majimbo mengine ni makubwa mno, lazima mfikirie namna ya kutuongezea kugawanya Kata na vijiji ambavyo ni vikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Jimbo langu mimi lina *square meters* 10,178. Dada yangu Mheshimiwa Anne alikuwa anaongelea hapa, kwamba Same ina *square meters* 5,000, nikashtuka; kwangu ni 10,000. Kijiji kimoja mpaka ukimalize, unatakiwa ufanye ziara kwa siku mbili. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri uone namna ya kutukubalia maombi yetu pale tutakapoyaleta ili tuweze kuongeza vijiji kwenye Kata ya Nguruka, Kata ya Itebula ili uanziswaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Nguruka utakapokuwa unaanza, basi tuweze kuwa na vijiji vya kutosha mamlaka hiyo iweze kuendeshwa vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie migogoro baina ya vijiji na hifadhi. Kwenye Kijiji changu cha

Sibwesa na Kalilani wamekuwa wana mgogoro zaidi ya miaka 30 na Hifadhi ya Mahale, lakini cha kushangaza, tunatambua kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu hivi karibuni alitoa tamko kwamba kila taasisi za Serikali zihakiki mipaka yao. Ninavyofahamu, unapotaka kufanya uhakiki wa mipaka, wewe kama ni Wizara fulani kwa mfano ya Maliasili, maana yake nazungumzia Hifadhi ya Mahale, lazima ushirikishe na Wizara ya TAMISEMI. Kwa sababu hivi vijiji vimewekwa kwa mujibu wa sheria na aliyetangaza tangazo kabla ya kutangaza hivi vijiji ni Waziri Mkuu; ni Ofisi hiyo hiyo ya Waziri Mkuu. Sasa iweje leo Mkurugenzi wa Mahale anakwenda kuweka alama (*beacons*) kwamba hapa ndiyo sisi Mahale tunatakiwa mipaka yetu iishie; anaingilia mpaka zile GNza Serikali ambazo zimewekwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri mambo haya yakafanyika kwa mashirikiano. Nimewahi kuwa DC pale Arumeru, migogoro yote ya Arumeru tulikuwa tunafanya kwa ushirikishwaji. Unahusisha Wizara ya Ardhi, unahusisha Wizara ya TAMISEMI na kama kuna hifadhi, unahusisha pia na Wizara ya Maliasili. Sasa tatizo ambalo tunalo, tuna Wakuu wa Wilaya wengine ambao hawaelewi watatue matatizo ya wananchi kwa namna gani. Napenda kumuelimisha ana... (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. HASNA S.K. MWILIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono, hoja japo muda ni mdogo, nilitaka niseme zaidi ya hapo. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea, Mheshimiwa Doto Biteko, atafuatiwa na Mheshimiwa Subira Mgalu na Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel, ajiandae.

MHE. DOTO M. BITEKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Kabla sijasema, namshukuru

Mungu kwa nafasi hii ambayo amenipa ili niweze kusimama kwenye Bunge hili na kusema machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kuwapongeza sana watoa hoja, Waziri wetu wa TAMISEMI pamoja na Waziri wa Utumishi, Mheshimiwa Simbachawene pamoja na Mheshimiwa Kairuki kwa kuwasilisha bajeti yao vizuri na bajeti ambazo kwa kweli zimebeba mambo mengi sana ambayo tunayaendea kwa mwaka wa fedha unaokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana tunatofautiana kutazama kitu kimoja, mimi nianze kwa kutoa shukrani kwa Serikali kwa kazi kubwa inayofanyika Bukombe. Wewe ni shahidi, kwa muda mrefu fedha za dawa zilikuwa hazipatikani kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali zetu, leo ninavyosimama hapa Wilaya ya Bukombe tulikuwa na mahitaji ya fedha za dawa kwenye vituo vya afya na zahanati zaidi ya shilingi milioni 600 na tunafurahi kusema kwamba sasa hivi tumeshapata shilingi milioni 512. Hii ni kazi kubwa sana, inahitaji kushukuriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile hatukuwa na magari kwa ajili ya wagonjwa, Wilaya yetu ya Bukombe tumepata magari mawili kwa ajili ya wagonjwa yatakayokuwa yanahudumia kwenye Kituo cha Afya cha Uyovu pamoja na cha Ushirombo. Tumepata fedha kwa ajili ya kupanua shule ya msingi Ibamba, shule ambayo imeandikisha watoto wa darasa la kwanza peke yake 1,200. Wasikivu hawa, tulipowafuata kuwaomba pesa, wametupa pesa shilingi milioni 92 kwa ajili ya kupanua shule hiyo. Naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Bukombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna shule maalum mbili Wilaya ya Bukombe, shule zenyewe ni shule ya msingi Uyovu pamoja na Ushirombo. Nafurahi kusema kwamba Serikali wametusikiliza, wametupatia fedha kwa ajili ya shule hizi shilingi milioni 100 tumekwisha patywa kwa ajili ya kuhudumia watoto hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapojaribu kuhangaika kuona vijana tunawasaidia vipi kwenye nchi yetu, Wilaya ya Bukombe maombi tuliyopeleka kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, tayari Serikali imetusikia imetupatia, imetupatia shilingi milioni 51 za kuanzia kuwapatia mikopo vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo ni lazima tuyaseme, usipoweza kushukuru kwa kidogo, huwezi kushukuru kwa kikubwa hata kama utapatiwa. Naomba kwa moyo wa dhati, niishukuru Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya na Mawaziri wake ambao kwa kweli Wabunge wote hapa na wananchi ni mashahidi, tunawaona wanavyohangaika kuona Tanzania inapata maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, niseme machache ambayo sasa yanahitaji kuangaliwa na Serikali ili tuweze kuboresha. Jambo la kwanza, kwenye Wilaya yetu ya Bukombe tumekuwa tukiomba watumishi kwenye Idara ya Afya, hatujapatiwa watumishi wa kutosha na bahati mbaya sana hata hao wachache waliopo, wanapewa uhamisho bila kuletwa watumishi wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano, Wizara ya TAMISEMI wamehamisha madaktari saba wa Hospitali ya Wilaya ya Bukombe. Nimeuliza hili jambo hapa Bungeni, nimewafuata na ofisini kuwauliza, jamani mnapohamisha madaktari saba kwa mara moja kwenye Wilaya ya Bukombe mnatarajia nini kwa wananchi wetu? Ninaomba kupitia bajeti hii, Waziri wa TAMISEMI utusaidie, madaktari wetu saba wale mliowahamisha mara moja mnatuletea lini fidia ya madaktari hao? Kwa sababu hali iliyopo kule siyo nzuri, wananchi wanahitaji huduma, lakini watoa huduma ni wachache sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeomba vile vile Hospitali yetu ya Wilaya ya Bukombe ambayo ni Hospitali ya Wilaya

ipanuliwe, *theatre* yake ni ndogo. Ilikuwa ya mwanzo, kwa ajili ya kutumika kwa muda tu, baadaye watajenga *theatre* nyingine. Nasikitika, toka miaka hiyo ya 1990 haijawahi kupanuliwa. Naomba hili jambo na lenyewe liangaliwe ili wananchi hawa waweze kupata huduma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo madai ya watumishi wa Idara ya Afya, wanadai fedha nyingi, *on-call allowance*. Wanadai *allowance* zao hizi hawalipwi, wanadai mishahara yao na malimbikizo yao, tunaomba na hili Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI utakapoanza kuhitimisha hoja yako, utuambie watumishi hawa wanaanza kulipwa lini? Kwa sababu bila hawa, wananchi wetu hawawezi kutibiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine niongelee suala la elimu na kwenye hili nitaongelea elimu yenyewe lakini nitaongelea walimu. Hakuna muujiza wa kukomboa elimu hii kama hatuwezi kuwaangalia walimu wa Tanzania. Fanya kila unachoweza, unaweza ukawa na darasa lina vigae, masofa na *television*, lakini kama hakuna mwalimu aliyepewa motisha, kazi inayofanyika pale haiwezi kuleta matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu wa Tanzania wana malalamiko yao mengi, tusipoweza kuyapatia majibu kwa awamu hii, dawa ya elimu ya nchi hii hatuwezi kuipata. Walimu 80,000 wa nchi hii wamepandishwa madaraja, hawajarekebishiwa mishahara yao. Leo nakuomba Waziri wa TAMISEMI utusaidie, uwape tumaini walimu wa Tanzania, madaraja yao haya mnaanza kuyarekebisha lini na kuwalipa mishahara yao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo walimu ambao wamepandishwa madaraja, baada ya kuwa wamepandishwa madaraja, wameonja mishahara mpya, mmewarudisha nyuma kwa sababu ya uhakiki. Mheshimiwa Waziri tunakuomba utuondoe kwenye kitendawili hiki. Wale waliopanda madaraja, wapatiwe mishahara yao ili waweze kushi sawa sawa na jinsi ambavyo walikuwa wanatarajia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri hili aliangalie. Wakati mwingine unaweza usiwe na fedha, lakini lugha nzuri kwa watu inaweza kuwapa motisha wa kufanya kazi. Wapo watendaji wa Serikali na nichukue nafasi hii kumshukuru sana na kumpongeza sana Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Amos Makalla, nilimuona kwenye *television*, anawatia moyo walimu wa Tanzania. Wapo watu wengine wanafunzi wakifeli, analaumiwa Mwalimu Mkuu, unamvua madaraka Mwalimu Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya mwanafunzi kufeli siyo kama kufyatua tofali kwamba utaweka udongo kwenye kibao cha tofali, tofali litatoka, haiwezekani! Nataka nikwambie unaweza kumlazimisha mwalimu kuhudhuria kazini, huwezi kumlazimisha mwalimu kufundisha. Suala la kufundisha ni suala la mapenzi. Walimu wakati sisi tupo nyumbani tunaangalia *television*, wao wamejifungia kwenye vyumba vyao wanajiandaa kwa ajili ya watoto wetu kesho yake. Walimu hawa hawana mishahara mikubwa, wanajinyima fedha zao waweze kuchukua fedha hizo wakanunue vifaa vya kufundisha na maandalizi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapowavunja moyo kwa kuwaambia maneno ya kejeli, ninaomba Mheshimiwa Waziri unaposimama, ulikemee jambo hili walimu wa Tanzania wasikie. Walimu hawa wanahitaji kuthamaniwa, kuheshimiwa, unamvua Mwalimu Mkuu madaraka kwa sababu ya kufeli mwanafunzi, mwalimu pekee sio sababu ya mwanafunzi kufeli, zipo sababu nyingi zinazosababisha mwanafunzi kufeli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya kwanza inaweza kuwa mzazi, sabab ya pili inaweza kuwa mazingira ya kazi na ya tatu inaweza kuwa mwanafunzi mwenyewe na sababu nyingine anaweza kuwa mwalimu. Unachukua sababu moja ya mwalimu peke yake, unamvua madaraka!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya walimu wa Tanzania na kwa niaba ya walimu wa Bukombe naomba nipaze sauti yao, tabia hii iachwe ya baadhi ya watu,

wanaichafua na wanaigombanisha Serikali na walimu wa Tanzania, hatuwezi kukubali kama Bunge tukaona walimu ambao sisi wametufikisha hapa wanaendelea kudharauliwa na kuonewa kwa maneno ya kutungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Waziri wa Utumishi ukemee hili kwa sauti kubwa, watendaji kule chini wasikie na mimi nafahamu wewe Mheshimiwa wa Utumishi unafahamu ni watu gani wamefanya haya. Walimu wa Tanzania hatuwezi tukakubali wakaendelea kuonewa kwa kiwango hiki. Tuwasaidie walimu kwa kuwapatia vifaa vya kufanyia kazi kwa kuwapatia fedha za kutosha, zile stahiki zao kama kupanda madaraja yao walipwe kwa wakati, mambo ya kuwapiga danadana inatosha, sasa hivi nao wanahitaji wapate chao mkononi na wafanye kazi kwa kujituma zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie Mfuko wa Barabara. Wilaya yetu ya Bukombe upande wa Kusini tunapakana na milima, maeneo ya Imalamagigo, Mchangani na Nifa, maeneo yote haya tumeomba fedha kwa ajili ya Mfuko wa Barabara turekebishe barabara hizo hatuwaji kupata hata shilingi moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekwenda TAMISEMI mara kadhaa kuwaomba ndugu zangu watusaidie, watu wanateseka, wanafunzi wanashindwa kwenda...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. DOTO M. BITEKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Kama nilivyosema mwanzo, sasa ni zamu ya Mheshimiwa Subira Mgalu.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii niweze kuchangia hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Utawala Bora.

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya ya kuweza kusimama ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili naomba nichukue nafasi kuwapa pole wananchi wenzangu wa Wilaya za Kibiti, Mkuranga na Rufiji kutokana na matukio yaliyojitokeza, lakini niliona nilisemie hapa kwa sababu tukio la mauaji linaloendelea Wilayani Kibiti na Rufiji kwa kiasi kikubwa limeathiri uendeshaji wa Halmashauri za Kibiti na Rufiji na naiomba Ofisi ya Rais, TAMISEMI waiangalie kwa jicho la huruma Halmashauri mpya ya Kibiti, wameshindwa kukusanya mapato kwa sababu katika maeneo ambayo mauaji hayo yanajitokeza mara kwa mara eneo la Bungu na Jaribu Mpakani ni eneo ambalo lina vyanzo vingi vya mapato na linalochangia mapato kwa kiwango kikubwa.

Kwa hiyo, naomba Serikali itambue Halmashauri ile ni mpya, inahitaji pesa ya uendeshaji wa Halmashauri na ina maeneo maalum ya ukanda wa delta. Kwa hiyo, naomba sana Waziri aitazame Halmashauri ile kwani kwa sasa hata malipo ya posho za Madiwani zitakuwa ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa pia wanaopata madhila hayo ni baadhi ya viongozi wa vijiji na vitongoji, naomba pia Mheshimiwa Waziri aangalie namna gani viongozi wa maeneo yale watakavyokuwa wanawajibika. Hapa hapa niwasemie viongozi hawa wa vijiji na vitongoji pamoja na Waheshimiwa Madiwani ambao ni wasimamizi wa shughuli mbalimbali za maendeleo kuwaongezea posho. Kwa mfano, Wenyeviti wa Vijiji hawana posho yoyote. Pia naipongeze Halmashauri yangu ya Chalinze kwa uamuzi wa kuwapa Wenyeviti wetu wa Vijiji shilingi 30,000 kila mwezi kwa ajili ya kuwawezesha kufanya shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hii pia ni Ofisi ya Rais, naomba nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na kwa Mkoa wa Pwani tunaishukuru ziara yake aliyoifanya mwezi wa Tatu. Ziara ile ilionesha azma yake ya ujenzi wa viwanda nchini kutimia ndani ya Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mazingira mazuri, tunavyo takribani 82 vinavyoendelea kujengwa kikiwemo kiwanda cha *tiles* ambacho kimekamilika Mkuranga, lakini kuna kiwanda cha *tiles* kinaendelea Chalinze, lakini pia kuna kiwanda cha usindikaji matunda Msoga, Chalinze. Kwa hiyo, hii inaonesha bado wawekezaji wana imani na Serikali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Mheshimiwa Rais kwamba anaendelea kukubalika na Jumuiya ya Ulaya imeshatoa msaada, imeahidi kuendelea kuisaidia nchi yetu dola milioni 205, ameshasaini. Pia Benki ya Dunia inaendelea kufadhili miradi mbalimbali ya ujenzi wa *flyover* Dar es Salaam, kuendelea kwa ujenzi wa mradi wa mwendokasi Dar es Salaam, yote hayo yanaonesha namna gani Mheshimiwa Rais wetu anaaminika na Benki ya Dunia, *African Development Bank* na wadau mbalimbali wa maendeleo. Tuendeleo kumuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze kwenye suala la elimu bure. Naipongeza sana Serikali, jambo hili siyo jepesi. Kwa bajeti ya mwaka huu, zaidi ya shilingi bilioni 201 zimetengwa kwa ajili ya elimu bila malipo. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kwa kutoa ufafanuzi mzuri namna ya kutofautisha elimu bure na elimu bila malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo baadhi ya wananchi wengi tu katika maeneo mbalimbali wameanza kulitekeleza hilo la kutoa michango yao. Hapa naipongeza Halmashauri ya Bagamoyo na Chalinze, Kibiti, Mkuranga, Mafia, Kisarawe kwa wananchi mbalimbali, tumeanza ujenzi wa miundombinu ya elimu ili kuchangia jitihada za Serikali. Kwenye Halmashauri ya Chalinze ninayohudumu tumetenga shilingi milioni 400 ya ujenzi wa miundombinu kwa mapato ya ndani kwa elimu ya msingi, shilingi milioni 400 ujenzi wa miundombinu kwa mapato ya ndani kwa elimu ya sekondari. Hii inaonesha namna gani sisi wawakilishi wa wananchi; Madiwani na Wabunge tunavyoona umuhimu wa kuisaidia Serikali katika suala zima la elimu bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo naiomba Serikali kwenye suala hili la elimu bure, ukiangalia namna ambavyo hizi fedha zimetengwa kwa uhalisia, uwiano wa wanafunzi katika Halmashauri zetu, uwiano wa walimu na uwiano wa uhaba wa mindombinu; hapa naomba Mheshimiwa Waziri aangalie ile randama kwenye Halmashauri zetu za Mkoa wa Pwani. Kwa mfano, Halmashauri ya Chalinze na Mkuranga inaongoza kwa idadi ya wanafunzi, inaongoza kwa idadi ya walimu, inaongoza na kwa idadi ya uhaba wa miundombinu, kwa hiyo, nadhani katika ule mchanganuo haujakaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuta Halmashauri nyingine idadi yao ni ndogo na hapa nia ni kufanikisha; kwa hiyo, naomba nimletee Mheshimiwa Waziri ile taarifa yetu kamili ya kuonesha namna gani ule mgawanyo ulivyo ili waweze kurekebisha. Ukizingatia hasa Halmashauri ya Mkuranga kwa kweli uhamiaji ulikuwa mkubwa na wanafunzi ni wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo pia naipongeza Serikali hususan Wizara hii ya TAMISEMI pamoja na Wizara ya Afya kwa namna ambavyo wameanza mgao wa vifaa tiba kwenye hospitali zetu. Hivi karibuni tumeona Serikali imenunua vifaa tiba vya thamani ya takribani shilingi 2,900,000,000 ambapo kila Halmashauri itapata vitanda 20, vitanda vitano vya kuzalishia, magodoro 25 na mashuka 50. Kwa kweli hii ni hatua nzuri katika kuboresha huduma za afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kwenye ukurasa wa 34 wa hotuba ya Waziri wa TAMISEMI, ameonesha ni namna gani Serikali kwa kushirikiana na hizi Wizara mbili itakavyokarabati vituo vya afya 100 ili kuboresha mazingira ya upasuaji kwa ajili ya afya za akina mama. Mpango huu utagharimu shilingi bilioni 63. Naipongeza sana Serikali.

Kwa hapa nizisemee Halmashauri zetu mpya Kibiti na Chalinze; Halmashauri hizi hazina Hospitali za Wilaya, lakini kwa Chalinze bahati nzuri Mheshimiwa Rais wetu Mstaafu

wa Awamu ya Nne amejitahidi tumepata majengo kwa Kata ya Msoga, lakini changamoto kubwa ni uhaba wa watumishi. Hatujapatiwa watumishi kwenye hospitali yetu ile ya Wilaya na majengo yamekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hata *Basket Fund* tumepata takriban shilingi milioni 488, lakini mpaka sasa kiasi cha shilingi bilioni 105 kinashindwa kutumika kwa kuwa hakuna hospitali yenye hadhi katika Halmashauri ya Wilaya wakati tunayo tayari na majengo tayari pia yamekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nikisemee Kituo cha Afya cha Chalinze. Kituo hiki kinapokea majeruhi wengi, naomba sana Serikali ijitahidi kutuboreshea wodi ya upasuaji, maana hakuna wodi hiyo pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala zima la uwezeshaji wa wananchi, naipongeza sana Ofisi ya Waziri Mkuu kwamba Mkoa wangu wa Pwani umepokea shilingi milioni 104 kwenye Mfuko wa Vijana, lakini sambamba na hilo, Mkoa wetu wa Pwani umetoa takribani shilingi milioni 477 ambayo ni asilimia 10 ya mapato yake ya ndani. Hapo naomba nishauri; kwa kuwa marejesho ya mfuko huu hayaonekani wazi wazi kwa kuwa hakuna akaunti maalum, naomba Serikali sasa ione namna ya kuanzisha akaunti maalum kwa ajili ya marejesho tu ya mikopo hii ya asilimia 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kwa kuwa fedha zinazotengwa ni nyingi, Serikali ione uwezekano wa kuanzisha benki za wananchi katika mikoa yetu. Kwa mfano, mwaka huu tulitenga shilingi 1,800,000,000; mwakani tumetenga shilingi 2,400,000,000; hizi zinatoshwa kabisa kuanzisha benki za wananchi katika mikoa ili kurahisisha na wakati huo sheria itakuwa imerekebishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, nadhani pia ile mikopo ya shilingi milioni 50, sijasikia neno kutoka kwa Waziri wa TAMISEMI, lakini nadhani Wizara yake ndiyo itakuwa

inaratibu, inaweza pia ikaongeza nguvu katika mikopo hii ya asilimia 10 kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwasemee walimu pia. Nampongeza sana Mheshimiwa Biteko na Waheshimiwa wote waliosemea hili, lakini hapo niseme tatizo lililopo sasa hivi la uhamisho. Walimu wengi wamepata watu wa kubadilishana nao, lakini vikwazo mbalimbali vinatokea na sekta hii kwa kweli na watumishi wengi wanakwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nampongeza Mheshimiwa Angellah Kairuki kwa namna alivyosimamia zoezi hili la uhakiki wa wafanyakazi, uhakiki wa vyeti *fake*, lakini ifike wakati sasa zile haki za kimsingi, hata zile ambazo hazihusiani na masuala ya malipo, walimu wenyewe wameomba kuhama kwa hiari yao, wamepata wa kubadilishana nao, basi TAMISEMI itoe hiyo orodha ili walimu wetu na kikwazo kingine masuala ya ndoa yaweze kufanyika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel atafuatiwa na Mheshimiwa Kiwelu.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata fursa hii lakini kabla sijasema naomba niweke sawia mambo mawili yaliyojitokeza jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtu jana alijaribu kuonesha kwamba Mwenyekiti wa Kambi Rasmi ya Upinzani ni mtu wa kawaida, lakini naomba niweke rekodi vizuri, Mheshimiwa Freeman Mbowe, alikipokea Chama cha

Demokrasia na Maendeleo kikiwa na Wabunge watano, lakini amekipeleka na akafika mahali mpaka ikaundwa UKAWA na leo Bunge hili lina Wabunge kutoka upinzani zaidi ya 100. Lakini ameweza kuunganisha nguvu na hata akatuletea magwiji wa siasa kutoka huko kwenu ambao wakikaa kimya CCM wote mnakusanyika kufukiria kwa nini yupo kimya. Kwa maana hiyo Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe ni profesa wa sayansi ya siasa, niweke rekodi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile jana kuna baba yangu alisema kwamba mama yetu Ruth Mollé kwamba eti kwa sababu amewahi kuwa kiongozi mkubwa katika nchi hii hastahili kuwa kwenye chama cha upinzani kwa sababu ana siri za Serikali. Ninataka niwaambie kwamba CCM sio masijala ya siri ya Tanzania. CCM ni chama kama chama kingine cha siasa, CCM ni kana CHADEMA ni kama CUF na mtu yeyote haijalishi ameshika nafasi katika nchi hii anaruhusiwa kuwa kwenye chama chochote ilimradi havunji Katiba ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefanya utafiti kuanzia miaka ya 1970 mpaka 2016 nimegundua ili kutekeleza mpango kazi wa mwaka mmoja katika nchi hii unahitaji miaka mitatu mpaka minne kwa hiyo sitazungumzia pesa kwa sababu nchi hii haina pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitakwenda kujikita tubadilisha fikra kwa babu fikra ndiyo tatizo leo kwa hiyo tukibadilisha namna tunavyofikiri nchi hii itakuwa na pesa na tunaweza kukabiliana na matatizo yaliyotukabili mbele. Wakati nawaza hilo, nikafikiria, hivi katika kubadilisha fikra na kuisadia nchi hii, *solution* ni kubana demokrasia? Ni kuzuia uhuru wa kutoa mawazo ya Bunge? Ni kuhakikisha vyombo vya habari havifanyi kazi yake vizuri? Nikagundua la hasha, kuruhusu uhuru wa mawazo ndipo tutakapogundua magwiji wa fikra katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sifa ya magwiji wa fikra ni watu wenye uwezo wa kufikiri katika upeo ulipitiliza ubongo

na sifa yake ni kwamba huko hakuna unafiki, hakuna uzandiki, hakuna u-CCM wala u-CHADEMA, tunalifikiria Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme, Rais wa Marekani alipokuwa anamkabidhi Makamu wake kazi, alimwambia naamini akili zako sana, akamwambia ninakupa *mission* ya kupeleka nchi yetu iwe nchi ya kwanza kufanya miujiza katika sayari ya *mars*. Tujiulize sisi tunapokabidhiana madaraka, tunakabidhiana madaraka kwa ajili ya kuishughulikia upinzani, kwa ajili ya kubonyeza demokrasia, tunakabidhiana madaraka kwa ajili ya kufanya nini? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujiulize kwa nini Marekani wanataka kwenda *mars*, wanataka wawepo, pamoja na mambo mengine, wawe wanaitazama dunia wakiwa mbali wanaiangalia Tanzania, wanaangalia mabara yote na mtu yeyote akitaka kuigusa Marekani wakati akiwa katikati ya Bahari ya Atlantiki, anagongwa kabla hajaifikia Marekani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujiulize sisi kama nchi, hivi tunajisifia kwa kutegua mtego wa Mheshimiwa Nape kuongea na waandishi wa habari halafu tunasema tumetumia akili na Usalama wa Taifa una akili sana katika nchi hii! Nchi yetu leo tunauliza maswali ya msingi kwamba Ben Saanane yuko wapi? Hatuna hata uwezo wa kueleza yuko wapi na ninategemea kwamba Usalama wa Taifa ndiyo darubini ya nchi, ndiyo maana tunaita *TISS*, ile 'I' ndicho kitu cha msingi; *intelligence!* Uwezo wa kutazama na kuona mambo yasiyoonekana kwa macho ya kawaida. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nchi inahangaika, Mwenyekiti wa Kambi ya Upinzani anasema, tuombe basi msaada Uingereza kwa watu wenye darubini ya kutazama mambo yasiyoweza kuonekana, tunazunguka zunguka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme hivi, hii nchi siyo ya CCM, siyo ya CHADEMA, ni yetu wote Watanzania. Ni lazima tuanze kufikiri ni namna gani tunaweza kuisaidia Tanzania

na tunatokaje sehemu hiyo ambayo sasa tupo. Juzi hapa na jana limejadiliwa suala la *East Africa*. Tumeingia kwenye uchaguzi na ningependa sana Spika angekuwepo hapa. Unajua ukiwa umelala uko nusu usingizi, huwa kuna akili nzuri zinakuja, lakini hizo akili huwa zinakuja wakati kuna msiba umetokea mkubwa wa mtu ambaye mnampenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa hapa kwenye msiba wa Sitta, Mheshimiwa Spika ndipo alipofikia akagundua sisi tunapita tu hapa duniani, akasema anatamani sana kufikia hata nusu ya utekelezaji wa Mheshimiwa Sitta, lakini juzi tumefanya uchaguzi wa *East Africa* hapa, yamefanyika madudu. Nataka umwambie Mheshimiwa Spika, huu mtego wa uchaguzi wa Afrika Mashariki ni mtego ambao unamfanya hata aweke *milestone* ya kwanza kumwelekea Sitta, hata kufikia nusu ya Mheshimiwa Sitta. Ndiyo mtego wa kwanza ambao tunampa Bunge hili. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vita kuhusu *East Africa* na uchaguzi wa *East Africa* siyo kati ya CCM na CHADEMA, ni kati ya Tanzania na dunia ya kibiashara na vita vya kibiashara vya kidunia. Tunahitaji akili kubwa kama ya Mheshimiwa Masha ambaye amewahi kuwa kiongozi ndani ya Serikali, anajua Usalama wa Taifa vizuri namna ya kushirikiana nao, anajua nchi hii ili tuweze kuunganisha nguvu tupambane kwenye vita vya kidunia katika uchumi wa dunia, siyo kutafutana na kutafuta CHADEMA nani mzuri nani mbaya. Hicho ndicho tunachokifikiria; tuache kuwaza katika akili ndogo. Bahati nzuri, tunaye Mheshimiwa Waziri mzuri, msikivu na mwelewa tumtumie, ni fursa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Waziri wa TAMISEMI nikwambie tu, unaye Naibu wako mzuri ambaye ametuonesha mfano mzuri wa utawala bora, Mheshimiwa Jafo.

Mheshimiwa Jafo amekuja kwenye Wilaya ya Siha, ametuunganisha wana-CHADEMA na wana-CCM tukaanza kuwaza tu kuhusu maendeleo ya Wilaya yetu, akaacha

mambo ya uchama ili twende mbele. Tunataka viongozi kama hao, hatutaki watu ambao wanakuja kwa shughuli za Kiserikali wanaanza kufikiria mambo ya vyama. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu, usalama wa nchi ni uchumi. Tujiuize maswali ya msingi, Usalama wa Taifa kama ina *microscopic eyes* na tunazungumzia hapa na wakati mwingine tukizungumzia Usalama wa Taifa watu wanafikiri tunadhaliisha Usalama wa Taifa, hapana tunatafutia Usalama wa Taifa uhuru wake na waanze kupelekwa Usalama wa Taifa watu wenye akili kubwa, ndicho tunachokipigania hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujiulize Kagoda ilivyokuwa imetokea, *Richmond, EPA*; Usalama wa Taifa walikuwa wapi? Leo Rais anahangaika na makontena huko, tujiulize kama hilo wazo la kuruhusu makontena yaende nje lilikuwa baya, Usalama wa Taifa walikuwa wapi wasimshauri Mheshimiwa Rais? Tujiulize kama Mheshimiwa Rais leo atakuwa amekosea kuzuia hayo makontena, Usalama wa Taifa wako wapi kama Mheshimiwa Rais wetu atakwenda kukosea kwa maana ya uamuzi huo anaofanya? Hiyo ndiyo akili tunataka nchi yetu isaidiwe na iongozwe kwa namna hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu tujiulize hivi hawa watu wanaompelekea Mheshimiwa Rais *message* kwamba kuna muuza duka huko amemtukana halafu muuza duka anakwenda kusimama na Rais Mahakamani eti ana kesi na Mheshimiwa Rais, ni nani huyo anayempelekea Mheshimiwa Rais anaanza kufuatilia mambo madogo madogo katika nchi kama hii maskini ambayo asilimia 48 ya bajeti yake inategemea misaada kutoka nje? Kuna mambo makubwa ya kumwelekeza Mheshimiwa Rais ili ayafikirie, siyo kuwa na kesi na watu wadogo wadogo wa mtaani kwenye shughuli za simu. Tuanze kutafakari, tuanze kufikiria, tuipeleke nchi yetu inavyotakiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua nawatibu akili, mimi ni Daktari wa binadamu, tuanze kuwaza, Mheshimiwa Mwinyi unanielewa. Ukianza kuona mtu ana *Ph.D* halafu

anajipendekeza kwa mkubwa kwa sababu tu huyo mkubwa anafanya mambo ya uteuzi, ni mojawapo ya kujitambua na kupima kwamba uwezo wako wa kufikiri ni mdogo, hata kama ulifaulu, ulikuwa na IQ ndogo tu ambazo zingekuwezesha kufaulu matokeo darasani, lakini IQ ni ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu tuanze kujipima IQ, zetu ni kwa nini mtu mwenye Ph.D anajipendekeza kwa mtu mkubwa? Inakuwaje zero inapigiwa salute na majeshi yetu? Mheshimiwa Mama Ndalichako anza kujiuliza, hivi kuna leakage gani inapitisha zero mpaka inakuwa Mkuu wa Mkoa katika nchi hii? Inatokeaje? Hatuwezi kukubali hicho kitu. Hizo zero hatuzidharau, tujiulize, hivi kama yeye ameweza ku-shake nchi mpaka Ph.D inampigia salute, tujiulize sisi wenye Ph.D na huyo mwenye zero ni nani mwenye akili zaidi? Hilo ndiyo la msingi. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujiulize, mimi nawarudisha, siwezi kuzungumzia tena maji maana naona...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Muda wako umekwisha! (Makofi)

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mimi...

MWENYEKITI: Mheshimiwa, muda wako umekwisha! Mheshimiwa Mollel, tafadhali, tuzingatie tu muda. (Makofi/Kicheko)

Ahsante. Muda unaanza kunisumbua. Mheshimiwa Kiwelu, atafuataiwa na Mheshimiwa Japhet Hasunga. Hiyo ndiyo tunamaliza uwiano. Nitacheza na muda ili twende vizuri round ya pili.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie

machache katika Bajeti hii ya Ofisi ya Rais. Nianze kwa kuziunga mkono hotuba zote mbili za Kambi ya Upinzani na niishauri Serikali isijisikie vibaya wala kuona aibu kuchukua yale mazuri yaliyomo katika hotuba zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la utawala bora. Utawala bora ni pamoja na kuviruhusu vyama vya siasa kutimiza wajibu wake kwa kufanya mikutano ya hadhara, lakini toka imeanza Serikali hii ya Awamu ya Tano, imekuwa na uoga na sijui ni kwa sababu gani wakati mnatamba kwamba mnafanya kazi zenu vizuri na hapa ni kazi tu, lakini mmekuwa mkivipiga marufuku vyama vya upinzani kufanya mikutano na kutoa ruhusa kwa Madiwani na Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkumbuke kuwa katika vyama vyetu tuna viongozi wa vyama wa Kitaifa, tunao Wajumbe wa Kamati Kuu ambao sio Wabunge na siyo Madiwani, je, hawa watafanyia wapi kazi zao. Kwa hiyo, nataka kuiambia Serikali ya Chama cha Mapinduzi waache kunyima haki kwa vyama vingine vya upinzani wakati wao wanapokuwa kwenye maeneo ambayo sio ya kwao wanahutubia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgombea wetu wa Urais alipata kura zaidi ya milioni sita na wa Chama cha Mapinduzi alipata kura milioni nane, tofauti ya kura milioni mbili. Yeye anapita kuwashukuru Watanzania, lakini huyu wa kwetu aliyepata kura milioni sita mnakataa asiende kuwashukuru wananchi ambao walimuunga mkono, hii siyo haki kabisa! Tunaomba Katiba iheshimiwe kwa sababu ninyi ndio mmekuwa mkivunja Katiba wakati vyama vya siasa vipo kihalali, vya upinzani na hata hicho cha CCM, kwa hiyo, tupewe haki sawa kuhakikisha tunazungumza na Watanzania. Kutuambia tusemba mpaka 2020 hamtutendei haki. Chama chochote cha siasa mtaji wake ni watu. Kwa hiyo, tunapokwenda kufanya mikutano, tunakwenda kuzieneza sera zetu na kupata wanachama wa kujiunga na chama chetu, lakini nashindwa kuelewa sijui uoga wenu ni nini. Niwaambie tu, huko nje Watanzania wameshakata tamaa na Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la afya. Kumekuwa na tatizo ndani ya nchi yetu la vifo vya akina mama na watoto. Naliomba Bunge na Serikali, ifike wakati tuhakikishe kwamba tunakwenda kupunguza vifo hivi kwa kuhakikisha tunatenga bajeti ya kutosha kwa akina mama ili waweze kupata huduma bora wanapofika kwenye vituo vya afya ikiwemo huduma ya upasuaji, kwa sababu akina mama wengi wamepoteza maisha kutokana na vituo vyetu kutokuwa na vifaa na hasa madaktari na wahudumu wa afya pamoja na dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba sana Serikali na sisi kama Bunge tuliseme hili ili kuhakikisha vifo vya akina mama na watoto katika nchi yetu vinapungua. Nawaomba Wabunge wenzangu tukatoe elimu kwenye maeneo yetu tunayotoka na kuwaomba akina mama pindi wanapokuwa wajawazito waweze kuhudhuria kiliniki, hii itasaidia sana kupunguza vifo vya akina mama na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni Bima ya Afya. Suala hili limekuwa ni tatizo kubwa sana, hata Waheshimiwa Wabunge wenyewe humu ndani ni mashahidi. Zipo hospitali ambazo zinakataa kupokea Bima ya Afya hata kwa Waheshimiwa Wabunge, sembuse huko kwa wananchi wetu ambao ni wengi. Yapo maduka ya dawa yanakataa kupokea kadi hizi.

Kwa hiyo, naiomba Serikali kwanza itoe elimu kwa wadau wote wahusika umuhimu wa hii Bima ya Afya ili wananchi wengi waweze kujiunga katika bima hii waweze kupata huduma nzuri ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la elimu. Hapa kwanza naomba nimpongeze na kumshukuru Mheshimiwa Simbachawene. Katika bajeti iliyopita nilizungumzia shule ya watoto walemavu Njiapanda. Kulikuwa kuna baadhi ya watumishi walikuwa hawajalipwa, nakushukuru kwamba watumishi wale wamelipwa, lakini pia namshukuru Waziri wa Elimu Mheshimiwa Mama Ndalichako,

alikuwenda kutembelea shule ile na niliongea na Mwalimu Mkuu akaniambia kwamba yale niliyoyasema yakiwemo shule ya sekondari ya watoto wenye ulemavu, mchakato umeanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, lakini naomba mchakato uende haraka kwa sababu watoto wale mwaka huu wanakwenda kufanya mihani wa darasa la saba. Tunaomba sana ili mwakani nao waweze kujiunga kidato cha kwanza, tusiwaache watoto hawa nyuma kwa sababu wanao uwezo na hawa ndio viongozi wetu wa baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nizungumzie shule za Kata. Mkoa wetu wa Kilimanjaro hasa kule Uchagani waliitikia vizuri sana ujenzi wa shule za Kata na kuna baadhi ya vijiji vina shule mbili mpaka tatu za sekondari na hii sasa imeleta upungufu wa wanafunzi; kwa mfano, katika kijiji cha Kitandu katika Kata ya Uru Mashariki tunazo shule mbili na katika shule moja ya Mawela tuna madarasa zaidi ya manne hayana wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali, pamoja na kuwa shule hizi zilijengwa na nguvu za wananchi, mngewashauri waweze kutumia shule moja aidha, kwa kufanya *hostel*, kuhamisha shule moja kwenda kwenye shule nyingine ili ile shule nyingine iweze kutumika *hostel* au tukaweza kuifanya *o-level* ili wale watakaomaliza pale waweze kuingia kwenye hii shule nyingine kuliko kuacha madarasa wazi, inakuwa haina faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine elimu yetu tumeona inaendelea kushuka na hii ni kwa sababu Wakaguzi hatujawatengea fedha za kutosha za kuweza kukagua shule zetu. Naiomba sana Serikali iweze kutenga fedha za kutosha ili Wakaguzi hawa waweze kufanya kazi zao ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la posho za Madiwani. Wabunge wenzangu wamesemea sana posho za Madiwani. Tunajua Waheshimiwa Wabunge wanapokuwa

hawapo, Madiwani wamekuwa wanafanya kazi kubwa sana. Naiomba Serikali, kwenye hotuba yetu ya Upinzani kwa upande wa TAMISEMI tumeomba kuongeza posho zao. Najua Madiwani wako kwenye ile Sheria ya Mafao, lakini mafao yao mwishoni yanakuwa ni madogo kwa sababau ya posho wanazozipata. Kwa hiyo, naomba posho zao ziongezwe na hii ni pamoja na Wenyeviti wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa. Halmashauri nyingi zimekuwa haziwapi fedha. Naiomba TAMISEMI, aidha, itoe mwongozo au itunge sheria ya kuzielekeza Halmashauri zetu kuhakikisha Wenyeviti hawa wanalipwa fedha zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho nizungumzie ujenzi wa *stand* ya Ngangamfumuni. Mheshimiwa Simbachawene tunakuomba sana, mchakato huu ulishakamilika na *TIB* tayari walishakubali kutoa fedha, kujenga na kusimamia ndani ya miaka 15 wakisharejesha fedha zao watukabidhi *stand*. Kwa hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri utukubalie kusaini ili tuweze kupata fedha hizo kwa maendeleo ya wananchi wetu wa Manispaa ya Moshi na kwa Taifa zima. Sioni ni kwa sababu gani unapata kigugumizi. Sitaki kuamini zile sababu zilizosemwa juzi kwa sababu yapo niliyokuomba na ukayafanya, kwa hiyo, nikuomba tena kwa mara hii *stand* ya Ngangamfumuni muweze kutupatia kibali na ujenzi huo uweze kuanza mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala la Ben Saanane. Mimi ninatoka Mkoa wa Kilimanjaro na ni Mbunge wa Viti Maalum, akina mama wa mkoa ule wanaulizia Ben Saanane yupo wapi na leo Kiongozi wa Upinzani ameuliza swali hapa, tungependa kujua Ben Saanane alipo, na kwa taarifa walizosema ambazo sina hakika nazo tunataka taarifa sahihi, kama kweli Ben yupo basi tumpate na kama hayupo ni vizuri mkatuambia ili familia yake ijue kama wameshampoteza Ben kama alivyosema Mbunge wa Rombo walie. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango wako. Mheshimiwa Japhet Hasunga atafuatiwa na Mheshimiwa Ibrahim Raza.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru sana kwa kunipatia hii nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Mawaziri wote waliowasilisha bajeti zao na kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya, kwa kweli hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kila sababu ya kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano na hiyo ndiyo kazi yetu kubwa na sababu kubwa ambazo zinafanya tuipongeze ni mambo makubwa ambayo imefanya katika kipindi cha mwaka mmoja na nusu; katika mwaka mmoja na nusu huu mambo makubwa yameonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kabisa jinsi nchi hii ambavyo sasa tunaibadilisha, kwa kweli hii tunajivunia sana. Lakini hii imeonesha dhahiri namna ya kupambana na rushwa katika nchi hii ambayo ilikuwa ni kikwzo kikubwa sana katika maendeleo yetu ya nchi, kwa kweli hii tunaipongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia imeonesha namna ya kupambana na dawa za kulevya, ni lazima tuziunge jitihada hizi kwa hali na mali ili kuhakikisha kwamba tunairekebisha nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwanza kwa kuanzisha rasmi mkoa wa Songwe, tunawashukuru sana tena sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia naomba niipongeze Serikali katika mambo ambayo yalishindikana miaka mingi yameweza kutekelezeka, suala la elimu bure, lakini suala kubwa zaidi na ambalo hatutalisahau kwenye historia, ni suala la kuhamia Dodoma. Serikali yote imehamia

Dodoma. Tumeimba miaka mingi sana, lakini sasa Serikali hii imeonyesha dhahiri kwa vitendo ndani ya mwaka mmoja na nusu Serikali karibu yote imehamia Dodoma na mimi naamini na ninamshauri Mheshimiwa Rais ahamie na yeye mapema kabisa kuliko ile ratiba tuliyoitoa. Kwa kweli tunawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali imefanya mambo mengine makubwa, tumeona kabisa tumeanza kujenga reli kubwa ya kati (*standard gauge*), reli ambayo tulikuwa tunaimba tu kwa muda mrefu. Hii itachangia katika kuongeza na kupanua uchumi wetu. Kubwa zaidi tumeweza kununua ndege ambazo hazikuwepo. Sasa tunalifufua Shirika letu la Ndege, haya ni mambo makubwa ambayo yamefanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali. Kwa Jiji la Dar es salaam tumeona, tulikuwa hatujawahi kuona *flyover* Dar es Salaam; sasa *flyover* zinaanza kujengwa. Sasa tunataka nini zaidi? Ni mwaka mmoja tu na nusu yote haya yameonekana. Kwa hiyo, tunaipongeza sana Serikali kwa yote haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie masuala ya utawala bora. Masuala ya utawala bora nashangaa! Tusiyaangalie katika upana mdogo, tuyaangalie masuala ya utawala bora katika uwanja mpana sana. Masuala ya utawala bora yana mambo mengi. Kwanza kuna misingi ambayo tunaita ni misingi ya utawala bora, misingi ambayo ipo na misingi hii imewekwa kwenye Katiba, imewekwa kwenye mihimili yetu mitatu. Utawala bora ni jinsi ninyi mnavyoliongoza Bunge, mnavyozingatia kanuni, sheria, yote hayo ni utawala bora. Jinsi Wabunge tunavyochangia hapa ndani na watu wanavyochangia mawazo, ni utawala bora, jinsi Mahakama zinavyofanyakazi, ni utawala bora na jinsi Serikali inavyotenda kazi ni utawala bora. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Sema, sema, sema! (*Makofi*)

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna Serikali duniani inayoweza ikafanya *100 percent*, upo upungufu mdogo mdogo, lakini mambo ya msingi yanakwenda lazima tuyafurahie. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Safi! *(Makofi)*

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala bora una mambo karibu kama nane hivi ambazo tunaita *pillars za good governance*. Kuna uwazi, uwajibikaji, demokrasia, ushirikishwaji, Serikali sikivu, kuna utawala wa sheria, kuna ufanisi na tija na kuna haki na wajibu. Haya yote yanasimamiwa vizuri na Serikali yetu. Sasa wapi kuna tatizo? *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Hakuna hata kidogo. *(Makofi)*

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mambo yanakwenda! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia sasa hivi uwajibikaji ndani ya Serikali ni mkubwa, ukiangalia tunavyopambana sasa na kuondoa wale wote wenye vyeti hewa ni mapambano mazuri, ni uwajibikaji, ni utawala bora, tunapojenga nidhamu ya utumishi ni utawala bora. Sasa tunataka nini zaidi ili tuseme utawala bora upo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mengine tunayoyasema, dosari ndogo ndogo zipo. Hata mtawala Lee Kuan Yew, Baba wa Taifa wa Singapore, alisema hakuna mtu anayeweza akawa *100 percent perfect* na hakuna njia sahihi duniani. Sisi tumeamua kuendeleza nchi, tutaendeleza, tutakwama, tutarudi nyuma, lakini tutasonga mbele, maadamu dhamira yetu iko pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tushirikiane, tuiunge mkono Serikali yetu jinsi ambavyo imekuwa ikitekeleza majukumu yake. Yapo masuala machache labda niseme madogo yanayohusu wachache wanaokwamisha utawala bora. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Baelezee!

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, sasa hivi labda niseme, kule Jimboni kwangu Vwawa, hivi tunavyoongea leo tunachangia Wizara ya TAMISEMI. Eti nao Mwenyekiti ameitisha vikao vya Madiwani kule leo, nao wanaendelea eti wanaitisha vikao. Sasa Serikali ilishaelekeza, vikao vya Madiwani vitenganishwe na vikao vya Bunge. Mtaitishaje vikao hivyo? Kwa nini hayo yanafanyika? Yanafanyika kwa sababu ya maovu machache ambayo wanayafanya wengine, wanataka Waheshimiwa Wabunge tusishiriki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Jimboni kwangu kuna matatizo mengine makubwa na hapo naomba Serikali ichukue hatua. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Kabisa.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tume ziliundwa kuchunguza upotevu wa fedha zaidi ya mwaka mmoja hazijatoa majibu. Hiyo inakuwa ni dosari, hebu rekebisheni hayo. Pale kwetu kuna shilingi milioni 450 zimeenda kwenye miradi, watu wakagawana. Kuna shilingi milioni 680 za mradi wa maji Harungu, watu waligawana wakafanya uongo uongo, maji hayapo. Kuna shilingi milioni 320 za maji ya lhanda, maji hayapo, wananchi wanahitaji maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ubadhirifu mwingi! Shilingi bilioni 1.8 yamefanyika Mbozi, hebu tupieni jicho angalieni Wilaya ya Mbozi, angalieni yanayoendelea mchukue hatua ili wananchi waendeleo kuipenda Serikali yetu na wakipende Chama cha Mapinduzi na mimi naamini haya yanawezekana. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara hizi naomba sana mtusaidie, kule tunahitaji maji. Kuna vijiji kama kijiji cha lyula, Kijiji cha lyula B, Vijiji vya Iduwiri, Igale, Nanyara, Senjere, vinahitaji maji. Huu mradi ulifanyiwa upembuzi yakinifu kwa

muda mrefu haujatekelezwa. Tunaomba tusaidieni ili tuweze kuinua mazao mbalimbali likiwemo zao la kahawa tunaombeni sana hilo mtupe ushirikiano. Pia kuna mradi mwingine wa kutoka vijiji vya Lukururu, Mlangali, Mlowo ambao ungesaidia kuimarisha maji katika vijiji kama 14. Naombeni sana hilo mtusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Mji wa Vwawa pale pana shida ya maji, Makao Makuu ya Mkoa, hebu tusaidieni haya yaishe. Naomba pia sasa hivi kwa kuwa mmetupa Mkoa, naamini Mheshimiwa Waziri unanisikiliza vizuri kwamba umetupa Mkoa na nimewashukuru, sasa mtatupa na Manispaa ya Mkoa wa Songwe ambayo itakuwa Manispaa sijui ya Jimbo la Vwawa au ya Mbozi, yoyote ile. Tunaombeni hiyo haraka ili tutekeleze majukumu yetu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaomba kwenye ule Mkoa barabara za mkoa; barabara ambayo itaunganisha Wilaya ya Mbozi na Wilaya yetu mpya ya Songwe. Tunaomba ile barabara mtupe, mtusaidie ili tuweze kuitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda suala la afya, kwenye Wilaya ya Mbozi wananchi wamejitahidi sana, wamejenga maboma, wamejenga zahanati, wamekamilisha wanahitaji wafanyakazi, wanahitaji dawa, hayo hayafanyika mpaka sasa hivi. Hebu tuungeni mkono, jitahidini kutuletea watumishi wa afya ili angalau tuweze kukamilisha na wananchi wawe na imani kwamba sasa mambo yanakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo ningependa nilizungumzie ni suala la ripoti ya Mkaguzi wa Nje *(CAG)*. Nimeshangaa watu wengi wanaongelea sana hii *CAG report*. *CAG report* naomba Kamati maalum za kufuatilia...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Muda, muda wako umekwisha.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nashukuru sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ibrahim Raza ili tusawazishe uwiano.

MHE. IBRAHIM HASSANALI MOHAMMEDALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia Wizara ya Utawala Bora na TAMISEMI. Sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha hapa nikiwa mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na utawala bora, kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya na sisi wote tukiwa ni mashahidi, kwa muda mfupi kwa kweli ameweza kutuletea maendeleo ambayo sisi wote tumestaajabu katika kipindi kifupi sana Mheshimiwa Rais Magufuli ameweza kufanya mambo ambayo yametupa imani na wananchi wamekuwa na imani kubwa sana juu ya Mheshimiwa Rais. Nikitolea mfano, kwa mambo makubwa ambayo Mheshimiwa Rais ameweza kuyafanya katika muda mfupi, kwanza ni katika kupiga vita rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nchi hii ya Tanzania ilikuwa inanuka kwa rushwa, hakuna mtu ambaye alikuwa haelewi, lakini leo ukienda Wizara yoyote au taasisi yoyote ya Serikali, unahudumiwa bila kuambiwa kutoa chochote, hii kwa kweli imetujengea heshima kubwa sana. Zamani ukienda kwenye nafasi yoyote nyeti, kama mfuko wako mdogo, huwezi kufanikiwa kupata haki yako. Kwa hiyo, namshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kurejesha nidhamu katika taasisi za Serikali na katika Wizara za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuwaondoa watumishi hewa. Kwa kweli pesa zetu mabilioni ya pesa yalikuwa yanaliwa na watu wajanja sana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais amefanya kazi nzuri

kupitia Wizara yake ya Utawala Bora ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Kairuki, ni dada mmoja ambaye kwa kweli amepewa Wizara na ameweza kuimudu vizuri sana. Nampongeza sana dada yangu Mheshimiwa Kairuki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kuwaambia, anachofanya Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, anafanya kwa ajili yetu sisi, kwa sababu mambo anayofanya sasa hivi katika kipindi cha mwaka mmoja na nusu, fikiria baada ya miaka mitano Tanzania itabadilika, na sisi tunataka kwenda mbele, hatutaki kurudi nyuma. Ndiyo maana Mheshimiwa Rais amesisitiza kwamba maendeleo kwanza, Tanzania kwanza. Kwa hiyo, sisi Waheshimiwa Wabunge, bila kujali itikadi zetu za kisiasa, lazima tumuunge mkono Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina imani kubwa sana na Mheshimiwa Rais katika kipindi cha miaka mitano yatakuja mambo kubadilika Tanzania hii na tulishaanza kuona mabadiliko. Ameanza mambo ya reli kiwango cha *standard gauge*, ameshaanza kuleta ndege mbili, kuna ndege mbili nyingine zinakuja mwakani, mambo ya *flyover bridge* haya; Mheshimiwa Rais ameweza kufanya mambo chungu nzima! Sasa mnasema kwamba utawala, utawala gani mnaotaka nyie? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwamba tuwe wastahimilivu katika kipindi hiki ambacho Mheshimiwa Rais anataka kujenga Tanzania mpya. Mimi nazidi kumwomba Mungu ampe umri, ampe afya ili tupate maendeleo ambayo itakuwa siyo maendeleo yetu sisi bali ya vijukuu vyetu ambao ni Taifa letu la kesho. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija katika Wizara ya TAMISEMI, kwanza nampongeza sana ndugu yangu Mheshimiwa Simbachawene pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya. Kwa kweli masuala ya elimu, leo Watanzania watoto wao wanakwenda kusoma shule bure. Mtoto wakati wa miaka ya nyuma alikuwa hawezi kwenda kusoma kwa sababu alikuwa hana ada. Leo Mheshimiwa Rais amesema kwamba watoto wote wasome bure na

Mheshimiwa Rais kwa kupitia Wizara yake TAMISEMI, wamejitahidi sana kwamba leo asilimia 75 ya shule zetu zina madawati. *Seventy five percent*, hayo mengine *twenty five percent*, basi ma-desk yatakuja tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda cha kuwaomba TAMISEMI, ni kwamba watupatie na walimu wazuri ili watoto wetu wawe na *education* bora. Hapa walipofika TAMISEMI kwanza niwapongeze sana na *Inshallah* Mwenyezi Mungu atawapa nguvu Mheshimiwa Simbachawene na Naibu wake ili kuona kwamba elimu na kwa sababu elimu ndio ufunguo wa maisha, sasa watoto wetu watakapopata elimu nzuri basi naamini na Taifa hili tutakuwa na watoto wenye vipaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye masuala ya Jiji letu la Dar es Salaam, nataka kumwambia Mheshimiwa Simbachawene kwamba sasa Dar es Salaam unapokwenda mtaa wowote pale mjini kama mitaa ya Libya, Bibi Titi Mohamed, Samora ukienda wapi pamukuwa na ombaomba ambao sasa wameweka magodoro yao na usiku wanaweka vyandarua, wana lala kabisa, asubuhi wanaoga pale pale, kwa kweli mandhari ya Jiji la Dar es Salaam inapotea kabisa na kama huamini mimi nipo tayari kufuatana na wewe usiku nikakuonesha hali ilivyo Dar es Salaam. Wakati wa asubuhi inanuka kwa sababu pale pale wanamaliza haja zao. Mimi mwenyewe binafsi nimeshuhudia mtu asubuhi anafanya haja yake, anamwaga maji.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Simbachawene kupitia Jiji lako la Dar es Salaam naomba sana, itafika wakati Dar es Salaam patakuwa tena ni kama Bombay ya pili. Hali ni mbaya sana, mimi ninashangaa Jiji la Dar es Salaam, Manispaa ya Dar es Salaam wamekaa kimya, sijui hawaoni! Ni kitu cha ajabu sana. *(Makofi)*

Vilevile wenzetu ambao wanafanya biashara ya nyama choma, kuku choma na chips, usiku wanakuja wanavunjiwa meza, wanavunjiwa viti na wanachukuliwa na wanadaiwa rushwa. Hivi juzi wamechukuliwa wafanyabiashara wote, wamepelekwa pale Manispaa, wamedaiwa rushwa na wametoa na ushahidi upo.

Mheshimiwa Rais Magufuli anajitahidi kupiga vita rushwa lakini bado watu katika kudai rushwa. Kwa hiyo, nilikuwa nakuomba Mheshimiwa Simbachawebe hawa watu ambao wanawekeza usiku wapo tayari kulipa kama kuweka viti, meza wapo tayari kulipa na mimi nitakupa mfano mmoja wa Bangkok, na hivi karibuni nilikuwa huko. Kuna mitaa fulani ikifika saa 12.00 wanaruhusiwa kuchoma nyama, kuku, chipis na kuweka nguo mpaka usiku saa 6.00 usiku, lakini hawapigwi wala hawatozwi rushwa. Hawa wenzetu wa Dar es Salaam, baada ya saa 12.00 jioni wapo tayari kulipa hata shilingi 500,000 au 1,000,000 kwa mwezi, lakini kila unapoenda kudai kibali, hawapewi wanazungushwa na matokeo yake wanakuja kudaiwa rushwa. Mheshimiwa Simbachawene, hili vilevile wanaipaka Serikali yetu matope.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu inafanya kazi nzuri lakini kuna baadhi ya watu wanaiharibu sifa ya Serikali yetu kwa tamaa yao tu na ubinafsi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwa Wizara ya TAMISEMI ni kuhusu hao wenzetu wanaopewa *parking* za magari, ni ruksa. Wanapewa kuanzia saa 2.00 asubuhi mpaka 12.00 jioni lakini utakuta mtu anamiliki *parking* saa 24, lakini ukimwambia muda hapa saa 12.00 jioni ondoa *parking* yako muda umekwisha, anakwambia hapana, mimi nimelipia. Hujalipia kwa saa 24. Mheshimiwa Simbachawene imekuwa ni matatizo ya *parking* Dar es Salaam ni sugu sana. Watu ikifika saa 12.00 jioni tunaomba uwaambie Manispaa waondoe kile kibao chake, kichukuliwe... (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. IBRAHIM HASSANALI MOHAMMEDALI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja Wizara zote mbili, Wizara ya Utawala Bora na TAMISEMI. Nakusuhuru sana kaka yangu Chenge.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lusinde.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili na mimi nichangie kuhusu hizi Wizara mbili. Wabunge wengi wamepongeza na mimi nawaunga mkono kwa pongezi walizotoa kwa Waheshimiwa Mawaziri kwa uchapakazi na hata zile tahadhari zilizotolewa kuhusu namna gani wanatakiwa kukaza buti kwa ajili ya kuhakikisha Taifa linasonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hizi ni Wizara nyeti sana na zimepewa watu barabara kabisa ambao wanafanya kazi kwa ufanisi na weledi mkubwa. Kazi yetu siis kama Wabunge ni kujaribu kuonesha ni maeneo gani Serikali iyatilie mkazo na ni maeneo gani yanahitaji uangalifu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mbunge kutoka jimbo la Mtera na ni jimbo la vijijini, naiomba Serikali itazame kwa jicho la huruma sana majimbo ya vijijini. Hata hili ongezeko la watu mijini tunalolisema linatokana na vijijini kukosa huduma nyingi za msingi, huduma nyingi za msingi zikipatikana vijijini, nataka niwahakikishie mlundikano wa watu mijini utapungua kwa kiwango kikubwa. Tukizungumzia maji safi tunazungumzia mjini, tukizungumzia umeme wa uhakika, tunazungumzia mjini na tukizungumzia matibabu ya uhakika tunazungumzia mjini. Vijijini watu hawatakaa, watakimbilila mijini ili waje wapate huduma hizo muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namuomba sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, suala la kuhakikisha kila kata, hata ikiwezekana kila tarafa ipate kituo cha afya cha uhakika, gari la kubeba wagonjwa la uhakika, hii itasababisha watu wabaki vijijini na wasukume mbele gurudumu la maendeleo. Tukiweka bajeti kubwa za maji mijini, tukaweka bajeti kubwa za afya mijini, watu wa vijijini hakuna namna yoyote ya kuwaacha wao wakae vijijini wasije huko mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie barabara. Barabara za vijijini Halmashauri nyingi hazina uwezo wa kuzitengeneza. Uharibifu wa barabara ni mkubwa! Kuna majimbo ni makubwa mno. Kwa mfano, Jimbo langu mimi, ukitoka hapa ilipodondoka treni wakati ule, ukatoka Igandu mpaka mwisho Ilanga kuna kilometa zaidi ya 220; haiwezekani *ambulance* ziwe mbili au moja, inachakaa haraka kabla ya muda, kwa sababu inapita kwenye barabara mbovu halafu hazitoshi *ambulance* zenyewe. Kwa hiyo, naiomba Wizara ya TAMISEMI ihakikishe inatoa msukumo mkubwa kwenye bajeti za kutengeneza barabara za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumza na Waheshimiwa Wabunge hapa, wamesema sana kuhusu Halmashauri zetu, kwa Waheshimiwa Madiwani. Tunawapozungumzia Waheshimiwa Madiwani kuna baadhi ya Halmashauri Madiwani wana hali mbaya, hata posho zao zile stahili zao hawapati, sembuse hiyo ya kuongeza! Hawapati hata zile za ndani za kwao. Wanakopwa kuendesha vikao, kwa sababu ya ugumu wa Halmashauri; katika vyanzo vya mapato wengine wanategemea kilimo; ukame umekuja, hawawezi kukusanya mapato ya ndani. Kwa hiyo, hata hiyo asilimia 10 tunazosema wapewe akina mama na vijana haziwezi kupatikana kwa sababu Halmashauri hazina makusanyo ya kutosha. Zile kodi za kero zilizofutwa, hakikisheni Serikali mnazifidia kuzilipa Halmashauri ili zipate uwezo wa kujiendesha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nazungumza sana kuhusu mapato ya Madiwani, tukiyaboresha Diwani ndio anayezika, anauguza, anasomesha. Akibaki na mapato yake madogo Diwani anakimbilia kwa Mbunge, anamkuta vilevile naye yupo taabani, inakuwa shida kubwa sana kuendesha majimbo. Kwa hiyo, naomba sana Waheshimiwa Madiwani wapewe uangalizi mkubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia maji. Miradi ya maji inasuasua sana. Ukienda unakuta hela ipo. Nauzungumzia mradi wa Kata ya Manzase, umechukua muda

mrefu sana. Tumempeleka Katibu Mkuu wa CCM, tumempeleka Waziri Mkuu, Mzee Pinda na ndio alikuwa aifungue, imeshindikana. Leo ukienda anakwambia *BOQ* imefanyaje; ukienda wanakwambia mkandarasi sijui amefanyaje, wananchi hawataki kusikia maneno, wanataka kuona wanapata huduma ya maji safi na salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, imefika wakati mpaka wananchi wanakata tama. Mheshimiwa Jafo kaenda pale kasukuma akaweka na tarehe, lakini bado. Wanakwambia sijui tutangaze tenda upya, tubadili kutoka mfumo wa *diesel* kwenda *solar*, maneno hayatusaidii, tunataka maji katika katika Kata ya Manzase, hatutaki maneno. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumze kwa utulivu sana kwenye suala la ulinzi na usalama; nadhani juzi siku pata muda wa kutosha. Nashauri Serikali iunde dawati kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani au Wizara yoyote, ambalo wananchi watakwenda kuripoti pale juu ya ndugu zao waliopotea. Tusizungumze pale anapopotea mtu maarufu tu, Watanzania wengi sana wamepotea katika mazingira ambayo watu wengi hawajui wako wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tengenezeni dawati halafu mruhusu wananchi waje watoe taarifa za upotevu wa ndugu zao, mtashangaa idadi ya watu waliopotea bila taarifa.

Kwa hiyo, nashauri Serikali badala ya kulaumiana sisi wenyewe sijui kuna kikundi kinafanya nini, nilisema juzi mimi mwenyewe ni muhanga, nina mjomba wangu anaitwa Nikanoli, aliondoka mwaka 1980 mpaka leo hatujui yuko wapi. Wala siyo maarufu, wala hakuwa Balozi wa Nyumba Kumi useme ametekwa; aliondoka akapotea. Yupo mwingine alikuwa anaitwa Yoel, ameondoka tangu miaka ya 1970, hata kumjua watu hawamjui. Kwa hiyo, ukienda kwa kila Mbunge inawezekana ukakutana na taarifa za upotevu wa watu kwenye majimbo mengi sana, kama siyo yote. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali, badala ya kuanza kushutumiana sijui nani anafanya nini, tutengeneze dawati watu wapeleke habari za upotevu wa ndugu zao, za upotevu wa jamaa zao ili waweze kutafutwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge hapa tunazungumzia juu ya heshima na Daktari tena kazungumza vizuri sana. Daktari akasema tubadilisha fikra na huu ni mchango wake karibu wa pili anatushauri tubadilisha fikra kwamba tuwe na mtazamo mpya. Sina hakika kama yeye anao, lakini anasema katika huo mtazamo mpya, tuache kushughulika na watu wadogo wanaomtukana Mheshimiwa Rais. Ila Daktari huyo huyo anayetaka tubadilisha fikra, anasema Kiongozi wa Upinzani aheshimiwe ni mtu mkubwa. Mheshimiwa Rais atukanwe, Mheshimiwa Mbowe aheshimiwe, hatuwezi kwenda hivyo! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunataka heshima, turudi kwenye Katiba inayosema kila mtu anastahili heshima, bila kuangalia cheo chake. Watanzania wanastahili heshima, Mheshimiwa Rais anastahili heshima, Kiongozi wa Upinzani anastahili heshima, Mbunge anastahili heshima, Diwani anastahili heshima. Tutaheshimiana na tutaona kuendesha nchi ni kazi rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukibadili fikra zetu tukaacha eti watu wadogo wadogo wanamtukana Mheshimiwa Rais kwenye simu, hao tusishuhulike nao, ila tushughulike na viongozi waliotengeneza, aaah, sidhani kama ni sawa sawa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nalishauri Bunge hili, kama tunataka kutoka hapa tulipo, kwanza kuna baadhi ya mazoea tuyaache. Pale tunaposema tunahitaji mabadiliko kwenye nyanja fulani, nina hakika kabisa Mheshimiwa Rais anafanya kazi nzuri kabisa ya kubadilisha mfumo wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi yetu kubwa badala ya kumrudisha nyuma tumpe moyo, tumtie nguvu, Mawaziri

tuwape moyo, tuwatie nguvu wasukume gurudumu mbele. Nani asiyejua maeneo mengi yaliyokuwa yamesimama? Wizara kama ya Ardhi ilikuwa na matatizo chungu nzima! Tulikuwa na kesi chungu nzima, lakini sasa hivi zinatatuliwa kwa *speed* kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe sana, tunapozungumzia heshima tuzungumze pande zote mbili. Nataka niseme kwamba, jana ilitolewa hoja hapa, watu wameidharau na wengine wakaona kama inachomekwa. Nasikia ninyi mna vyombo hapa mnaweza kutuambia, kuna Mbunge amekamatwa na konyagi anaingia nayo Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi juzi hapa Serikali imemwajibisha Kitwanga kwa kudhaniwa tu amelewa, akawajibishwa. Leo Mbunge anaingia na konyagi ndani ya Ukumbi wa Bunge, huko amekamatwa. Tunataka tuone na ninyi meno yenu yako wapi katika kumwajibisha huyo Mbunge, kama mtaweza! Maana kazi yenu ni kusema tu, siyo kutenda. Bahati nzuri Mbunge mwenyewe anatoka upande huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka tuone mtakuwa wakali kwa kiwango gani kwa Mbunge anayeingia amelewa, halafu ana chupa ya konyagi ndani ya eneo la uzio wa Bunge! Sisi tumeshaonyesha njia, Mheshimiwa Waziri amekuja anatikisika, hana chupa, hana nini, mkasema ooh, amelewa sijui nini na Uwaziri kaupoteza. Ninyi sasa tuone sasa mtachukua hatua gani ili...*(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MBUNGE FULANI: Aendelee. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na nianze kwa kuunga mkono hoja na vilevile kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI na mwenzake wa Utumishi na Utawala Bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamesemwa mengi hapa ambayo yanahitaji ufafanuzi ili tusiupotoshe umma. La kwanza ni kauli tuliyoanza kuisikia jana hapa, imesemwa kwa nguvu hapa, ooh, Mawaziri wa Tanzania ni waoga, hawana ujasiri. Nimekuwa najiuliza, ujasiri wa aina gani? Wa kumkaidi Waziri Mkuu? Kumkaidi Rais? Ujasiri upi wa kukataa pengine *three-line whip?* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni hivyo, umeona wapi dunia ya leo ambapo Mawaziri hawaongozwi na kanuni ya kuwajibika kwa pamoja Bungeni katika *Parliamentary system*? Hii ndiyo inaitwa *collective responsibility*, siyo kwamba tumeiokota tu, iko katika Katiba, twende Ibara ya 53.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 53(2) inasema: “Mawaziri, chini ya uongozi wa Waziri Mkuu watawajibika kwa pamoja Bungeni.” Sasa tnapowajibika kwa pamoja Bungeni, aah, hawa sio majasiri.

MBUNGE FULANI: Waoga!

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Nyie mkija kuunda Serikali, maana ni mwaka 2090 huko, bahati nzuri mimi sitakuwepo. Mtakuwa watu gani ambao mna Serikali moja kila mtu anaongea la kwake? Siyo hivyo tu, Waziri Mkuu mwenyewe ambaye sisi tunafanya kazi chini yake, Katiba inasema 53(1), Waziri Mkuu atawajibika kwa Rais kuhusu utekelezaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo *chain* ya *accountability* katika Serikali. Kwa hiyo, tusiwapotoshe wananchi, waoga, tunaogopa kitu gani? Mmeona mtu yeyote anayetemeka hapa? Hatuogopi chochote hapa. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashangaa sana, tunapenda kuongelea wenzetu wakati sisi wenyewe tuna...; mimi nimeona, Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni alipoingia hapa, watu mpaka mikanda inalegea, wanayetemeka hapa, kimya! Sisi leo kumheshimu Waziri Mkuu wetu ambapo tuna wajibu, lazima tutamheshimu. Lazima! *It is our obligation*, ni kitu cha ajabu! Tuache mizaha hapa, wananchi wanatuzikiliza, wanatuona *we are not serious*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, suala la Richmond, hili suala limebuliwa jana na Mbunge wa Arumeru Mashariki Mheshimiwa Nassari kwamba Kamati Teule iliyochunguza suala hilo haikumtendea haki Mheshimiwa Edward Lowassa kwa sababu haikumhoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naelewa, ni kazi ngumu sana leo hii kutaka kumsafisha Mheshimiwa Edward Lowassa kutokana na kesi ya Richmond ambayo ilishakwisha. Ndiyo maana sioni ajabu ili kusema aliyosema, ilibidi Mheshimiwa Nassari anywe pombe kwanza. Ninayasema haya Kiongozi wa Upinzani Bungeni ajue kwamba tuna tatizo hilo. Na mimi ninawapongeza sana vijana wetu wa Usalama waliokamata hiyo chupa hapo. Maana angeruhusiwa na hiyo chupa, huenda hata angetapikia rangi zetu za Taifa humu ndani, ingekuwa ni *scandal* kubwa kabisa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeelezea mara nyingi sana katika Bunge hili, hata Bunge la tisa lililoshughulikia suala la Richmond kuwa Kamati Teule iliyoundwa na Bunge hili kazi yake ilikuwa kuchunguza, siyo kutoa maamuzi. Unapochunguza *requirement* ya *audi alteram partem* rule, hiyo *requirement* haipo pale wakati wa uchunguzi; ipo wakati wa maamuzi. Ndiyo maana sisi tulikuja hapa tukaleta kesi hapa tukiwa na mashahidi zaidi ya arobaini wakisubiri nje.

Aliyetakiwa kuhojiwa hapa, akajiuzulu. Unamlaumu Mwakyembe kwa hilo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba msipotoshe umma. Ooh, hakuhojiwa. Ahojiwe vipi? Unajua ni aibu! Ni sawa na mtu anaenda mahakamani, anasema unajua polisi hawakunipa haki ya kuhojiwa. Polisi? Upo Mahakamani ndipo pakuhojiwa hapo. Pakuhojiwa ilikuwa hapa! Kwa hiyo ndugu zangu, naomba tusipotoshe watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tulipata nyaraka za Serikali 104; na tukahoji watu 75, tuliwauliza maswali 2,717. Ipo kwenye *Hansard!* Hatukuona sababu yoyote ya kumwita Mheshimiwa Lowassa. Hatukuona! Tulikuwa na kila kitu, tulikuwa na ushahidi wote. Naomba kama kuna mtu yeyote hapa bado anakereketwa na kesi ya Richmond, aache maneno maneno hapa, alete hiyo kesi iibuliwe kama hatutawanyoa nywele kwa vipande vya chupa, ilete hapa! Acha maneno ya kienyeji hapa! Tumeshachoka! *We are tired of this!* Jamani eeh, ileteni hiyo kesi hapa, mnaruhusiwa na kanuni. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwamba, mimi naahidi, siku ambayo kuna moja atakuwa jasiri hapa kusema nalileta suala la Richmond lirudiwe tena, mimi nitamwomba Mheshimiwa Rais anipumzishe Uwaziri niweze kuishughulikia hii kesi sasa kikamilifu iishe moja kwa moja. (*Makofi*)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja nyingine aliyoleta hapa kuwa kwenye *Ph.D Thesis* yangu nilikiri kuhusu Serikali tatu, lakini sasa hivi nasema Serikali mbili.

Anyway, la kwanza ni kwamba kwanza alilewa ndiyo maana alikuwa anasema tu hayo, maana ameambiwa, hajasoma hata hiyo *Ph.D Thesis*, lakini la pili ni kwamba watu wanaelewa watu wenye *integrity*, watu wasio na *integrity* tunawajua hapa ambao wanakesha miaka mitano kumtukana mtu kumwita fisadi, leo wanamkumbatia, wanalamba na nyayo zake, ndio vigeugeu namba moja hao! Halafu leo mnajidai kuja kumsafisha! Huwezi ukasafisha madoa ya lami eti kwa kutumia kamba ya katani au maji, haiwezekani! Lileteni hili suala hapa tulimalize. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu kwamba katika hiyo *Ph.D Thesis* zaidi ya kulasa mia 400 nili...

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu!

MWENYEKITI: Kuhusu Utaratibu, kifungu kipi?

Mheshimiwa Waziri, kaa kidogo. Ehe, Kuhusu Utaratibu. Kifungu kipi?

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1)(a) inasema Mbunge bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli. Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe sasa hivi wakati akizungumza...

MWENYEKITI: Isome na Kanuni ya 63(3).

MHE. SAED A. KUBENEA: *Yes!*

MWENYEKITI: Isome na Kanuni ya 63(3).

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 63(3)... (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Shuka ya nne ili tuokoe muda. (*Kicheko*)

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sikusikii, Kanuni ya ngapi? Sikusikii!

WABUNGE FULANI: Uyooo! (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Nasema hivi, umeanza vizuri 64(1)(a), iunganishe sasa kwa sababu umesema ni taarifa ambayo haina uhakika, nenda nayo sasa ukasome 63(4).

MHE. SAED A. KUBENEA: Kanuni ya 63(4) inasema; "Mbunge anayetoa madai kwamba kwa mujibu wa fasili ya (3) ya Kanuni atakuwa na wajibu wa kuthibitisha ukweli kuhusu jambo au suala hilo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge."

WABUNGE FULANI: Aaaah!

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao ushahidi. Ninazungumza mambo mawili ambayo Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe ameyazungumza kwenye Bunge hili. Jambo la kwanza amezungumza juu ya suala la Richmond.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ripoti ya Kamati Teule ya Bunge, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe akiwa Mwenyekiti wa Kamati Teule, aliliambia Bunge hili Tukufu kwamba mtu anaweza kuwajibika kwa mambo mawili; moja, kwa kuwa yeye mwenyewe alihusika ama pili, kwa kuwajibika kwa mambo yaliyofanywa na walio chini yake. Kwa mujibu wa *Hansard* za Bunge, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe alisema Mheshimiwa Edward Lowassa alijiuzulu kwa mambo yaliyofanywa na walio chini yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe anasema ana ushahidi wa asilimia 100 kwamba Mheshimiwa Edward Lowassa alihusika mia kwa mia na jambo hilo. Kwa hiyo, sasa naomba kwa idhini yako unipe muda niwasilishe *Hansard* hapa kwenye Bunge hili

kuthibitisha maneno ya Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe ya mwezi Februari, 2008; hilo la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, hapo hapo kwa Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe; ameliambia Bunge kwamba Mheshimiwa Joshua Nassari, jana alikuwa na konyagi, aliingia nayo Bungeni. Siyo kweli! Nina uwezo wa kuthibitishia Bunge hili kwamba Mheshimiwa Joshua Nassari jana hakuwa amelewa, tulikuwa naye mchana kutwa na alikuwa amekuja Bungeni na soda iliyoko kwenye chupa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hilo naweza kulithibitishia Bunge hili Tukufu, nakushukuru.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu.

Mheshimiwa Kubenea ameyasema hayo. La pili la Mheshimiwa Nasali kiti kilivyosikia; na kama nitakuwa nimesikia vibaya, *Hansard* ipo. Ni kwamba katika maeneo ya Bunge, siyo humu ndani kwamba ameingia na chupa aliyodaiwa kuwa ina konyagi. Kwa hiyo, hajasema kwamba aliingia nayo humu ndani, hilo la kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, la pili, kuhusu Richmond ni uamuzi wa Bunge. Kama mtu anataka kufufua hoja hiyo, taratibu zetu za kikanuni ziko wazi. Lete hoja hiyo kwa taratibu ambazo zinakubalika, Bunge lenyewe litapima hoja hiyo. Huo ndiyo uamuzi wangu. Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe endelea kuchangia, muda wako umelindwa. (*Makofi*)

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, WASANII NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

Mimi nafikiri niendeleo moja kwa moja tu, nimeshazoea changamoto za uelewa za Mheshimiwa Kubenea. Naomba niseme tu kwamba katika ile *thesis* yangu, naongelea kuhusu mfumo wa *two governments, three jurisdictions*; na mfumo huo katika hiyo *thesis* tunasema *it is*

not sui generis; siyo pekee, inatumika katika mataifa mbalimbali yanayotaka ku-*partner* yakiwa na tofauti kubwa sana ya ukubwa wa eneo, yakiwa na tofauti kubwa sana ya idadi ya watu, yakiwa na tofauti kubwa sana ya rasilimali watu na vilevile maliasili, ndiyo unatumika huo utaratibu. Sasa soma yote, kurukaruka tu, hutaelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema tu kwamba *it is a federal variant*, ndiyo hoja kubwa katika hiyo *thesis*. Kwa hiyo, naomba tu bwana mdogo akipata muda asome kama atapata muda, mimi sijui, mtoto wa Mchungaji yule lakini ndiyo hivyo, ameingia hapa na kachupa ka pombe. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie suala la mwisho. Naomba nirudie tena, wengine hapa katika kupambana na udhalimu, kupambana na matendo mbalimbali, sisi wengine hapa tumeumia sana, unapoleta masuala hapa kimzaha mzaha; tutakujibu *to the maximum*. Mimi *I am ready for anything*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba akina Mheshimiwa Kubenea na magazeti yao, leteni kesi ya Richmond hapa, nawaomba, chonde chonde, ileteni hapa! Jamani, naomba kwa Mungu, mkiileta hapa, nitafurahi! Kwa sababu ninachosema hapa na ushahidi nilionao hapa ni kwamba sisi tulimkuta huyu jamaa *in flagrante delicto*, ndivyo wanasema wanasheria, *we have everything* na mpaka leo hatujafa, tutakuwa hapa kuthibitisha hilo suala.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa. Anapotosha huyu!

MWENYEKITI: Mheshimiwa kaa chini. Hebu kaa chini Mheshimiwa.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, WASANII NA MICHEZO: Kwa sababu mmekuwa na makubaliano ya kumsafisha, hamtaweza kumsafisha. Leteni kesihapa! *(Kicheko/Makofi)*

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, Taarifa.
(Makofi)

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa
Mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Muda wako umekwisha. Mheshimiwa
Dkt. Mwakyembe, muda wako umekwisha.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mnajua Mheshimiwa Jakaya
Kikwete anahusika?

MWENYEKITI: Mheshimiwa AG!

MBUNGE FULANI: Kaa wewe kaa!

MHE. ESTER A. BULAYA: Kama wengine walikuwa
wanaleta siri upinzani, wewe kigeugeu tunakujua!

MBUNGE FULANI: CCJ.

MWENYEKITI: Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa
Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kunipa
fursa na mimi niweze kuchangia hapa. Nakushukuru wewe
pia kwa kunipa nafasi hii.

Pia nachukua nafasi hii kumpongeza sana Rais wa
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa utendaji wake wa
ufanisi uliotukuka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza na Mawaziri
wawili wanaomsaidia na timu nzima ya ofisi yake na
watendaji wote kwa hotuba nzuri ambayo imeonesha
mambo ambayo Serikali imeyafanya katika mwaka huu na
inayokusudia kuyafanya mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo,
naomba kushauri mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili suala la utekaji nyara na mambo ya hofu, yanajitokeza sana hapa na sijui ni kwa nini? Naomba kushauri kwamba polisi waendeleo kushirikana na watu walio karibu sana na huyu mtu anayedaiwa amepotea. Waisaidie polisi ili tupate ukweli; kwanza familia yake, watu ambao amekuwa akifanya nao kazi kwa karibu, watoe ushirikiano kama ambavyo Bunge wameshauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala hili hatuwezi kuwa na *double standard*. Kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 26, kila mmoja anawajibika kutii Katiba na sheria ya nchi. Mheshimiwa Mbowe ametusaidia, kwenye hotuba yake amesema hakuna aliye juu ya sheria. Moja, akatueleza tangu huyu mtu anayedaiwa kupotea au kufariki. Alipopotea, ilichukua muda gani kutoa taarifa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu familia au watu waliokuwa karibu na huyu mtu, kwa mfano, wameshapeleka taarifa kwenye vyombo vya habari kwamba huyu mtu labda amepotea, hebu mtu yeyote aliyopo kwenye *public* atusaidie, *then tu-take action accordingly*. Mimi ninavyojua polisi ilivyokuwa inafanya kazi, siku hizi wanafanyaje kazi? Sasa hivi tungekuwa na watu wanaisaidia polisi kwa karibu mno! Sasa *this is how we can handle this matter so much successful*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabla hatujaenda huko *Scotland Yard*, watu waliokuwa wanafanya kazi kwa karibu na familia yake, watoe taarifa, vyombo vyetu vifanyie kazi kwa karibu mno, hilo ni la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, hili siyo suala la uhuru wa mijadala humu Bungeni. Ibara ile ya 100 uisome ina vifungu viwili vidogo; kifungu cha kwanza na cha pili, hata uhuru wa mijadala, haukuwekwa uhuru wa haki ya kuvunja sheria. Ukisoma Ibara ndogo ya (1) na ya (2), unayo hiyo haki tu kama katika mjadala wa kutekeleza majukumu yako ya Kibunge unazingatia Katiba na Sheria za nchi, la sivyo, basi

wewe ungekuwa tu unaua mtu, unapiga mtu, unasema mimi nina haki sijui ya nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri tusitumie vibaya uhuru wa mijadala. Hata huku kutangazwa, wanaita matangazo mubashara, someni Ibara ya 100 kama ipo hiyo haki. Someni Sheria ya Haki, Kinga na Mamlaka za Bunge kama ipo hiyo haki ya kutangaza mubashara. Someni Kanuni 143, haki tuliyonayo ni ya Taarifa za Bunge. Ibara ya 18 ya Katiba inatoa haki ya watu kupewa taarifa na mpaka sasa hivi Serikali haijakataza vyombo vya habari kuripoti mambo yanayoendelea humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja niwashauri Waheshimiwa Wabunge, kama mnataka kurudi katika Bunge hili, tetedni mambo yanayowanufaisha wapigakura wenu. Bunge la mwaka 2015 lilikuwa na hiyo *live broadcasting*, lakini Wabunge wengi hawakurudi. Kitakachowafanya watu wenu wawakubali ni yale mnayotekeleza. Matangazo mubashara hayasaidii chochote, eeh! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kuna hoja imezungumzwa jana hapa, ni aibu! Unasema Serikali hii inaongozwa na watu wasio *competent; how can this be?* Serikali ni nini? Huyu Rais mwenyewe amekuwemo Bungeni humu tangu mwaka 1995. Mawaziri wanaomsaidia wengi walikuwepo hapa; sisi watumishi wa umma tumekuwemo humu. Mimi nimeanza kazi mwaka 1994. Kinachobadilika ni wanasiasa; nanyi wenyewe mlienda kwenye kura. Mkashindwanishwa walio na uzoefu na wasio na uzoefu. Walio na uzoefu wakashinda, ndiyo wameunda Serikali, mnasema *they are not competent. How can this be? This is not seriously at all, we need to be serious!* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyo Rais mnayemsema, mimi nilikuwepo pale Ubungo mwezi jana, siku linawekwa jiwe kwenye ujenzi wa barabara sijui mnaita ya magorofa, yule Rais wa Benki ya Dunia alisema hivi; "mimi nimekuja Tanzania kwa sababu huko duniani viongozi wanasema

nenda Tanzania kwanza.” Hatujisifu! Leo udhaifu wa aina gani? Naweza kusema hivyo. *(Kicheko/Makofi)*

MWENYEKITI: *Order* Waheshimiwa Wabunge! Tumpe heshima Mwanasheria Mkuu wa Serikali ayaseme yale anayotaka kusema. *(Makofi)*

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoweza kushauri Bunge lako Tukufu ni kwamba Serikali hii inaongozwa na watu wanaomudu majukumu yao kwa ufanisi ipasavyo na ndiyo maana imeweza kutekeleza mambo hayo katika muda ambao haujafiakia hata miaka miwili na Serikali imeripoti kupita hizi Wizara mbili na Ofisi ya Waziri Mkuu *so far* na mwenye macho haambiwi tazama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba nimemsikia Mheshimwia amesema huu ushirikiano mnaoutaka Serikali ni lazima uanzie humu Bungeni, uta-*extend* mpaka kwenye majimbo yenu. Hamwezi mkawatukana Mawaziri hapa, *Attorney General* mnamtukana, Waziri mnamtukana halafu kesho mnasema aje Jimboni kwako, aje kufanya nini? *(Kicheko/Makofi)*

MBUNGE FULANI: Vunja, vunja, vunja! *(Kicheko/Makofi)*

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuwe *courtesy*. Ni naomba kushauri, Serikali kwa maana ya mihimili yote ya dola, *I am talking about the government now*.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: *Executive, Judiciary and Legislation*.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Kaa chini.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Taarifa Mheshimiwa Mweyekiti.

MWENYEKITI: Mheshimiwa kaa chini. Nakuomba ukae chini.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Anatumkana!

MWENYEKITI: Nakuomba ukae chini.

MBUNGE FULANI: Mnamwitia nini Jimboni?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Kwanza wewe unasema Waziri hayuko *competent*, mnamwitia nini Jimboni? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba kushauri jambo hili, Serikali kwa maana ya *government* haiwezi kuruhusu watu wachache wakaharibu mustakabali wa Taifa hili ama kwa vitendo au kwa kauli zao au kwa mienendo zao, ni lazima turudishe nidhamu ndani ya Bunge hili. (*Kicheko/Makofi*)

MBUNGE FULANI: Uko sawa. (*Makofi/Kicheko*)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Ni lazima amani na usalama vitawale. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Waheshimia Wabunge, naomba utulivu ndani ya ukumbi wa Bunge. (*Kicheko/Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nashukuru kwa michango yenu, hatua ya kwanza hiyo. Mchana tutaanza na Mheshimiwa Jafo, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, atachangia kwa dakika 15 *then* watoa hoja wataingia; Mheshimiwa Simbachawene na Mheshimiwa Kairuki.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo, kuna orodha ya nyongeza ya shughuli za leo ambayo ndiyo inagawiwa sasa hivi, nitaomba muipitie kwa sababu kutakuwa na hati ya kuwasilisha mezani ambayo itawasilishwa tutakaporejea saa 11.00 jioni.

Baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge kwa sasa mpaka saa 11.00 jioni.

(Saa 7.00 mchana Bunge lilitishwa mpaka saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilitudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu!

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

MWENYEKITI: Hati ya kuwasilisha mezani!

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud nakuomba uketi.

Waheshimiwa Wabunge, tumepewa Orodha ya Nyongeza ya Shughuli za leo, kwa hiyo, namwita Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Naibu Waziri, Mheshimiwa Joel Mpina.

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani:-

**NAIBU WAZIRI OFISI YA MAKAMU WA RAIS MUUNGANO
NA MAZINGIRA:**

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira Fungu la 26 Sita na 31 kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018.

MWENYEKITI: Ahsante. Katibu!

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 - Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora

(Majadiliano yanaendelea)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Jafo, Naibu Waziri – TAMISEMI una dakika 15.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Muumba Mbingu na Nchi ambayo ametuwezesha katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuweza kupata fursa kuwasilisha hoja yetu hapa na Wabunge wamechangia, lakini pia napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye kwa imani yake kwangu amenipa fursa ya kuhudumu katika Ofisi hii ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kipindi chote hiki. Kwa kweli Mheshimiwa Rais, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa imani yake kwa uongozi wake. Sambamba na hilo pia napenda kumshukuru Waziri wetu Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania Mheshimiwa Majaliwa kwa fursa kubwa anayotupa sisi wasaidizi wake tukiwa humu Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimshukuru kipekee, Waziri wangu mwenye dhamana, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene kwa maelekezo mazuri, lakini umekuwa sio Waziri peke yake isipokuwa umekuwa kama kaka kwangu, pia ni kocha unayenipa fursa ya kuweza kutimiza majukumu yetu katika ofisi hii kubwa ambayo inawakilisha wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Namshukuru sana Waziri wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Spika wetu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Job Ndugai, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge na viongozi wote wa Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia napenda sana kumshukuru Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Serikali za Mitaa na Utawala, ndugu yetu Mheshimiwa Rweikiza pamoja na Kamati yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii ndiyo Kamati pekee ambayo ukija kuiangalia inajadili mafungu yapatayo 28. Kwa kweli tunawashukuru sana na timu yako kwa msaada mkubwa katika ofisi yetu. Hatuna cha kuwalipa, mmekuwa Walimu, mmekuwa waelekezaji wazuri mpaka leo hii tunapohitimisha hoja yetu hii ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, nitoe shukrani zangu za dhati kwa watumishi wote wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ushirikiano wao mzuri, kwa upendo wao, wametusaidia sana na kaka yangu Mheshimiwa Simbachawene kuhakikisha kwamba tunatekeleza majukumu yetu katika kipindi hiki cha mwaka huu na mpaka leo hii tunakuja kuomba sasa Bajeti nyingine ya mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru familia yangu; namshukuru mama yangu mzazi kwa malezi mazuri.

Kwa kweli nawakumbuka sana na ninajua mmeni-*miss* sana, lakini yote hii ni kwa ajili ya kulitumikia Taifa letu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Kisarawe kwa msaada na dua zao njema siku zote wanaoniombea ninapotimiza majukumu yangu nikiwa hapa Bungeni, nikiwa Jimboni halikadhalika, nikiwa maeneo mbalimbali kuhakikisha kwamba dhamana aliyotupa Mheshimiwa Rais tunaitekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Wajumbe tukiwasilisha hoja yetu, Waziri wangu mwenye dhamana akiwasilisha hoja hii, tulipata fursa ya kubaini michango mbalimbali ikitoka kwa Waheshimiwa Wabunge, nami niliyojifunza katika haya ni jambo moja kubwa. Lengo kubwa la Wabunge ni kuona Ofisi hii inaweza kufanya kazi yake vizuri na Wabunge wengi sana walijielekeza katika suala zima la sekta ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ukija kuangalia, nami nimepata fursa ya kutembelea maeneo mbalimbali. Nilipotembelea kweli katika nchi yetu hii, ukienda maeneo mbalimbali utakuja kubaini kwamba sekta ya afya ina changamoto kubwa. Ndiyo maana kiongozi wangu akinituma nipite sehemu mbalimbali, tumeweza kuzibaini na ndiyo maana humu tunapangia mipango ya pamoja, nini tufanye ili mradi twende mbele zaidi na tunajua wazi kwamba, nchi yetu ambayo tulikuwa tunataka katika Sera yetu ya Afya kuwe na ujenzi wa zahanati takriban kila kijiji, tulipaswa kujenga zahanati 12,545, lakini mpaka sasa hivi tumefikia zahanati 4,470.

Halikadhalika katika vituo vya afya, tulikuwa na sababu ya kuweza kujenga vituo vya afya 4,420, lakini mpaka leo hii tumejenga vituo vya afya 507. Kwa hiyo, tuna kazi kubwa sana ya kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hospitali zetu za Wilaya, kati ya Wilaya zetu ambapo Wilaya zetu 139, hivi sasa sehemu zenye huduma tunapata Hospitali 119 peke yake.

Maana yake tuna kazi kubwa ya kufanya. Katika hili nawashukuru Wabunge wote. Waziri wangu akija hapa kwa sababu atakuwa na muda mrefu wa kufafanua, atazungumza mambo haya kwa undani zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao katika njia moja au nyingine, nilivyokuja *site* kule tulishirikiana vizuri. Hili naomba nikiri wazi, mama yangu Mheshimiwa Anne Kilango Malecela hapo ulizugumza kwa uchungu sana, hasa katika kituo chako cha Ndungu kule, na mimi bahati nzuri nilifika kule Same mama yangu. Kilio chako unasema kwamba Same ni kubwa na hapa ulitoa *reference* kwamba ni kilometa za mraba karibu 10,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia wananchi wa pale na nilipofika pale, ndiyo kilio ambacho wewe ulikileta siku zote, nilipofika pale kweli nilikikuta. Nikuhakikishie kwamba mimi na kaka yangu Mheshimiwa Simbachawene, tulishirikiana na Wizara ya Afya ambapo wenzetu wapo katika upande wa sera, katika ile haja yako hasa ambayo umeipigia kelele kipindi chote na ukaacha maagizo kwa viongozi wako nilivyofika pale *site*, tutahakikisha mwaka huu huenda mwaka Mungu akijaalia, kabla ya mwezi wa saba kazi ya ujenzi wa *theatre* utaanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutafanya hivyo katika maeneo mbalimbali. Katika agenda yetu tulisema tutafanya ujenzi wa vituo vya afya vipatavyo 100. Lengo letu ni nini? Ni kuhakikisha sasa tunapeleka huduma kwa wananchi. Ndiyo maana wakati mwingine Hospitali zetu za Wilaya na zile za Rufaa zinahemewa kwa sababu huku chini vituo vya afya uwekezaji ulikuwa mdogo, ndiyo maana Serikali hii sasa imeamua kufanya maamuzi katika mpango wake hasa katika suala zima la ujenzi wa zahanati tumetenga takriban shilingi bilioni 22.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo ni kuhakikisha kwamba tunaenda kuendeleza ule ujenzi wa zahanati takriban 370 huku tukishirikiana na nguvu za wananchi; tutaenda kufanya suala zima la ukarabati wa vituo vya afya

144, sambamba na kuhakikisha tunajenga maboma mengine 100, kuyamalizia 539. Hili tutaenda kulifanya katika katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika katika mpango mwingine mkakati tumetenga takriban shilingi bilioni 11.4. Katika eneo hilo, tutafanya? Lengo letu ni kwamba kuna vituo vya afya vinavyojengwa vipatavyo 94; tutaenda kuongeza nguvu hapo. Lengo ni kwamba tuweze kuvimalizia wananchi waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kuna vituo vyetu vingine 12 kama ni maboma yanataka umaliziaji, tutahakikisha tunashirikiana na wananchi ili hizi shilingi bilioni 11.4 na maeneo mengine twende tukawekeze katika suala zima la vituo vya afya tuweze kupata sasa mpango mkakati mzuri tuwasaidie wananchi Watanzania waweze kupata huduma nzuri. Mwisho wa siku ni kwamba wananchi waliipa ridhaa Serikali hii ya Awamu ya Tano, imani yao kubwa ni kwamba Serikali itaenda kuwatumikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami na kaka yangu hapa naomba niwaambie kwamba tumejipanga kuhakikisha tunafanya mabadiliko makubwa katika sekta ya afya tukiwa sisi ni watekelezaji wa sera katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, katika kipindi cha sasa mnafahamu zamani tulikuwa na changamoto sana ya dawa na ninyi Wabunge mara nyingi mmekuwa mkiuliza maswali hapa kuhusu suala zima la ukosefu wa dawa; na ndiyo maana katika mwaka huu ambao tunaenda nao, tulitenga takribani shilingi bilioni 106.3 na mpaka tunafika katika miezi ya katikati, mwezi wa tatu tulipeleka takribani shilingi bilioni 79.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto iliyokuwepo hivi sasa ni kwamba wakati mwingine Serikali inapeleka fedha, lakini usimamizi wa fedha siyo mzuri. Katika hili naomba nimshukuru Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, TAMISEMI anayeshughulikia suala la afya, katika kuzunguka kwake huko ametuibulia mambo mengi sana na ya msingi.

Ndiyo maana naomba mtuwie radhi ndugu zangu Wabunge, kwamba wakati mwingine tukifika kama mtaalam hasa aliyepewa dhamana ya uongozi kama *DMO*, huenda fedha zipo, zinashindwa kutumika kwa ajili ya kuwasaidia wananchi, jambo hilo hatutalivumilia kwa maslahi mapana ya wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani hata kidogo! Tulipofika mwezi wa saba mwaka 2017 mwaka unaanza, takriban shilingi bilioni 20.5 zilikuwa hazijatumiwa ambapo wataalam wetu walitakiwa wazitumiwe kwa ajili ya kununua dawa na vifaa tiba. Hili jambo haliwezekani hata kidogo. Katika utaratibu wa sasa tutaenda kufanya kila liwezekanalo kuhakikisha tunasimamia vyema sekta yetu ya afya, wananchi waweze kupata fursa nzuri ya kuamini kwamba Serikali yao sasa iko vitani kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma nzuri ya afya. Nawapongeze sana wadau mbalimbali, Waheshimiwa Wabunge, katika maeneo mbalimbali mmetumia mifuko yenu ya Mfuko wa Jimbo kuhakikisha kwamba mnajenga kusaidia nguvu za wananchi katika ujenzi wa zahanati na vituo vya afya, hongereni sana katika hilo. *(Makofi)*

Pia niwapongeze badhi ya Wakuu wa Wilaya, wamethubutu kwa kiwango kikubwa; kwa mfano, nilifika kule Tunduru, kuna Mkuu wa Wilaya ya Tunduru pale Bwana Homera, nimekuta amefanya harakati kubwa za ufyatuaji wa matofali. Nilipokuwa *site* juzi juzi nilimwuliza, akaniambia kuna takriban matofali milioni 14 yameshafyatuliwa. Lengo ni kuhakikisha anasaidia ujenzi wa zahanati na vituo vya afya, halikadhalika na katika sekta ya elimu. Tunataka mfano kama huu. Tunataka mfano kama *DC* yule wa Korogwe aliyefanya kazi kubwa katika maeneo hayo. Tushikamane kwa pamoja, lengo letu twende mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nizungumzie suala zima la matumizi mifumo ya elektroniki; mkumbuke kwamba kama Ofisi ya TAMISEMI, tumefanya uwekezaji mkubwa sana katika suala zima la kimifumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani tulikuwa tunatumia zile risiti za kawaida za karatasi, lakini sasa hivi Idara yetu ndiyo Idara ambayo ina miundombinu iliyojitosheleza, lengo kubwa ni tujielekeza katika mifumo ya elektroniki. Ndiyo maana mpaka mwezi Machi, tumeweza kukamilisha kuweka mifumo katika Halmashauri zetu zipatazo 177. Hii ni kazi kubwa! Tumebakiza Halmashauri nane tufikie Halmashauri 185. Lengo letu ni kwamba ikifika mwezi Juni, tuwe tumekamilisha zoezi katika zile Halmashauri chache ambazo zimebaki, ambazo zote ni Halmashauri mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa naomba nikiri wazi, katika eneo hili tumepata mafanikio makubwa sana. Kwa mfano, ukiangalia na hata ukienda Mikindani kwa ndugu yangu pale Mheshimiwa Maftaha, tulikuwa tunakusanya takriban shilingi milioni 600 tu kwa mwaka, lakini baada ya mfumo wa sasa hivi, taarifa inaniambia kwamba karibuni shilingi bilioni 2.6 zimeshaanza kukusanywa. Hii ni kazi nzuri inayoendelea kufanyika. Hata kule Arusha tulikuwa tunakusanya takribani shilingi bilioni tano, leo hii tumefikia shilingi bilioni 10 *point something*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata suala zima la vituo vya afya, kwa mfano nilitembelea kituo cha afya cha pale Kaloleni, Arusha, walikuwa wanakusanya shilingi milioni nne tu kwa mwezi; lakini baada ya kuwaambia wasimike mifumo, baada ya hapo wanakusanya kuanzia shilingi milioni 24. Haya ni mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jukumu letu sisi Wabunge ni kuhakikisha tunaenda katika Halmashauri zetu; Serikali inapoenda kujipanga tuhakikishe na sisi tunachukua nafasi yetu kusimamia mifumo iende ikasimikwe vizuri, siyo kusimika peke yake, lazima matumizi ya mifumo yaweze kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie, Ofisi ya Rais, TAMISEMI itatoa ushirikiano wa kutosha. Lengo letu ni kwamba *own source* zikusanywe vizuri ili mradi wananchi waweze kupata fursa ya maendeleo katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja katika suala zima la Mfuko wa Vijana na Akina Mama; na mkumbuke katika mwaka huu wa fedha 2016/2017 ilikuwa imetengwa bajeti ya shilingi bilioni 56.8, lakini mpaka tunapozungumza hapa juzi juzi, ni shilingi bilioni 15.6 zimepelekwa.

Kwa hiyo, nawaombe ndugu zangu Wabunge, kwamba zile *own source* za asilimia tano za vijana na akina mama hazifiki kwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mpango; fedha zile zinaishia katika Halmashauri zetu. Niwasihi sana, tunaposimama katika vikao vyetu vya Kamati ya Fedha tuombe kuelekeza kwamba fedha itakayokusanywa lazima ipelekwe kwa vijana na kina mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie, sisi Ofisi ya TAMISEMI tutachukua jukumu hili kwa nguvu zote kuhakikisha kwamba tunasimamia; lengo kubwa ni vijana na akina mama waweze kupata mikopo washiriki katika shughuli za uchumi wa nchi yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipata hoja ya msingi kutoka kwa Mheshimiwa Ikupa pale akisema walemavu wamesahaulika katika jambo hili. Naomba tuwaambie Mheshimiwa Ikupa na wenzako ni kwamba jambo hili tumelichukua na Mheshimiwa Waziri wangu ataliwekea utaratibu vizuri, tuone jinsi gani ya kufanya katika asilimia kumi angalau na walemavu waweze kukumbukwa, wananchi hawa waweze kushiriki vyema katika suala zima la uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ajenda kubwa ilizungumzwa hapa ya barabara. Katika ajenda hii ya barabara ukizungumzwa kila mtu anaguswa na ajenda ya barabara. Ndiyo maana ukikumbuka mwaka 2016 tulitengewa karibu shilingi bilioni 249.7 hapa na mpaka mwezi Machi, tulipelekwa karibun shilingi bilioni 142, lakini kuna kazi kubwa sana ilifanyika; tumejenga maboksi kalavati kama 23, tumejenga madaraja, tumejenga barabara ya kilometa 11,111.57. Hii ni kazi kubwa inafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, leo hii ukitembea katika Miji mbalimbali kazi kubwa iliyofanya TAMISEMI inapimika kwa vigezo vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda katika hii Miji yetu Mikuu kupitia mradi ya *TCSP Project*, tumefanya kazi kubwa sana katika maeneo haya nane; lakini ukienda zile Halmashauri za Miji 18, zamani ukipita maeneo hayo utakuta barabara za vumbi, lakini leo hii, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeamua kuweka ujenzi wa barabara za lami katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwahakikishie, katika bajeti ya mwaka huu ambayo imetengwa takribani shilingi milioni 247.7 tutaenda kufanya kazi kubwa ya kuondoa vikwazo hasa ujenzi wa madaraja na kuondoa vikwazo na ndugu yangu mmoja nimemsikia hapa jana alikuwa anazungumza kwamba sisi hatufikiki, hili ni jukumu la ofisi yetu. Nami bahati nzuri naomba niwaambie kwamba tumejipanga vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo letu ni kuacha *legacy* kwamba tukiondoka na kaka yangu hapa, hata tukihama watu waseme hapa alikuwa Mheshimiwa Simbachawene na Jafo, walifanya hii kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini binadamu aliyekuwa sahihi lazima afanye kazi aache *legacy* katika maeneo yake. Na sisi naomba niwaambie, tutaenda kuacha *legacy* katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua wazi kwamba Ofisi hii ni Ofisi ya wananchi, ndiyo bajeti ambayo inabajetiwa mwananchi kijijini, Mwenyekiti wa Kijiji, Diwani na Waheshimiwa Wabunge na kila...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya kama ni bashrafu tu, naomba niseme sasa naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa namwita Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Simbachawene. Una muda usiozidi dakika 30.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na kusimama mbele kwa kazi ya kujumuisha mjadala wa bajeti ya mwaka 2017/2018 juu ya bajeti ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla wa pande zote mbili kwa michango yenu mizuri na muhimu ambayo lilenga kuboresha utendaji kazi wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wa pande zote mbili wametoa michango yao; walioweza kuchangia kwa maandishi ni 47 na waliochangia kwa kuongea ni 34. Michango yao yote tumeizingatia na tumeijibu hoja kwa hoja katika jedwali hili la majibu ya hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa michango ni mingi na waliozungumza ni wengi, pengine haitakuwa rahisi kuweza kutumia muda huu wa kuzungumza kumjibu kila mmoja alichokisema, lakini muamini tu kwamba kila mmoja alichokisema tumekizingatia na tutakizingatia wakati wa kutekeleza bajeti itakayopitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu kwenu ni kwamba mtusaidie tuweze kupata fedha hizi tulizoziomba ili tuweze kutekeleza majukumu kama tulivyoainisha katika malengo ya Wizara, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza kujibu hoja za Wabunge, nataka niseme maneno. Michango mingi imetolewa na Wabunge, pamoja na uzuri wa michango hiyo, iko baadhi ya michango ilileta hali ya kutokuelewana. Kutokuelewana huko kumetokana na lugha na pengine matamshi yanayotamkwa ambayo kimsingi, hata kama katika utaratibu unaambiwa tunakuja huku Bungeni kupewa ushauri kama Serikali, lakini unaona huo utayari wa kupewa ushauri haupo kwa sababu anayetoa ushauri tayari ana hukumu na kutumia lugha ambayo haiko sawa sawa kimaadili, lakini pia hata katika kanuni zetu za uendeshaji wa shughuli za Bunge. Ndiyo maana katika mjadala kulitokea kusimama kwingi na vurugu nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme tu, ukitaka kujua historia ya nchi yoyote lazima uangalie vipindi vyake vya utawala. Nchi hii toka tulivyopata uhuru Rais wetu wa kwanza alikuwa Mheshimiwa Julius Kambarage Nyerere ambaye naye katika wakati wake, hasa alipoamua kujenga Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea alipata shida kubwa. Walitokea wapinzani, walitokea waasi na mtakumbuka akina Oscar Kambona, akina Kasanga Tumbo; na mnakumbuka katika historia nini kilitokea kwa baadhi ya watu waliokuwa wapinzani wa misingi ya Ujamaa na Kujitegemea ambao leo hii hapa tunajivunia kwamba imeliweka Taifa hili salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi cha pili amekuja Mzee Mwinyi. Rais Mwinyi katika kipindi chake akafungua milango ya uchumi akaleta uchumi huria; na kwa maneno yake alisema unapofungua milango na madirisha basi nzi wataingia, matakataka yataingia, wadudu wataingia, hewa chafu itaingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufungua milango ya uchumi akaonekana yeye ni mtu asiye na weledi wa uchumi, ni mtu ambaye amefungua kila kitu, mambo yanaenda holela, wakapatikana wa kulaumu na wakalaumu sana. Hata hivyo, kipindi hicho kikapita na leo hii tunakumbuka Awamu hizo zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amekuja Mkapa akaleta *discipline* ndani ya Serikali, akaboresha utumishi ndani ya Serikali, akaboresha heshima ya Serikali. Kwa kufanya hayo naye akaambiwa huyu ni Mkapa amelea ugumu wa maisha na akalaumiwa sana. Kipindi hicho kikapita na chenyewe tunakikumbuka na tunakipongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amekuja Kikwete ambaye amemaliza Awamu ya Nne, Rais mpole, mjuzi wa Diplomasia amejenga nchi yetu kujulikana sana Kimataifa, amejenga uchumi na miundombinu, amefanya mambo makubwa akaambiwa ni Rais dhaifu, tena ni mpole aliyepitiliza hafai kuwa Rais; hapa hapa humu ndani na bahati nzuri waliosema wamo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo anapongezwa sana kwamba ni Rais mzuri hajapata kutokea, amefanya mambo makubwa, anakumbukwa kwa mema na makubwa aliyoyafanya na anakumbukwa na watu wa pande zote mbili na ushahidi ni namna alivyoshangiliwa juzi alipokuja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa stadi hii na mifano hii, leo hii kuweka mipango na mikakati ya baadhi ya wenzetu humu ndani ya kumdhallilisha na kumtukana Mheshimiwa Rais si jambo la kwanza; kumbe inawezekana akimaliza atapongezwa na kusifiwa. Kwa hiyo, ninachotaka kumwambia Mheshimiwa Rais wangu, haya yanayosemwa ni utaratibu wa kawaida wa miongo yote ya utawala wa nchi yetu, yeye aendelee, tunasonga mbele na sasa nchi inakwenda mbele katika uchumi wa viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi majuzi *IMF* na *World Bank* wiki iliyopita imezindua taarifa ya hali ya uchumi ya Tanzania na imepongeza uchumi wa Tanzania kwamba ni miongoni mwa nchi tano ambazo uchumi wake unakua kwa kasi na uko *stable*. Uchumi wa Tanzania kwa sasa uko *very stable*, unakua kwa asilimia saba nukta moja. Kwa Afrika inazidiwa na *Côte d'Ivoire* ambayo uchumi wake unakua kwa asilimia

saba nukta tisa. Kwa ukanda huu wa *East* Afrika hakuna nchi inayotukuta, sisi katika Afrika ni wa pili, katika sifa kama hii bado watu wanasema hawaoni kitu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini leo hii Rais huyu anazindua ujenzi wa reli ya treni ya *standard gauge* inayotaka kutupeleka sasa kwenye miundombinu ya usafirishaji pamoja na barabara zinazojengwa zilizounganisha mikoa yote na za lami sasa watu wanasafiri. Zamani ukisema unatoka hapa kwenda Moshi ni hadithi, leo hii kaka yangu Selasini akiwasha gari saa hizi, saa tatu yuko Moshi anakula nyumbani kwake chakula; haya ni maendeleo makubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Rais huyu ambaye sasa anajenga nchi na uchumi mkubwa unajengeka na unatupeleka kwenye viwanda, viwanda vingi vinafunguliwa bado wanasema hawaoni anachokifanya. Rais huyu anayesisitiza uwajibikaji, anaondoa rushwa, amesababisha Watanzania wanapata huduma nzuri wanapokelewa vizuri maana huko nyuma ilielezwa kwamba watumishi wa umma ni miungu watu, leo hii watumishi wa umma wamegeuka wanawahudumia Watanzania, wamegeuka wanawapokea vizuri. Ukienda hospitali unapokelewa na nesi vizuri unahudumiwa vizuri, wanasema Watanzania wamekuwa waoga, Watanzania ambao wamekuwa waadilifu na wanaona mambo yanavyokwenda vizuri, wanaambiwa wamekuwa waoga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie watumishi wa umma wa nchi hii kwamba, Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Dkt. John Pombe Joseph Magufuli inafanya kazi nzuri na muiunge mkono; na sisi tunatambua changamoto mlizonazo watumishi wa nchi hii; kwa kuhakikisha kwamba mnafanya wajibu wenu bila kushinikizwa. Naamini kabisa matunda haya yanayopatikana yataivusha nchi yetu kutoka mahali ilipo na kufika mahali pazuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimezungumzwa hoja nyingi lakini nianze na moja ambayo inakera hivi. Huwezi ukasema

kitu bila kuwa na takwimu na bahati mbaya sana takwimu tunazileta sana humu. Kibaya zaidi ni kwamba kumbe mtu akiamua kukupinga hawezi kukubali hata takwimu utakazomletea hawezi kukubali chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa elimu ya Tanzania inashuka, lakini kinachoweza kutusaidia kujua kwamba elimu inashuka au inapanda ni matokeo ya wanafunzi wanaofanya mtihani. Kama kipo kigezo kingine labda ni baadaye lakini cha kwanza ni matokeo. Sasa nifanye ulinganisho, katika sekta ya elimu matokeo ya darasa la nne mwaka 2014, ufaulu ulikuwa ni kwa asilimia 64, leo 2016 matokeo ni kwa asilimia 93, watoto wamefaulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, darasa la saba mwaka 2012 watoto walifeli sana, ilikuwa ni asilimia 33 ya ufaulu, leo hii ni asilimia 70. Matokeo ya kidato cha pili, mwaka 2012 ilikuwa asilimia 57, leo hii ni asilimia 91. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya kidato cha nne mwaka 2012 ilikuwa ni asilimia 45, leo hii ni asilimia 70 ya ufaulu. Matokeo ya kidato cha sita yanatisha ni karibu wanafunzi wote wamefaulu. Mwaka 2012 ilikuwa asilimia 88 tu ndio waliofaulu, leo hii ni asilimia 99 ndio waliofaulu. Ahsanteni Walimu wa Tanzania, tunawashukuru sana Walimu wa Tanzania. Ninyi ni wazalendo wa nchi hii, Walimu wa Tanzania ni wapenda maendeleo ya elimu ya nchi hii, tekelezeni wajibu wenu na Serikali inatambua mchango wenu; na wala ninyi sio waoga. Msijazwe upepo wa kuambiwa ni waoga, sidhani kama kwa mwoga huenda kilio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini, Serikali tunatambua na ndiyo maana tumechukua hatua. Hadi sasa tumelipa madeni ya Walimu wote nchini bilioni thelathini na tatu, madeni yasiyo na mshahara. Kwa mwaka 2015/2016 – 2016/2017, tumelipa bilioni thelathini na tatu na tumelipa kwa takribani mikoa yote na madeni ambayo yamebaki yanadaiwa ni yale tu ambayo ni ya mshahara, lakini yale

yasiyo ya mshahara yote tumeyalipa na tunahakikisha kwamba na madeni ya mshahara na yenyewe tutayalipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu bila malipo imebezwa humu ndani sana na katika ubezwaji huo ni ubezwaji wa kupotosha. Serikali inatumia billioni ishirini na mbili nukta tano kila mwezi. Wakati fulani ili kumwandikisha mtoto darasa la kwanza ilikuwa ni lazima mzazi atoe kati ya Sh. 30,000/= mpaka Sh, 100,000/=, Serikali imesema marufuku, itagharamia gharama hizo za uandikishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatoa ruzuku ya uendeshaji wa shule, wazazi hawachangishwi, Serikali inatoa chakula kwa shule za bweni, lakini Serikali inagharamia mitihani, ilikuwa wazazi wanalipia mitihani sasa hivi ni bure. Ilikuwa hakuna vitabu sasa hivi tunapeleka vitabu na tumegawa vitabu zaidi ya milioni sita, ukijumulisha vyote vya kuanzia elimu ya msingi na sekondari, vitabu vingi tumegawa na sasa uwiano wa mwanafunzi wa vitabu ni kitabu kimoja wanafunzi watatu. Kwa hiyo, tunakaribia kufika kwenye lengo la milenia lakini watu wanasema hakuna kinachofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwasihi Watanzania kwamba elimu yetu inaboreshwa na inatazamwa kwa ukaribu sana na Serikali na tutahakikisha kwamba pale ambapo Serikali ina wajibu wa kufanya mambo tutaendelea kuyafanya zaidi. Kwa sasa tunatumia billioni karibu ishirini na tano kwa kila mwezi kwa ajili ya kuondoa zile gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haimaanishi kwamba kwa kusema tu elimu bure na kuchukua gharama hizi zilizokuwa zinawaumiza wazazi na kusababisha udahili wa wanafunzi kupungua; leo hii kwa mwaka tumeandikisha wanafunzi wa chekechea na darasa la kwanza zaidi ya milioni moja na laki nne wakati lengo lilikuwa laki tisa. Haya ni mafanikio makubwa ambayo wazazi sasa wanawatoa watoto wao kwa sababu hakuna gharama za lazima wanazotakiwa kuzilipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio haya makubwa yanatokana na fedha hizi ambazo Serikali inagharamia, lakini mtu anasema uwepo wa elimu bure basi Mwalimu Serikali ilipie kila kitu, ihakikishe mtoto huyu amechukuliwa kutoka nyumbani kupelekwa shuleni, mtoto huyu amepewa kila kitu jamani, hii tafsiri ni ya upotoshaji ni tafsiri isiyowatakia mema Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwasihi wazazi wa nchi hii kwamba watoto ni wa kwetu lazima tushiriki kusaidiana na Serikali kuhakikisha kwamba wanapata elimu kwa sababu mwisho wa siku haipati faida Serikali peke yake bali hata sisi wazazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie sasa Sekta ya Afya. Sekta hii ina changamoto kadhaa na zimesemwa na Waheshimiwa Wabunge. Moja ni changamoto ya upatikanaji wa dawa. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, hadi mwezi Machi tumepeleka kiasi cha Shilingi bilioni 79.7 za dawa. Tulipofanya ukaguzi tumekuta baadhi ya Hospitali za Wilaya zina fedha za dawa zipo kwenye akaunti hawataki hata kuzitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawataki kuzitumia ili zibakie baki mle baadaye wajue cha kufanya, huu ni wizi tu. Hizo fedha zimetolewa kwa ajili ya dawa, ni lazima zinunue dawa na watu wapate dawa, lakini wananchi wakienda kule wanaambiwa dawa hakuna. Niseme, Waheshimiwa Wabunge sisi ndio Madiwani, tuko kule, tufike hatua hata tukague akaunti za Halmashauri, si kosa kwa sababu Mbunge unashiriki kwenye Kamati ya Fedha na kule kwenye Kamati ya Fedha ndiko mnakohoji mpaka akaunti kwamba zina fedha au hazina pesa.

Waheshimiwa Wabunge, msije kulalamika huku, sisi tunakwenda kukagua kwenye akaunti ambazo ninyi mko kule, tunakuta kuna fedha zimebaki, unamuuliza Mganga Mkuu hizi fedha zimebaki za nini, anajiuma uma tu. Kwa

hiyo, tunawasihi Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Madiwani kusimamia kuhakikisha kwamba dawa zinapatikana, Serikali inapeleka fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka huu wa fedha Serikali imepanga kutumia Shilingi billioni 96.433 kwa ajili ya dawa; tunahakika ni dawa nyingi, lakini bado hapo hujazungumzia CHF, hujazungumzia Mfuko wa Afya ya Jamii ambao na wenyewe unaingiza fedha nyingi sana. Mnapowauliza hizi zilizopelekwa na Serikali waulizeni hata yale makusanyo yao, ambapo katika yale makusanyo yao asilimia 33 ni kwa ajili ya *motivation*, inatakiwa ilipe hata *on call allowances*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko Wilaya zinafanya hivyo na nyingine hazifanyi. Niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Madiwani tusimamie sana kuhakikisha kwamba rasilimali hizi zinatumiwa katika kuwahudumia wananchi wetu lakini tukibaki tunabishana na kuona ni sifa kusema hakuna dawa, Serikali hii imeshindwa, imefanya nini, tunapoteza maisha ya watu wetu bure kwa uzembe wa watu wachache ambao si waaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa upelekaji wa dawa sasa tunauboresha, tunataka sasa pesa hizi sasa zipelekwe mpaka kule kwenye vituo vya kutolea huduma kwenye zahanati, kwenye vituo vya afya, kwenye hospitali za wilaya na kwenye hospitali za mikoa. Hela zipelekwe kule, na tumeweka utaratibu ambao sasa kutakuwa kuna maafisa mahususi kwenye kila kituo cha afya na zahanati zinazozunguka kituo cha afya watakaosimamia ununuaji na upangaji wa dawa kuhakikisha kwamba zinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa utaratibu tumeuboresha zaidi kwamba MSD watakapopelekwa ile *quotation* ya dawa na Halmashauri husika watakapokuwa *out of stock* hawana hizo dawa, lazima watoe hilo jibu mara moja ili sasa hao waende wakanunue kwenye maduka mengine kwa sababu na yenyewe hiyo haikatazwi tena sasa.

Kwa hiyo, nina hakika kwamba kama tutasimamia vizuri na Waheshimiwa Wabunge na Madiwani tutasimama vizuri nina hakika kwamba tatizo hili halitakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa watumishi. Ni kweli kwamba tuna upungufu wa wataalam wa kada mbalimbali, mahitaji ni tisini na sita elfu na ushehe hivi lakini waliopo ni arobaini na sita elfu na upungufu ni kama hamsini elfu. Changamoto hii ni kubwa, tuna shida ya ikama hiyo kwenye upande wa Walimu na kwenye upande wa Sekta ya Afya. Utaratibu wa Serikali ni kwamba tutaendelea kuboresha ikama hizi kadiri tutakavyokuwa tunapata uwezo wa uchumi kuweza kubeba ajira zinazotakiwa kuzitoa katika Sekta ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunavyozungumza *wage bill* ya nchi yetu sasa *is almost seventy percent* ya GDP. Unapokuwa na *wage bill* kubwa kiasi hicho halafu bado una upungufu wa watumishi muhimu kama wa afya na elimu lazima kuna tatizo mahali. Ama tumeajiri katika kada nyingine watu wasiohitajika kuwepo, ama tumefanya *over employment* katika maeneo ambayo si muhimu kwa Taifa kwa sasa. Kwa hiyo, iko haja ya kuangalia ndio maana Serikali sasa tunaangalia masuala ya miundo, nafikiri atakuja kuzungumza Waziri wa Utumishi ili tuweze kuona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoweza kusema kwa sasa ni kwamba kwa watumishi wa afya tumepata kibali cha hawa Watumishi madaktari 258 ambao nina hakika hawa tutawapanga kwenye vituo vyetu vya kutolea huduma hospitali za wilaya na za halmashauri pamoja na vituo vya afya mara moja. Kuanzia siku ya Jumatatu hawa tutaanza kuwa-*deploy* na kuwapeleka huko na tunasubiri vibali zaidi vikitolewa ili tuweze kuwapeleka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa Walimu tumepata kibali cha ajira zaidi ya elfu nne na tumeweza kupeleka Walimu takribani elfu tatu na mia kadhaa hivi ambao tumewachukua wote wa masomo ya sayansi

waliomaliza mwaka 2015. Hata hao tuliowachukua tumebaki na nafasi ya kibali ambapo hawajatosha. Tunaamini wengine waliokosa kwa sababu ya kukosekana kwa barua zao tumewaambia wazilete Wizara ya Elimu na zingine kama wakiweza hata TAMISEMI tutazipeleka kwa Waziri wa Elimu wazihakiki ili waweze kupata nafasi; wale waliokosa, ambao walimaliza mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilizungumzwa hapa habari ya ujenzi wa miradi ya afya na elimu, unazungumzia zahanati, madarasa, matundu ya vyoo na kadhalika na kadhalika. Mwaka uliopita tulipata hela ile ya maendeleo isiyo na masharti, inajulikana kama *Local Government Development Grant*. Tulipata fedha ingawa haikuletwa kwa kiwango kizuri tumepokea kiasi cha bilioni hamsini na nane. Waheshimiwa Wabunge, mkumbuke kwamba fedha hii kwa miaka mitatu mfululizo ilikuwa haijawahi kutolewa na ndiyo ilipelekea maboma mengi kubakia kwenye maeneo yetu bila kumaliziwa kwa sababu fedha hii ndiyo ambayo huwa inatumika kumalizia maboma haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo furaha kuwajulisha kwamba katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, kiwango hiki cha fedha kimeongezeka hadi kufikia billioni 256. Hizi shilingi billioni 256 zikisaidiana na utaratibu wetu wa kawaida wa nchi yetu ya Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, ambapo ni lazima wananchi washiriki katika shughuli za maendeleo yao, wakatoa nguvu zao, wakasogeza mchanga, wakasogeza mawe, wakanyanyua mabomba au hayo yaliyopo hizi fedha zina uwezo wa kutusaidia kumalizia kwa kiasi kikubwa na kwa hivyo tutaongeza zahanati, vituo vya afya, tutapunguza upungufu wa madarasa na nyumba za Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwa wananchi wa Tanzania kushirikiana na Mamlaka za Serikali zao za Mitaa kuhakikisha kwamba wanachangia nguvu zao ili kwa uchumi wetu ulivyo na kiwango hiki cha fedha kidogo kiweze kuwa na tija kwa kumaliza kero hii ya wananchi katika maeneo ya huduma za afya na elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilizungumzwa *issue* ya mapato ya ndani. Kama maombi mengi yalivyokuwa yanatolewa na niishukuru sana Kamati kwa kupitia Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Jasson Rweikiza, walishauri sana kwamba sasa ile fedha inayopelekwa kwa ajili ya maendeleo kuwa sera ile ya asilimia sitini na kwa arobaini, yaani sitini iende kwenye maendeleo na arobaini ibakie kwa uendeshaji ilikuwa inapelekea Halmashauri nyingine zisizokuwa na uwezo kushindwa kujijendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imesikia na tumeibadilisha ile sera sasa tutazipanga hizi Halmashauri kutokana uwezo wake. Zile ambazo hazina uwezo zitapeleka asilimia arobaini tu kwenye maendeleo na asilimia sitini itatumika katika uendeshaji wa Halmashauri. Hapa itatusaidia sana kuhakikisha kwamba Madiwani sasa hawakopwi posho zao, lakini pia uendeshaji hata wa shughuli nyingine za kiutawala utawezekana ikiwa ni pamoja na usimamiaji wa miradi ukiondoa *OC per se* ambayo italetwa na Serikali Kuu, lakini pia hii *own source* ni sehemu ya *OC*. Kwa hiyo, hii nayo ikitumika vizuri, ikisimamiwa vizuri itatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwenye Halmashauri zetu huwa tunaambiwa tu *OC* haijaja, lakini *OC* ni pamoja na *own source*, ikijumlishwa ndipo unaipata *own source* unapoipata *OC total*. Hii *OC* ndiyo inayoweza ikatumika hata kupunguza baadhi ya changamoto ndogo ndogo. Unamkuta Mkurugenzi anadaiwa na Mwalimu Shilingi 45,000 ya matibabu. Hivi kama una *own source* kwa nini usimilipe Mwalimu huyo akaondoka akaenda kufanya kazi yake? Tumeona mfano mzuri uliofanywa na Mkurugenzi wa Arusha, ndugu Kiamia. Nafikiri Wakurugenzi wote waige mfano huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki za watumishi. Waheshimwa Wabunge wamezungumzia haki za watumishi. Tunalo tatizo kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa ambako Waheshimiwa Wabunge mpo, Madiwani mpo. Wapo Maafisa Utumishi ambao wanawatesa wenzao, hawataki kuwahudumia wenzao, wanataka wahudumiwe wao.

Waheshimiwa Wabunge, ninyi ndio mamlaka za utawala. Mwalimu au mtumishi anasema mke wangu yuko mahali fulani nataka kuhamia kwa mke wangu anakwambia sitaki hata kama ni ndani ya Wilaya moja, hata kama ni ndani ya mkoa mmoja. Hii haiwezekani lazima Sheria za Utumishi zizingatiwe. Walimu hawa wanayo haki ya kutoka sehemu moja kwenda nyingine lakini pia na kuishi na wenza wao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtumishi anapoomba ahamishwe kwa sababu anamfuata mwenzake utadhani *it is a privilege*, ni hiari, *no*, ni haki yake ya msingi. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge, tusimamie haki hizi za watumishi, na ninyi ndio mamlaka za utawala na nidhamu kwenye maeneo ya Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unyanyasaji wa wananchi katika dhana ya uchumi wa viwanda, ujasiriamali na biashara ndogo ndogo. Hii habari ya kuwasumbua wamachinga, Mheshimiwa Rais alishatoa maelekezo. Wafanyabiashara ndogo ndogo hawa wakirasimishwa; alisema Mheshimiwa Mabula Mbunge wa Mwanza; wanaweza kuchangia makusanyo makubwa sana ya Halmashauri. Wanaweza kuchangia uchumi wa Taifa. Hata hivyo, wako wengine wanaona kama wafanyabiashara ndogo ndogo ni mkosi, nuksi, balaa, washughulikiwe na waondoke, hapana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachosema sisi ni kwamba mamlaka hizi ndizo ziwapangie maeneo mahsusi ya kufanyia shughuli zao. Maeneo mengine kwenye miji mingine ukienda wanapangwa vizuri hata wakati wa masaa fulani wanafanya ile biashara yao, ikifika kwa mfano saa moja watu wanaondoka, wanapanga biashara zao vizuri, wako kwenye maeneo mazuri na asubuhi baada ya saa nne, au saa tano wanaondolewa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimeambiwa na yule Mbunge rafiki yangu Raza kwamba kule Dar es Salaam

wanawafukuza. Mheshimiwa Raza nitalishughulikia, hii si sawa. Hatuwezi kuwa na nchi ambayo ina watu wote wanataka kuwa na uchumi rasmi. Duniani kote, watu wasio na uchumi rasmi ndio wengi kuliko wenye uchumi rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hili tumelifahamu lakini Halmashauri zote nchini zitenge maeneo mahsusi kwa ajili ya uwekezaji wa watu hawa wadogo wadogo. Ukiwa na Wilaya yako, hata kama ni wilaya si mji, ukawapangia wale washonaji, wanaosindika mafuta, ukaandaa eneo mahsusi, ukapeleka umeme, ukapeleka maji, ukapeleka barabara ni dhahiri eneo hilo litakuwa eneo la kiutalii, hata mtu akienda kwenye wilaya hiyo ataenda kutembelea eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, tuko huko, rasilimali zile ni zetu. Tuwaelekeze Wakurugenzi kuhakikisha kwamba wanatenga maeneo haya na kuyapatia miundombinu ili wafanyabiashara wetu wadogo wadogo hawa tukawaweke kule kwenye maeneo mahsusi si kama wanavyokaa kwenye barabara, kwa sababu pia na wao lazima wafahamu kwamba wako wananchi wengine wenye haki pia za kutumia maeneo ambako wao wanataka kufanya biashara ambapo pia si sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya mipaka. Migogoro iko ya aina nyingi, iko migogoro ya mipaka ya mikoa, vijiji, wilaya, iko migogoro mingi sana. Kwa ujumla tuna migogoro zaidi ya 288 inayohusiana na mipaka ya vijiji na Hifadhi za Serikali; za misitu au za Taifa za utalii. Migogoro hii ni 288, lakini tunayo migogoro mingine takriban 56 ya mipaka na tunayo migogoro mingine takriban 18 na migogoro inayohusiana na ujenzi wa Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, niwasihi, sisi ndio tuko kule. Sisi katika Serikali tumeamua kujipanga na Wizara ya Ardhi, tumetengeneza *task force* ambayo inaipitia migogoro hii yote na tumeihakiki migogoro hii yote, tunataka ifike hatua tuje tufanye maamuzi ya

pamoja. Kwa hiyo, niwasihi sana kwa sasa tushiriki katika kuhakikisha kwamba tunatuliza migogoro hasa ya wakulima na wafugaji. Waheshimiwa Wabunge na sisi wanasiasa kwa ujumla tusiwe chachu ya kuhakikisha kwamba migogoro hiyo inakua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia limezungumzwa hapa suala la Utawala Bora, kwamba iko migongano ya mamlaka kati ya ma-DC, ma-RC, ma-DED, na Madiwani kuna migongano. Waheshimiwa Wabunge, kwanza hawa wote wanaotajwa wapo kwa mujibu wa Sheria na uwepo wake hauwi *choice* ya mtu mwingine, *they are all supposed to be there*, kwa hivyo hakuna namna ni lazima waelewane. Sasa kuelewana msingi wake mkubwa ni sheria.

*(Hapa kengele lilia kushiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya na mengine, najua tutapata fursa wakati wa mafungu. Naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

MWENYEKITI: Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tutaishughulikia baadaye. Ahsante.

Namwita sasa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mheshimiwa Angella Kairuki, una muda wa nusu saa, karibu. *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi

Mungu mwingi wa rehema aliyenijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuweza kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kuchukua fursa hii kwa mara nyingine tena kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa namna ambavyo amekuwa akiniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kusimamia Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee pia nimshukuru sana Mheshimiwa Makamu wa Rais pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwani wao pia wamekuwa wakituongoza vyema na wamekuwa wakitoa msaada mno na ushauri ambao umenisaidia sana katika kutekeleza majukumu ya ofisi yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru pia Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wenyeviti wote wa Bunge, Katibu wa Bunge pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati yangu kwa namna ambavyo wamekuwa wakifanikisha majukumu ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Sera, Mikakati mbalimbali Pamoja na Mipango. Wote tunafahamu namna ambavyo inahitaji kuwa na watumishi wa umma wenye weledi, uadilifu na walio makini kwa kuwa wote tunajua utumishi wa umma ndiyo nguzo ambayo ni muhimu katika maendeleo ya Taifa letu. Nia ya Serikali yetu ya Awamu ya Tano ni kuendelea kuiboresha Sekta yetu ya Utumishi wa Umma, kuhimiza katika misingi ya weledi, kuendelea kuweka mifumo ya menejimenti inayowezesha watumishi kuwajibika vyema, kuwa na maadili ili waweze kutoa huduma iliyo bora na kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wa umma endapo watazingatia sifa hizo nilizozitaja basi kwa hakika tutaweza kujionea utendaji mzuri zaidi wenye matokeo na

hii itatuwezesha kuwa na tija zaidi, kuwa na mapato makubwa zaidi na hatimaye kuweza kuboresha zaidi maslahi ya watumishi wetu wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali tunaendelea kuhakikisha kwamba utumishi wa umma unaongozwa na kusimamiwa ili kuhakikisha kwamba hauendi kinyume na misingi hiyo niliyoitaja awali. Ili kuhakikisha kwamba tunalinda misingi hiyo, kama Serikali tumekuwa tukifanya mabadiliko na maboresho mbalimbali katika Sekta yetu ya Utumishi wa Umma, lakini vile vile katika sekta mbalimbali tumeshuhudia maboresho katika utendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia programu yetu ya Maboresho katika Utumishi wa Umma hadi mwaka 2014, lakini vile vile tumeanza kuchukua hatua kwa kushirikiana na *DFID* pamoja na *World Bank* kuona ni kwa namna gani tunaweza kuweka utaratibu mwingine na kubuni maboresho yatakayoendeleza mipango ya matokeo makubwa katika utoaji wa huduma kwa kuondoa vikwazo katika utumishi wetu wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu kuanza kwa Serikali ya Awamu ya Tano, tumekuwa tukichukua hatua mahsusi za kusimamia Sera na mifumo ya kimenejimenti, matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano, masuala mazima ya nidhamu, mapambano dhidi ya rushwa, uadilifu na uwajibikaji navyo pia tumekuwa tukiendelea kuweka mkazo. Sisi tunaamini kwamba tutakapozingatia haya, basi watumishi wa umma watafanya kazi kwa weledi na kwa bidii kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, niwaahidi tu kwamba kama Serikali tutaendelea kuimarisha vita dhidi ya rushwa ambapo kama hatua ya uadilifu, tutaendelea pia kuhakikisha kwamba viongozi na watumishi wa umma wanatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia viapo vya taaluma zao, viapo vya uadilifu na pia kuhakikisha

kwamba wanawajibika kwa matokeo ya kazi na maamuzi yao ili kuhakikisha kwamba tunaondokana na maamuzi na matumizi mabaya ya madaraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hotuba yangu. Niwashukuru sana Wabunge 47 walioweza kuzungumza, niwashukuru pia Wabunge 27 ambao waliweza kuchangia kwa maandishi. Nawashukuru Wabunge hawa kwa kuongozwa na Mheshimiwa Rweikiza Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa pamoja na Makamu wake mwanamama machachari Mheshimiwa Mwanne Nchemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimtambue na kumshukuru Mheshimiwa Ruth Mollel Waziri kivuli wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa maoni na michango yao ambayo naamini kabisa itaweza kutusaidia kuboresha utumishi wa umma na utawala bora nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda hautoshi kuweza kujibu hoja zote, nitajitahidi kadri nitakavyoweza, lakini niwahakikishie tu kwamba katika Mkutano huu wa Saba wa Bunge la 11 Wabunge wote mtaweza kupata majibu yetu kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na hoja chache zilizojitokeza katika Utumishi wa Umma. Kulikuwa kuna hoja ya Kamati yetu ya Bunge, kwamba Chuo cha Utumishi wa Umma ni vyema kikawezeshwa ili kiweze kumiliki majengo yake katika *campus* zake na hususan walitolea mfano wa *campus* ya Mbeya ambayo wamekuwa wakitumia gharama kubwa sana kwa aili ya kulipia pango. Niseme tu kwamba nawashukuru Kamati kwa namna ambavyo wamekuwa wakifuatilia utendaji wa Chuo hiki. Waliweza kufika katika *campus* ya Chuo chetu cha Mbeya, waliweza kujionea na kuweza kutoa ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende tu kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba, tayari tumeshawasilisha maombi kwa

Ofisi ya Rais, TAMISEMI na wanaliangalia jambo hili kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Mbeya ili kuona ni namna gani sasa Chuo cha Utumishi wa Umma tunaweza tukamilikishwa majengo haya kwa taratibu ambazo tutaweza kupangiwa na kuelewana kwa pamoja. Kwa hiyo, niseme tu kwamba tunasubiri maamuzi ya TAMISEMI na tunaenda vizuri, tunaamini tunaweza tukafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja pia ya Kambi Rasmi ya Upinzani ambayo pia Mheshimiwa Sannda aliitolea maelezo pamoja na Mheshimiwa Bobali. Hii ni kuhusiana na umuhimu wa mafunzo kwa watumishi wetu wa umma, lakini wao walienda mbali kwamba tupanue wigo sasa, katika mafunzo haya basi tuangalie pia ndani ya nchi lakini twende pia na nje ya nchi ili kuhakikisha kwamba watumishi wanakuwa *exposed* zaidi katika kupata mafunzo. Niwashukuru wote kwa hoja hii. Hakuna anayebisha hata kidogo umuhimu wa mafunzo kwa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie tu kwamba tunayo Sera yetu ya mafunzo kama Serikali lakini vile vile tunayo Sera ya Menejimenti na Ajira ya mwaka 1999 ambayo ilirekebishwa mwaka 2004. Kimsingi Sera hii pia inasisitiza katika umuhimu wa waajiri kuweka kipaumbele katika kuandaa mipango ya mafunzo ambayo itazingatia mahitaji yao halisi lakini pia kuhakikisha kwamba wanaongeza ufanisi katika sehemu zao za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kusema tu kwamba kupitia ofisi yangu pia katika Idara ya Uendelezaji wa Rasilimali watu tumekuwa tukitafuta fursa mbalimbali za mafunzo ili kuhakikisha kwamba watumishi wa umma wengi zaidi wanaweza kujiendeleza na kuweza kupata ujuzi. Nikichukua tu katika mwaka 2015/2016 zaidi ya watumishi wa umma 395 waliweza kupatiwa mafunzo ya muda mfupi na ya muda mrefu nje ya nchi. Pia katika Mwaka huu wa Fedha zaidi ya watumishi wa umma 654 nao pia waliweza kupata mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba ni eneo ambalo tunalipa

kipaumbele. Nipende kutoa rai kwa waajiri wetu mbalimbali, kama ambavyo wanatenga fedha kwa kuzingatia masuala mbalimbali ya kuzuia virusi vya UKIMWI pamoja na masuala mengine yanayowekewa mipango katika *MTF*, ni vyema sasa *first priority* katika bajeti zao wahakikishe kwamba kipaumbele kinawekwa katika mafunzo. Tusitafute visingizio na sababu kwamba hakuna fedha. Humo humo katika kidogo, tuone namna gani tunawajengea uwezo watumishi wetu.

Mheshimiwa Mweyekiti, kulikuwa na hoja ya utumbuaji wa watumishi na kwamba utumbuaji huo uchukuaji wa maamuzi ya kinidhamu ulikuwa hauzingatii sheria na umekuwa ukifanywa kwa ukiukwaji na hata umepingwa na Tume ya Haki za Binadamu. Nipende tu kusema kwamba waliotoa hoja hii hususan Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, wanajua kabisa taratibu nzima za maamuzi ya kinidhamu, Sheria Namba 8 ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2002 imeeleza kabisa bayana taratibu. Zaidi ya hapo tunazo Kanuni za Utumishi wa Umma. Ukiangalia katika Kanuni ya 46 na 47 imeeleza bayana ni masuala gani na hatua zipi za kuzingatiwa pindi mamlaka ya ajira na nidhamu inapotaka kuchukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba, hatua hizi za kutengua teuzi, kusimamisha mtu kazi na kuwafukuza kazi zimeelezwa bayana. Ni yule tu mwenye mamlaka ya nidhamu ndiyo anatakiwa kufanya hivyo. Kwa hiyo, niombe sana watu waendeleo kufuata taratibu hizo na zaidi ya yote nisingependa kusikia sehemu zingine inaelezwa mchakato mzima usizidi siku 120 katika hatua za kinidhamu, lakini unashangaa kuna mwingine zaidi ya miezi minne tangu amepewa hati ya mashtaka shauri hilo halijahitimishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana na tunaendelea kuwafuatilia na kwa mwajiri yeyote tutakayembaini amekiuka taratibu, amekiuka masharti ya

Kanuni ya Utumishi wa Umma katika kuchukua nidhamu tutahakikisha tunamchukulia hatua na ajira yake pia itakuwa mashakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende tu kuendelea kusisitiza, hakuna mamlaka yoyote ya nidhamu inayoruhusiwa au inayopata ruksa ya kukiuka haki za watumishi kwa namna yoyote ile. Kwa hiyo, ni vyema tu waajiri wahakikishe kwamba wanazingatia Sheria, wanazingatia Kanuni, Miongozo pamoja na Taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja nyingine kuhusiana na upungufu mkubwa wa watumishi katika sekta ya utumishi wa umma, mifano iliyotolewa ni kada ya afya pamoja na elimu. Waheshimiwa Wabunge walitaka kufahamu Serikali itaajiri lini watumishi wa kada hizo. Hoja hii ilitolewa na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani lakini vile vile Mheshimiwa Rashid Chuachua, Mheshimiwa Bura, Mheshimiwa Atashasta na wengine wengi walilisemea hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana kaka yangu Simbachawene ameanza kuliwekea utangulizi kidogo na niseme tu kwamba kama Serikali tunatambua umuhimu wa kuwa na rasilimali watu inayotosheleza kuweza kuhudumia wananchi wetu kwa utoshelevu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende tu kusema, kama nilivyoeleza katika maelezo ya hotuba yabgu, tayari tulishatoa vibali zaidi ya 9,700 na wameshaingia kazini. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais pia, kwa kuona umuhimu wa Madaktari zaidi ya 258 na tayari Jumatatu wanaingia kazini. Nipende tu kusema huo si mwisho, tunaendelea pia na watumishi wengine katika kada zingine ili kuhakikisha kwamba kweli tunakuwa na utumishi wa umma wenye watumishi wa kutosha. Niwahakikishie tu kwamba kabla ya mwaka wa fedha haujakwisha mtakuwa mkisikia na kushuhudia watumishi katika sekta mbalimbali wakiendelea kuajiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ili kuweza kutoa neno lingine la kutia moyo, katika mwaka ujao tena wa fedha wa 2017/2018 tutaajiri tena kwa nyongeza watumishi wengine 52,436. Kwa hiyo, niwahakikishie tu kwamba kama Serikali tunalionga na tunaendelea kuajiri kwa awamu kwa kuhakikisha kwamba haturudii makosa yale ya wakati ule ya kuwekwa wale watumishi hewa, kurudia makosa ya kuwa na watumishi ambao hawana sifa na weledi unaohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja kwamba Serikali hii imekuwa ni ya kuhakiki tu. Kwa kweli ni hoja ambayo imenishangaza sana mimi. Duniani kote, kama kweli unataka kuwa na utumishi wa umma uliotukuka hutaacha kufanya uhakiki wa rasilimali watu wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi tukakaa tukawa na watumishi wa umma zaidi ya laki tano na arobaini na mbili elfu na mia moja na sabini na sita bila kujua kila mmoja ana sifa na weledi, bila kujua kama kweli *work load analysis* kwa kila sehemu kila mtu ana kazi inayomtosheleza, bila kujua kama kila mmoja anatekeleza majukumu yake inavyotakiwa, bila kujua kama kweli ana sifa na weledi unaotakiwa katika utumishi wa umma, lakini pia bila kujua kama kweli yuko kazini au hayuko kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nipende tu kusema kwamba kwa sasa zoezi la jumla la uhakiki ni kama limeisha lakini uhakiki ni endelevu. Mkija mkisikia uhakiki mwingine unaendelea wala msishangae, tutaendelea kufanya hivyo na wala hatutafanya hivyo kwa kuwa tunaogopa mtu yoyote au kusikiliza maneno kwamba tunatishwa tusifanye uhakiki kwa kuwa Serikali hii itaonekana ni Serikali ya kufanya uhakiki kila kukicha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako ambao walitaka kufahamu uhakiki huu matokeo yake yamekuwaje. Nipende tu kusema kwamba kama mlivyofahamu, zaidi ya watumishi hewa 19,708 waliweza kubainika katika orodha yetu ya malipo ya mishahara na waliondolewa. Endapo

tungewaacha hawa katika ajira ingeigharimu Serikali kila mwezi Shilingi bilioni 19.8, hivi ni fedha ndogo hizo? Si fedha ndogo hata kidogo! Ziko baadhi ya Wizara zingine ndiyo bajeti yake ya mwaka mzima huo. Kwa hiyo nipende tu kusema kwamba Waheshimiwa Wabunge watuelewe, tunapofanya haya tunafanya kwa nia njema kuhakikisha kwamba hakuna mianya hata kidogo na kuhakikisha kwamba fedha za Serikali zinatumika kwa matumizi sahihi ili walipa kodi waweze kujionea manufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hiyo tu, tumewaeleza hapa ajira mpya tutakazozitoa zaidi 52,000 katika mwaka ujao wa fedha. Tunapoendelea pia kutoa watumishi hawa hewa, pia inatengeneza fursa zingine kwa ajili ya watu wengine wahitimu ambao wako nje wanasubiri ajira. Hivi tusingewatoa hawa 19,000 si tungeendelea kuziba ajira? Tunaendelea kila mwezi kulipa zaidi ya bilioni 19.8. Kwa hiyo, nipende tu kuwahakikishia Wabunge pia hiyo ni fursa nyingine kwamba wahitimu wetu wataendelea pia kupata fursa hizo za ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini watu walitaka kufahamu pia kwamba mpaka sasa katika watumishi hawa hewa 19,700 waliondolewa, wale maafisa walioshiriki katika kuhakikisha kwamba watumishi hao hewa wamekuwepo wamechukuliwa hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende tu kusema kwamba katika zoezi zima la kuondoa, tumehakikisha pia kwamba kwa yeyote aliyeshiriki na mpaka sasa tumeshawabaini zaidi wa watumishi 1,595 wa madaraka mbalimbali au ngazi mbalimbali ambao wamehusika katika uwepo wa watumishi hewa katika orodha ya malipo na mishahara na tayari tumeshawachukulia hatua mbalimbali. Wako ambao tayari wana kesi mahakamani, wengine wamechukua hatua nyingine za kisheria na wako ambao wamefukuzwa kazi, lakini zaidi ya yote, zaidi ya bilioni 9.3 zimesharejeshwa Hazina na tunaendelea kufanya hivyo ili kuhakikisha kila fedha iliyochukuliwa basi fedha hiyo itarudi Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja nyingine ya Walimu ambao walipandishwa vyeo na hii inaendana pia na watumishi wengine wa umma, lakini baadaye mshahara wao ukarudi kwenye mshahara wa zamani na watu walitaka kufahamu mishahara hiyo itarekebishwa lini na hiyo ni pamoja na watumishi wa umma waliopandishwa madaraja wakarekebishwa mishahara yao kwa wakati ni nini kitafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende tu kusema, kwanza kabisa wapo ambao walisema miaka mitatu mtu *automatic* ana sifa ya kupanda cheo. Nipende kutofautiana nao, mtumishi anapanda cheo kwa kuzingatia muundo wake wa maendeleo ya utumishi, mtumishi atapanda cheo kwa kuwa ameshatimiza sifa si chini ya miaka mitatu, siyo *fixed* kwamba ni lazima miaka mitatu unapanda.

Pili, ni lazima bajeti hiyo ya wewe kupandishwa cheo iwe imekasimiwa na mwajiri, lakini tatu uwe na utendaji uliotukuka katika kipindi chote hicho na uwe umejaziwa tathmini ya *form* ya *OPRAS* kwa zaidi ya miaka mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nipende tu kusema kwamba tutaendelea kufuatilia na kuhakikisha kwamba watumishi wanapanda kwa kuzingatia sifa na kwa kuzingatia utendaji uliotukuka. Kwa hiyo, kupanda cheo si *automatic*, tutaangalia vigezo hivyo kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, wako kweli ambao walipandishwa hadi kufikia mwezi Juni, 2016. Wako ambao walishapata mshahara uliorekebishwa mwezi mmoja, wako waliopata mishahara iliyorekebishwa miezi miwili, wakarudishwa katika mishahara ya zamani. Nipende tu kusema kwamba, Serikali ilifanya hili kwa nia njema na lengo lilikuwa ni kuwapa fursa Serikali kuweza kuupitia muundo wake upya ili pia kuhakikisha kwamba tunaondoa watumishi wale hewa, lakini pia kutoa nafasi ya kuendelea kuhakiki vyeti vya kidato cha nne, kidato cha sita na vya vyuo vya ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende tu kusema kwamba, tayari zoezi hili limekamilika. Kwa upande wa uhakiki wa vyeti vya kidato cha nne tunategemea mwezi huu litakamilika na matokeo yake naamini mmeshaanza kumsikia Mheshimiwa Rais na tsubiri baada ya hapo ni nini kitakachofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende tu kusema, kwa wale waliopandishwa wote ndani ya mwaka huu wa fedha, wataweza kupandishwa na kurudi katika madaraja yao sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa pia kuna hoja kuhusiana na *TASAF*. Wako ambao, *especially* Kamati, ilisema kuwa kwamba kuna kasoro katika usimamizi, katika utambuzi na katika uandikishaji wa kaya za walengwa wetu wa mpango wa kunusuru kaya maskini. Pia wako Waheshimiwa Wabunge wengi kina Mheshimiwa Nditiye, Mheshimiwa Sikudhani, Mheshimiwa Ikupa na wengine wengi, walieleza hisia zao kwa namna ambavyo waliona zoezi hili kwa namna moja au nyingine utambuzi haukwenda sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wao walitoa maoni zaidi, katika suala zima la kuondoa kaya ambazo zilikuwa hazistahili na hasa walikuwa wanaamini kwamba wako wengine waliondolewa bado ni maskini, lakini mbaya zaidi wametakiwa warejeshe fedha. Nipende tu kusema kwamba, uhakiki huu ulifanyika kwa nia njema na tayari tumeshatoa miongozo katika halmashauri zote nchini pamoja na halmashauri zote za Zanzibar kusitisha kuwaondoa walengwa ambao ni kaya maskini, ambazo ziliingizwa katika mpango kwa kufuata taratibu zote ambazo zilitakiwa na tayari kaya hizo zimeshaanza kurejeshwa kwenye mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya yote, tatizo kubwa lililojitokeza unakuta wengine walikofanyiwa uhakiki walipoonekana hali zao zimeboreka wakaondolewa. Kwa hiyo, tumetoa maelekezo kwamba mtu ataingia kwenye *graduation strategy* baada ya kuwa tathmini imeshafanyika

ili kuhakikisha kwamba kweli hali yake imeboreka na hataweza kurudi katika umaskini. Kwa hiyo, niwape tu *comfort* kwamba wameshaanza kurudishwa na hakuna atakayedaiwa fedha hizo kama kweli mtu huyo ni maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaotaka kuhangaika nao ni wale ambao waliingizwa kama ni kaya zisizo na sifa, ni wale ambao waliingizwa ni watumishi wa umma, ni wafanyabiashara na wenye kipato na wameingizwa na kuonesha kwamba hawana uwezo wakati uwezo huo wanao. Kwa hiyo, niwahakikishie tu kwamba hili litafanyika vizuri na hakuna atakayeonewa lakini zaidi niwashukuru kwa namna ambavyo mmelisemea kwa hisia kubwa na kwa namna ambavyo mmekuwa mkilifuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako Wabunge wengi pia wamekuwa wakilisemea hili, kuhusiana na asilimia 30 ya vijiji vya walengwa wa *TASAF* ambavyo bado havijafikiwa, sasa hivi tumefikia asilimia 70. Kamati ya Bunge imelieleza hili, Mheshimiwa Bobali amelieleza, vile vile Mheshimiwa Rhoda Kunchela naye pia ameweza kulisemea. Nipende tu kusema, mpaka sasa hatujafikia mitaa, vijiji na shehia 5,690.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo letu ilikuwa ni mwaka huu tufanye utambuzi pamoja na uandikishaji lakini bahati mbaya kutokana na ufinyu wa bajeti, zoezi hilo la utambuzi halikuweza kufanyika. Niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge, katika awamu hii ya kwanza itakapomalizika Serikali imetuhakikishia kwamba itatenga fedha kupitia mchango wake wa ndani ili kukamilisha zoezi la utambuzi pamoja na uandikishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa na hoja ya hatua gani zimechukuliwa dhidi ya walio vuruga utaratibu na kuingiza walengwa wa *TASAF* ambao hawastahili. Mheshimiwa Lubeleje, Mheshimiwa Malembeka, Mheshimiwa Maige na wengi tu pamoja na kamati wamelieleza vizuri sana. Kwanza niwashukuru kwa namna ambavyo mmekuwa mkifuatilia, lakini niwaombe pia, kwa kuwa na ninyi ni Madiwani na tumewagawia orodha pia muweze kufuatilia

katika orodha ya ruzuku iliyofika katika maeneo yenu, kujiridhisha kama kweli pia ruzuku hiyo katika mizunguko yote hiyo imefika au haijafika ili muweze kuwa pia jicho na sikio letu kwa niaba ya Serikali huko katika maeneo yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshachukua hatua, zaidi ya waratibu wa mpango 84 walioko katika halmashauri wameshachukuliwa hatua na wamesimamishwa na sasa hawawezi kushughullikia au kuratibu shughuli za *TASAF*. Vilevile Watendaji wa Vijiji pamoja na Kata na Mitaa 156 nchi nzima wamesimamishwa kazi kupisha uchunguzi lakini si hiyo tu hata *TASAF* kwenyewe Makao Makuu kwa sababu nako pia wamehusika katika usimamizi. Zaidi ya watumishi 106 walisimamishwa kazi na hatimaye wameweza kuchukuliwa hatua na wengine wamepewa onyo ili kuhakikisha kwamba upungufu kama huu hauwezi kujirudia tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, watumishi saba waliokuwa makao makuu ambao mikataba yao imekwisha na walionekana pia utendaji wao ulikuwa haujaridhisha nao pia mikataba yao haijaweza kuhuisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja ya Mfuko wa Rais kujitegemea kuweza kuwezesha kifedha. Nipende tu kusema kwamba, tunamshukuru sana Mheshimiwa Mama Kilango, Mheshimiwa Ritta Kabati na wengine wote ambao wameweza kuusemea Mfuko huu wa Rais wa Kujitegemea. Ni kweli ni Mfuko ambao ni wa muhimu sana, ni Mfuko ambao una historia ya muda mrefu, tangu hayati Sokoine mwaka 1984 ambaye alidiriki hata kuchangia sehemu ya mshahara wake, kuweza kuanzisha Mfuko huu. Niwashukuru sana lakini nipende tu kusema kwamba katika mwaka huu tumeutengea Shilingi milioni 500 na tunaamini itaweza kusaidia katika kutimiza malengo yake na Serikali itakuwa ikiongezea fedha kila mara itakapokuwa na uwezo ulioboreka katika Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa kuna hoja ya Mheshimiwa Mama Kilango, kwamba ni lini Mfuko huu wa *PTF* utaanza kutoa huduma zake Kilimanjaro pamoja na mikoa

mingine. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mama Kilango kwamba katika mwaka 2018/2019, *PTF* imejiwekea mipango ya kwenda Kilimanjaro pamoja na Tabora pamoja na mikoa mingine tutakuja kuitangaza huko baadaye. Kwa mwaka huu tutaenda Dodoma, Iringa pamoja na Kagera. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kulikuwa kuna hoja Mfuko huu unaonekana ni wa Muungano, kwa nini haufanyi shughuli zake Zanzibar? Ni hoja nzuri sana. Nipende tu kusema kwamba, Zanzibar upo Mfuko wa Rais wa Kujitegemea pia kupitia SMZ ambao unafanya kazi nzuri, ambacho tunakifanya sasa ni Mifuko hii miwili kuwa na ushirikiano na kuweza kufanya kazi pamoja lakini hoja hii tumeisikia tutaona ni namna gani pia inaweza ikafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja ya Mheshimiwa Kishoa kwamba Serikali hii imekosa utawala bora, kiasi kwamba haipati mikopo, kiasi kwamba haipati misaada. Kwa kweli nipende tu kusema ni hoja ambayo kidogo imenishangaza na inasikitisha. Kwa takwimu zilizopo Waziri wetu wa Fedha amekuwa akifanya majadiliano mengi tu na amekuwa akisaini mikataba mingi tu na mikataba hii imekuwa ikiwa na mafanikio makubwa. Nitoe tu mfano, ukiangalia hadi sasa kupitia Kuwait *Fund* na Serikali wameingia mkataba na zaidi ya dola milioni 51 tayari kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Chaya-Nyahuwa umepitishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba wa *EU* na Tanzania Rais amehakikishiwa fedha zitatoka; lakini nisiende mbali nikienda kwenye *TASAF* tu peke yake, *DFID* imetoa zaidi ya dola milioni 170, ndogo? Benki ya Dunia imetoa zaidi ya dola milioni 420, *Irish Aid* imeahidi kutoa zaidi ya dola milioni 11, *USAID* inatoa dola zaidi milioni 10 hapo sijaenda mbali kwenye Wizara zingine, niangalie tu zinazonihusu kwa harakaharaka. Sijaangalia TAKUKURU, sijaangalia Maadili na kwingineko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nipende tu kusema kwa kweli, hebu tusiupotoshe umma kuonekana kwamba

ni Serikali ambayo haina utawala bora. Utawala bora upo, fedha zimetoka, Abu Dhabi *fund* wametuahidi, barabara zinajengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata huko Iramba kwa Mheshimiwa Kishoa naamini mafanikio yako mengi tu na wananchi wako wanakusikia unaposema uongo, watakapokuja kuona hizo fedha hazipo tutakuja na tutafanya ziara huko Iramba pia kuweza kusema kama ni uongo au ni kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja kuhusiana na semina elekezi kwa viongozi walioteuliwa. Tumekuwa tukifanya hivyo, tukitoa mafunzo kwa kutambua umuhimu wa viongozi wenye uwezo wa kitaalam, lakini ambao wanatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia utawala bora. Kila mara tulipoona inahitajika tumekuwa tukitoa semina hizo na mafunzo kuhakikisha kwamba wateule wetu na watumishi wetu wanapata mafunzo kuhusiana na namna Serikali inavyofanya kazi, wanapata mafunzo kuhusiana na namna Serikali ilivyo na utamaduni wake, kupata mafunzo ya namna ya kuwa mtumishi bora wa umma pamoja na wao kuelewa majukumu yao mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nipende tu kuhakikisha kwamba, tutaendelea kufanya hivyo na hata katika mwaka huu wa fedha tunaoumaliza mpaka Juni zaidi ya viongozi 80 watapata mafunzo na mpaka ikifika Desemba viongozi wote watakuwa wamepatiwa mafunzo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya madai ya malimbikizo na namshukuru kaka yangu Simbachawene ameeleza. Katika madai yasiyo ya mishahara, zaidi ya bilioni 33 zimeshalipwa na imekuwa ikifanya hivyo kila mara. Niwahakikishie tu watumishi wa umma, Serikali yenu inawajali, Serikali yenu inawathamini, tunatambua mchango wenu na kila mara tutaendelea kuangalia maslahi ya umma na kuyaboresha kwa kadri uwezo na bajeti ya Serikali itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu tu katika haya madai mbalimbali, wako baadhi ya watumishi wamekuwa wakiwasilisha madai ambayo si sahihi na ndiyo maana tunasema uhakiki unachukua muda mrefu. Unachukua muda mefu kwa sababu huwezi ukalipa, hii ni fedha ya walipa kodi, ni lazima ujiridhishe kila hela unayoilipa ni hela ile ambayo kweli ndilo deni ambalo ni sahihi na ambalo limepitia katika michakato mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kulikuwa kuna hoja kwamba tuna Makatibu Tawala zaidi ya mmoja katika mkoa, tuna Wakurugenzi Watendaji zaidi ya mmoja..... hilo na tayari kila mmoja kwa nafasi yakena wale wengine wamepangiwa majukumu katika ofisi zao zinazowahusu.

*(Hapa maneno mengine hayakusikika
kutokana na hitilafu ya mtambo)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge na niombe kwa wale ambao sijawataja waweze kuridhika na tutahakikisha kwamba majibu hayo mnayapata kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuhitimisha kwa kuwaomba Waheshimiwa Wabunge mWendelee kuunga mkono hoja hii, ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora na taasisi zake kwa ufanisi katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, hoja imetolewa na imeungwa mkono, mtaiamua baadaye.

Kabla hatujaendelea kuna wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ambao ni Kocha Mkuu wa Singida *United, Hans van der Pluijm*, ameambatana na Afisa Mahusiano wa Singida *United* Ndugu Festo Sanga, karibuni sana. Endeeleni kuinoa Singida *United. (Makofi)*

Katibu!

NDG. RAMADHAN ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MATUMIZI

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge na Wajumbe wa Kamati ya Matumizi muda wetu si rafiki, tuna haya mafungu mengi tunaanza na mafungu yanayosimamiwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Baada ya hapo Bunge litarejea, mtafanya maamuzi kama mtakavyoona inafaa na baadaye tutarejea tena kumaliza mafungu ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Katibu!

NDG. CHARLES MLOKA-KATIBU MEZANI:

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 2 – Tume ya Utumishi wa Walimu

Kif. 1001 – *Administration and HR Management*.....Sh. 1,598,042,495/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud.

MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza muwashe taa, naona mambo si mazuri leo hapa. Kwenye *vote 2* kwenye *subvote 1001 item 221000 travels in country*. Kwenye Tume ya Utumishi wa walimu ningependa kupata ufafanuzi kwenye *vote* hiyo niliyoisema 221000,

kwamba kwenye mwaka 2016/2017 kulikuwa na 383,280,000 lakini mara hii kuna milioni 57, 600,000 tu, kuna upungufu mkubwa kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa upungufu huu kwenye Tume ya Utumishi wa Walimu malalamiko yamekuwa ni mengi, ningependa kupata ufafanuzi wa kina, sababu zipi za msingi zilizosababisha mpaka kupunguzwa kwa fedha hizi karibu milioni mia tatu, 221000? Naomba ufafanuzi wa kina.

MWENYEKITI: Ahsante, kwenye randama umesoma vizuri? Mheshimiwa Waziri! Mheshimiwa Jafo, Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kifungu hicho Mheshimiwa Mbunge kwa sababu anafanya *reference* na ile ya mwaka jana kwamba, fedha ilikuwa nyingi, lakini mwaka huu imeshuka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, mwaka jana ukija katika *sub-votes* nyingine huko mwanzo hazikuwa na fedha zote ziliwekwa sehemu moja. Mwaka huu sasa zitakuwa zinasafiri kutokana na vitengo. Kwa hiyo, tukifika huko mbele utakuja kuona kwamba *travel – in - country* katika sehemu nyingine utakuja kuona kwamba fedha zimepelekwa huko.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2001 – *Recruitment and Development Division*.....Sh. 1,184,406,000/=

Kif. 2002 – *Teachers' Service Commission District*.....Sh. 9,639,843,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 56 – OFISI YA RAIS – TAMISEMI

Kif. 1001 – *Administration and HR Management*.....Sh. 3,557,879,000/=

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Kifungu hicho naona, haya! Kama ilivyo ada naona. Mheshimiwa Masoud, Mheshimiwa Jaffari Michael, Mheshimiwa...

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Oscar!

MWENYEKITI: Mnafahamu, ili nikate ngebe, mnafahamu mimi napenda kutenda haki tu. Mheshimiwa Sakaya!

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Oscar!

MWENYEKITI: Naendelea!

Mheshimiwa Mukasa, Mheshimiwa Salma Kikwete na Mheshimiwa Stanslaus Mabula. Kwa sababu ya muda, mnajua muda, mimi natenda haki. Mheshimiwa Jitu Soni Nafunga huku! Mheshimiwa Jitu Soni. Tunaanza sasa na Mheshimiwa Masoud.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kwenye mshahara wake Waziri. Sina ugomvi naye mkubwa kaka yangu Mheshimiwa Simbachawene, naomba uendele vizuri, lakini nina mambo kidogo, naomba kupata ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Kuboresha Maslahi ya Walimu. Majibu mengi ya Waheshimiwa Mawaziri waliokuja hapa, kuanzia Mheshimiwa Simbachawene mwenyewe na Dada yangu Mheshimiwa Angella Kairuki. Ni kwamba, lengo ni kuonesha namna gani ya kuboresha maslahi ya Walimu. Majibu yenu yalilenga namna gani ya

kupandishwa vyeo lakini pia hamkueleza vizuri namna ya kuchelewa kurekebishwa kwa mishahara yao, mkaeleza kidogo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka niwambie tu kwamba, kuna wale ambao wamekwenda likizo tangu mwaka 2016 hadi leo hawajalipwa. Vilevile jambo kubwa kuliko yote naomba nipate ufafanuzi wa kina, Serikali iliahidi kwamba, itatoa posho ya kufundishia (*teaching allowance*) Tangu mwaka 2012 hadi leo fedha hizo Serikali imeshindwa kutoa; na fedha hizo mnatoa kwa Wakuu wa Shule na Waratibu wa Elimu. Mheshimiwa Jafo kuna siku hapa tuliuliza swali akasema kwamba, wamepewa viongozi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sera ya elimu ya kuboresha maslahi ya Walimu haipo (*teaching allowance*). Walimu hawa mmewapuuza, Walimu hawa wamenyonywa, mmewadhulumu. Kama sikupata maelezo sahihi juu ya Walimu wote nchini kupatiwa kile ambacho Serikali iliahidi (*teaching allowance*); posho ya kufundishia mshahara wenu leo naukamata kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi wa kina, muweke vizuri, tuone kwamba, Walimu wanapata maboresho yao, fedha zao mlizowaahidi tangu mwaka 2012 wanapatiwa!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza niseme tu uachie tu, usihangaike kushika Shilingi ya Mheshimiwa Simbachawene, kwa sababu kwanza ukiangalia katika jitihada mbalimbali ambazo Serikali imezifanya katika posho kama hizi, hata hizo posho za madaraka za wakuu wa shule hazikuwepo huko nyuma. Kwa hiyo, hilo lenyewe ni kuonesha kwamba ni jitihada ambayo Serikali imeifanya mwaka 2014 ikaona umuhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija katika posho ya kufundishia. Ni kweli huko nyuma ilikuwepo, lakini ambacho

kama Serikali sasa tunataka kuangalia kwa mapana yake, kupitia Bodi yetu ya Mishahara na Maslahi tumeanza kufanya tathmini ya kazi na tunakwenda vizuri na Mungu akijalia, *inshallah*, mpaka ikifikia mwezi Mei mwaka huu tunaweza kufika katika sehemu nzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana ukaiona posho tu hiyo ya kufundishia, lakini kunaweza kuwa kuna posho nyingine muhimu ambazo Walimu wangeweza kuhitaji. Kwa hiyo, tunataka tulimalize suala hili kwa mapana yake. Kwa hiyo, tupatie fursa kama Serikali, tutakapomaliza ripoti hiyo, basi tutaweza kuona ni posho za aina ipi kwa Walimu, lakini na watumishi wengine wa umma kwa ujumla wake. (*Makofi*)

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Je, Serikali itakiri kwamba, iliwadanganya Walimu wetu nchini? Ilisema uongo? Kwa sababu moja tu kubwa, kwamba ikiwa mmechukua muda wa miaka mitano hivi sasa, Walimu wanalalamika kwamba mmeweza kutoa fedha kwa Waratibu tu na Wakuu wa Shule, halafu Mheshimiwa Waziri unasema kwamba, kuna mambo ambayo mmeyaanza. Hivi miaka mitano yote Walimu wote nchini ambao binafsi kila siku wanalalamika hamuoni kama mnawadanganya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali iko tayari kutoa sasa *commitment* kwamba, kuanzia lini? Pia, Serikali iko tayari kwamba mtaomba radhi hapa leo mbele ya Bunge kwamba mliwadanganya Walimu? Naomba maelezo ya kina.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme kwamba hakuna cha kuomba radhi, lakini pili niseme, mchakato wa masuala haya ya kimaslahi una hatua zake, si jambo ambalo unaweza kuibuka tu siku moja pia, ukafanya. Nipende tu kumhakikishia Mheshimiwa Masoud, masuala mazima ya maslahi ya watumishi wa umma, wakiwemo Walimu, tunayachukulia

kwa uzito mkubwa na unaostahili. Si hilo tu unaweza ukaanzisha posho halafu badaye ikawa si posho endelevu. Ukaanzisha posho pia ghafla kwa kiwango ambacho baadaye hakihimiliki, ukaanzisha posho labda baadaye inakuletea madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunafanya uhakiki, tunaendelea kulfanyia kazi litakapokamilika basi majibu yataweza kutolewa. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Masoud aweze kuridhika, kama Serikali tunawathamini Walimu na tunatambua ugumu na uzito wa kazi wanayoifanya na tutalichukua kwa mapana yake.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nimekubali, lakini msizoe Serikali, uongo punguzeni. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Sawa tunaendelea, Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie, wakati nachangia, hakuweza kujibu pengine kwa sababu ya muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu waliopata bahati ya kusoma *Bachelor* ya Elimu walikubaliana katika Mikataba yao na Serikali kulipa mkopo wa Serikali, kwa asilimia saba, lakini kwa bahati mbaya sana Serikali kinyemela wamekiuka utaratibu ule na sasa hivi wanawakata asilimia 15 kwenye mishahara yao. Kwa kuangalia hali ya mishahara ni midogo haikidhi mahitaji hivyo Walimu wanapata hali ngumu sana ya maisha kutokana na kipato chao kidogo. Tunaomba Serikali itusaidie kwa nini wanawakata asilimia 15 badala ya asilimia saba ambazo walikubaliana kwenye mikataba yao na Serikali? Ahsante.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ningependa kumpa majibu Mheshimiwa Magdalena Sakaya kama ifuatavyo:-

Kwamba, utaratibu wa marejesho ya mikopo kwanza haukuwepo kwa mujibu wa sheria. Ilikuwa tu kwamba utaratibu unawekwa na Mheshimiwa Waziri Mwenye dhamana. Ukiangalia zamani makato yalikuwa yanakatwa kwa kiasi cha 50,000/= kwa kila mwanafunzi ambaye ni mnufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilipofika mwaka 2011, Waziri mwenye dhamana ndipo kwa kutumia *GN* akaanzisha utaratibu wa asilimia nane. Kwa hiyo, kilichofanyika ni kuyafanya makato hayo yawe kwa mujibu wa sheria na sasa hivi yameingia kwenye sheria, lakini zamani ilikuwa ni Waziri mwenye dhamana anabadilisha utaratibu. Kwa hiyo, hakuna kitu ambacho kimekiukwa.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati hata sisi wenyewe tulisoma pia kwa mkopo wa Serikali, tunashukuru na kuna mikataba tuliingia kwa maandishi na hata hao Walimu pia waliingia mikataba; tuliandika mikataba kabisa. Mikataba ile inasema ni asilimia saba, kwa hiyo kama utaratibu ulikuja kubadilishwa baadaye wangeangalia kwamba mikataba inasemaje kwenye maandishi, lakini kuja kinyemela kwamba unashangaa tu mshahara umekatwa asilimia 15. Kisheria nakubali, lakini pia wangezingatia makubaliano yao na wale wanafunzi wakati wanasoma kwa sababu sasa hivi ni Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni kinyume na utaratibu ambao walikubaliana kwa sababu ni kinyemela, hawajawahi kujulishwa, wanashangaa tu kuwa mishahara yao inakatwa bila kuwepo na utaratibu. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iangalie, pamoja na kuwa imekuja kisheria lakini wazingatie mikataba kwa maana mkataba ni makubaliano na ni ya maandishi sio ya maneno.

MWENYEKITI: Mpeni *assurance!* Mtazingatia maelewano ya mkataba?

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme tu kwamba, hakuna

jambo ambalo Serikali inafanya kinyemela; na sheria zote kabla ya kupitishwa lazima Waheshimiwa Wabunge waridhie. Kwa hiyo, utaratibu umefanyika katika kufuata mujibu wa sheria na taratibu na ulipitishwa hapa Bungeni. Tunafanya makato hayo ili kusudi vijana wengine ambao wana mahitaji ya mikopo waweze pia, kunufaika. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Sawa tunaendelea, Mheshimiwa Michael.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Naomba nijielekeze kwenye suala la kodi ya majengo katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tumepitisha sheria kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2016 kurejesha chanzo cha mapato cha *Property Tax* kwenda Serikali Kuu. Waheshimiwa Wabunge wengi waliochangia katika Hotuba ya Waziri wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI wameonesha kwamba hawajaridhishwa na hali ya ukusanyaji wa mapato katika halmashauri zetu na mojawapo ya chanzo ambacho kimeathiri sana halmashauri ni chanzo cha *Property Tax*. Serikali yenyewe imekiri kwamba, katika bilioni 29 wamefanikiwa kukusanya bilioni 4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa jana tulishauri sana kwamba Serikali isiharakishe kukiondoa hiki chanzo katika halmashauri kwa sababu wanaopaswa kujipanga katika kipindi hiki cha *transition* ili waweze kuhakikisha kwamba wanapokichukua chanzo hiki wanakusanya vizuri. Bahati mbaya Serikali haikukubali na matokeo yake wameshindwa kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba majibu ya Serikali na kama sitaridhika nitashika shilingi ya Mheshimiwa Waziri. Kwamba hawaoni sasa ni wakati muafaka wa kuleta *Finance Bill* yenye marekebisho ya kukirejesha chanzo hiki halmashauri ili sasa zikusanye kwa sababu tayari halmashauri zina *manpower* ya kutosha kukusanya chanzo hiki, zina uzoefu wa muda mrefu wa kukusanya chanzo hiki, kwa misingi hiyo

walipokuwa wanakusanya walikuwa wanafanya vizuri na Serikali imechukua ikafanya vibaya. Je, Waziri ana neno gani katika eneo hili kabla sijaamua kuchukua shilingi yake?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, Serikali iliona ni muhimu na kwa sababu ya mazingira chanzo hiki kikakusanywa na Serikali Kuu (*TRA*) na mchakato huo haukufanyika kwingine, ulifanyika humuhumu ndani ya Bunge kwa kupitisha *Finance Bill* ya Mwaka wa Fedha uliopita. Pia ulibainisha kubadilisha Vifungu vya Sheria ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Sura Namba 287 na 288. Tukakubaliana humu kwamba, Waziri wa Fedha kwa kuwasiliana na Waziri mwenye dhamana ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa wanaweza wakaaainisha baadhi ya halmashauri kwamba, zinaweza kukusanyiwa hizo fedha na *TRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wala si halmashauri zote, maana ni kama inaeleweka kama halmashauri zote, ni halmashauri 30 tu; na sasa hivi ni pamoja na hizi mbili za Ubungo na Kigamboni ambazo zinakuwa 32 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukusanyaji umekwenda vizuri sana ambapo sehemu kubwa ya mchakato ilikuwa ni kuandaa ile *frame work* yenyewe na namna watakavyofanya kazi na kujiandaa, kwa maana ya mfumo. Hata hivyo, hadi sasa taarifa tuliyoitoa ya kama bilioni nne ilikuwa ni taarifa ya ule mwezi siku 15 tu za kwanza walivyoanza maana wameanza kwenye mwezi wa Tatu katikati, lakini huko kote ilikuwa kuna *GN* na inatakiwa ichukue muda wake. Kwa hiyo, mchakato wote wa kisheria umefuatwa ukiwa umeanzia ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimsihi tu Mheshimiwa Jaffari, asiondoe shilingi kwa sababu hiki tunachokizungumza tulikipitisha wote hapa. Sasa kinachotekelezwa sasa ni kitu kilekile ambacho kilipitishwa kwenye *Finance Bill*. Kwa hiyo, ni jambo ambalo lipo na halmashauri hizo ambazo zinakusanyiwa hizo fedha *basically*

kwa mujibu wa sheria inavyosema, fedha ile itarudishwa tena kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwa hiyo si kwamba inakwenda moja kwa moja, walikuwa wanatusaidia kwa sababu wenzetu wana *muscles* nyingi, wana miundombinu mikubwa na wana uwezo mkubwa wa kuweza kukusanya. (Makofi)

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wakati wa majibu ya hotuba yake na Mheshimiwa Naibu Waziri wake wamesema wanataka kuacha *legacy*TAMISEMI. Mojawapo ya *legacy*wanayotakiwa kuiacha TAMISEMI ni kuhakikisha wanasimamia Sheria ya *D by D* ambayo lengo lake ni kuziwezesha halmashauri zifanye kazi zao vizuri na halmashauri haziwezi kufanya kazi vizuri bila kuwa na mapato mazuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo cha *Property Tax* ni mojawapo ya vyanzo muhimu sana katika halmashauri katika mapato. Unasema mmekusanya vizuri, lakini mna *4 billion out of 29 billion*, tena katika halmashauri 30 tu au 32. Maana yake ni kwamba chanzo hicho kimeshindwa kufanya kazi vizuri kama ilivyokuwa halmashauri. Lengo la mabadiliko ni kufanya jambo lililokuwa nyuma kidogo liende mbele zaidi. Haiwezekani mabadiliko yakafanya jambo lililokuwa mbele lirudi nyuma na yaitwe maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kushawishi Bunge lako Tukufu kuishika shilingi ya Mheshimiwa Waziri ili papatikane mjadala mpana kuhusu jambo hili la *Property Tax* ili ikiwezekana tukubaliane kuleta marekebisho ya sheria kama tulivyofanya mwaka jana, ili chanzo hiki kirudi katika halmashauri, kikusanywe na halmashauri kwa sababu, halmashauri zina uwezo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Mmhh! Waheshimiwa Wabunge sawa tu kwamba mnatumia demokrasia yenu kwa mujibu wa kanuni. Wachukueni wale wachache tu, muda si rafiki.

Haya, muda, mimi nazingatia muda na muda mnaujua kwa mujibu wa kanuni. Tunaanza na Mheshimiwa Mtolea.

MHE. MAULID S. A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Yako masuala ambayo kweli, kama tunataka kulijenga Taifa hili ni lazima tukubaliane nayo kwa pamoja ili tuweze kwenda sambamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la *Property Tax*, nichukulie tu mfano lilivyotuathiri sisi Temeke. Kwenye Bajeti ya 2016/2017, tulikuwa tunategemea kukusanya zaidi ya Shilingi bilioni nane kupitia chanzo hiki; na mapema mwaka huo halmashauri iliingia mkopo na *CRDB* ili tuweze kutekeleza miradi yetu ya *DMDP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakopa Shilingi bilioni kumi na tisa tukitegemea kurejesha Shilingi bilioni tano kila mwaka, na sehemu kubwa ya marejesho haya tulikuwa tunategemea tuyapate kupitia hiki chanzo cha *Property Tax*. Tumekuja kwenye bajeti tunarudi Julai, chanzo hiki kimeondolewa. Kwa hiyo, maana yake tumeondolewa Shilingi bilioni nane wakati huohuo tuna deni la kurudisha Shilingi bilioni tano kila mwaka, tunazipata wapi halmashauri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ghafla mnaondolewa shilingi bilioni nane na mna deni la shilingi bilioni tano kila mwaka, tunazipata wapi kama halmashauri? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mpaka sasa hivi kwa kuondoa tu hicho chanzo, maana yake mmetupa deni la Shilingi bilioni tano ambazo hatujui wapi tunazitoa. Sasa kama mmekichukua chanzo hiki, na kibaya zaidi hamkusanyi, maana afadhali mngekuwa mnazikusanya, ukweli ni kwamba, hazikusanywi, na hapo ndipo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Ruth Mollel.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami naungana na Mheshimiwa Japhary kuhusu *Property Tax*. Nasikitika kwa sababu, nilikuwa ni mmojawapo aliyehusika sana na hii Sera ya *D by D*, na Sera hii ya *D by D* lengo lake ilikuwa ni kuteremsha madaraka kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapoteremsha Madaraka kwenye Halmashauri unapeleka na *resources* ambayo ilikuwa pamoja na rasilimali fedha na rasilimali watu. Inaelekea sasa tunarudi nyuma kwa sababu kile chanzo kikubwa cha *property tax* ambacho ndiyo kingepeleka maendeleo maana yake afya, jamii, kila kitu kilichoko kwenye *Local Government*) ina maana inakuwa *compromise*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tulikwenda Iringa. Iringa *TRA* wameshindwa kabisa kukusanya *Property tax*, inabidi sasa wawarudie *Local Authorities* ndio wawasaidie kukusanya *property tax*. Hata inapokusanywa ile *thirty percent* ambayo inatakiwa *irudi kwenye Local Government* hairudi, sasa hizi *Local Government* watawezaje kuendesha maisha na kusimamia huduma za jamii ikiwa Serikali Kuu haitaki kuachia na kuwaruhusu kuwapa na *resources* waweze kuendesha mambo yao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE.FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mchango wangu ni kidogo sana kwenye hilo lakini wa uzito mkubwa sana. Hivi tunajenga nchi mbili tofauti ama tunajenga nchi moja? Serikali Kuu mnaona shida gani kwa Serikali zetu za Mitaa zikiweza kuwa na chanzo cha mapato cha uhakiki zikaweza kujijenga kiuwezo, zikaweza kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo? Au ni kwa sababu sheria zinabadilishiwa njiani baada ya kuona manispaa hizi nyingi zimekamatwa na vyama vingine ambavyo si Chama cha Mapinduzi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini tunajenga nyumba moja kwa nini tunapigania fito? *TRA* ina mamlaka makubwa

sana ya kukusanya kodi katika vyanzo vingine ambayo mpaka sasa hivi bado ina *under capacity* kiasi kwamba kama halmashauri au hizi manispaa zimeshaonesha uwezo wa kukusanya na kweli zilikuwa na uwezo wa kukusanya mara nne kuliko *TRA*; tungezijengea uwezo zaidi ziweze kukusanya zaidi ili *TRA* ika-*focus* na ika-*concentrate* kwenye miradi mingine ya Kitaifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi Halmashauri za Wilaya zinaendelea kuwa mzigo na zitaendelea kuwa mzigo kwa Serikali Kuu kwa sababu ya maamuzi kama haya ambayo yanafanywa kwa misingi ya kiitikadi badala ya kufanya mambo ya msingi ambapo hizi Halmashauri zinakuwa namna gani. Hizi Halmashauri kesho zitakuwa zinarudi CCM, nyingine zitachukuliwa na Chadema, nyingine zitachukuliwa na CUF au vyama vingine. Kama tutakuwa na utamaduni wa kubadilisha sheria katikati kwa sababu tunakomoa vyama fulani, nina hakika hatujengi Taifa moja kwa pamoja, tunakuwa kama tunafanya kazi mbili watu wawili tofauti. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Jitu Soni.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naungana na mfumo huu ambapo tulikubaliana wote hapa kwa kujadili kwa kina kwamba *TRA* ikusanye mapato yote. Hata mapato tuliyopitisha si hii ya *Property Tax* peke yake ni vyanzo vyote, mpaka Leseni, *TANESCO* vyote inatakiwa ikusanywe na *TRA*, *one source* ndiyo inakuwa mkusanyaji mkuu.

Property Tax haijaondolewa kwenye vyanzo vyetu huko Halmashauri, ni kwamba *TRA* itakusanya kwa niaba ya Halmashauri, kama ni bilioni nane ama bilioni tano utarudishiwa hizo fedha zako. Sasa hivi Halmashauri ambazo zimepoteza mimi naungo mkono waendeleo kuidai Serikali yale mapato yaliyopotea wapelekewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikubaliana hapa kwenye *Property Tax* Halmashauri zetu na Manispaa zitashirikiana na TRA mwaka wa kwanza kujenga hiyo mfumo wa *database*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo TRA imefika mahali, kwa mfano Babati, hata kama ni mapato mengine yoyote unaenda kulipa kwenye *container* kwa Wakala hata saa nne usiku. Tunataka *one stop center*, malipo yote uweze kufanya TRA ili kuhakiki kwamba kuna biashara unafanya, TIN namba zote zinahakiwa upya ili hata kodi zingine zote ambazo watu wanakwepa *informal sector* irudi kuwa *formal sector*. Lengo kuu hapa tunataka kwamba mapato yote yakusanywe na *center* moja, Serikali ni moja huduma zote zinazotolewa kwa Wizara zote zinakwenda kufanyika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Kigwangalla.

NAIBU WAZIRI WA AFYA MAENDELEO YA JAMII JINSIA WAZEE NA WATOTO. Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nimeshangaa kwamba eti Mheshimiwa Mbowe anahisi sheria hii imebadilishwa kwa sababu za kisiasa kwa sababu CCM ni chama kikubwa hakiwezi kutishwa na Chama kama Chadema ambacho kina Halmashauri chache mpaka tufikie kubadilisha sheria kabisa kwa sababu ya kuwalenga wao, hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu zilizotufanya tukabadilisha Sheria hii ni kuongeza *effectiveness* kwenye *collection* ya mapato. Kwamba, katika nchi yetu hakuna chombo ambacho kina *best practice* ya kukusanya mapato zaidi ya TRA; na Serikali imeona kwamba katika vyanzo vya mapato vya uhakika ambavyo hatujawahi *exhaust fully* ni pamoja na *property tax*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo Serikali ikaonelea itumie TRA kukusanya tu mapato haya ya *property tax* kwa

ajili ya Halmashauri zetu na baada ya kukusanya kurudisha hizo pesa kule kwenye Halmashauri zenyewe kwa ajili ya matumizi. Kwa hiyo, ile hoja kwamba tunazikata miguu Halmashauri zetu kwa kukusanya kwa kupitia *TRA* haipo kwa sababu mwisho wa siku makusanyo haya yatapelekwa kwenye Halmashauri zenyewe kwa ajili ya kujipangia matumizi yake. Kwa hivyo...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Mwigulu Nchemba.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nami niunge mkono hoja ya Serikali utaratibu huu kuendelea kama ulivyoletwa na Waziri. Sababu ya kwanza kubwa ni kwamba, wenzetu wanaosemea utaratibu kubaki kwenye majiji wanachukulia mifano ya majiji ya nchi za wenzetu ambapo miradi yote mikubwa inatekelezwa na majiji hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nchi yetu hapa hapa Wabunge kila Mbunge akisimama anaomba barabara zake ziende *TANROADS*, anaomba miradi yake mikubwa ya maji ifanywe na Wizara, anaomba miradi mikubwa ya Elimu ifanywe na Wizara, anaomba Zahanati zake zikamilishwe na Wizara. Maana yake ni kwamba lazima fedha hizo zitoke Serikalini. Naongea kwa kuwa nilikuwa Wizara ya Fedha nina kumbukumbu sawa za kila miradi na kila fedha ambazo zinailiwa kwenye halmashauri zetu zinazokuwa zinaliliwa ni zile zilizokusanywa na *TRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, ili tupate haki ya kudai fedha ku-*finance*, bajeti zetu ni lazima tutoe kwanza ruhusa ya *TRA* kukusanya fedha hizo ambazo ndizo tunaweka kwenye bajeti. Hapa tunang'ang'aniana nini kuhusu vyanzo wakati suala hili ni la kibajeti? Sisi tung'ang'anie kudai bajeti ambazo tumetengewa katika Halmashauri zetu na tuwape jukumu hawa wanaoruhusiwa kukusanya hizo fedha,

wakishakusanya sisi twende kwenye bajeti. Kwa sababu kwenye utaratibu ule uliokuwepo hizi zilionekana kama vile ndio fedha za matumizi mengine katika Halmashauri zetu halafu fedha za maendeleo... (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Simbachawene kwa kifupi na baadaye nitampa mwenye hoja tumalize.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka tuelewane tu kwamba Serikali haijanyang'anya chanzo, Serikali Kuu inasaidia mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kusaidia huku uhusiano wa dhana ya *D by D* na mfumo ulivyo ni kama mahusiano ya baba na mtoto. Baba akisema anataka kusaidia mtoto kufanya jambo fulani wewe mtoto unakataa wakati mengine yote unamwomba, mishahara Serikali Kuu inalipa...

MWENYEKITI: Anaweza kwenda kwa mama ee!
(Kicheko)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa miradi maendeleo yote tunafanya na Serikali Kuu inatoa fedha. *OC* za kuendesha Halmashauri inatoa leo hii chanzo hiki kidogo inasema tukusaidie, tena kwa Halmashauri 30 ambazo unasema habari ya upinzani. Mheshimiwa Mbowe *with due respect* za CCM ni karibu robo tatu, za UKAWA ni nne tu, lakini *almost* karibu 28 zote ni za CCM, kwa hiyo dhana hiyo si kweli. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili angalia miradi mikubwa ambayo Serikali imepeleka kwenye maeneo hayo yote. Sasa je tukisema leo hii Serikali Kuu inataka kunyang'anya basi tuangalie pia uwezo mkubwa wa

upelekaji wa *resource* kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa ambayo inafanywa na Serikali Kuu. Ukifanya hiyo *comparison* mtahama kwenye hiyo *reasoning* na kwa hiyo mtakubaliana na mimi kwamba sisi kubwa hapa tudai. Kama utaratibu ni kwamba Serikali Kuu inakusanya ili itupatie tuseme tu ziko wapi hizo fedha, basi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo namwomba sana mtoa hoja ndugu yangu Japharyari hatuna matatizo mimi na yeye, Waziri kivuli, ukinikwamisha mimi na wewe umejikwamisha. Naomba uunge mkono tuendelee. (*Makofi*)

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua wakati mwingine mimi huwa nachanganyikiwa sana nikiwa Bungeni. Wakati gari likirudi nyuma watu wanasema linakwenda mbele, yaani mimi huwa nakuwa *very puzzled* kwa sababu suala la mapato ya Serikali za Mitaa ni la msingi kwa sababu ndizo zinasaidia Serikali Kuu. Sasa mkilipuuza kwa kiwango hicho mnachotaka kulipuuza kuna wakati *ma-ent* mahali ambapo hamtapaamini na mtakuja tena kulalamika hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena, nataka niihakikishie Serikali kwamba chanzo hiki cha *proper tax* hakitakusanywa *for another five years* kwa sababu *mechanism* ya TRA imejitosheleza na vyanzo vyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema hapa ni kwamba, kwanza kuna sura mbili. Kwanza hata Serikali yenyewe mna-*contradict* alichokizungumza Mheshimiwa Mwigulu ndio mtazamo wa Serikali. Kwamba mnataka kuchukua hizi fedha kutoka sehemu moja m-*redistribute* katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtazamo wa kwako Mheshimiwa Simbachawene unadhani kwamba fedha hizi zitakusanywa halafu zitarudishwa katika Halmashauri. Mpaka leo Halmashauri ya Manispaa ya Moshi ambayo ilikuwa inakusanya *seven hundred million* haijapata hata Shilingi moja

na hapa mna *four billion* mlizokusanya, inaendeshaje mambo yake? Mna-*expect* kwamba hiyo hela itapatikana tuidai wapi wakati haijakusanywa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TRA* wameshaonesha kwamba hawana uwezo, hawaambii tu ninyi; hawana uwezo wa kukusanya hii fedha. Kwa hiyo, naendelea kushauri tufanye marekebisho katika *Finance Bill* ya sasa hivi ili hiki chanzo kikusanywe na halmashauri mpaka mtakapojiandaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo niombe kusisitiza kwamba naomba jambo hili liamuliwe na Bunge lako Tukufu ili *record* zikae sawasawa sio kwa lengo la kukomoana ila ni kwa nia ya kutakia nchi hii mema kama ambavyo wewe unaitakia mema. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa Waheshimiwa Wabunge tuiamue hoja hii. Nitawahoji wanaoafikiana na Hoja ya Mheshimiwa Raphael Japhary Michael kwamba suala hili lirejeshwe Bungeni lifanyiwe marekebisho ili *Property Tax* iendelee kukusanywa na Halmashauri zetu, Majiji na Manispaa.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)

MWENYEKITI: Tunaendelea na kundi lingine, Mheshimiwa Salma Kikwete.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote naomba nizipongeze Wizara zote hizi mbili, inayoongozwa na Mheshimiwa Simbachawene na ninyingine inayoongwa na Mheshimiwa Angella Kairuki kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wameifanya kwenye maeneo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka nijielekeze sana kwenye eneo la afya hasa kwenye hospitali ya Sokoine pale Lindi. Kama tunavyofahamu Hospitali ya Lindi ilijengwa miaka ya hamsini na mbili na Hospitali hii ilipojengwa lengo

kubwa lilikuwa ni kuwahudumia watu wachache waliopo pale. Leo hii ile hospitali inahudumia mkoa mzima, maana yangu ni kwamba ndani ya Mkoa wa Lindi hakuna hospitali ya mkoa. Kama ile Hospitali inafanywa ni ya Mkoa je, Hospitali ya Wilaya iko wapi? Sasa ninachoomba nihakikishie kwamba ni lini Lindi itapata hospitali ...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS,TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kama alivyosema Mheshimiwa Salma Kikwete ni kweli hospitali ile ni hospitali ya siku nyingi sana imejengwa miaka ya hamsini na kweli kwamba ilikuwa kwa madhumuni ya kuhudumia watu wachache na si hospitali hasa ya mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini imeenda ikibadilika kwa hatua mbalimbali na ilikuwa inakwenda ikijengewa uwezo mbalimbali mpaka ikafikia hatua ya kuwa na baadhi ya maeneo ambayo yana sifa ya kufanya huduma hizo za Mkoa. Kwa kuwa sasa pale Lindi hatuna hospitali nyingine kubwa ya kiwango kile nipende tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba ni utaratibu wetu wa Serikali, yapo maeneo ambayo yalikuwa zahanati, zikawa vituo vya afya, zikawa hospitali za Wilaya na baadaye zikawa za Mikoa kwa mujibu wa historia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia yapo maeneo ambayo hospitali hizi hizi za kawaida za Wilaya zimebadilishwa kuwa za Mikoa. Utaratibu huu ni ule wa kukua taratibu taratibu. Kwa hiyo Serikali kadri inapopata uwezo imekuwa ikizijengea uwezo na baadaye zinakuwa na hali hiyo iko katika maeneo mengi. Kwa hiyo nimsihi tu kwamba ile sasa inaitwa ya mkoa na sasa kama kunahitajika Hospitali ya Wilaya tuone wao watakavyopanga *Priority* za kuanzia kule Lindi kwenye Halmashauri na wakileta mapendekezo yao kwa mujibu wa bajeti na ukomo wa bajeti tunaweza kuanzisha mradi wa kujenga hospitali nyingine ya Wilaya ili kuziba *gape* ya hospitali ya Wilaya katika eneo lile.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Salma Kikwete umeridhika naona.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi nimeridhika na majibu haya, lakini nataka nimwaarifu Mheshimiwa Waziri kwamba mara baada ya kumaliza Bunge hili la bajeti tutaleta taarifa kwenye Wizara yake juu ya suala zima la Hospitali ya Wilaya. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kipekee tu na mimi nitumie nafasi hii kumshukuru na kupongeza Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri na leo tu ametukumbusha historia, ametufundisha lakini pia ametukumbusha wajibu wetu, tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijielekeze tu kwenye suala dogo la ukusanyaji la mapato ya ndani. Kama ambavyo nilishauri, kwamba ukusanyaji wa fedha za mapato ya ndani tunaweza tukautumia kwa njia nyingine mbadala. Nikasema kwa kuwa sasa hivi wafanyabiashara ndogo ndogo (wamachinga) wameenea sana kwenye maeneo ya majiji, manispaa na miji bado kwa namna ya kipekee wafanyabiashara hawa badala ya kuwabezana na kuwaona watu wasiokuwa na thamani wanaweza kuwa *source of income* kubwa sana kwenye *own source* kwenye Halmashauri zetu za miji na majiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutalikubali hili litatusaidia sana kuongeza mapato kwenye halmashauri zetu. Pia fedha hizi ambazo wao watalipa kodi zitasaidia kwenda kuwajengea miundombinu. Kwa msingi huu licha ya kuwajengea miundombinu zitasaidia kuongeza kuinua kipato kwenye mitaji...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakusudia kutoa Shilingi kwenye mshahara wa Mheshimiwa Waziri kama majibu hataniridhisha sana. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba mawazo ya Mheshimiwa Mabula ni mazuri sana na kama Halmashauri zetu zitatumia ile kama fursa Wamachinga wale wana uwezo wa kuchangia pato kubwa sana ya hizi Halmashauri zetu kama kutawekwa utaratibu nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi kama Serikali tunauchukua na tutahakikisha kwamba tunaweka mfumo mzuri kwa kuhakikisha kuwa tunatambua shughuli hizi za Wamachinga na kuziwekea utaratibu mzuri, usiwe kero kwa watu wengine; lakini pia wakachangia mapato ya ndani ya Halmashauri na uchumi wa Taifa kwa ujumla. Kwa hiyo wazo lake tunalichukua Mheshimiwa.

MWENYEKITI: Mnalichukua kwa maana kwamba mtatoa Waraka au?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo, tutatoa waraka wa maelekezo mahsusi wa namna ya kufanya ili kuweza ku-*manage* hilo kundi kwa ajili ya kuongeza ajira, lakini pia kwa ajili ya kuongeza pato la Halmashauri. (*Makofi*)

MHE. STANLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ingependeza sasa Mheshimiwa Waziri kwa sababu atatoa waraka watuambie muda, pia waraka huu uwe ni wa maelekezo thabiti ya kile ambacho Mheshimiwa Waziri amekizungumza, usije ukakiukwa kama nyaraka nyingine ambavyo zimekuwa zikikiukwa na kuacha kutekeleza yale

yaliyokusudiwa. Naomba sasa Mheshimiwa Waziri anithibitishie ili niweze kuona kama nisiondoe ile Shilingi. Ahsante.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali hii ya Awamu ya Tano inatambua na kuthamini mchango mkubwa unaofanywa na Wajasiriamali wadogo wadogo katika uchumi wa nchi hii. Sisi tunaitumia hii kama fursa na kwamba tutakapotoa waraka huo tuko tayari hata kutoa Semina kwa Wabunge wote ili tusaidiane namna ya kuli-*treat* kundi hili kwa sababu *mistreatment* zimekuwa ni nyingi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, Bunge lipo, Serikali ipo, kama litachelewa mtahoji. Tunaendelea, Mheshimiwa Jitu Soni.

MHE. JITU V. SONI: Mwenyekiti ahsante. Kwanza niwapongeze Waziri, Naibu wake na *team* nzima ya TAMISEMI kwa kazi nzuri sana wanayoifanya kwa kuleta matumaini makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilishauri kwamba kwa sehemu kubwa katika shughuli hizi ambazo tunazifanya huko kwenye TAMISEMI, kwenye halmashauri zetu na kwenye mikoa, hatutumii kwa sehemu kubwa takwimu kufanya na kupanga maendeleo. Naomba Waziri atuhakikishie kwamba atatoa waraka au elimu ili kazi zote ambazo tunaenda kupanga huko ziweze kutumia takwimu ambazo zipo; si kwamba hazipo; ili tuweze kupanga maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi sehemu kubwa tunafanya kazi ya kuzima moto. Kwa mfano mwaka wa jana tulimaliza tatizo la madawati, lakini mwaka huu bado limerudia pale pale kwa sababu hatukupanga kwamba mwaka huu ni wangapi wataingia darasa la kwanza au wataingia chekechea au sekondari. Hivyo hivyo kwenye zahanati pamoja na kwenye vituo vya afya. Sasa suala la

takwimu ni muhimu sana, naomba watuhakikishie kwamba litatumika ili wakati tunapanga maendeleo takwimu zitumike.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SEREKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ushauri wake ni ushauri mwema kwetu sisi Serikali; ndiyo maana hapa ukiangalia kuna majedwali mengi sana yanayoelezea takwimu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, hivi sasa ofisi yetu imefanya mabadiliko makubwa sana katika kitengo chetu cha *TEHAMA*. Pale sasa kuna utaratibu wa takwimu wa sekta mbalimbali kuanzia sekta ya afya hali kadhalika na sekta ya elimu na mambo mengine. Lengo letu ni kwamba tunapofanya maamuzi sasa tufanye maamuzi halisia kutokana na hali halisi iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumza hapa kwamba sasa hivi; hata Mheshimiwa Waziri wangu hapa nakumbuka kwamba alizindua ile Tovuti yetu ambayo ipo chini ya TAMISEMI; kikubwa zaidi tunataka tupate takwimu za hali halisi ya kila maeneo ili tuweze kupanga mipango inayotekelezeka, itakayojibu matatizo ya wananchi. Kwa hiyo Mheshimiwa Jitu Soni nimwambie kwamba hoja yake ni hoja ya msingi na sisi tumeshawekeza vya kutosha katika kitengo chetu cha *TEHAMA* ili eneo hilo tulifanye vizuri zaidi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jitu V. Soni unaafiki taarifa hiyo.

MHE. JITU V. SONI: Nashukuru na nakubaliana kazi wanayofanya lakini watuhakikishie itafika ngazi ya chini, Halmashauri na kwenda uko chini zaidi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SEREKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo hakikisha yetu na tutaenda mbali zaidi, tutatumia hadi simu za mikononi.

MWENYEKITI: Sawa, mwisho Mheshimiwa Oscar Mukasa.

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naungana na wenzangu kupongeza kazi nzuri ya Wizara zote mbili, lakini tunawajibu wa kuboresha, ndiyo kazi iliyotuleta hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najikita kwenye suala mahsusi la kushuka kwa mapato ya ndani kwenye halmashauri zetu, lakini lina mambo mawili madogo ndani yake. Moja, kwenye hotuba ya Waziri wa TAMISEMI ukurasa wa nane mpaka wa tisa anaongelea namna ambavyo kwa wastani makusanyo ya ndani ya Halmashauri yamekuwa ni asilimia hamsini na mbili tu...

MWENYEKITI: Mheshiwa nikukumbushe ni jambo moja tu mahsusi.

MHE. OSCAR R. MKASA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni asilimia 52 tu makusanyo ya ndani. Sababu ya makusanyo ya ndani kuwa chini zinaweza kuwa kadhaa. Moja baadhi ya vyanzo kuhama kutoka Halmashauri kwenda Serikali Kuu, mbili labda makadirio ya juu kuliko hali halisi, tatu kutokuwa fursa zote za kuzalisha mali na kuzalisha huduma ndani ya Halmashauri kuwa zimetumika. Mheshimiwa Mabula ametoa mfano wa fursa ya Wamachinga tu lakini ukiangalia kwenye Halmashauri zetu ziko fursa nyingine nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano unakuta halmashauri ina wafugaji ambao wapo tayari kuzungumza na Serikali ili kufanya mifugo yao ifanyiwe miundombinu ya kuifuga kwa namna ya kisasa na kulipa kodi lakini

Halmashauri na Serikali Kuu upande huu hawauoni wanaona upande wa kutumia nguvu tu na kukimbizana nao. Ama kwenye Halmashauri fulani kuna vijana wanaosha magari mahali ambapo kwa siku wanaosha magari 50 lakini wanachafua mazingira. Halmashauri... (*Makofi*)

(*Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

MWENYEKITI: Ahsante Sana Mheshimiwa.

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakusudia kukamata shilingi kama sitopata majibu sahihi.

WAZIRI WA INCH OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SEREKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba liko tatizo katika ukusanyaji wa mapato ya Mamlaka ya Serika za Mitaa kwenye baadhi ya Halmashauri. Lakini ni kweli kwamba *under collection* hii inatokana na sababu mbalimbali na moja wapo ni hiyo aliyoisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vyanzo vya mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa vipo kwa mujibu wa Sheria ya fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa na vimetajwa vyote. Kwa hiyo, Serikali za Mitaa haibuni vyanzo kila siku, ina vyanzo vyake na vimetajwa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Mamlaka na za Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, utekelezaji tu ndio unaotofautiana kwa eneo moja na eneo lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine kubwa la kupotea kwa mapato mengi ya Halmashauri ni pale ambapo kuna *conflict of interest*. Tumeelekeza Serikali kwamba fedha zote za mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinapokusanywa hata kama mme-*outsource* mkapata mkusanyaji lazima ziwekwe kwenye akaunti za Halmashauri. Hata hivyo, Halmashauri zingine wanafanya kama kwa makusudi hivi hawataki ziingie kwenye akaunti za Halmashauri. Unakuta pale gwiji mmoja amekaa

anakwambia mimi ndiye Mwenyekiti wa Halmashauri, mimi ndiye Meya pale, anasema chanzo hiki hakiwezi kuingia kwenye Halmashauri, ziko Halmashauri hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini unapata shida zaidi pale unapokuta wakati mwingine hata Mbunge anashiriki. Kwa hiyo, kwenye vyanzo vya Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuna matatizo mengi na kubwa ni *conflict of interest*. Kwa hiyo, niwasihi sana Waheshimiwa Wabunge kwamba tuache wataalam wetu wakusanye haya mapato kwa utaratibu unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikubaliane naye kwamba namna bora ya ukusanyaji nayo ni jambo la msingi na kwa hivyo tutazisihia na kuzielekeza Mamlaka ya Serikali za Mtaa kuhakikisha kwamba zinakuwa na mikakati mizuri kwa mujibu wa sheria na vyanzo vilivyoainishwa kwa mujibu wa sheria kuhakikisha kwamba vinakusanya kwa taratibu mzuri maana wengine wanaacha kwa makusudi au wengine wanakusanya kwa fujo kwa sababu ya kutaka kukomoa watu; haya yote hayatakiwi kwa sababu kodi lazima idaiwe kirafiki.

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sijaridhika hapo. Kwa kauli ya Mheshimiwa Waziri ambayo ni kweli, kwamba mapato ya Halmashauri yanaratibiwa na sheria, hii inatudhibitishia kwamba halmashauri zimefungwa haziruhusiwi kufikiri kuongeza vyanzo vipya vya mapato. Maana yake tutaendelea kugombania kama tunavyogombania hapa, Mheshimiwa Mbowe anagombania na Serikali kwa sababu kule chini haturuhusiwi kufikiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri angalau utupe kusudio la kuleta mabadiliko ya sheria ili tufunguke na sisi turuhusiwe kufikiri kwa sababu fursa zipo, tukizileta mbele mkaona zinawafaa nyie, hakuna shida mtachukua, sisi tutabuni nyingine kwa sababu zipo nyingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba utoe kusudio la kuturuhusu kuleta marekebishi ya sheria ili hata walio ngazi ya Wilaya turuhusiwe kufikiri na kuongeza vyanzo ili tusigombanie vilivyopo, bado nakusudia kukamata Shilingi.

MWENYEKITI: Saa ngapi muda ndo ulikuwa ni huo.

MHE. OSCAR R. MKASA: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja ya kukamata Shilingi, naomba ijadliiwe.

MWENYEKITI: Haya! Ngoja Waziri ningelipenda akujibu kwa sababu hili ni suala zuri tu umejenga hoja ya msingi. Naamini Serikali ina jibu. Imeshaunga mkono kama unataka kuendelea, lakini ukiridhika wewe si unaitoa wewe kwa idhini ya Kamati.

WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SEREKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namsihi Mheshimiwa Mukasa; mimi najua yeye ni mweledi na ni msomi mzuri. Nilivyosema kwamba Sheria hizi za Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mtaa zimeainisha vyanzo. Kifungu cha 7 kinazungumzia *Sources of Revenue of District Councils*. Yaani ime-*exhaust* popote utakapocheza hata kwenye vyanzo hivyo vingine unavyosema unataka kuvitafuata ukivileta, kwa *nature* ya hii Sheria zipo zingine ni *general provision* ambayo inakupa wigo tena wa kuweza kubuni vingine na Vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sidhani kama unaweza kutoka nje ya hiki kifungu namba 7 ambacho kimeanza na (a) imefika mpaka (z). Yaani imekwenda ikamaliza (x) kutoka (a) mpaka (z) ikaanza (aa), (ab); yaani *exhaust*. Kwa hiyo, nikusihi tu kwamba chanzo chochote unachokitaka hatukatai wala hatubishani. Kama kuna chanzo sawa kaieleze Halmashauri yako na haya kayaseme kule ili uwaongeze vyanzo. Ukiiangalia hapa naamini itaku-*accomodate* tu hicho unachokisema na kule Halmashauri yako itakusanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna ugomvi na Serikali, kwamba eti Serikali inakataa vyanzo, hapana, sisi tunakubali tu na wala asitoe shilingi wala kusiwe na mjadala kama anavyo vyanzo aniletee, kama atahitaji mimi nisaidie kuelezea Halmashauri yake, nitaelezea, kama ni yeye atafanya hivyo afanye. Kwa hiyo, wala hakuna tatizo wala hakuna mgogoro hapo Mheshimiwa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mukasa baada ya maelezo haya na Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa kifungu cha 7 kilivyo kipana nadhani unaweza ukakubaliana na Serikali ondoa tu hoja yako kwa idhini ya Kamati tuendeleo mbele.

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana naomba tujadili. (*Makofi*)

MWENYEKITI: tunaanza Mheshimiwa Keissy

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa taarifa ya Mheshimiwa Waziri anasema tunaweza kukaa kwenye Halmashauri tukaanzisha vyanzo. Tumepiga kelele hapa Bungeni, kodi ya mifugo ilikuwepo tangu zamani lakini tukaifuta. Halmashauri zetu zinataka kodi ya mifugo irudishwe kule kwetu ili tupate vyanzo maana vyanzo vyote viko Serikali Kuu, sisi wengine hatuna vyanzo vyovyote kwenye Halmashauri zetu. Mifugo imekuwa mingi, tuna laki moja elfu hamsini katika Wilaya yangu hailipi kodi; tunataka kodi ya mifugo katika Wilaya ya Nkasi mara moja. Halmashauri yetu ikapange kodi kama ng'ombe shilingi ngapi, turuhusiwe kupanga kodi. (*Makofi*)

MHE. JOSEPH SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kodi ni suala linalotakiwa kufanyiwa study kidogo. Ningeomba Serikali tu-*commission study* tuangalie hali halisi nchini kuhusu hivi vyanzo. Inawezekana tukaachiwa sisi tutengeneze vyanzo vikawa ni kero kwa wananchi wetu. Ningeomba sana tujitahidi tuangalie ukweli halisi, hali halisi ya nchi yetu; na kwa sababu eneo moja kwenda eneo lingine kuna tofauti; kuna wengine wana ng'ombe wengine

hawana, kuna wengine wana kahawa. Leo kwenye kahawa kuna tozo nyingi sana, mimi nataka zitoke, kuna wengine wanapenda zije. Kwa hiyo, nasema ingekuwa ni vizuri tu-*commission study* ili tusiamue bila kuwa na *study*, tunaweza tukafika matatizo na badaye tukarudi kwenye kutaka kuifuta tena. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kanyasu.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza naunga mkono hoja ya Serukamba na Mheshimiwa Keissy lakini nataka kusema kwamba mara nyingi sana ukitazama migogoro mingi ambayo kuna maeneo mifugo ni mingi ni kwa sababu *perception* ya Serikali kwamba mifugo ni mzigo na imekuwa ni mzigo na imekuwa ni mzigo kwa sababu haina *direct income* ambayo inaonekana kuingia Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoshauri na ambacho nakubaliana nacho, kama Serikali iliondoa kodi ile kwa maana ya kuwafurahisha wafugaji na wafugaji wenyewe wapo tayari waweze kuletewa miundombinu kulipa kodi ,ni vizuri sasa atoe ruhusa Mheshimiwa Waziri Halmashauri zenye mifugo zikae upya na wafugaji waweze kulipia na waweze kuwekewa miundombinu waachane...(Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Freeman Mbowe

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sipo mbali na wazungumzaji watanguliaji, lakini nisisitize jambo moja tu la msingi sana. Mfumo ambao tunao sasa hivi wa ukusanyaji wa mapato katika Halmashauri za Wilaya unaua *Local Initiative*. Serikali Kuu kama itaendelea kujilimbikizia vyanzo vyote vya mapato na vilevile kutoa amri ikubali ama ikatae *Local Government* zifanye nini tutakuwa hatufiki. Nitoe mifano miwili tu *Specific*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jiji la Moshi limeomba kujenga *bus terminal* kwa muda mrefu, miaka zaidi ya minne tunabishana hapa na Serikali kuhusu kutoa kibali kwa manispaa ya Moshi kujenga *bus terminal*. Sasa wanasema lazima mamlaka ama ruhusa itolewe na Waziri, ruhusa haitolewi.

Kif. 1015 - *Information and Comm.
Tech. Unit*.....Sh. 52,000,000/=

Kif. 2001 - *Planning and Coordination*.....Sh. 36,000,000/=

Kif. 2002 - *Economic and Productive
Sector*.....Sh. 8,776,000/=

Kif. 2004 - *Social Sector*.....Sh. 126,094,000/=

Kif. 2005 - *Local Govt. Mgt Services*.....Sh.160,000,000/=

Kif. 2006 - *Education Sector*.....Sh. 24,463,000/=

Kif. 2007 - *Water Sector*.....Sh. 41,575,000/=

Kif. 3001 - *Regional Hospital*.....Sh. 850,000,000/=

Kif. 8091 - *Local Gvt. Authorities*.....Sh. 45,607,824,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

FUNGU 76 – MKOA WA LINDI

Kif. 1001 - Administration and HR Mgt.....	Sh. 45,000,000/=
Kif. 2001 - Planning and Coordination.....	Sh. 61,202,000/=
Kif. 2002 - Economic and Productive Sector.....	Sh. 10,175,000/=
Kif. 2003 - Infrastructure Sector.....	Sh. 1,199,160,000/=
Kif. 2004 - Social Sector.....	Sh. 155,917,000/=
Kif. 2005 - Local Gvt. Mgt. Services.....	Sh. 170,000,000/=
Kif. 2006 - Education Sector.....	Sh. 24,463,000/=
Kif. 2007 - Water Sector.....	Sh. 37,575,000/=
Kif. 8091 - Local Govt. Authorities.....	Sh. 26,372,397,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

FUNGU 77 – MKOA WA MARA

Kif. 1001 - Administration and HR Mgt.....	Sh. 50,000,000/=
Kif. 2001 - Planning and Coordination.....	Sh. 185,000,000/=
Kif. 2002 - Economic and Productive Sector.....	Sh. 25,000,000/=
Kif. 2003 - Infrastructure Sector.....	Sh. 2,665,537,000/=
Kif. 2004 - Social Sector.....	Sh. 133,549,000/=
Kif. 2005 - Local Government Management Services.....	Sh. 160,000,000/=
Kif. 2006 - Education Sector.....	Sh. 24,463,000/=
Kif. 2007 - Water Sector.....	Sh. 37,371,000/=
Kif. 3001 - Regional Hospital.....	Sh. 0
Kif. 8091 - Local Govt. Authorities.....	Sh. 42,719,427,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

FUNGU 78 – MKOA WA MBEYA

Kif. 1001 - Administration and HR Mgt.....	Sh. 469,135,000/=
Kif. 2001 - Planning and Coordination.....	Sh. 449,689,000/=
Kif. 2002 - Economic and Productive Sector.....	Sh. 15,242,000/=

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Kif. 2005 - <i>Local Govt Management Services.....</i>	Sh. 160,000,000/=
Kif. 2006 - <i>Education Sector.....</i>	Sh. 24,463,000/=
Kif. 2007 - <i>Water Sector.....</i>	Sh. 29,516,000/=
Kif. 3001 - <i>Regional Hospital.....</i>	Sh. 826,094,000/=
Kif. 8091 - <i>Local Govt. Authorities.....</i>	Sh. 51,222,598,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 79 – MKOA WA MOROGORO

Kif. 1001 - <i>Administration and HR Mgt.....</i>	Sh. 1,800,000,000/=
Kif. 1005 - <i>DAS-Morogoro.....</i>	Sh. 10,000,000/=
Kif. 1006 - <i>DAS-Kilosa.....</i>	Sh. 5,000,000/=
Kif. 1007 - <i>DAS-Kilombero.....</i>	Sh. 10,000,000/=
Kif. 1008 - <i>DAS-Ulanga.....</i>	Sh. 5,000,000/=
Kif. 1009 - <i>DAS-Mvomero.....</i>	Sh. 5,000,000/=
Kif. 1010 - <i>DAS-Gairo.....</i>	Sh. 5,000,000/=
Kif. 1011 - <i>DAS-Malinyi.....</i>	Sh. 5,000,000/=
Kif. 2001 - <i>Planning and Coordination.....</i>	Sh. 65,000,000/=
Kif. 2002 - <i>Economic & Productive Sector.....</i>	Sh. 0
Kif. 2005 - <i>Local Govt. Mgt .Services.....</i>	Sh. 190,000,000/=
Kif. 2006 - <i>Education Sector.....</i>	Sh. 0
Kif. 2007 - <i>Water Sector.....</i>	Sh. 45,287,000/=
Kif. 3001 - <i>Regional Hospital.....</i>	Sh. 133,549,000/=
Kif. 8091 - <i>Local Govt. Authorities.....</i>	Sh. 57,272,296,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 80 – MKOA WA MTWARA

Kif. 1001 - <i>Administration and HR Mgt.....</i>	Sh. 540,000,000/=
Kif. 2001 - <i>Planning and Coordination.....</i>	Sh. 490,000,000/=
Kif. 2004 - <i>Social Sector.....</i>	Sh. 165,575,000/=
Kif. 2005 - <i>Local Govt Management Services.....</i>	Sh.160,000,000/=
Kif. 2006 - <i>Education Sector.....</i>	Sh. 0
Kif. 2007 - <i>Water Sector.....</i>	Sh. 43,575,000/=

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Kif. 3001 - *Regional Hospital*.....Sh. 300,000,000/=

Kif. 8091 - *Local Govt. Authorities*.....Sh. 50,123,741,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, muda wetu naona unakimbia, naongeza muda usiozidi dakika 30 ili shughuli hii iendelee. Natambua kwa sababu tuna Mafungu mengine itabidi hoja itolewe na Serikali kwa mujibu wa Kanuni hizi ili tuweze kukaa hadi hapo tutakapomaliza shughuli iliyo mbele yetu. Tunaendelea.

FUNGU 81 – MKOA WA MWANZA

Kif. 1001 - *Administration and HR Mgt*.....Sh. 55,000,000/=

Kif. 2001 - *Planning and Coordination*.....Sh. 55,500,000/=

Kif. 2002 - *Economic and Productive
Sector*.....Sh. 11,000,000/=

Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*..... Sh. 2,305,500,000/=

Kif. 2004 - *Social Sector*.....Sh. 129,822,000/=

Kif. 2005 - *Local Gvt. Mgt. Services*..... Sh. 170,000,000/=

Kif. 2006 - *Education Sector*.....Sh. 23,000,000/=

Kif. 2007 - *Water Sector*.....Sh. 41,409,000/=

Kif. 3001 - *Regional Hospital*.....Sh. 0

Kif. 8091 - *Local Govt. Authorities*.....Sh. 64,938,148,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

FUNGU 82 – MKOA WA RUVUMA

Kif. 1001 - *Administration and HR Mgt*.....Sh. 1,458,000,000/=

Kif. 2001 - *Planning and Coordination*.....Sh. 0

Kif. 2002 - *Economic & Productive Sector*.....Sh. 2,000,000/=

Kif. 2004 - *Social Sector*.....Sh. 129,822,000/=

Kif. 2005 - *Local Govt. Mgt. Services*.....Sh. 160,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Kif. 2006 - <i>Education Sector</i>	Sh. 0
Kif. 2007 - <i>Water Sector</i>	Sh. 37,575,000/=
Kif. 3001 - <i>Regional Hospital</i>	Sh. 150,000,000/=
Kif. 8091 - <i>Local Govt. Authorities</i>	Sh. 52,572,050,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 83 – MKOA WA SHINYANGA

Kif. 1001 - <i>Administration and HR Mgt</i>	Sh. 35,000,000/=
Kif. 2001 - <i>Planning and Coordination</i>	Sh. 75,000,000/=
Kif. 2002 - <i>Economic and Productive Sector</i>	Sh. 20,000,000/=
Kif. 2003 - <i>Infrastructure Sector</i>	Sh. 1,282,835,000/=
Kif. 2004 - <i>Social Sector</i>	Sh. 227,775,000/=
Kif. 2005 - <i>Local Govt. Management Services</i>	Sh. 140,000,000/=
Kif. 2006 - <i>Education Sector</i>	Sh. 24,000,000/=
Kif. 2007 - <i>Water Sector</i>	Sh. 3,000,000/=
Kif. 3001 - <i>Regional Hospital</i>	Sh. 0
Kif. 8091 - <i>Local Govt Authorities</i>	Sh. 38,045,928,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 84 – MKOA WA SINGIDA

Kif. 1001 - <i>Administration and HR Mgt</i>	Sh. 1,615,000,000/=
Kif. 2001 - <i>Planning and Coordination</i>	Sh.141,400,000/=
Kif. 2002 - <i>Economic & Productive Sector</i>	Sh.8,000,000/=
Kif. 2004 - <i>Social Sector</i>	Sh. 126,094,000/=
Kif. 2005 - <i>Local Govt. Mgt Services</i>	Sh. 140,000,000/=
Kif. 2006 - <i>Education Sector</i>	Sh. 20,000,000/=
Kif. 2007 - <i>Water Sector</i>	Sh. 37,575,000/=
Kif. 3001 - <i>Regional Hospital</i>	Sh. 1,515,600,000/=
Kif. 8091 - <i>Local Govt. Authorities</i>	Sh. 32,949,716,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 85 – MKOA WA TABORA

Kif. 1001 - Administration and HR Mgt.....	Sh. 918,112,000/=
Kif. 2001 - Planning and Coordination.....	Sh.111,500,000/=
Kif. 2002 - Economic and Productive Sector...	Sh. 7,000,000/=
Kif. 2004 - Social Sector.....	Sh. 129,822,000/=
Kif. 2005 - Local Govt. Mgt. Services.....	Sh. 170,000,000/=
Kif. 2006 - Education Sector.....	Sh. 24,463,000/=
Kif. 2007 - Water Sector.....	Sh. 46,000,000/=
Kif. 3001 - Regional Hospital.....	Sh. 300,000,000/=
Kif. 8091 - Local Govt. Authorities.....	Sh. 51,738,166,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 86 – MKOA WA TANGA

Kif. 1001 - Administration and HR Mgt.....	Sh. 1,928,280,000/=
Kif. 2001 - Planning and Coordination.....	Sh. 153,200,000/=
Kif. 2005 - Local Govt. Management Services.....	Sh. 200,000,000/=
Kif. 2006 - Education Sector.....	Sh. 29,120,000/=
Kif. 2007 - Water Sector.....	Sh. 140,327,000/=
Kif. 3001 - Regional Hospital.....	Sh. 1,141,005,000/=
Kif. 8091 - Local Govt. Authorities.....	Sh. 56,752,198,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 87 – MKOA WA KAGERA

Kif. 1001 - Administration and HR Mgt.....	Sh. 1,174,355,000/=
Kif. 2001 - Planning and Coordination.....	Sh. 50,000,000/=
Kif. 2002 - Economic and Productive Sector...	Sh. 5,677,000/=
Kif. 2003 - Infrastructure Sector.....	Sh. 0
Kif. 2004 - Social Sector.....	Sh.129,822,000/=
Kif. 2005 - Local Govt. Management Services.....	Sh. 190,000,000/=
Kif. 2006 - Education Sector.....	Sh. 66,963,000/=
Kif. 2007 - Water Sector.....	Sh. 41,409,000/=

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Kif. 3001 - *Regional Hospital*.....Sh. 170,000,000/=

Kif. 8091- *Local Govt. Authorities*..... Sh. 46,879,613,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 88 – MKOA WA DAR ES SALAAM

Kif. 1001 - *Administration and HR Mgt*.....Sh. 2,807,000,000/=

Kif. 2001 - *Planning and Coordination*.....Sh. 234,337,000/=

Kif. 2002 - *Economic and Productive Sector*.....Sh. 0

Kif. 2004 - *Social Sector*.....Sh. 118,638,000/=

Kif. 2005 - *Local Government Mgt.*

Services.....Sh. 140,000,000/=

Kif. 2006 - *Education Sector*.....Sh. 25,000,000/=

Kif. 2007 - *Water Sector*.....Sh. 63,623,000/=

Kif. 8091 - *Local Govt. Authorities*.....Sh. 240,111,778,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 89 – MKOA WA RUKWA

Kif. 1001 - *Administration and HR Mgt*.....Sh. 1,218,072,000/=

Kif. 2001 - *Planning and Coordination*.....Sh. 20,000,000/=

Kif. 2005 - *Local Government Management*

Services.....Sh. 182,038,000/=

Kif. 2006 - *Education Sector*.....Sh. 17,200,000/=

Kif. 2007 - *Water Sector*.....Sh. 45,265,000/=

Kif. 3001 - *Regional Hospital*.....Sh.114,911,000/=

Kif. 8091 - *Local Govt. Authorities*.....Sh. 23,181,707,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 90 – MKOA WA SONGWE

Kif. 1001 - *Administration and HR Mgt*.....Sh. 40,000,000/=

Kif. 2001 - *Planning and Coordination*.....Sh. 138,542,000/=

Kif. 2003 - *Infrastructure Sector*.....Sh. 3,697,000,000/=

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Kif. 2004 - <i>Social Sector</i>	Sh. 327,835,000/=
Kif. 2005 - <i>Local Govt. Mgt. Services</i>	Sh. 140,000,000/=
Kif. 2006 - <i>Education Sector</i>	Sh. 24,540,000/=
Kif. 2007 - <i>Water Sector</i>	Sh. 15,893,000/=
Kif. 3001- <i>Regional Hospital</i>	Sh.0
Kif. 8091 - <i>Local Govt. Authorities</i>	Sh. 26,656,714,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 95 – MKOA WA MANYARA

Kif. 1001 - <i>Administration and HR Mgt</i>	Sh. 779,404,000/=
Kif. 2001 - <i>Planning and Coordination</i>	Sh. 145,000,000/=
Kif. 2004 - <i>Social Sector</i>	Sh. 126,094,000/=
Kif. 2005 - <i>Local Govt. Mgt. Services</i>	Sh. 160,000,000/=
Kif. 2007 - <i>Water Sector</i>	Sh. 39,575,000/=
Kif. 3001 - <i>Regional Hospital</i>	Sh. 1,900,000,000/=
Kif. 8091 - <i>Local Govt. Authorities</i>	Sh. 36,574,518,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa Taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi ya kupitia mafungu ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI pamoja na Mikoa yake.

(Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja taarifa. *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na kwa furaha kubwa, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia makadirio ya matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Taasisi zote zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

2017/2018, kifungu kwa kifungu bila mabadiliko, hivyo naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa nitawahoji katika hatua hii sasa hoja hiyo muiamue, kwamba Makadirio ya Matumizi ya Mafungu yote ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI kama yalivyotolewa taarifa na Mtoa Hoja, taarifa ya Kamati ya Matumizi.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Serikali ya Mwaka 2017/2018
Ofisi ya Rais, TAMISEMI yalipitishwa na Bunge)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, natamka rasmi kwamba makadirio ya Matumizi Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa Mafungu yote yanayohusika yameidhinishwa na Bunge rasmi. Kwa hiyo, namshukuru Waziri kwa kazi nzuri aliyofanya na timu yake na wataalam wote wa Ofisi ya Rais, bila kumsahau Rais na Makamu wa Rais na Waziri Mkuu, timu ya Serikali ndiyo inaanzia hapo. Nawapongeza sana mmepata idhini ya Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, kila la heri. Katibu. *(Makofi)*

NDG. RAMADHAN ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MATUMIZI

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba mkae. Ili twende vizuri na muda, kwa sababu huwezi ukatoa hoja tukiwa kwenye Kamati, kwa hiyo namwomba Waziri

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

wa Nchi kwa mujibu wa Kanuni ya 28, tutengue tu Kanuni za Bunge turuhusiwe Bunge likae hadi hapo litakapomaliza majukumu yaliyo mbele yake.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

HOJA YA KUTENGUA KANUNI

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda wa kuahirisha shughuli za Bunge umefika kwa mujibu wa Kanuni na kwa kuwa kazi ambazo zilikuwa zimepangwa leo kwenye *Order Paper* hazijaweza kukamilika, hivyo kwa mujibu wa Kanuni ya 153, naomba kutoa hoja ili kutengua Kanuni inayoongoza muda wa shughuli za Bunge ili Bunge lako liweze kuketi na kuendelea na kazi iliyopangwa kufanyika leo mpaka pale itakapokuwa imekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante. Hoja imetolewa na imeungwa mkono, sasa nitawahoji wanaoafiki tufanye kazi kwa niaba ya wananchi hadi tutakapomaliza shughuli za leo.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

MWENYEKITI: Walioafiki wameshinda. Katibu.

NDG. RAMADHAN ABDALLAH ISSA– KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MATUMIZI

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

FUNGU 32 – MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA

Kif. 1001 - *Administration & HR Mgt.*.....Sh. 11,868,679,000/=

MWENYEKITI: Sawa. Kwa mujibu wa Kanuni zetu mnajua wote sihitaji kuwakumbusha, lakini kwa sababu ya muda Waheshimiwa Wabunge, nitawaita Mheshimiwa Vedasto Ngombale, Mheshimiwa Ruth Mollel. Mheshimiwa Bulembo kwa orodha niliyonayo mtaniwira radhi mna utaratibu ndani ya Vyama kuleta majina haya yaliyopo hapa, bahati mbaya jina lako halipo.

Mheshimiwa Mwanjelwa, Mheshimiwa Chikota, Mheshimiwa Mlata, Mheshimiwa...

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mchengerwa!

MWENYEKITI: Mheshimiwa *Engineer* Nditiye, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mheshimiwa Anna Lupembe na Mheshimiwa Esther Mmasi na Mheshimiwa Richard Ndassa. Haya ndiyo majina ambayo nimeletewa rasmi, tunaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, nianze sasa, mtaniwira radhi tutazingatia Kanuni lakini na ninyi mnatambua kazi iliyo mbele yetu, siyo lazima utumie dakika zako zote, weka maneno mengine akiba kama ninavyoweka mimi. Tunaanza, Mheshimiwa Ngombale.

MHE. VEDASTO E. NGOMBALE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tabia kwa Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa kutumia madaraka

yao vibaya. Madaraka haya yanatumia vibaya hasa kwa kupoka au kunyang'anya au kwa kuwavua madaraka Wenyeviti wa Serikali za Vijiji na wale wa Vitongoji. Naomba nipate ufafanuzi wa Serikali kwamba mtindo huu wa kutumia madaraka vibaya kwa kupoka na kuvua mamlaka ya Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji yataisha lini? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili lilizungumzwa kwenye michango ya Waheshimiwa Wabunge sana, labda tukumbushane sheria na taratibu za namna ya kushughulika na mahali katika kijiji ambapo pametokea tatizo la mivutano ya wananchi kutokukubali uongozi wa kijiji kwa maana ya Mwenyekiti wa Kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pana shida ya tafsiri kwa nini Mkuu wa Wilaya anafika pale, sheria imemtaja; kunapokuwa kuna mgogoro katika kijiji na wananchi wakawa na mivutano huitisha Mkutano Mkuu wa Kijiji na mkutano huo hautakuwa halali mpaka pale ambapo Mkuu wa Wilaya atakuwepo ili wazungumze, kwamba wanataka kumwondoa Mwenyekiti na pale atasimamia kura ya kutokuwa na imani atakayepigiwa Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine wamekuwa wakipiga kura wanashinda wale Wenyeviti wanabaki na hawa Wakuu wa Wilaya wanasimamia. Maeneo mengine wakisimamia zile kura inapigwa kura inamwondoa Mwenyekiti, ndiyo inayolalamikiwa, hii nyingine hailalamikiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, uwepo wa Wakuu wa Wilaya kwenye hiyo *process* ni takwa la kisheria sio kwamba wanakuwepo tu na kazi yao ni kuwaondoa tu Wenyeviti, hapana. Kwa hiyo, chanzo chote ni wananchi wale. Kwa hiyo, sisi kama viongozi wa maeneo yetu kunapotokea mgogoro twendeni tukatulize. Wakati mwingine pale wanaondoana kwa vitu havina maana

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kabisa, ni lazima twende kutuliza kusema kuna nini, tunasaidia. Siku unayosikia *DC* amefika, akifika pale kwa sababu yeye ni muamuzi, hawezi kuwa na upande wowote, akifika pale mmeitisha mkutano, anasimamia ule mkutano, mtakachokuwa mmeamua ndiyo ameondoka au anabaki. Kwa hiyo, sio kwamba wanakwenda kwa ajili ya kuwaondoa, hapana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ngombale, maelezo ya Serikali safi kabisa, yanalingana na sheria...

MHE. VEDASTO E. NGOMBALE: Mheshimiwa Mwenyekiti, takwa hilo la kisheria limekuwa likiendelea kutumika vibaya na kadri tunavyozidi kujadili na kulikemea hapa Bungeni ndivyo ambavyo Wakuu hawa wa Wilaya wanazidi kufanya ama kutekeleza hilo bila kufuata utaratibu. Sasa Serikali iko tayari kutoa tamko rasmi la kuhakikisha kwamba Wakuu wa Mikoa na Wilaya wanafuata sheria katika kutekeleza takwa hili? (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nimefahamika vizuri, nilichokisema ni kwamba Wakuu wa Wilaya wanakwenda mahali ambapo wananchi wale wameitisha mkutano wao na wanataka awepo Mkuu wa Wilaya kwa sababu bila kuwepo yeye ile *process* inakuwa hajazingatia matakwa ya kisheria. Kama inafanyika kinyume na hivyo inavyofanyika inaweza ikawa ni *special case* atuletee, kama kweli inatokea kwamba *DC* anafika tu anasema wewe Mwenyekiti hufai, nadhani hiyo ni *special case* atuletee tutai-*treat* na tutaishughulikia ipasavyo. (*Makofi*)

MHE. VEDASTO E. NGOMBALE: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika na maelezo ya Mheshimiwa Waziri, hivyo basi nakusudia kutoa shilingi ili Bunge hili liweze kujadili ili tuweze kupata hatma ya jambo hili ambalo linasumbua sana wananchi wetu.

MWENYEKITI: Unajadili nini, uwe *very specific*, tunajadili nini?

MHE. VEDASTO E. NGOMBALE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuiondoa hiyo shilingi kwa sababu bado suala hilo linatekelezwa vibaya na Waheshimiwa hao niliowataja na wananchi wetu wanaendelea kupata shida. Kwa hiyo, niombe Bunge hili lijadili ili basi tuweze kujua hatma ya utekelezaji wa sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud Abdallah, Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mheshimiwa Mwita Waitara, inatosha huku. Waheshimiwa Wabunge, *gender* basi, haya Mheshimiwa Cecilia Paresso.

Tunakwenda upande huu, Mheshimiwa AG, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Mheshimiwa Kakunda, Mheshimiwa Injinia Stella Manyanya. Inatosha tuanze na Mheshimiwa Masoud.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naungana kabisa na maelezo sahihi, maelezo murua kabisa ya Mheshimiwa Vedasto Ngombale Mwiru. Ni kweli kabisa hawa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya katika maeneo yetu, hata kama katika sheria kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wametajwa, lakini wakifika katika maeneo ya mikutano hawafanyi hizo kazi zinazostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ni Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, amekwenda katika Mtaa wa Mlimwa Kusini. Huu mtaa unaongozwa na Upinzani Chama cha Wananchi CUF na maelezo alivyokwenda pale alikaa muda mfupi tu akasema mimi nimekuachisha muda wa siku saba, wewe sio kiongozi tena. Wananchi wenyewe wamekasirika, hakuna lolote ambalo amefanya, hili jambo ni baya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi yao ya madaraka Wakuu wa Wilaya si mazuri, ni mabaya sana. Mfano mzuri ndiyo huu hapa Dodoma, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma mwenyewe amefanya hilo. Sitaki mwende maeneo mengi,

na mikutano hii hawaitishi, wakifika ni maamuzi yao tu kutokana na madaraka yao na joto lao la kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba suala hili...

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waitara.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ngombale na bahati nzuri mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Utawala na TAMISEMI, kwa hiyo nina taarifa za Wakuu wa Mikoa. Kwanza, hawatekelezi sheria wanavunja sheria kwa sababu sheria inachosema ni kwamba Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya kwa mujibu wa sheria ambayo tunayo tunajua, anapaswa akienda mahali kama kuna tatizo, kuna mkutano, kama huyu anataka kupelekea uvunjifu wa amani ndiyo anaweza akakamatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanachokifanya, kwanza wanapata taarifa, mkutano unaitishwa, Mwenyekiti wa Mtaa au Kijiji au Kitongoji hapewi nafasi ya kujitetea anakuja na maamuzi, ndiyo shida inayozungumzwa hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshangaa ndugu yangu Mheshimiwa Waziri ambaye yeye ni Mwanasheria. Hoja hapa ambayo Wabunge tunataka ni kwamba atoe tamko Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wasome sheria kama ilivyo watekeleze ni hilo tu, sioni kama kuna namna ya kuvutana hapa. Kwamba wale watu ambao na siyo wote, wale ambao hawafuati utaratibu, hawafuati sheria, mtuhumiwa apewe nafasi ya kujitetea, apeleke utetezi wake, wananchi hawaulizwi maswali waweze kuamua, hao waelekezwe, yaani kuna haja gani ya kubishana au kwa sababu ninyi ni wengi hapa? Sasa hakuna sababu ya maana sana, wewe ni Mwanasheria, ni Waziri unafanya kazi nzuri....

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa, muda ndiyo huo umekwisha. Mheshimiwa Mbowe.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti,

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ngombale na niifafanue kwa kifupi sana. Wala hatuna nia ya kubishana na Serikali, lakini ukweli ni kwamba kuna Ma-DC wanatumia Ofisi zao vibaya, wanadhaliisha, wanaonea Watendaji wa Serikali na kuna maeneo mengine wanaonea wananchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachomwomba Waziri alitambue hili na nitampa mfano rahisi. Nimekwenda Kibaha Vijijini, Kijiji cha Msangani kuna Mwenyekiti wa Kijiji pale anaitwa Gandhi. Mwenyekiti huyu wa Kijiji kwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita ameshawekwa ndani kwa amri za DC mara tano. Anawekwa ndani kwa masaa 48, akibishana tena ama wakishindwa kuelewana jambo yeye akiwakilisha wananchi ambaye yeye ni Mwenyekiti wa Kijiji, DC akikasirika anamweka ndani masaa 48 na DC huyu ni Mama Assumpter Mshana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubishi wao na ugomvi wao ni kwamba Mwenyekiti wa Kijiji aliidhinisha *project* ya kujenga zahanati. Baadaye Halmashauri ikataka kuchukua zahanati, wanakijiji wameshachanga fedha zao nusu, wakashindwa kuelewana. Hili jambo badala ya kuweka kikao cha pamoja na kuelewana, wakaamua kutumia nguvu. Mwenyekiti wa Kijiji anaambiwa achia *Account* yenye shilingi milioni 25 akawa anabisha kwa sababu anataka kikao na wananchi wa kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoomba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

naomba dakika moja samahani sana. Serikali mkubali tu kuna Ma-DC wanafanya majukumu yao vibaya, wanaichafua Serikali, kubalini tu toeni tamko kwamba mtafuatilia. Huu utaratibu wa kuweka ndani watu masaa 48, Walimu wanawekwa ndani, Watendaji wa Vijiji wanawekwa ndani, Watumishi wa Halmashauri wanawekwa ndani...

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mbowe. Mheshimiwa Parezzo.

MHE. CECILIA D. PAREZZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Kwanza naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ngombale. Ni kweli kwamba baadhi ya Ma-DC katika Awamu hii ya Tano wamekuwa wakitumia vibaya sana madaraka yao, wamekuwa wakiwaondoa hawa Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji hata bila kufuata taratibu. Unakuta hata mikutano ambayo imeitishwa, kwa sababu taratibu inataka mikutano mikuu ya vijiji ikitishwa angalau nusu kwa maana ya akidi iweze kutimia ndiyo hao Wenyeviti waweze kuondolewa, hizo taratibu hazifuatwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawaona hawa baadhi ya Ma-DC wanaingilia hata Mabaraza ya Madiwani, wanafuta mikutano ya Baraza la Madiwani wakati mikutano hiyo ipo kwa mujibu wa sheria. Wanafuta, wanamuagiza Mkurugenzi kwamba Madiwani wasilipwe posho wakati posho hizo zimepitishwa kwa mujibu wa taratibu, zipo kwenye bajeti, lakini wanaamuru hata hizi posho za Madiwani zisilipwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wapo baadhi ya Wakuu wa Wilaya, mfano DC wa Arumeru, Mheshimiwa Mnyeti, kama anataka bajeti ya Halmashauri ipite kwanza kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama ndiyo iende kwenye Baraza ni utaratibu gani? Mheshimiwa Waziri unachokieleza hapa hakifanyiki na hao Ma-DC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani toka tumepata uhuru ukiwaacha Ma-DC waliokuwa chini ya ukoloni, hawa waliopo sasa hivi ni zaidi ya... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Injiniya Stella Manyanya.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa bahati nzuri niliwahi kuwa Mkuu wa Mkoa na Wakuu wa Wilaya pia nawafahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba kila binadamu ana namna yake ya kutenda kazi, sawa na ilivyo kwa sisi Wabunge, kila mtu ana *style* yake. Hata hivyo, niseme tu kwamba, Serikali ili ikamilike ni pale inapokuwa *structure* yake inafika mpaka huko chini ambako ni Wenyeviti wa Vijiji. Kwa hiyo, Serikali inatambua umuhimu wa Wenyeviti wa Vijiji, lakini pale inapojitokeza unakuwa na Mwenyekiti ambaye anafanya mambo ambayo hayaeleweki na ni hatarishi. Kwa mfano; nilipokuwa Rukwa, kuna baadhi ya Wenyeviti walikuwa wanafikia hatua hata ya kuwaingiza watu kutoka nje ya nchi bila utaratibu. Ukishafuatilia unakuta kwamba yuko anafanya hivyo na vitendo vyake vimekithiri au anachukua ardhi anawauzia watu zaidi ya heka 50 ambazo zilitakiwa apitishwe kwenye mikutano wa kijiji na mambo mengine. Sasa unamuacha huyo mtu kwamba aendelee kufanya hivyo kabla hujachukua hatua za kuona kwamba jambo linasimama na linafanyiwa utaratibu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu kwamba jamani Wabunge tusione kwamba wenzetu wanapotimiza majukumu yao wao hawafai, hawajui.....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Mwigulu Nchemba.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge niongelee kwenye upande wa kiusalama. Moja, ukiona mpaka *DC* ameenda kwenye kijiji hicho, kuna tatizo kubwa sana ambalo wale wanakijiji wakiachwa peke yao; kwanza usalama wa Mwenyekiti yule wenyewe tu upo mashakani. Hakuna sehemu ambako Mkuu wa Wilaya anakwenda tu

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

na pana amani, kwanza Mkuu wa Wilaya akienda tu pakawa pana amani hata wanakijiji wenyewe hawatakubali Mwenyekiti wao kuondoka. Kwa maana hiyo, panakuwepo na tatizo la msingi na Mkuu wa Wilaya anapokwenda anakuwa ame-*rescue* usalama wa Mwenyekiti mwenyewe, lakini kama ilivyo *DC* ni Mwenyekiti wa Ulinzi na Usalama wa Wilaya anakuwa ame-*maintain* usalama katika kijiji hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la msingi ambalo hata sisi hapa tu tumetofautiana, hoja ya msingi ambayo imetolewa kuhusu kuondolewa kwa Mwenyekiti wa Kijiji maelezo aliyotoa Waziri ndiyo ya msingi, lakini kumekuwepo na *generation* nyingine ya maswali mengine ambayo siyo hoja iliyokuwa imewekwa mezani hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye utaratibu wa mahitaji haya ambayo mtoa hoja alitoa, hili jibu alilotoa Mheshimiwa Waziri ndicho ambacho ni sahihi na ndicho ambacho kitawasaidia hata hawa Wenyeviti. Sehemu ambako hakuna tatizo Wenyeviti wa Vijiji hawaondolewi, lakini sehemu ambako Wenyeviti wamefanya matatizo, Waheshimiwa Wabunge hata sisi tunatoka kwenye hivyo vijiji tuunge mkono Wenyeviti wa namna hiyo waondolewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mmoja, mimi nilitoa fedha kwa ajili ya maji kwenye mkutano, yule Mwenyekiti kapokea, kaingia nazo mitini. Wanakijiji wenyewe walikuwa wanasema huyu haogopi hata wewe uliye Waziri wa Mambo ya Ndani, wakamwambia *DC* huyu tunataka awekwe ndani ili ajifunze, sasa mtu kama huyo Mkuu wa Wilaya unamlaumu kwa lipi? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa AG.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI amefafanua vizuri kuhusu suala hili. Hoja ya Mheshimiwa Ngombale ilikuwa ni kwamba Serikali itoe kauli ya hawa Ma-

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

DC sijui wafanye nini. Masuala haya yamewekwa kwenye sheria, mambo ambayo yamekuwa kwenye sheria hayawezi kutolewa tamko ama kauli, ni sheria kutekelezwa tu ndiyo msingi wa Ibara ya 26 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Yule ambaye ana hakika huyu amevunja Katiba anaenda Mahakamani, hili suala huwezi kulitolea kauli, unalitolea kauli pale ambapo hakuna sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya maelezo mazuri yaliyotolea na Waheshimiwa Mawaziri, naomba Waheshimiwa nishauri, kama kweli hizo kesi ziko, watu wanavunja sheria kwa nini hamwendi Mahakamani? Eehh ndiyo ukweli tu kwa sababu Katiba inasema hivi:

“(1) Kila mtu ana wajibu wa kufuata na kuitii Katiba hii na sheria za Jamhuri ya Muungano;

(2) Kila mtu ana haki, kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria, kuchukua hatua za kisheria kuhakikisha hifadhi ya Katiba na sheria za nchi.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, maelezo haya yaliyotolewa na Waheshimiwa Mawaziri yanatosha. Nimshauri Mheshimiwa Ngombale ana hekima sana, airudishe tu ile shilingi na kama kuna hoja Serikali imesikia, kwa sababu Serikali haiwezi kufumbia macho watu wanavunja tu sheria hivi. Kwa hiyo, naomba kumshauri Mheshimiwa Ngombale arudishe ile shilingi.

MWENYEKITI: Ahsante sana AG. Mheshimiwa Jenista Mhagama, *Chief Whip*.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tunataka tu kuweka msisitizo katika msingi wa jambo lenyewe. Ninavyoliona msingi wa jambo hili ni kuangalia utendaji wa kimamlaka walio nao Ma-DC, walionao Wenyeviti wa Serikali za Vijiji, Halmashauri zetu.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Sheria ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Sura Namba 287 na Namba 288, Mkuu wa Wilaya anayo Mamlaka kabisa ya kisheria ya kusaidia utawala bora kwenye vijiji vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anayekubalika kisheria kuitisha mkutano wa hadhara kwenye kijiji ni Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji. Hata kama Waziri nataka kwenda kijijini, Mwenyekiti wa Kijiji asipoitisha kikao sina uwezo wa kufanya mkutano pale. Sasa kama Mamlaka imempa Mwenyekiti wa Kijiji anaitisha mkutano, DC anaalikwa kwenda kusimamia utawala bora, unamtuhumuje DC badala ya yule Mwenyekiti aliyelitisha kikao yeye mwenyewe? (Makofi)

Mheshimiwa DC akifika pale atakwenda kuangalia misingi ya utawala bora kwa wananchi wa kijiji husika. Mbunge mmoja hapa amesema kwa nini Ma-DC wanaingilia hata masuala ya posho sijui za Madiwani, posho sijui za Wenyeviti wa Vijiji. Ni lazima kwa msingi wa sheria hiyo. Hivi kama Madiwani wanapangiana posho kinyume cha sheria DC aangalie tu na wakati sheria inamruhusu kuangalia utawala bora pale? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Mheshimiwa Waziri, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu hakika wote ni mashahidi wako huko Wenyeviti wa Vijiji wanavuruga utawala bora isivyokuwa kawaida, kwa hiyo ni lazima twende na sheria. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie moja tu, ni kwamba, hivi tunamtaka Waziri atoe tamko hapa, sasa atoe tamko kwa ajili ya DC gani? Maana yake tuna-generalise mambo hapa, kama ni specific case twende tukazishughulikia kesi kwa kesi, lakini tuwaache Ma-DC wafanye kazi ya kusimamia utawala bora kwa manufaa ya wananchi wetu kwenye vijiji vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuunga mkono Mheshimiwa Waziri. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ngombale umesikia na mwelekeo wa michango, unajeresha shilingi? Karibu.

MHE. VEDASTO E. NGOMBALE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia mjadala ulivyokuwa unaendelea, lakini tu niseme kinachoelezwa ndicho ambacho kipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wenyeviti wa Vitongoji na Wenyeviti wa Vijiji ni wateule wa wananchi, wanahitaji heshima kubwa. Tunapokwenda kupoka madaraka yao bila kufuata utaratibu ni kitu ambacho ndicho tunakipigia kelele. Mheshimiwa Waziri nakurudishia shilingi yako, lakini niombe Serikali ishughulikie suala hili, kwa sababu viongozi wetu wananyanyasika sana. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Tunakushukuru sana kwa uelewa wako, tunaendelea na Mheshimiwa Richard Ndassa.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Langu ni dogo lakini ni kubwa. Katika michango yetu baadhi yetu tumetuhumu sana Usalama wa Taifa chombo ambacho ni nyeti sana. Tulikianzisha sisi wenyewe kwa mujibu wa Sheria ya mwaka 1996.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, sikumsikia Waziri mwenye dhamana akielezea, kwa sababu chombo hiki sote tunafahamu umuhimu wake kwa Taifa na nchi yetu. Sasa kama chombo hiki Waheshimiwa Wabunge tukianza kukibeza wakati tumekianzisha sisi, tunajua kabisa faida ya chombo hiki ni nini kwa nchi yetu, nataka nipate maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, nini msimamo wa Serikali kuhusu yale yaliyozungumzwa humu ndani kuhusu chombo hiki? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea, unataka kujibu sasa hivi? Haya.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nipende tu kujibu hoja ya Mheshimiwa Ndassa. Kwanza kabisa nimshukuru kwamba ameweza kuona umuhimu wa chombo hiki muhimu kwa Taifa letu, kwa chombo hiki ambacho ni nyeti kwa Taifa letu, zaidi nipende tu kusema kwamba chombo hiki kiliundwa mahsusi kwa ajili ya kuangalia ustawi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa siku za hivi karibuni tumejionea mazoea au imeibuka tabia na mbaya zaidi tukisema unaambiwa Waziri wa Utawala Bora anakataza watu kusema masuala haya. Hatujasema Waziri wa Utawala Bora akataze watu kusemea masuala haya, tunachokisema ni umuhimu wa chombo chenyewe, majukumu ya chombo chenyewe, kilianzishwa kwa ajili ya masuala ya aina gani.

Nipende tu kusema Mheshimiwa Mbunge, maelezo au msimamo ambao naweza kutoa ni kwamba ni vema kwa kweli wananchi wote wakiwemo pia Waheshimiwa Wabunge wakaona umuhimu wa kuheshimu na kuthamini chombo hiki ambacho ni muhimu kwa ustawi wa Taifa letu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ndassa.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo ya Mheshimiwa Waziri nimeridhika, lakini niombe kiti chako kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kwamba chombo hiki ni muhimu sana sana kwa nchi yetu, kwa hiyo, sisi Wabunge ni lazima tukiheshimu na tukiunge mkono kuliko kukibeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea Mheshimiwa Mary Mwanjelwa.

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Nami langu ni dogo lakini kwa umuhimu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rushwa ni adui wa haki pia ni mdudu aliyeota *cancer*. Wote tunaelewa TAKUKURU *at this time around* wameokoa takribani zaidi ya bilioni 53, lakini tukiangalia chombo *instruments* zake wallizonazo hazitoshi, mimi la kwangu ni moja dogo, kubwa la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *grand corruption* na zile Mahakama za Kifisadi mpaka sasa hivi ni kizungumkuti, adhabu zinazotolewa ni kama tunaleta utani kwa sababu haziendani na uzito wa kosa. Mheshimiwa Waziri Angella ni rafiki yangu sana lakini nahitaji sana *commitment* ya Serikali, nahitaji itoe tamko, vinginevyo nitashika mshahara wa rafiki yangu Angella.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri *commitment*.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA): Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwanza niendeleo kumpongeza Mheshimiwa Mwanjelwa ambaye amesema ni rafiki yangu, amekuwa akisimamia sana haya mapambano dhidi ya rushwa, amekuwa Mwenyekiti wa Chama cha Wabunge wa Wanaopambana na Rushwa Tanzania, vilevile alikuwa ni Mjumbe wa Bodi ya Kamati tendaji ya *APNAC-Africa*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija katika hoja yake kwa kweli amelezea vizuri na niseme tu kama Serikali pia tunaiona, tunaona umuhimu wa kuifanyia mabadiliko Sheria hii ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia sheria hii tangu enzi za ukoloni miaka ya 1930 kulikuwa na *regimes* mbalimbali za mapambano dhidi ya rushwa. Ukiangalia pia mwaka

1958, mwaka 2003, mwaka 1971 na mingineyo imekuwa ikibadilishwa mara kwa mara. Ni kweli imefika wakati sasa sheria hii imepitwa na wakati takribani miaka 10, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge tumeliona hili na tutachukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo masuala mengi, ukiangalia kama alivyosema katika adhabu kuwa ndogo, hivi sasa ukiangalia mtu mwingine hata anadiriki kutenga faini kabisa, anatenda kosa la jinai au anachukua rushwa akijua kabisa kwamba huko baadaye hata ikitokea amehukumiwa kulipa faini, anakuwa ameshajitengea fedha ambayo ataitumia kwa ajili ya kulipa faini. Kwa hiyo, tunataka tuje na sheria kali, ni imani yangu Waheshimiwa Wabunge tutakapoleta hapa tumeshaanza mchakato, basi mtaweza kutuunga mkono ili kuhakikisha kwamba hili linatendeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, hata ukiangalia katika namna ambavyo sasa hivi makosa ya rushwa yanatendeka, kuna mabadiliko makubwa pia hata katika mifumo yetu ya kiteknolojia. Tunayo *M-pesa*, *Halopesa* pamoja na nyinginezo. Watu wameanza kutumia mbinu nyingine za kielektroniki na teknolojia katika kutenda makosa haya ya rushwa. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tutahakikisha mara moja tunaleta sheria hii, maana tumeshaanza mchakato wa kuibadilisha katika ngazi ya Serikali.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwanjelwa.

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru. Kwanza nimefurahishwa na jibu la Mheshimiwa Waziri kwamba ataleta sheria hiyo Bungeni ili iweze kuhuishwa, tunaisubiri kwa hamu kubwa ili tuweze ku-endorse.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, tunasubiri utekelezaji. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Martha Mlata.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nina dogo tu kwa mshahara wa Mheshimiwa Waziri Angella ni kuhusu MKURABITA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa MKURABITA ni mpango ambao kwa kweli una tija na ni mzuri, lakini utaratibu wake umewekwa kwamba kila Wilaya *at least* vijiji viwili. Ukizingatia kwamba mpango huu unaleta manufaa makubwa sana kwa wananchi, lakini ukirudi kwenye utekelezaji wake Halmashauri nyingi zinakuwa haziwezi kutenga fedha kwa ajili ya kutekeleza mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Ibara ya 58, imeongea wazi kwamba Serikali iweke mfuko maalum ambao utawezesha Halmashauri, kukopa fedha ili kuendeleza mpango huu. Naomba Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi ili nchi nzima vijiji vyote viweze kupatiwa mpango huu na kunufaika. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nipende kujibu hoja ya Mheshimiwa Martha Mlata kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze kwa kufuatilia masuala ya urasimishaji na kwa Mkoa wa Singida wamekuwa wakifanya vizuri sana ikiwemo pia na Wilaya ya Mkalama. Nipende tu kutoa maelezo machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia wenzetu wa Peru, ambao na sisi ndio tumeasisi suala zima hili la urasimishaji kwa biashara na ardhi, walifanya vizuri na sisi tumejitahidi kuakisi yale ambayo walipata mafanikio katika eneo hili.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia tangu mwaka 2004 mpaka sasa, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika urasimishaji wa ardhi bila kwenda katika urasimishaji wa biashara, tatizo kubwa au changamoto kubwa ni katika mfuko wa kifedha. Serikali mwaka 2009 iliona kuna haja sasa ya kuwa na mfuko ambao ni endelevu utakaosaidia shughuli nzima za urasimishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie kuwa Mheshimiwa Mbunge pia amenukuu ibara ya Ilani ya Uchaguzi, Ibara ya 58, nimhakikishie tu kwamba kama Serikali na hata ukipitia katika hotuba yangu nilieleza masuala haya tumeanza hatua katika mwaka huu wa fedha, tutaanzisha mfuko huu endelevu wa urasilimishaji katika nyanja ya majaribio katika Halmashauri mbili za Mkoa wa Songwe, pia tutaenda katika Manispaa ya Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakachokifanya ni kwamba tutashirikiana na TAMISEMI kuhakikisha kwamba kwa benki ambazo zitakuwa zimechaguliwa na Halmashauri wataweza kuingia makubaliano katika mfumo wa mawasiliano ambao unaingiliana na TAMISEMI na fedha hizi zitaweza kukopwa na Serikali itaweza kutoa dhamana ili Halmashauri zetu kwa wingi zaidi waweze kupata kwa ajili ya urasimishaji.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Martha Mlata kuna la yongeza hapo?

MHE: MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo. Nashukuru na azingatie kwamba nimesema inakuwa ni vema vijiji vyote, vingine visije vikakosa, lakini aongezee kwamba kwenye vijiji basi kuwe na masjala za kuweza kuhifadhi zile *certificates* ambazo wananchi watazipata kwa haraka zaidi wanapotaka kuzitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA): Mheshimiwa

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mwenyekiti, nashukuru kwa kunikumbusha kwenye hilo. Sambamba na hilo nipende tu kusisitiza umuhimu wa kuwa na Masjala ya Ardhi ya Vijiji. Tunapoongelea suala zima la urasimishaji wa ardhi, lakini tunapoongelea umuhimu wa kuwa na hatimiliki katika ardhi unaoimiliki, ukiangalia katika maeneo yetu mengi ya vijijini, hati ambazo wanapatiwa kwa mujibu wa Sheria ya Vijiji Namba 5 ya mwaka 1999, ni Hati za Miliki za Kimila. Inapotokea katika eneo husika hakuna masjala ya ardhi ya kijiji ni *obviously* kwamba urasimishaji hauwezi kufanyika au hata ukifanyika basi hati haziwezi kutolewa.

Nipende kutoa rai kwa Halmashauri zetu kupitia TAMISEMI na nashukuru sana kaka yangu ananisikiliza hapa. Wanapotenga fedha mbalimbali katika mipango yao ya kibajeti, basi waone umuhimu wa kupima maeneo, wa kupanga ardhi yao vizuri, zaidi ya yote kuweza kuunga mkono jitihada za Serikali kwa kujenga masjala za ardhi za vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge kwa maeneo ambayo tumeshaanza kujenga masjala za ardhi kupita MKURABITA, tutahakikisha maeneo hayo tunamaliza. Lengo kubwa ni kuwa na mfuko endelevu wa urasimishaji ili katika kila eneo, ardhi ile ipimwe, ipangwe, igawiwe vizuri kila eneo lijulikane kwa mpango wa matumizi bora ya ardhi, lakini zaidi ya yote tuwe na masjala za ardhi za vijiji na kuweza kutoa hizo hatimiliki za kimila. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Abdallah Chikota.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mnamo mwezi Juni mwaka jana, Serikali ilitoa maagizo kupitia kwa barua ya Katibu Mkuu Utumishi ya tarehe 13 Juni, 2016, ambayo ilikuwa na mambo sita, lakini nitazungumzia mambo mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza iliahirisha utekelezaji wa ajira mpya, vilevile iliahirisha marekebisho ya mishahara

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kwa watumishi ambao walipanda vyeo. Wakati wa utekelezaji kwa mfano, hili suala la kuahirisha utekelezaji wa ajira, kuna watumishi ambao walikuwa wameshapata ajira katika mamlaka mbalimbali za ajira na taratibu zote za utumishi zilikamilika lakini watumishi wale wakaondolewa kwenye *payroll* na wakaaambiwa wasubiri, wamekaa majumbani huu ni mwezi wa nane sasa hakuna maelekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kuna watumishi wengi wao ni Walimu walipanda vyeo, wakapata mshahara mpya na wao wakarudishwa kwenye vyeo vyao vya zamani, wakapewa mshahara wa zamani. Nini kauli ya Serikali kwa sababu maagizo yote yameshakamilika sasa hivi, ule uhakiki wa vyeti umeshakamilika na uhakiki wa watumishi hewa umeshakamilika. Kauli ya Serikali ni nini kuhusu hao watumishi ambao wameathirika na maagizo hayo mawili? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Napenda kujibu hoja ya Mheshimiwa Abdallah Chikota, Mbunge wa Nanyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze kwa kufuatilia hoja hii hususan kwa watumishi walioathirika na agizo hili. Amezungumzia suala zima la ajira lakini upande wa pili ni katika suala zima la vyeo halisi vya watumishi ambao walipandishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na hoja ya kwanza ya walioahirishiwa ajira, yapo makundi matatu. Kundi la kwanza ni wale ambao walishaingia kwenye ajira, michakato yote ikakamilika katika mamlaka zao za ajira mpaka wakapewa *check number* na hata wengine ikafikia wakapata mshahara wao wa kwanza. Kundi la pili, ni wale ambao unakuta Maafisa Utumishi waliwachelewesha walisharipoti katika vituo vyao vya ajira, lakini wakacheleweshwa kuingizwa katika mfumo na hatimaye

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kuidhinishwa na Ofisi ya Rais, Utumishi. Kundi la tatu ni la wale ambao wana barua za ajira lakini walikuwa hawajafika katika vituo vyao vya ajira. Sasa nipende kusema malezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kundi la kwanza ambao walishafika kazini na walishapata mshahara na unakuta wengine walisharudishwa nyumbani, tumeshawarudisha zaidi ya watumishi 421, wakiwemo wengine wa Mahakama na tayari napenda kusema kuwa wapo kazini tangu mwezi Machi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kundi la pili ambao unakuta walishaingia kazini lakini hawajaingizwa katika utaratibu lenye watumishi 2,213 na wenyewe pia tumeshaanza utaratibu mwezi huu wa Aprili mwishoni na wenyewe pia wataingizwa kazini tena. Kundi la mwisho, lenye watumishi watarajiwa 535 ambao walikuwa na barua za ajira au *placement letter* lakini walikuwa hawajafika katika vituo vyao na wenyewe pia mwezi Mei watakuwa wameshaingia kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa kwa upandishwaji wa vyeo ametaka pia kujua *commitment* ya Serikali. Takribani watumishi 14,000 walikuwa wameshaingizwa katika mfumo lakini walikuwa hawajaidhinishwa. Nimhakikishie tu kwamba, kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha kukamilika, basi watakuwa wamerudishwa katika vyeo vyao sahihi na marekebisho yatafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Chikota vipi?

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba pamoja na majibu mazuri, lakini bado kuna watumishi wa kundi la kwanza hawajarejeshwa. Katika Halmashauri yangu ya Nanyamba kuna Mhandisi wa Maji hadi leo bado

hajarejeshwa, wewe kwa sababu unajua uchapakazi wake na una *commitment* yake, atafanya *asement* wale ambao hawajarejeshwa warejeshwe haraka sana. Kwa sababu majibu yake yameridhisha sitakamata shilingi yake. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nashukuru sana. Nadhani amekusikia kwa *Engineer* huyo. Tunaendelea na Mheshimiwa Hasunga Japhet.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilikuwa nimetoa maelezo juu ya Miundo ya Utumishi wa Umma, ambapo wafanyakazi wengi sasa hivi Miundo yao ya Utumishi ilikuwa imepitwa na wakati. Vilevile kwa kipindi cha sasa hivi kwa kuzingatia hali halisi ya teknolojia ilivyobadilika na mazingira yalivyobadilika, kada mpya ambazo zimejitokeza kama za mafuta na gesi, nataka kujua Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba inafanya mapitio ya Miundo ya Utumishi ili iendane na ujuzi na maarifa inayohitajika katika kipindi cha sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nipate maelezo thabiti ya Mheshimiwa Waziri.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimshukuru Mheshimiwa Hasunga, huyu alikuwa ni mtumishi wa Chuo cha Utumishi wa Umma, kwa hiyo, anayafahamu vizuri masuala haya huenda kuliko hata mimi. Pili, ni kweli mchango wake wa maandishi tumeuona na nipende tu kusema kwamba tunaiona haja ya kufanya mapitio katika Miundo yetu ya Utumishi, mingi ni miundo ambayo ilifanyiwa marekebisho kati ya mwaka 1999 mpaka 2000 Serikali ilipofanya zoezi la tathmini ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu kwamba Mheshimiwa Mbunge kama nilivyoeleza mwanzoni wakati

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

ule nikijibu hoja ya kurudisha posho ya kufundishia au *teaching allowance*. Tunapoendelea na zoezi hili la tathmini ya kazi, tutakapopanga mishahara kwa mujibu wa majukumu na uzito wa kazi tutaangalia pia suala zima la ngazi za mishahara pamoja na miundo ya maendeleo ya utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo pia tunaendelea kuangalia ukubwa wa Serikali kuhakikisha kwamba inakuwa na miundo ambayo inahimilika, kwa kufanya hivi pia itaweza kutupa picha nzuri zaidi katika kupitia miundo ya maendeleo ya utumishi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hasunga uko sawa?

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri maelezo ya Mheshimiwa Waziri nayakubali, lakini naomba Serikali isichukue muda mrefu sana. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante tunakushukuru sana. Mheshimiwa Ester Mmasi.

MHE. ESTER M. MMASI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia katika hitimisho la Wizara. Ni kweli kwamba Ofisi ya Rais, Menejimenti na Utumishi wa Umma, inafanya kazi kubwa sana katika kuboresha ufanisi kwa ngazi za Serikali lakini pia kwa upande wa Mheshimiwa Rais, amefanya kazi kubwa katika kuboresha ufanisi hata katika Mhimili wa Bunge, kupitia *appointment* mbalimbali kwa Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mwanajumuiya wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, nachukua nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kutupa nafasi ya kipekee kabisa hata tukaweza kutoa viongozi wengi katika Serikali hii ya Awamu ya Tano. Hii ni heshima pekee ambayo kwetu tunailinda na tunaithamini sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina langu moja, ni kweli kabisa nia ya Serikali tumeiona pia ni dhahiri kwamba ifike mahali kwamba tuone kabisa kuna umuhimu wa kipekee

kuweza kuona kwamba katika *appointment* hizi tunakuwa na *replacement*, ni dhahiri kwamba Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Muda umekwisha, Mheshimiwa Waziri jaribu kumjibu kabla hajakasirika. (*Kicheko*)

MHE. ESTER M. MMASI: Mheshimiwa Mwenyekiti, langu lilikuwa ni *replacement* za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kwa hiyo, naomba kutoa hoja Mheshimiwa Waziri, anipe majibu ya kina tuone ni kwa namna gani tutalinda historia ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wakati huo tunaweza kujenga Taifa lililoelimika kwa kuona *replacement* zinafanyika.

MWENYEKITI: Ungeenda *straight* kwenye *point* tangu mwanzo, lakini hayo madoido ndiyo tatizo. (*Kicheko*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Ester Mmasi Mbunge wa Viti Maalum anayewakilisha Vyuo Vikuu anaitendea haki nafasi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali tunatambua umuhimu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, pamoja na vyuo vingine vya elimu ya juu. Kwa kweli tunajivunia sana kwa wateule wa Rais ambao wametokana na vyuo hivi na ni imani yangu pia Mheshimiwa Rais amekuwa akiridhika na ndiyo maana amekuwa akichota watu ambao wakitoka katika taasisi hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na *replacement* au ajira mbadala ambazo zimekuwa wazi kutokana na teuzi hizi lakini na nafasi nyingine ambazo zimekuwa wazi, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge katika mwaka huu wa

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

fedha kabla hatujamaliza Juni tumetenga nafasi 254 kwa ajili wa Wahadhiri wa Vyuho Vikuu ikiwemo na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ester Mmasi baada ya majibu hayo.

MHE. ESTER M. MMASI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naridhika kabisa na majibu ya Waziri, Mheshimiwa Angella Kairuki, Mheshimiwa Waziri sisi tuna imani na wewe, tunaomba hili lifanyike hasa ukiangalia hata Katibu Mkuu wako Profesa Ndumbaro ametoka kwenye Jumuiya hii ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Tunawapeni dhamana, tunaombeni twende katika muktadha huu.

MWENYEKITI: Tunakushukuru sana. Mheshimiwa *Engineer* Nditiye.

MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nitaongelea suala la *TASAF*, katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri alizungumzia kwamba anafahamu watu ambao waliofaidika na Mfuko wa *TASAF* lakini hawakuwa wanastahili. Kwa upande wangu mimi naona wale hawana makosa yoyote. Nataka kauli ya Mheshimiwa Waziri, kuhusu hao waliopewa ambao hawastahili hatma yao ni ipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nataka nijue wananchi wale ambao wamefanya shughuli ambazo zinaletwa na *TASAF* ambao mpaka sasa hivi hawajalipwa, Serikali inazungumzaje. Mwisho, kuna wale watumishi wa *TASAF* ambao walichukuliwa katika Halmashauri mbalimbali wakaenda kusaidiana na *TASAF*.

MWENYEKITI: Niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge, kwenye suala hili la sera ya nchi ni suala moja tu mahsusi, endelea lakini Waziri atachagua suala moja tu.

MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, basi naomba lile la swali la kwanza lipatiwe

majibu, hilo moja mahsusi. Kwamba wale walionufaika ambao hawastahili mustakabali wao ni upi, nataka nipate maelezo ya Waziri.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nditije kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Nditije hata katika mchango wake wakati alipozungumza aliongelea suala hili kwa hisia kubwa na hasa alipoeleza kwamba ilifikia wakati baadhi ya wapiga kura wake wamekuwa wakimfuata na pia Waheshimiwa Wabunge wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu yangu nilipokuwa nikihitimisha nililieleza pia kwa ufupi. Nipende tu kusema yafuatayo: Tumeondoa kaya zaidi ya 68,914 katika uhakiki huu, ni uhakiki ambao umekuwa ni *massive* na kwa mara ya kwanza tumeweza kutoa kiasi kikubwa kwa idadi hiyo tuliyoweza kuipata. Niombe tu Waheshimiwa Wabunge waendeleo kuunga mkono tunapoendelea na uhakiki wa aina hii. Tutakuwa tukifanya hivyo kila mara tutakapokuwa tukifanya malipo mara moja kila baada ya miezi miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikija katika hoja yake, nipende kusema kwamba, hapa kuna watu wa aina mbili, kundi la kwanza ambao sisi tulililenga zaidi ni wale ambao hawakustahili kuwepo kabisa na waliingizwa kimakosa hawana sifa. Unakuta mwingine ni Mtumishi wa Umma, mwingine hata anadiriki kwenda na gari anapaki pembeni, anavaa nguo kuu kuu halafu anaenda kupanga foleni kupokea hela za *TASAF*. Hao ndiyo tuliwalenga ili *in the first place* hakuwa na sifa na vigezo vilivyowekwa katika mkutano wa wananchi. (*Makofi*)

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu ambaye anatakiwa kuwepo ni yule ambaye hata mlo mmoja kwa siku hana, mtu ambaye hawezi kumudu gharama mbalimbali za matibabu, mtu ambaye ana watoto walio chini ya miaka mitano na wengine wanatakiwa kwenda shule lakini hawezi kumudu gharama za kuwapeleka watoto wake shule na kukidhi baadhi ya vigezo vingine vya elimu na afya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kusema kwamba, kama kuna sehemu wameondolewa ambao kweli ni maskini, labda kwa bahati mbaya tu wamejitahidi wameweza kuboresha hali ya maisha yao, tumetoa maelekezo waendeleo kubaki katika mpango mpaka hapo tutakapofanya tathmini ya kina ya kitaalam kwa vigezo ambavyo tumeviweka. Si hiyo tu, hata ikifikia wakati atakapohitimu katika *graduation*, lazima akae kwa miaka mitatu na baada ya hapo tutampatia *notice* ya kusudio la kumwondoa miezi sita kabla ili aweze kujiandaa na tutakuwa tukiendelea kumfuatilia.

Kwa hiyo, nipende kusema kwamba, wananchi wasibughudhiwe, wale ambao kweli wana umaskini kwa mujibu wa vigezo hivyo na wakati wa kuandikishwa walikuwa kweli wana umaskini. Kwa wale ambao walikuwa hawana vigezo na walipokea hizi fedha, fedha zote watazirejesha.

MWENYEKITI: Ahsante. Injiniya Nditiye baada ya maelezo ya Waziri una maelezo ya ziada?

MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nina maelezo ya ziada kidogo, kwenye hotuba yake alizungumzia kwamba wale ambao walipata ile pesa bila kustahili watakiwa wakatwe halafu walipe ile pesa. Hofu yangu ni utekelezaji wa suala hilo, kwa sababu kule vijijini kauli kama hii ikienda, kwa kuwa waliofanya makosa ni *TASAF* wenyewe, wanaweza kuanza kuwanyanyasa wananchi. Kwa hiyo, naomba Serikali iamue kwamba watu waliopata kimakosa wasidaiwe isipokuwa waondolewe wale ambao hawakustahili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kauli ya Serikali.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kama ni kauli napenda kusema hiyo ndiyo kauli ya Serikali. Waliopata ambao waliwekwa kimakosa hawastahili kudaiwa, lakini tunaendelea kusisitiza wale ambao walikuwa hawana vigezo na kwa kughushi kabisa wakijua kwa makusudi wanachokifanya ni kosa la jinai, hao ndiyo tutahangaika nao mpaka mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuseme kuwa tumeshatoa waraka huu na nitahakikisha mimi mwenyewe pia nalifuatilia kuweza kulisimamia na Waheshimiwa Wabunge waendeleo kutusaidia pia katika kufuatilia suala hili.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Anna Lupembe.

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nataka ufafanuzi tu, naishukuru Serikali imetoa ajira kwa Madaktari pamoja na Walimu lakini kuna kada nyingine haina ajira, ni lini Serikali itaajiri kada nyingine?

MWENYEKITI: Kada nyingine kada ipi sasa msaidie kama wapi?

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wengine Watendaji, Wenyeviti, Makatibu, acha Walimu, kada ya Walimu ipo lakini kuna wafanyakazi.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Watendaji wa Vijiji.

MWENYEKITI: Haya. Mheshimiwa Keissy usimsemee yeye ndiye aliyeomba kuchangia. Amelewa Mheshimiwa Waziri.

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Waziri ameelewa.

MWENYEKITI: Ameelewa.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS(MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nimelelewa. Napenda tu kumpongeza Mheshimiwa Lupembe na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamekuwa wakifuatilia suala zima la ajira kwa wahitimu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba, azma ya Serikali kwanza kabisa hatuwezi kuajiri wahitimu wote, lazima hiyo ieleweke, tumekuwa tukisikia watu wengi hapa wakisema wahitimu wamekuwa wakiendesha bodaboda, wamekuwa wakifanya shughuli zingine, wamekuwa wakikaa hawana kazi na masuala mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapopanga idadi ya watumishi wapya wa kuajiri tunaangalia vigezo vingi. Tunaangalia uwezo wa kibajeti, tunaangalia maeneo ya kipaumbele, tunaangalia mahitaji na maeneo yenye upungufu mkubwa. Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaliona na kama nilivyoeleza tulishatoa vibali na watu walishaajiriwa na watu zaidi ya 9,200.

Pili, umeshasikia kuna ajira za Walimu wa sayansi na hisabati tayari Mheshimiwa Simbachawene alishawapangia vituo zaidi ya 3000 na tutaendelea kufanya hivyo; Wasanifu wa Maabara zetu za sayansi mashuleni pia Madaktari tumeshaanza 258, Jumatatu wataripoti kazini. Niseme tutaendelea na kada zingine ikiwemo wataalam wa Ardhi, Wapimaji, Maafisa Mipango Miji, Wataalam wa Maji, Wataalam wa Nishati, Mafuta na Gesi, Wataalam wetu wa TEHAMA, Walimu wengine pia, Wahadhiri pamoja na sekta nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kabla hatujamaliza mwaka huu wa fedha mpaka Juni, tutakuwa tumeajiri kwa idadi hiyo ambayo tutakuwa tumeipanga kwa awamu, pia mwaka ujao wa fedha tutaendelea kuajiri watumishi wengine wa umma zaidi ya

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

52,436. Muhimu tu ninachoomba kwa Waheshimiwa Wabunge, tatizo kubwa ni mgawanyo wetu *redistribution* hapo ndiyo kwenye shida. Unakuta sehemu zingine zina watumishi wengi zaidi wakati kuna sehemu zingine unakuta hazina watumishi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuendeleo kusaidiana, tumeshaanza kuandaa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA): *delivery points* kuhakikisha tunajua kila mtumishi yuko wapi, anafanya nini, na kama kweli pale panajitosheleza au anahitaji kuongezewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana, Mheshimiwa Waziri nadhani ameridhika kabisa, Mheshimiwa Lupembe.

MHESHIMIWA LUPEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Waziri amenijibu vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema kada nyingine kwa sababu tumeajiri Madaktari, ametuambia Madaktari lakini tuna Wauguzi, Wauguzi hakuna kabisa, kuna vituo vingine vya afya havina Wauguzi, tunahitaji Wauguzi. Ndio maana tunasema kada nyingine hatujasikia Wauguzi kama wameajiriwa ndiyo maana lazima tupate ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile sisi tuna Maafisa Maendeleo, tunawahitaji sana Maafisa Maendeleo ndani ya maeneo yetu, akinamama wanatakiwa wafundishwe ujasiriamali, akinamama wanatakiwa wapate maelekezo, lazima sasa tupate ufafanuzi. Nimefurahi kusikia Serikali inalifuatilia hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Haya tunashukuru sana. Mheshimiwa Ritta Kabati.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nitambue kazi nzuri sana inayofanywa na Serikali hii ya Awamu ya Tano ikiwa ni pamoja na Serikali kuanza kulipa madeni ya Walimu yaliyofanyiwa uhakiki, bado kuna sekta nyingine ambazo wafanyakazi wake wanayo madai yao kwa Serikali. Mfano; Afya, Kilimo,Utawala na kadhalika. Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha kwamba inalipa madeni kwa kada nyingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikia uchungu sana ninapoonza kwamba wafanyakazi wanataka kuipeleka Serikali Mahakamani, wafanyakazi wanataka kuitisha mgomo kitu ambacho nafikiri ni aibu kwa Serikali, nikitambua kwamba Mheshimiwa Rais wetu ameamua kwamba watu wote sasa watendewe haki kwa sababu hizi rasilimali ni za kwetu wote. Naomba sasa jibu la Serikali kuhusiana na wafanyakazi ambao bado nao madai yao hayajalipwa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa hoja ya Mheshimiwa Ritta Kabati. Bahati nzuri na mimi mwenyewe ni Mbunge ninayetokana na Vyama vya Wafanyakazi, kwa hiyo nipende tu kusema kwamba hoja yake naiona. Pia kwa niaba ya Serikali napenda kusema kwamba Serikali inatambua na kuthamini Watumishi wote wa Umma, pia itakuwa ikiendelea kutenga bajeti ili kuweza kulipa madai haya mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba kwanza chanzo cha madai ni nini? Nikija kwenye madai ambayo ya mishahara, kwanza kabisa unakuta kuna

Watumishi waliopandishwa vyeo lakini hawajarekebishiwa mishahara, unakuta kuna watumishi wengine wanastahili posho mbalimbali kama za kukaimu lakini wanajikuta mpaka hela inakuja kufika tayari imeshatengeneza deni. Kwa hiyo, napenda kutoa rai kwa mamlaka zetu za ajira kwanza wajitahidi kuingiza katika mfumo mapema sana pindi mtumishi anapofanyiwa mabadiliko ya kiutumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nipende kusema kwamba Serikali imekuwa ikitenga fedha kulipa malimbikizo ya mishahara na madai mengine yasiyo ya mishahara. Niipongeze sana TAMISEMI pamoja na Wizara ya Elimu kupitia Hazina, wamekuwa wakifanya kazi nzuri. Katika miaka hii miwili tu ya fedha wamelipa zaidi ya billioni 33 na mlimsikia Mheshimiwa Simbachawene.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa malimbikizo ya mishahara nipende tu kusema kwamba, katika mwaka wa 2015/2016, tuliweza kulipa zaidi ya shilingi bilioni 28.9. Katika mwaka huu wa fedha pekee yake tumeweza kupokea *claims* za malimbikizo ya mishahara takribani shilingi bilioni 56.4, kati ya hizo tumeshahakiki madai ya zaidi ya shilingi bilioni 35.5 na madai ya shilingi bilioni 21.1 tunaendelea kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa nyingine tumepokea madeni ambayo yaliyokuwa na kasoro na tumeyarudisha kwa waajiri ili kasoro hizo zirekebishwe. Napenda tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge madeni haya tunayatambua, madeni haya tunayafahamu tutahakikisha tunatenga fedha kila uwezo wa kibajeti utakaporuhusu kuhakikisha kwamba watumishi hawawi na madeni, tusiwavunje moyo.

MWENYEKITI: Nakushukuru. Mheshimiwa Ritta Kabati una cha kuongeza?

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Waziri, naomba kama ambavyo madeni ya Walimu yameshaanza kulipwa basi na hizi kada nyingine zilipwe kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ruth Mollel.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nina dogo ambalo ningependa kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Katika hoja yangu ya hotuba yangu, nilizungumzia pia kuhusu hizi teuzi za kisiasa na katika wale walioteuliwa kwa hawa Watendaji tunao karibu 65 kati ya 195. Najua pia sina idadi ya ma-DAS na ma-RAS na kwa mtazamo huo ningependa kujua kwa sababu katika Utumishi wa Umma kuna waraka ambao unasema hizi nafasi ni kutoka ndani, unaangalia katika Utumishi wa Umma ni wapi wale Maafisa Waandamizi waweze kupata nafasi ya kupanda na kushika vyeo vya utendaji. Najua Rais mwenye mamlaka ya uteuzi anaweza kuteua mtu yeyote lakini kuna utaratibu ambao umewekwa katika utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inatoa nafasi kwa ajili ya hawa Watendaji Waandamizi waweze kupata upenyo wa kupanda kwenda kuwa Watendaji Wakuu katika Utumishi wa Umma. Siyo hivyo tu, pia tunajenga kitu kinaitwa *Civil Service Culture*, ambayo hiyo *culture* inajengeka tangu unapokuwa katika Utumishi wa Umma unapanda na kuijenga hiyo *culture*. Hiyo *culture* huwezi kui- *acquire* tu *from nowhere* na kwa utaratibu huo tumeona teuzi za watu wengine ambao hawajawahi kufanya kazi katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maoni ya Kambi ya Upinzani kwamba kwa mtindo huu tunaua ile *culture* ya Utumishi wa Umma. Ningependa kujua Mheshimiwa Waziri tuna mkakati gani au una ushauri gani hata kwa Mheshimiwa Rais kuona kwamba huu utaratibu uliowekwa wa kupandishwa watu vyeo ni muhimu sana katika Utumishi wa Umma kuweza kujenga *culture* na utumishi ambao uko imara hauna siasa..... (*Makofi*)

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI UMMA NA UTAWALA BORA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Alitaka kujua pia idadi ya ma-DAS ni 71 ambao waliteuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende tu kusema kwamba kwa mujibu wa Ibara ya 36(2) ya Katiba yetu, Mheshimiwa Rais anayo madaraka ya kuteua watu kushika nafasi mbalimbali za Madaraka ya Uongozi ambao wanawajibika kuweka sera mbalimbali katika Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kusema kwamba Mheshimiwa Rais anayo madaraka ya kufanya hivyo. Ukiangalia katika hao allowateua wana sifa na ndiyo maana wameteuliwa kushika madaraka hayo. Mheshimiwa Rais na Serikali hatutasita kuteua watu wengine ambao wana sifa ili mradi tu hatuvunji Katiba, hatuvunji sheria, kanuni na miongozo mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Ruth Mollel.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, naona nitashika shilingi kidogo ya Waziri. Pamoja na kwamba Mheshimiwa Rais anayo mamlaka, nakubali kabisa anayo mamlaka, katika mamlaka hayo vilevile kuna nyaraka zinatolewa zinazoongoza hizi teuzi. Je, ni kitu gani ambacho wewe utaweza kukifanya kwa ajili ya kumshauri Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Utumishi wa Umma unakuwa imara na unakuwa hauna mlengo wowote wa kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida itakayokuja ni kwamba hawa wenye mlengo wa kisiasa walioteuliwa, kesho kikija Chama kingine naye atawaondoa ataweka wa kwake, kwa

hiyo tunakosa utumishi *stable* katika Utumishi wa Umma. Mawaziri na Wabunge miaka mitano tumeondoka, Utumishi wa Umma ndiyo ambao ni *sustainable*, unakuwa *permanent* kuweza kuendesha nchi. Kwa hiyo, sijakubaliana kabisa na hoja hiyo. Naomba hoja hiyo ijadiliwe.

MWENYEKITI: Haya. Tuchukue wawili tu upande huu au watatu, maana Waheshimiwa napenda sana mnavyojitolea kufanya kazi za wananchi, lakini pia ziwe na tija kidogo. Tuanze na Mheshimiwa Mnyika, Mheshimiwa Paresso, Mheshimiwa Suzan Kiwanga, huku inatosha.

Sasa tuhamie upande huu Mheshimiwa Obama, Mheshimiwa Mary Nagu, Mheshimiwa Kakunda na Mawaziri hawa wawili, Waziri wa Viwanda na Mheshimiwa mwenyewe mwenye dhamana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Mheshimiwa Mnyika.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ruth Mollé ya kupinga Rais kuteua makada wa Chama cha Mapinduzi kwenye nafasi za utumishi. Mheshimiwa Ruth Mollé ametaja idadi ya makada 65, hawa 65 ni wale ambao moja kwa moja waligombea kura za maoni za CCM, wameteuliwa kuwa Wakugenzi wa Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ambalo Mheshimiwa Rais amelifanya ni wazi kwanza linakiuka Katiba ya nchi, kwa sababu Ibara 74 ya Katiba ya nchi inaeleza juu ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Ibara mojawapo inatamka kwamba,

“Yeyote ambaye anahusika kwa niaba ya Tume ya Uchaguzi kwenye masuala ya uchaguzi, hatakiwi kuwa mwanachama wa Chama chochote cha Siasa.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha kuteua Wakurugenzi ambao kwa kadi kabisa kwa kuwa waliingia kwenye kura za maoni, inathibitika kabisa ni makada wa

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Chama cha Mapinduzi, si kitu sahihi. Si hivyo tu, tumeona namna ambavyo Mheshimiwa Rais baada ya uchaguzi ameondoa sehemu kubwa ya Wakurugenzi hasa wale ambao kwa kiwango kikubwa waliwatangaza Wabunge wa Upinzani kwenye maeneo mbalimbali kuwa ndiyo wameshinda. Kitendo cha kuwaondoa wale waliotangaza Wabunge wa Upinzani wameshinda na kuingiza makada.....

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mnyika umeeleweka, muda wako umekwisha. Mheshimiwa Kiwanga.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ongea polepole tu hakuna shida.
(Kicheko)

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ruth Mollé, ni ukweli usiopingika kwamba, nachukua mfano moja kwa moja, katika Bunge lililopita niliwahi kumuuliza swali aliyekuwa Waziri wa Utumishi wa Umma Mheshimiwa Hawa Ghasia, nikasema watu wamemaliza masomo, watoto wetu wana *degree* na kada mbalimbali, lakini wanashindwa kuteuliwa kwenye nafasi mbalimbali za Ukurugenzi na Ukuu wa Idara. Vile vile, katika Halmashauri kuna wafanyakazi wengi wamefanya kazi kwenye hizo Halmashauri mpaka sasa wanakaimu hizo nafasi, wanasema mpaka wapekuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Hawa Ghasia alinjibu hawawezi wakateua watu bila kupekuliwa. Leo katika Awamu hii ya Tano ni kinyume kabisa na utaratibu, hawa watu hawajawahi kufanya kazi kwenye hizo Halmashauri wala kwenye Utumishi wa Umma, kutoka Wajumbe wa *NEC*.

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Mkurugenzi wa Ubungo, Mjumbe wa *NEC* leo amekuwa Mkurugenzi, Wajumbe mbalimbali wa *NEC* wamekuwa ma-*DAS*. Ni Serikali gani ambayo inajichanganya yenyewe na kuteua watu ambao hawastahili na hawajafanyiwa upekuzi...

MWENYEKITI: Ahsante sana. Naona umeanza kuchangamka. Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, karibu.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nipate kuwaeleza watu kwamba Utumishi wa Umma ni kweli ni mahali ambapo panahitaji uadilifu, panahitaji weledi, panahitaji mtu atakayemudu kazi aliyopewa. Kwanza nisichokubaliana ni kwamba hivi mnajuaje kwamba hawakupekuliwa? (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Bashite.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, siamini mtu anaweza kuwa Mkurugenzi bila ya kupekuliwa. Sina sababu ya kutoamini Serikali yangu, naamini imefanya upekuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa hata Watumishi wa Serikali hawakukataliwa kwenda kugombea, ila unapokwenda kugombea na kuwa Mbunge lazima uondoke, lakini kama hujawa Mbunge na hasa ukirudia kwenye kura ya maoni hujafika mbali. Kwa hivyo, ndugu zangu nafikiria kwamba, Mheshimiwa Rais amepewa mamlaka ya kuweza kufanya uteuzi na kama amepewa dhamana hiyo, anajua vigezo ambavyo vinatumika na naamini vigezo hivyo vimetumika, kwa sababu nimewahi kuwa Waziri wa Utumishi, nina hakika hilo lilifanyika. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Nagu kwa maelezo yako mazuri. Ni kweli Waheshimiwa Wabunge someni Katiba ya Jamhuri ya Muungano, someni

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Sheria ya Uchaguzi; ni pale unapoteuliwa na Tume ya Uchaguzi ndiyo unatakiwa kuondoka. Makundi ambayo yamekatazwa yanafahamika.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Watumishi wa Tume yenyewe ya Uchaguzi, Watumishi wa Mahakama na vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, isomwe lbara ya 74, lbara ndogo ya 14.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, kwanza sijakupa ruhusa ya kuongea, usibishane na mimi tafadhali, kwa hiyo, hilo ni la kisheria. Serikali ina watalaam wake. Tunaendelea na Mheshimiwa Kakunda.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kuna aina ya unafiki kidogo katika suala hili, kwa sababu Mheshimiwa boshi wangu Mama Mollel, wakati akiwa Katibu Mkuu, Utumishi, ndiye aliyesimamia *meritocracy* katika Utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ule mwaka 2002 mpaka 2005 watu walikuwa wanasailiwa kutoka kokote kule mpaka *private sector*, mtu anatoka *private sector* anapewa Ukurugenzi, sasa leo anasimama hapa anapinga kile kile ambacho yeye ndiye alikiongoza pale Utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nimkumbushe tu hilo ili alijue na aondoe hoja yake. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Obama amesema hakuwa amesimama, kwa hiyo hakuna shida. Mheshimiwa Waziri Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kupoteza muda, mimi nataka niisome Katiba na Madaraka ya Rais yanatamkwaje kwenye jambo hilo, kama Katiba haijavunjwa basi hakuna Sheria ambayo imevunjwa. Ibara ya 36(2) Inasema hivi:

“Rais atakuwa na Madaraka ya kuteua watu kushika nafasi za madaraka ya viongozi wanaowajibika kuweka sera za Idara na Tasisi za Serikali, na Watendaji Wakuu wanaowajibika kusimamia utekelezaji wa Sera za Idara na Taasisi hizo, katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, nafasi ambazo zimetajwa katika Katiba hii au katika sheria mbalimbali zilizotungwa na Bunge kwamba zitajazwa kwa uteuzi unaofanywa na Rais.” (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Rais juzi hapa amemteua Profesa Kitila Mkumbo kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji hiyo haihojiwi, lakini utaratibu wa kuwateua watu mbalimbali kutoka hata kwenye *private sector*, ulikwishakuwepo, ndiyo maana leo tuna akina Ndugu Nehemia Mchechu ambaye anaendesha *NHC* vizuri sana, tulikuwa na Ndugu Lawrence Mafuru wametoka kwenye *private sector* ndiyo ma-*CEO* wa Tanzania wanaoweza kukumbukwa kwa kufanya kazi nzuri. Kwa hiyo, utaratibu huu ulianza muda mrefu ni basi tu leo inazungumzwa kwa Wakurugenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, *vetting* ilifanyika tena ya uhakika, vijana hawa wana uwezo mkubwa na wameweza kufanya kazi nzuri na nataka niseme tu Waheshimiwa Wabunge tuwaunge mkono na tuwasaidie badala ya kupambana nao. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nichangie dogo nikiongezea kwenye mchango wa Mheshimiwa

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Simbachawene, uteuzi wa Mheshimiwa Rais kwa macho ya haraka unatia mashaka, kinachomwongoza Mheshimiwa Rais ni *performance*, kama unaweza kwenda kwa kasi yake anakupa *steering* unaendesha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia Wilaya nyingi alizoweka watu mabadiliko yameonekana. Mheshimiwa Simbachawene hakuliona, Wakurugenzi wapya wamefunua mambo ambayo hayakujulikana, ndicho kinachotakiwa, anabadili mazoea, yeyote atakayefanya vizuri kutoka popote kama ilivyozungumzwa kwa Profesa Kitila, yeyote atapewa kazi, kwa hiyo msiwe na wasiwasi. Kama alivyosema Mwenyekiti unagombea leo, unakana Chama chako, unakuja na wanaotaka kuja treni ndiyo hii, waje tuondoke.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI UMMA NA UTAWALA BORA): Hata Mheshimiwa Mnyika anaweza kuteuliwa.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa baba njoo hapa ukikana tunakupaa nafasi unafanya kazi. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Ruth Mollel.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naona nimechangamsha Bunge kidogo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hao wote mliowataja ni *public sector*, mimi nazungumzia makada wa CCM. *Public sector* inakubalika na tunasema tunataka utumishi ambao ni *impartial* ambao hauna mlengo wowote wa kisiasa. Hao wote aliotaja ndugu yangu pale sijui akina Ndugu Mafuru wote walikuwa kwenye *public sector including private*, wote walikuwa kwenye *public sector*, nazungumzia wale makada ambao walikwenda wakashindwa huko wakarudi wakawa Wakurugenzi kwenye nafasi za Utendaji wa Utumishi wa Umma...

TAARIFA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu nimtaarifu kwamba hawa, kwenda kugombea siyo kwamba hawakuwa watumishi. Wapo waliokuwa Walimu, waliokuwa Waratibu wa Elimu, wapo watu wengi ni Watumishi wa Umma ila tu walikwenda kugombea, kama ambavyo wewe ulikuwa Katibu Mkuu lakini kimya kimya umekuja ukawa Mbunge. *(Makofi/Kicheko)*

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kwa Mheshimiwa Simbachawene aliyekuwa anazungumza.

MWENYEKITI: Sawa. Waheshimiwa Wabunge huwa nawaambieni ukiwa kwenye Kamati mambo ya taarifa haya, sasa ndiyo maana...

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio kuashiria kutokubaliana na Mwenyekiti)

MWENYEKITI: Nilikuwa sijamruhusu hata kuongea, lakini nasema hivi kila siku tunajifunza. Sasa nasema tunaendelea. Mheshimiwa Ruth Mollel, malizia hoja yako tuiamue. *(Makofi)*

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningetamani wote mkubaliane na mimi, kwa sababu leo ninyi mko kwenye madaraka, kesho tunaweza tukawa sisi. *(Kicheko/Makofi)*

MBUNGE FULANI: Haiwezekani.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Itafika. Sasa niseme hivi, *on a serious note*, Mheshimiwa Waziri natoa ushauri wa bure kwamba, tujaribu kuifanya *civil service impartial* kwa ajili ya mustakabali wa nchi hii. Tuache kuteua watu ambao wapo

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kwenye *NEC*, wako sijui kwenye nini, wanaingia Serikalini, kwa kweli siyo utawala bora. Kwa hiyo shilingi yako nakurejeshea, lakini huo ndiyo ushauri wangu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Tunakushukuru kwa kurejesha shilingi umekuwa ni muungwana kama ilivyo kawaida yako. Sasa tunaendelea amesharejesha shilingi.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif.1002 - *Finance and Accounts*.....Sh. 329,795,000/=

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge kabla sijawahoji, nimeangalia huo mudana kwa kutambua kwamba kesho tuna tukio zito linalotuhusu sote, nitumie mamlaka niliyonayo kwa mujibu wa Kanuni ya tano (5) twende moja kwa moja kwenye *guillotine*. Ahsanteni. (*Makofi*)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1003 - *Govt. comm. Unit*.....Sh. 202,530,000/=
Kif. 1004 - *Procurement Management Unit*...Sh. 159,082,000/=
Kif. 1005 - *Internal Audit Unit*.....Sh. 240,243,000/=
Kif. 1006 - *Planning Division*.....Sh. 287,096,000/=
Kif. 1007 - *Information and Comm. Tech. Unit*.....Sh. 151,690,000/=
Kif. 2001 - *Policy Dev. Division*.....Sh. 436,041,000/=
Kif. 2002 - *Management Services Div.*Sh. 593,310,000/=
Kif. 2003 - *Establishment Division*.....Sh. 500,627,000/=
Kif. 2004 - *Ethic Promotion Division*.....Sh. 280,300,000/=
Kif. 2005 - *Human Capital Management Division*.....Sh. 931,053,000/=
Kif. 2006 - *Performance Contracting*.....Sh.247,940,000/=
Kif. 3001 - *Human Resources Dev. Division*...Sh. 5,794,277,000/=
Kif. 3004 - *Diversity Management Unit*.....Sh. 189,200,000/=
Kif. 4002- *Mgt Information system Div*.....Sh. 4,483,175,000/=

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 4 – Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa

Kif. 1001 - <i>Administration and HR Mgt.</i>	Sh. 935,027,000/=
Kif. 1002 - <i>Finance and Account</i>	Sh. 405,880,000/=
Kif. 1003 – <i>Planning, Monitoring and Evaluation Unit</i>	Sh. 43,380,000/=
Kif. 1004 – <i>Information and Communication Tech Unit</i>	Sh. 72,525,000/=
Kif. 1005 – <i>Legal Services Unit</i>	Sh. 16,750,000/=
Kif. 1006 – <i>Internal Audit Unit</i>	Sh. 24,370,000/=
Kif. 1007 – <i>Government Comm. Unit</i>	Sh. 34,210,000/=
Kif. 1008 – <i>Procurement and Mgt. Unit</i>	Sh. 30,460,000/=
Kif. 4001 – <i>Archive Management Division</i>	Sh. 227,645,000/=
Kif. 4002 – <i>Records Management Division</i>	Sh. 278,355,000/=
Kif. 4003 – <i>Records Center Division</i>	Sh. 199,304,000/=
Kif. 4004 – <i>The Founders of the Nation Centre Division</i>	Sh. 107,820,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 11 – Ofisi ya Ushauri wa Mafuta na Gesi

Kif. 2001 – <i>Corporate Services</i>	Sh. 711,073,000/=
---	-------------------

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 20 – Ikulu

Kif. 1001 – <i>Administration and HR Mgt</i>	Sh. 16,267,586,000/=
--	----------------------

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 30 – Sekretariati ya Baraza la Mawaziri

Kif. 1001 - Administration and HR Mgt.....	Sh. 363,167,232,000/=
Kif. 1002 - Finance and Accounts.....	Sh. 497,920,000/=
Kif. 1003 – Policy and Planning.....	Sh. 486,612,000/=
Kif. 1004 – Internal Audit Unit.....	Sh. 290,540,000/=
Kif. 1005 – Information and Communication Tech. Unit.....	Sh. 243,650,000/=
Kif. 1006 – Procurement and Mgt. Unit.....	Sh. 274,360,000/=
Kif. 2001 – Cabinet Secretariat.....	Sh. 1,676,791,000/=
Kif. 2002 – Government Comm.....	Sh. 370,970,000/=
Kif. 2003 – Good Governance.....	Sh. 476,975,000/=
Kif. 2004 – Public Service Appeal.....	Sh. 469,500,000/=
Kif. 2005 – Public Sector Reform Coordination Unit.....	Sh. 359,595,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 33 – Sekretariati ya Maadili ya Viongozi wa Umma

Kif. 1001 - Administration and HR Mgt.....	Sh. 1,461,345,000/=
Kif. 1002 - Finance and Accounts.....	Sh. 392,722,400/=
Kif. 1003 – Planning monitoring & Evaluation Unit.....	Sh. 486,612,000/=
Kif. 1004 – Gvt. Comm. Unit.....	Sh. 115,984,200/=
Kif. 1005 – Procurement and Mgt. Unit.....	Sh. 98,012,200/=
Kif. 1006 – Internal Audit.....	Sh. 183,721,722/=
Kif. 1007 - Information & Communication Tech. Unit.....	Sh. 163,523,200/=
Kif. 1008 - Legal Services Unit.....	Sh. 204,716,000/=
Kif. 2001 - Public Service Leaders Division.....	Sh. 960,399,3000/=
Kif. 2002 – Political Leaders Division.....	Sh. 616,712,000/=
Kif. 2003 – Zonal Offices.....	Sh. 2,638,924,600/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 67 – Sekretariati ya Ajira Katika Utumishi wa Umma

Kif. 1001 - Administration and HR Mgt.....	Sh. 952,206,000/=
Kif. 1002 - Finance and Accounts.....	Sh. 150,781,000/=
Kif. 1003 – Planning, Monitoring and Evaluation.....	Sh. 58,153,105/=
Kif. 1004 – Government Comm. Unit.....	Sh. 59,525,895/=
Kif. 1005 - Legal Services Unit.....	Sh. 67,262,000/=
Kif. 1006 – Procurement and Mgt. Unit.....	Sh. 72, 540,000/=
Kif. 1007 – Management Inform. Systems.....	Sh. 140,380,000/=
Kif. 1008 – Internal Audit.....	Sh. 100,505,000/=
Kif. 2001 – Recruitment Mgt. Division.....	Sh. 578,690,000/=
Kif. 2002 – Quality Control.....	Sh. 185,932,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 94 - Tume ya Utumishi wa Umma

Kif. 1001 - Administration and HR Mgt.....	Sh. 2,724,861,891/=
Kif. 1002 - Finance and Accounts Unit.....	Sh. 115,752,000/=
Kif. 1003 – Planning, Monitoring and Evaluation Unit.....	Sh. 519,902,000/=
Kif. 1004 – Internal Audit.....	Sh. 70,580,000/=
Kif. 1005 – Procurement and Mgt. Unit.....	Sh. 39,100,000/=
Kif. 1006 - Legal Services Unit.....	Sh. 49,760,000/=
Kif. 1007 – Government Comm. Unit.....	Sh. 85,389,109/=
Kif. 1008 - Information Communication and Tech. Unit.....	Sh. 84,860,000/=
Kif. 2001 – Civil Service.....	Sh. 444,313,000/=
Kif. 2002 – Local Government Service.....	Sh. 408,495,000/=
Kif. 2003 – Teachers’ Service.....	Sh. 0
Kif. 2005 – Health Service.....	Sh. 366,503,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

MIRADI YA MAENDELEO

Fungu 4 – Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa

Kif. 1001 - *Administration and HR Mgt*.....Sh. 2,000,000,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 30 - Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri

Kif. 1003 – *Policy and Planning*Sh. 379,570,890,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Fungu 32 - Menejimenti ya Utumishi wa Umma

Kif. 1001 – *Administration and HR Mgt*.....Sh. 3,000,000,000/=

Kif. 1006 – *Planning Division*.....Sh. 0

Kif. 1007 – *Information and Comm. Tech. Unit*.....Sh. 0

Kif. 2001 – *Policy Development Division*.....Sh. 0

Kif. 2002 – *Management Services Division*.....Sh. 0

Kif. 2004 – *Ethic Promotion Division*.....Sh. 0

Kif. 2005 – *Human Capital Management Division*.....Sh. 0

Kif. 2006 – *Performance Contracting*.....Sh. 0

Kif. 3004 – *Diversity Management Unit*.....Sh. 0

Kif. 4002 – *Mgt. Info. System Division*.....Sh. 4,000,000,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 33 - Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma

Kif. 1001 – *Administration and HR Mgt*.....Sh. 57,200,000/=

Kif. 1002 - *Finance and Accounts*.....Sh. 42,100,000/=

Kif. 1003 - *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*.....Sh. 280,549,992/=

Kif. 1004 – *Government Comm. Unit*.....Sh. 58,099,600/=

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Kif. 1007 – Information and Communication Tech. Unit.....	Sh. 50,000,000/=
Kif. 1008 - Legal Services Unit.....	Sh. 5,900,000/=
Kif. 2001 – Public Service Leaders Division.....	Sh. 50,700,000/=
Kif. 2002 – Political Leaders Division.....	Sh. 647,661,748/=
Kif. 2003 – Zonal Offices.....	Sh. 457,788,660/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 67 - Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma

Kif. 1007 – Management Inform. Systems.....	Sh. 750,000,000/=
---	-------------------

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake ya kujadili Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

(Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja taarifa. *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu mkubwa naomba kutoa taarifa kuwa Bunge limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia makadirio ya matumizi ya Ofisi ya Rais, Ikulu; Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Taasisi zake, kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018, kifungu hadi kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo basi, naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.
(Makofi)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante. Hoja imetolewa na imeungwa mkono, sasa nitaitoa kwenu muiamue, wanaoafiki hoja ya makadirio ya matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na Taasisi zake, yaidhinishwe na Bunge.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Serikali ya mwaka 2017/ 2018
Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na
Utawala Bora yalipitishwa na Bunge)*

MWENYEKITI: Walioafiki wameshinda. Kwa hiyo, natamka rasmi kwamba, taarifa ya Kamati ya Matumizi kuhusu makadirio ya matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, pamoja na Taasisi zilizo chini ya ofisi hiyo, yamepitishwa rasmi na Bunge hili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, niwashukuruni sana kwa kazi nzuri na nzito mliyoifanya kwa siku ya leo, yamekuwa ni mafungu mengi Ofisi ya Rais – TAMISEMI lakini na hii ambayo tumemaliza nayo sasa hivi. Mmefanya kazi ya kujituma kama ulivyo wajibu wetu.

Nawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri, Waziri Angellah Kairuki, Mheshimiwa George Simbachawene na timu yake yote na hasa wataalam wa Serikali ambao hamuwaoni hapa, walioweza kufanikisha bajeti hizi. Tumeifanya kazi yetu kama Bunge, tumeidhinisha pesa hizi kwa hiyo tunatarajia pesa itapatikana kwa mtiririko ambao Bunge tunatarajia iwe hivyo, watekeleze majukumu yao kwa uadilifu katika kipindi cha mwaka ujao wa fedha 2017/2018. Kila la Kheri Waheshimiwa Mawaziri. *(Makofi)*

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tunajua ratiba ya shughuli ya kesho imeshagawiwa kwetu, kwa hiyo kati ya saa 3.30 mpaka saa 4.00 tuwe tumefika katika maeneo ambayo tumeelekezwa kufika. Ni tukio kubwa ambalo linatugusa wote la kumwomba mwenzetu ambaye ametangulia mbele ya haki.

Waheshimiwa Wabunge, sina matangazo mengine, kwa maana hiyo sasa, baada ya kuwashukuru kwa kazi nzuri mliyoifanya, naomba kuliahirisha Bunge hadi siku ya Jumatatu, tarehe 24 Aprili, saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

(Saa 3.27 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 24 Aprili, 2017, Saa Tatu Asubuhi)